

# TUJIFUNZE UISLAMU





# TUJIFUNZE UISLAMU

KIDATO CHA PILI



---

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

**Jina la Asili:**

Dinimi Öğreniyorum İslam - Orta 2 (Şafii)

**Watunzi:**

Faruk SALMAN

Nazif YILMAZ

Dr. Recep ÖZDIREK

Dr. Faruk KANGER

**Mfasiri:**

Ibrahim Hamisi KABUGA

**Mhariri:**

Jopo

**Mratibu:**

Muhammad Aşır KARABACAK

**M pangiliaji:**

Hamza Daudi MSUYA

Zulfikal Kamal SALUM

**Kuhakikiwa kwa mujibu wa madhehebu ya imam Shafii:**

Prof. Recep ÖZDIREK

Mehmet Şirin KIZILKAYA

**Mchapishaji:**

Rehema Friendship and Solidarity Trust.

**Anuani:**

Plot 80395 block D Mbezi Beach Tangibovu, Dar es salaam.

**Simu:**

+255 656 639 558

**Barua pepe:**

refso2010@gmail.com

**Tovuti:**

[www.islamicpublishing.org](http://www.islamicpublishing.org)

**Mchapaji:**

Erkam Printhouse

**ISBN:**

978-605-302-274-9

**Istanbul - 2022 / 1443 H**

**Language:** Swahili / Kiswahili

---



## DIBAJI

*ك*imidi zote ni za Mola wetu aliyetupa heshima na furaha ya kuishi kama Waislamu!

Salamu ziende kwa Mtume wetu Mpandwa (rehma na amani ziwe juu yake), familia yake na mas-wahaba zake walioutekeleza na kuufundisha Uislamu kwa namna bora kabisa!

Mtume wetu Mpandwa (rehma na amani ziwe juu yake), alikuwa mwalimu adhimu kabisa aliyefundisha Uislamu kwa wanadamu. Kitabu alichofundisha ni Qur'an Tukufu, muujiza usiomithilika. Mtume huyo aliyebarikiwa, aliisoma na kuifafanua Qur'an. Na alitekeleza imani, matendo ya ibada na maadili yaliyofundishwa na Qur'an kwa namna nzuri kabisa. Baada yake, Maswahaba, shakhsia adhimu kabisa wa Uislamu na watangulizi wetu walifanya juhud kubwa katika kuitekeleza dini hii adhimu na kuipeleka kwa vizazi nya baadaye. Hivyo, maarifa ya Uislamu yamefikishwa kwetu kutoka moyo mmoja kwenda mwingine na kutoka kinywa kimoja kwenda kingine. Na sasa, ni zamu yetu kujifunza.

Kitabu cha "Tujifunze Uislamu" kimeandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wa ngazi ya sekondari. Kitabu hiki kina sura kuu nne:

Sura ya kwanza inatufundisha kuhusu imani yetu.

Sura ya pili inatuelekeza namna sahihi ya kufanya ibada.

Sura ya tatu inatupatia kipengele kutoka katika maisha ya mfano ya Mtume wetu Mpandwa.

Na sura ya nne inatupatia mafunzo kuhusu tabia njema ambazo Muislamu anatakiwa kuzifuata na kuzitekeleza.

Ni matumaini yetu kuwa tunaweza kujifunza dini yetu nzuri kwa namna bora kabisa, na kuwa mionganoni mwa Waislamu ambao Mtume aliyebarikiwa atatabasamu pindi atakapotuona huko Akhera.

Tunamuomba Allah aijaze imani katika nyoyo zenu, aujaze Uislamu katika maisha yenu, na roho zenu azijaze usafi wa moyo. Malaika wasuhubiane nanyi, na watu wema wawe marafiki zenu!

Tunamuomba Allah Mtukufu awapende na kuwasidia!

Tunamuomba aifanye njia ya maisha yenu iwakeleke Peponi!

Hivyo kwa jina la Allah:...

رَبِّ يَسِّرْ وَ لَا تُعَسِّرْ رَبِّ تَمَّمْ بِالْخَيْرِ

"Mola wangu, yafanye kuwa mepesi, usiyafanye kuwa mazito, na uyahitimishe kwa kheri".



# YALIYOMO

## KUMUAMINI ALLAH: MOLA WA ULIMWENGU: / 9

<b>Kisa:</b> MTOTO ALIYEMUAMINI ALLAH.....	10
Kila Kazi ya Usanifu ni Ishara ya Msanifu .....	12
<b>Shairi:</b> Allah .....	14
<b>Kisa:</b> JIBU LA ABU HANIFA.....	15
M pangilio Kamili Katika Ulimwengu wa Ndani na Nje .....	17
<b>Kisa:</b> JIBU MOJA KWA MASWALI MATATU .....	19
Tunamtambua Allah Mtukufu Kupitia Sifa Zake .....	21
Sifa za Allah .....	22
<b>Kisa:</b> BINTI WA MUUZA MAZIWA.....	24
ALLAH ANAONA KILA KITU .....	28
Mola Wangu! Nimekutambua na Kukuamini kwa Moyo wangu wote .....	29
<b>Kisa:</b> KIJANA MWENYE IMANI .....	31
Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa (AL-Asma al-Husna) .....	34
Faida za kumuamini Allah .....	37
Upendo wa Allah .....	40
Kiini cha ibada yetu: Dua .....	42
Nimekuitikia ewe mja wangu.....	43
<b>Kisa:</b> NITAFAGIA, UTAMWAGILIA.....	44
Nini maana ya kuwa Muislamu? .....	46
<b>Kisa:</b> NANI ATAKAYEKUOKOA? .....	47
Mtume (s.a.w) alimpenda sana Allah .....	48
<b>MASWALI</b> .....	51

## ALAMA YA WEMA NA UZURI: KUAMINI MALAIKA / 55

<b>kisa:</b> SAUTI YA MALAIKA .....	56
Viumbe Wanaoonekana na Wasioonekana .....	58
Kuamini Malaika .....	59
Malaika huwaombea wagonjwa.....	61
Malaika Humuombea Aliyefunga.....	62
Faida za Kuamini Malaika .....	63

Malaika Huwaombea Waumini .....	67
Malaika huwaombea wanaotafuta elimu .....	68
<b>kisa:</b> MALAIKA, SHETANI NA MWANADAMU.....	69
Shetani .....	72
Mtume (s.a.w) na Malaika .....	75
Msaada unaoletwa na malaika .....	77
<b>MASWALI</b> .....	79

**MIIRAJ YA MUUMINI, NGUZO YA DINI YETU :**  
**SWALA (AL-SALAH) / 83**

<b>kisa:</b> SWALA YA KWANZA .....	84
Swala ni nini? .....	86
Kwa nini tunaswali? .....	87
FAIDA ZA SWALA .....	88
Nani anayewajibika kuswali? .....	90
Aina za Swala .....	90
MATENDO YA FARADHI KATIKA SWALA .....	94
Adhana (Al-Adhan) .....	95
Iqamah .....	97
Jinsi ya kuswali .....	98
Utekelezaji wa Swala Tano za Kila Siku .....	104
Baadhi ya Dua zinazosomwa Wakati wa Swala .....	109
DUA NA DHIKIR ZINAZOSOMWA BAADA YA SWALA .....	110
Sunnah za swala .....	112
Matendo yasiofaa wakati wa Swala .....	114
Tuswali kwa Unyenyekevu .....	115
UMUHIMU WA SWALA YA JAMA'AH .....	118
Baadhi ya Swala zinazoswaliwa kwa Jama'ah .....	123
Swala ya Mgongwa .....	127
Swala ya Msafiri .....	128
Kulipa Swala (Salat al-Qadhaa) .....	128
Sajda ya Kusahau (Sajdat al-Sahw) .....	130
Sajda ya Kisomo (Sajdat al-Tilaawah) .....	132
Nyakati zisizofaa Kuswali .....	133
<b>kisa:</b> SWALA ZANGU .....	134
Mtume wetu alipenda sana Kuswali .....	137
Misikiti na Vyumba vya Kuswallia .....	138
<b>MASWALI</b> .....	141


**NINAJIFUNZA KUHUSU MTUME WANGU:**  
**SIRA / 149**

<b>MACHOZI YALIYOGEUKA KUWA CHEMCHEM .....</b>	150
<b>1- MIAKA YA HUZUNI .....</b>	151
a) Kifo cha Abu Talib na Khadija .....	151
b) Zlara ya Taif na watu wenye hasira wa Saqif (Mwaka 620).....	152
<b>2- MJUMBE WA ALLAH AWALINGANIA WATU KWENYE UISLAMU .....</b>	153
a) Mikutano ya Aqaba na kiapo cha utii (Mwaka 621 na 622).....	154
b) Kiapo cha utii cha kwanza na cha pili cha Aqaba (mwaka 621 na 622).....	154
c) Miujiza ya Isra (Safari ya Usiku) na Mi'raj (kwenda mbunguni) (Mwaka 621) .....	157
d) Ukaidi wa Wapagani mbele ya Miujiza.....	158
<b>3- KIMBILIO LA MWISHO: HIJRA, HUZUNI YA KUIACHA MAKKA .....</b>	160
a) Mpango Hatari wa Wapagani .....	161
b) Wauaji waingia Kazini.....	162
c) Siku tatu Pangoni.....	162
<b>NYOKA MWENYE KUNG'ATA .....</b>	164
d) Kuwasili Madina na Swala ya Kwanza ya Ijumaa.....	165
e) Mwezi umetuchomozea.....	166
<b>4- MAISHA KATIKA MAKAO MAPYA YA MJI WA MADINA .....</b>	167
a) Ujenzi wa Msikiti wa Mtume (s.a.w).....	167
<b>MACHOZI.....</b>	168
b) Maswahaba walioishi msikitini ili kutafuta elimu: As-hab al-Suffah.....	168
c) Adhana ya kwanza.....	169
d) Udugu wa Kipekee .....	170
<b>CHUKUA UIPENDAYO NDUGU YANGU .....</b>	171
e) Chuki isiyokwisha ya Wapagani .....	171
f) Ruhusa ya kupigana (Mwaka 623 – 624) .....	172
<b>5- VITA VYA BADR (Mwaka 624).....</b>	173
a) Uadui usiokwisha .....	173
b) Hatua kwa hatua kuelekea Vitani .....	175
c) Vita yaanza .....	177
d) Ushindi wa Waliomuamini na Kumtegemea Allah .....	177
<b>MWENYE HURUMA HATA KWA MAADUI.....</b>	178
e) Wapagani Waliochukuliwa Mateka katika Vita vya Badr.....	179
<b>MASWALI .....</b>	180

## TABIA ZINAZOMFANYA MTU KUWA MUISLAMU MZURI:

### ADABU / 185


<b>NDOTO .....</b>	186
<b>ADABU ZA KUSALIMIANA .....</b>	187
Mambo gani tunayotakiwa kuzingatia wakati wa kutoa salamu? .....	188
Raha ya kutoleana salamu .....	190
<b>ADABU ZA KULALA NA KUPUMZIKA .....</b>	192
<b>ADABU ZA KULA NA KUNYWA .....</b>	194
<b>KUMBUKUMBU YA LADHA YA TENDE .....</b>	197
<b>ADABU ZA KUPIGA MWAYO, KUPIGA CHAFYA, KUKOHOA NA KUBEUA .....</b>	198
<b>UFUNGUO WA MASWALI .....</b>	201



KUMUAMINI ALLAH:

# MOLA WA ULIMWENGU

- ✿ *Uwepo na Umoja wa Allah*
- ✿ *Sifa na Majina ya Allah*
- ✿ *Faida za Kumuamini Allah*
- ✿ *Upendo wa Mtume wetu (s.a.w) kwa Allah*



## MTOTO ALIYEMUAMINI ALLAH

Katika nchi ya Babylon aliiishi mtoto aitwaye Ibrahim. Alikuwa akimvutia kila mtu kwa tabia njema na werevu wake. Watu wa nchi hii walikuwa wakiabudu masanamu, mwezi, jua, nyota, moto, maji, na vitu vingine. Mahekalu yao yalijaa picha na masanamu ya miungu hawa wa batili. Walimuacha Allah wakazisujudia picha na masanamu haya waliyoamini kuwa ni miungu na kuyaabudu.



Walikuwa wakiyaomba masanamu hayo yawatekelezee mahitaji yao au kuwalinda dhidi ya shari.

Ibrahim aliitazama imani hii ya kuchekesha kwa mshangao na kuchukua mazingatio. Hakuona mantiki yoyote ya watu hao kuwa na imani hizo za kushangaza. Hata Azar, baba wa Ibrahim, alikuwa na imani hizo. Azar alikuwa mchonga masanamu mashuhuri. Alikuwa akichonga miti na mawe kwa ajili ya kutengeneza masanamu, na watu walikuwa wakiyaabudu.

Ibrahim alipowaona watu wakiyasujudianakuyaombamasanamu hayo, aliwasikitikia. "Inawezekanaje vitu ambavyo muda mfupi uliopita vilikuwa miti au mawe viwe miungu wakati kuna fundi aliyevigeuza kuwa masanamu? Vinawezaje kuwalinda watu au kukidhi mahitaji yao?"

Japokuwa alikuwa mtoto, Ibrahim hakuwahi kuabudu masanamu. Alijaribu pia kuwashawishi wengine wasiyaabudu masanamu.

Siku moja Ibrahim alikwenda kwa wale waliokuwa wakiabudu vitu vy a angani kama vile nyota, mwezi na jua. Watu hao walikuwa akisubiri giza ili miungu yao ilijitekeze. Wakati wakijiandaa kuviaabudu Ibrahim alifika.

Baada ya muda anga ilijawa na giza. Nyota ya jioni ilijitekeza wakati watu wakizama kwa wasiwasi.

Nyota ya jioni ilionekana kwa uwazi zaidi kuliko nyota nyingine. Ibrahim

alinyoosha kidole angani, akawaambia wale waliokuwa wamekusanyika jirani naye, "Uzuri ulioje wa nyota hii! Huyu ndiye mola wangu."

Wale waliokuwa wakiabudu nyota ya jioni walidhani kuwa Ibrahim alikuwa akiamini kile walichokuwa wakikiamini na kwamba alikuwa amepata njia sahihi. Baada ya muda mfupi, nyota ya jioni ilipotea. Hapo Ibrahim akasema, "Hapana, huyu hawezi kuwa Mola wangu. Mola wangu hawezi kupotea na kuzama. Sipendi wale wanaotoweka na kuzama". Baadhi ya watu walioyasilika maneno haya ya kimantiki na ya hekma walikubaliana naye. Maelezo haya ya kimantiki yaliwafanya baadhi yao waanze kuwa na shaka dhidi ya imani zao wenyewe. Wengine walimkasirikia. Hao ni wale ambaa hawakumpenda mtoto huyu aliywatilia shaka miungu yao katika mahekalu yao wenyewe.

Baada ya muda mfupi, mwezi ulichomoza. Ulikuwa na mwangaza na mzuri zaidi ya ile nyota ya jioni. Kwa mara nyingine, Ibrahim akasema kwa sauti:

"Huyu ni mkubwa na ana mwanga mkubwa zaidi! Huyu ndiye mola wangu."

Baada ya muda, mwezi nao ukapotea. Hapo Ibrahim, akasema "Huyu naye amezama kama ilivoyozama nyota. Kama Mola wangu asingeniongoa, ningekuwa mionganini mwa wale wanaoamini kitu kisichokuwa na uhalisia. Hakika, huyu pia hawezi kuwa Mola wangu." Baada ya maelezo yake, watu walianza kukubaliana naye. Hata hivyo, baadhi yao hawakutaka kubadili imani zao walizozizoea, na hivyo hawakukubaliana na maelezo yake yenye mantinki.

Jua ilipochomoza, Ibrahim akasema "Huyu ndiye mola wangu. Huyu ni mkubwa kuliko wote!" Watu waliokuwa karibu naye

wakamshawishi kwa kusema "Sasa umeupata ukweli. Jua ndilo linalostahiki kuwa Mola." Lakini, baada ya jua kuzama Ibrahim aliwaambia wale waliokuwa wakiabudu vitu vyaa angani:

"Enyi watu wangu! Ni ujingga kuabudu hizi nyota ambazo hazina uwezo wa kuamua wakati gani wa kuchomoza na wakati gani wa kuzama na havina uwezo wa kufanya chochote. Hakika, mimi siabudu wala kuwaheshimu miungu yenu. Ninamuamini Allah mmoja na wa pekee, Mola wa walimwengu aliyewumba mbingu na ardhi."

Watu waliokuwa karibu naye wakajibu "Ewe Ibrahim, wafanya nini? Ukitsema hivyo utapooza. Miungu yetu itachukia na kukudhuru. Hasira zao zitakuangukia na utajuta kwa ulichosema."

Ibrahim akawajibu, "Hamumuamini Allah mwenye nguvu na uwezo juu ya kila kitu na aliyewumba ulimwengu wote. Kadhalika, mnnavifanya kuwa miungu yenu viumbi visiviyokuwa na uwezo na haviwezi kunufaisha. Mnawafanya kuwa washirika wa Allah. Hamna khofu kwamba mtawajibishwa kwa hatua hii batili! Pamoja na hayo yote, hivi mnadhani kuwa nitawaogopa hao miungu wenu wa uongo? Acheni imani hiyo potofu. Muaminini Allah, Mola wa kweli aliyewumba mbingu na ardhi, aliyepamba mbingu kwa nyota, mwezi na jua. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu sawa sawa Kwake aliyezumba mbingu na ardhi, wala mimi si mionganini mwa washirikina."

(Tazama Surah An'am, 6: 74-79 kwa maelezo juu ya kisa hiki)

## KILA KAZI YA USANIFU NI ISHARA YA MSANIFU

Kila kazi ya usanifu ambayo huyafurahisha macho yetu na kuonekana kuwa nzuri lazima kuna aliyeifanya, aliyeisanifu; kama fundi seremala anayetengeneza kiti kwa ajili ya makazi au shule, au kama ilivyo kwa mtunzi wa kitabu tunachokisoma. Nyuma ya kila matukio tunayoyashuhudia ulimwenguni, kuna Muumba Mwneye Uwezo na Nguvu. Haiwezekani kuwaza kuwa mfumo kamili wa ulimwengu ulitokea kwa sadfa au bahati. Tunaweza kulifafanua hili kwa mfano ufuatao:

Umekwenda kwenye ufukwe bahari siku yenye joto. Bahari ya bluu iko mbele yako, imetulia na ni safi mno. Unapotembea ufukweni, unakutana na kasri zuri lilitengenezwa kwa mchanga. Unatazama katika eneo hilo huoni mtu yeyote. Unashangaa na kustaajabu iwapo kuna mtu anayeweza kuwa amelitengeneza kasri hilo.

Unaweza kuwa na dhana mbili kuhusu uwepo wa kasri hilo la mchanga:

Dhana ya kwanza: Kasri hili lilitengwa kwa kuweka juhudhi na ufundi. Kwamba mtu mwenye kipaji na uzoefu wa kutengeneza makasri ya mchanga ndiye anayeweza kulifanya hilo. Dhana ya pili: Kasri hili lilitokea kutohana na mawimbi yaliyopiga ufukweni. Kwamba mawimbi yaliyopiga ufukweni, mchanga ulijikusanya na ghafla kasri hili zuri likatoka kwa sadfa.

Ni dhana ipi katika hiso inayoingia akilini na unayoikubali?

Kasri hapo pichani  
limetengenezwa na mtu mwenye



kipaji cha makasri ya mchanga kwa kufanya kazi kwa saa kadhaa. Mpaka leo hakuna aliywahi kuona au kusikia kuwa mawimbi yanaweza kusababisha kutokea kwa kasri la mchanga kwa sadfa. Kasri hili litavunjwa na upopo mkali au wimbi dogo. Elimu, uzoefu na juhudhi ni mambo muhimu hata kwa kasri hili rahisi la mchanga.

Sasa tuutazame msikiti unaoonekana katika picha.



Masjid Suleymaniye, unaopatikana katika moja ya vilima katika mji wa Istanbul nchini Uturuki na kuwa pembezoni mwa bahari, ulijengwa na msanifu mkubwa wa majengo, Sinan. Jengo hilo linachukuliwa kuwa miongoni mwa kazi kubwa kabisa za kiuhandisi na usanifu duniani, kwa muundo wake wa ndani na nje. Humvutia kila mtu kwa minara yake mirefu, yenye kuvutia, quba kubwa na muonekano adhimu. Ubora wa vifaa viliviyotumika katika ujenzi na nguvu kazi, umaridadi katika maeneo mbalimbali, na uwiano wa mazingira yake humvutia kila mtu. Haiwezekani kuwaza au kudai kuwa kazi hiyo nzuri inaweza kutokea bila msanifu na mhanidisi yeyote kuitengeneza.

Kama ni hivyo basi, yawezekanaje kwa mbingu inayotufunika kama quba, dunia tunayoishi, watu wanatuzunguka, wanyama, mimea, milima, viumbi hai na samaki wanaoishi katika vina vya bahari, jua, sayari na nyota kubwa zinazoipamba anga ya nje, na viumbi vingine vingi tusivyovijua na tusivyoviona view vimetokea kwa sadfa? Nani



aliyeyafanya yote hayo kwa mpango bora, usanifu maridhawa, nguvu, ujuzi na adhama kuu?

Njia pekee tunayoweza kujibu swalii hili ni: kuna muumba wa ulimwengu na kila kitu kilichomo kuanzia kwenye atomu ndogo kabisa mpaka kwenye nyota kubwa kabisa. Muumba huyu ni Allah Mtukufu Mwenye Nguvu na Uwezo juu ya kila kitu.





## ALLAH

Unasoma kutabu, na  
Unataka kujua nani aliye kitunga.  
Unapoona jengo zuri,  
Unamtafuta aliye lijenga.

Je hakuna anayezimiliki mbingu na ardhi?  
Utawenza kuelewa ukitafakari.  
Kila kitu kinatuthibitishia kuwa,  
Yupo Allah Mwenye nguvu na Uwezo.

Ni wajibu wetu kuuliza na kujua  
Yule aliye tumba.  
Ni wajibu wetu lakini  
Dini ndiyo itakayotufundisha hayo.

**İbrahim Alaattin GÖVSA**

## JIBU LA ABU HANIFA

Imam Abu Hanifa, miongoni mwa wanazuoni wakubwa wa Uislamu, alikuwa akiishi mji Baghdad. Aliwalea wanafunzi wengi na kuaminiwa na kuheshimiwa na kila mtu.

Wakati huo kulikuwa na msomi mwengine ambaye alikanusha uwepo wa Allah na alikuwa akijadiliana na wasomi wengine aliokutana nao katika safari zake.



Msomi huyu kafiri alisikia kuhusu umaarufu na umashuhuri wa Abu Hanifa. Alisafiri mpaka Baghdad kwa lengo la kujadili naye masuala hayo. Alipokutana naye alianza kufanya mjadala. Lakini Abu Hanifa hakujibu mara moja hoja yake. Alimuomba wakutane kesho mahali palepale. Hapo ndipo angempatia jibu.

Siku iliyofuata, Abu Hanifa hakuonekana kwenye mkutano kama alivyoahidi.  
Msomi yule kafiri hakulipenda hilo. Alipokaribia kuondoka, Abu Hanifa akatokea.

Msomi yule  
akamwambia Abu  
Hanifa:

— Kwa nini  
umechelewa? Ulikuwa  
ukiogopa kujadiliana nami?

Abu Hanifa akajibu:

— Hapana, sikuogopa. Unajua kwamba mto Tigris unazigawa pande mbili za Baghdad, nami ninaishi upande wa pili wa mto. Usiku upepo ulivuma na kulipeperusha daraja. Nikataku kujenga daraja jipya bila seremala au mhandisi. Niliiamuru miti na mawe kunijengea daraja. Nikasema: "Miti na mawe! Njooni haraka mnitengenezee daraja." Nilichotaka kilitokea lakini ilichukua muda mrefu kinyume na matarajio yangu. Nilivuka na kuja hapa, japokuwa nimechelewa. Sasa niko hapa."

Msomi huyo akacheka na kuuliza:

— Enyi watu! Huyo ndiye mtu mwerevu zaidi kati yenu? Je yawezekana kujenga daraja bila fundi na mhandisi? Je, si ujinga kuamini hivyo?



Abu Hanifa akatoa hoja yake:

— Ewe usiye na busara! Kwa kuwa wadai kuwa daraja haliwezi kujijenga lenyewe, unawezaje kudai kuwa ulimwengu huu mkubwa unaweza kutokea wenyewe?!

Msomi yule hakuwa na la kujibu zaidi ya kusema: "Hili suala limekwisha. Sasa nioneshe Allah nami nimuamini."

Abu Hanifa akachukua glasi ya maziwa na kuuliza:

— Niambie siagi inatokana na nini?

— Hakika hutokana na maziwa.

— Sasa, waweza kunionesha hayo mafuta katika maziwa haya?

— Ni kweli katika maziwa haya kuna mafuta, lakini hayaweki kuonekana. Kwa sababu yamemezwa ndani ya maziwa, hayo katika eneo maalumu.

— Unaamini kwamba mafuta katika maziwa haya hayaweki kuonekana. Kwa hoja hiyo hiyo, kwa nini huamini kuwa Allah Muumba yupo lakini haweki kuonekana?


Kwa maneno hayo, msomi yule akatambua kosa lake. alikiri kwamba kuna Muumba wa ulimwengu huu lakini haiwezekani kuonekana. Aliomba msamaha, akaachana na madai yake ya mwanzo. Alikiri na kutambua uwepo na umoja wa Allah.

## MPANGILIO KAMILI KATIKA ULIMWENGU WA NDANI NA NJE

Uwepo na umoja wa Allah ni ukweli usiopingika. Tukijichunguza sisi wenyewe na huu ulimwengu kwa umakini inatosha kutambua uwepo, umoja na ukuu wa Allah.



Katika mwili wa mwanadamu, ambao unaanza na seli moja, kuna takribani seli triliuni 100. Katika kila kiini cha seli, kuna molekuli moja ya DNA. Kila taarifa kuhusu sifa za mwili wa mwanadamu zinatunzwa katika molekulu za vinasaba hivi. Katika seli ya mwanadamu, kuna vinasaba vipatavyo bilioni 3. Kwa maneno mengine, kuna taarifa zilizofichika katika mada bilioni 3 katika DNA ya kila seli. Taarifa zote kutuhusu kuanzaia kwenye rangi ya ngozi mpaka kwenye rangi ya macho na maradhi ya vinasaba vyetu hutunzwa katika DNA zetu na kupelekwa kwenye vizazi vijavyo kupitia DNA zetu.



### Allah Mtukufu anasema:

"Sema: Yeye ndiye aliye kuumbeni tangu mwanzo, na akakupeni masikio na macho, na nyoyo. Ni kidogo kabisa shukrani zenu."

(al-Mulk, 67:23)

Utendaji kazi usiokuwa na idadi katika miili yetu, kama vile mapigo yetu ya moyo hutokea bila sisi kuwa na udhibiti na hiari yoyote. Hata hivyo, kuna nidhamu kamili katika mifumo yote tuliyonayo.

Kila tunachokifanya, kufikiri, kusema na kuhisi, hutokea katika ubongo wetu. Mawasiliano yanayowezesha hili katika ubongo wetu huundwa na niuroni zilizo katika ubongo wetu. Katika ubongo wa mwanadamu, kuna niuroni zipatazo milioni 100, au kwa maneno mengine seli za neva. Ili ufkiri, uone, na uhisi, mawasiliano kati ya seli hizi ni lazima. Niuroni bilioni 100 katika ubongo wetu huwasiliana kupitia viunganishi triliuni 100 vya mawasiliano.

Unaposoma misitari hii, mabilioni ya michakato inatokea ndani ya macho yetu. Miale ya mwanga inayoyafikia macho yetu huanza kwenda kwenye konea, kisha kwenye kiini, na kisha kwenye lenzi. Hapa seli za kubaini mwanga huibadilisha miale ya mwanga kwenda kwenye ishara za kumeme na kuzituma kwenye vimalizikio vya neva kama taarifa. Ubongo huyaunganisha maoni yanayotoka kwenye macho yote mawili na kuwa uoni mmoja. Hutambua umbile na



rangi ya kitu husika. mchakato wote huu hufanya ndani ya muda wa kumi ya sekunde.

Asilimia 75 ya ardhi na karibu asilimia 70 ya mwili wa mwanadamu ni maji. Maji yanaweza kwenda katika kila seli ya mwili wa mwanadamu na yanaweza kusafiri ndani ya kila mshipa ulio ndani mwetu. Hubeba vurutubisho kupeleka kwa kila seli kati ya seli trilioni 100 zilizo katika mwili wa mwanadamu na kuzipatia oksijeni na nishati. Maji ni neema isiyokuwa na kifani kwa uhai wetu.

Matunda na mbogamboga yanayotokana na ardhi ileile na kumwagiliwa maji yaleyale yana utofauti wa ajabu.

Ladha na harufu tofauti ya matunda na mbogamboga zinazopata msaada wa ardhi, maji, na madini, zimeendelea kuwepo mpaka leo bila kubadilika au kuchanganyika.

Kila taarifa kuhusu mmea fulani zimehifadhiwa katika mbegu ndogo inayouzalisha mmea huo. Mbegu zinakuwa na taarifa zote kuhusu mimea yao kama vile muundo wa majani na matawi, rangi, ukubwa, ladha, harufu na muundo wa matunda yake. Ili kiumbe hai kiweze kuishi katika ulimwengu huu, kinahitaji vitu vingi kama vile umbali kutoka kwenye juu, hali joto baina ya viwango fulani, kaboni, ozone, na mzunguko wa maji, madini ambayo huletwa na vidubini, usanidinuru, mteremko wa ardhi, nguvu ya uvutano, nguvu inayofanya viini vya atomu viendelee

### Allah Mtukufu anasema:

"Tutawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenye..."

(Fussilat, 41: 53)

kuwa pamoja, na mambo mengine mengi. Ardhi tunayoishi imeumbwa katika namna inayohakikisha vitu vyote hivyo vinakuwepo na imehifadhiwa katika namna maalumu.

Inaaminika kuwa makundi bilioni 300 ya nyota kubwa katika ulimwengu. Kundi la Milky Way ni kundi moja tu. Jua, ambalo lina ukubwa mara 103 ya dunia ni moja kati ya nyota bilioni 250 katika kundi la Milky Way. Umbali kati ya Jua na sayari ya dunia ni kilometra millioni 150. Sayari zote angani huzunguka kwenye mhimili maalumu katika mfumo huu.



### Allah Mtukufu anasema:

"Ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji."

(Al-Muuminun, 23: 14)

## JIBU MOJA KWA MASWALI MATATU

Hapo zamani alikuwepo mtu mmoja ambaye hakumuamini Allah. Alikuwa akimwambia kila mtoto aliyeutana naye kuwa amebaini kuwa Allah hayupo, kwa

sababu kama angekuwepo angemuona. Kafiri huyu alikuwa na jirani mzuri sana aitwaye Yunus. Yunus alimuamini Allah, akaswali na kamwe hakusema uongo.



Alikuwa akiishi vizuri na kila mtu. Alikuwa akiwakusanya watoto na kuwa uliza: "Nani alyewaumba?" Kama hawajui jibu, alikuwa akiwafundisha kusema: "Allah ndiye aliye kuumba mwanangu!"

Siku moja, yule kafiri alikuja kwa Yunus na kumuuliza akidhani kuwa hataweza kujibu maswali yake: "Nitakuuliza maswali matatu kuhusu dini na imani. Ngoja tuone kama utaweza kuyajibu". Yunus akajibu kwa ujasiri na kujiamini kutokana na imani aliyo kuwa nayo:

— Uliza tuone. Aliiambia nafsi yake "Uliza utapata jibu lako!"

— Swalil langu la kwanza: Unadai kwamba Allah yupo. Kama Allah angeku wépo tungemuona. Kwa kuwa hatumuoni, hayupo. Kama yupo basi nioneshe! Swalil langu la pili: Anasema kuwa Shetani ataadhibiwa kwa moto, lakini mnaamini kwamba Shetani aliumbwaa kwa moto. Inawezekanaje moto uunguze moto? Swalil langu la tatu: Kwa kuwa kheri na shari hutoka kwa Allah, kwa nini aniadhibu kwa kutomuamini?

Yunus alimsikiliza kwa makini, akasema: "Hili hapa jibu la maswali yote matatu", akachukua jiwe na kumpiga kichwani.

Mtu yule akamshitaki Yunus mahakamani. Walipofika mahakamani, hakimu akamuuliza Yunus:

— Ulimpiga jiwe mtu huyu kichwani? Yunus akajibu:

— Ndiye mheshimiwa. Lakini nilifanya hivyo ili kumjibu maswali yake matatu aliyo ni uliza. Akaanza kueleza kilichotokea.

Kwanza, aliniambia kuwa hamuamini Allah kwa sababu hawezu kumuona. Alitaka nimuoneshe ili aamini kuwa yupo. Nikampiga kichwani, na sasa anadai kuwa kichwa chake kina maumivu, nataka anioneshe hayo maumivu, vinginevyo siwezi kumuamini. Kwa kuwa anakataa vitu ambavyo havioni, nami ninayakataa maumivu yake.

Pili, aliniuliza inawezekanaje Shetani achomwe moto wakati aliumbwaa kwa moto. Mtu huyu ameumbwa kwa udongo. Kwa kuwa moto hauwezi kuunguza moto, dongo nililompiga haliwezi kumuumiza.

Tatu, alidai kuwa yeye kuwa kafiri ndio majaliwa yake. Aliniambia kuwa haiingii akilini kwake kuadhibiwa kwa sababu ya hilo. Inaonekana pia kuwa ilikuwa majaliwa kupigwa na dongo kichwani mwake. Kwa nini anampotezea muda hakimu kwa mashitaka haya?




Hapo, hakimu akamuuliza yule kafiri:

- Unasemaje kuhusu hili?

Mtu yule aliona aibuu kwa alichokisema mwanzo na kutambua kosa lake:

— Mheshimiwa hakimu! Yunus amesema kweli, na yuko sahihi. Sina malalamiko tena na ninataka kuwa Muislamu. Tafadhalii muache anisaidie.

Yunus na jirani yake waliondoka mahakamani pamoja na kuwa marafiki wazuri sana.



## TUNAMTAMBUA ALLAH MTUKUFU KUPITIA SIFA ZAKE

Viungo vyetu vya hisia vinavyotusaidia kuelewa mambo vina kikomo. Kwa sababu hii, hatutaweza kuona na kusikia kila kitu.

Kwa mfano, hatuwezi kuona vijidudu na virusi pembezoni mwetu, hatuwezi kusikia sauti ya chini kama ile ya nyayo za sisimizi au sauti ya juu kama vile sauti ya mzunguko wa dunia kwenye mhimili wake.

Kama ilivyo kwa viungo vyetu vya hisia, uwezo wa akili zetu pia una kikomo. Miongoni mwa maeneo ambayo akili zetu zina ukomo ni Dhati ya Tabia za Allah.

Tunaweza kufikia hitimisho kuhusu uwepo wa Allah na umaja Wake kwa kutumia akili zetu na kutazama ushuhuda mbalimbali unaopatikana katika ulimwengu. Hata hivyo, hatuwezi kutengeneza wazo kuhusu Dhati Yake. Tunaweza kumtambua Allah na kumuamini katika njia aliyoturuhusu, kupitia sifa zake.

### Allah Mtukufu anasema:

"Macho hayamfikili bali Yeye anayafikilia macho..."

(al-An'am, 6: 103)

### Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Kila kinachokujua akilini mwako kuhusu dhati ya Allah, basi huyo siye. Fikiria kuhusu alivyoviumba Allah, usifikirie kuhusu dhati ya Allah. Hilo liko nje ya uelewa wetu."

(Haithami, Majma al-Zawa'id, I, 81)



Mola wetu Mtukufu amezitaja sifa Zake ndani ya Qur'an Tukufu ili tupate kumtambua vyema. Ili tumtambue Allah na kumuamini ipasavyo, yatupasa kuzijua sifa hizi.

Tunaweza kuzichunguza sifa za Allah katika makundi mawili, zinazohusu dhati Yake, uumbaji wa ufalme Wake na hukmu Zake:

### SIFA ZA ALLAH


Sifa asili za Allah

Sifa thabiti za Allah

#### I) Sifa za asili za Allah (AL-SIFAT AL-DHATIYYAH)

Ni sifa za Allah makhsusi Kwake tu. Sifa hizo ni sita:

#### Sifa za asili za Allah



##### Uwepo (Al-Wujuud)

Yeye ni mwenye kuwepo

##### Utangu (Al-Qidam)

Uwepo wake hauna mwanzo.  
Yeye ni wa tangu na tangu.

##### Kubaki (Al-Baqaa)

Uwepo wake hauna mwisho.  
Yeye ni wa milele.

##### Umoja (Al-Wahdaniyyah)

Yeye ni mmoja na wa pekee.

##### Kutofanana na chochote

(Al-Mukhalafatun lil Khawadith)  
kutofanana na viumbi.

##### Kujitosheleza (Al-Qiyam bi'nafsihi)

Allah hamtegemei ye yeyote ao chocte katika uwepo  
Wake. ni Mwenye kujitosheleza.

**1. Uwepo:** Allah yupi. Kutokuwepo ni jambo lisilowezekana Kwake.

**2. Wa tangu na tangu;** Allah ni wa tangu na tangu; uwepo Wake hauna mwanzo. Hakuna mwanzo wa kufikirika ambao Allah hakuwepo.

**3. Wa milele;** Allah ni wa milele; uwepo wake hauna kikomo. Umbali wowote wa baadaye ambao mtu anaweza kuufikiria, hauwezi kufika muda ambao Allah hatokuwepo.

**4. Umoja;** Allah ni mmoja na wa pekee. Hakuna mwingine au kitu kingine chenyé sifa Zake.

**5. Kutofanana na yejote au chochote;**  
Allah hafanani na kiumbe chochote. Ametakasika dhidi ya umbo lolote au mawazo yoyote ambayo mwanadamu anaweza kuyawazia.

**6. Kujitosheleza;** Allah haitajii kitu kingine. Hakuna aliyemuumba Allah. Ni mwenye kujitoesheleza katika uwepo Wake.

#### Allah Mtukufu anasema:

"Enyi watu! Nyinyi ndio wenyé haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha, Msifiwa."

(Faatir, 35: 15)

#### Allah Mtukufu anasema:

"Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana naye hata mmoja. "

(Al-Ikhlas, 112: 1-4)



## BINTI WA MUUZA MAZIWA

Umar (r.a) alipiga marufuku kitendo cha kuongeza maji kwenye maziwa. Usiku mmoja, wakati akitembea katika mji wa Madina kwa ajili ya kuangalia utekelezaji wa sheria na nidhamu, alichoka. Aliegermea kwenye ukuta wa nyumba moja ili kupumzika. Kwa bahati alisikia mazungumzo kati ya mama na binti yake:

Mama:

— Mwanangu kaongeze maji kwenye maziwa.

Binti:

— Mama! Khalifa hajakataza kufanya hivyo?

— Mwanangu! Usiku huu atatuonaje?

— Mamangu! Hata kama Khalifa hawezi kutuona, Allah hawezi kutuona?

Umar (r.a) aliondoka taratibu baada ya kusikiliza kilichoendelea. Baada ya juu kuchomoza, aliwatuma ndugu kwenda kumchumbia binti yule. Mmoja wa mabinti kutohana na ndoa hii alipata mtoto aitwaye Abdulaziz. Mtoto huyo ni Umar ibn Abdulaziz ambaye anajulikana pia kama "Umar wa pili" katika historia ya Kiislamu. Kama alivyokuwa babu yake Umar (r.a), wakati wa utawala wa Umar ibn Abdulaziz, ambaye alijulikana kwa uadilifu wake, watu wake waliishi kwa furaha na amani.



## II) SIFA THABITI ZA ALLAH (AL-SIFAT AL-THUBUTIYYAH)

Hizi ni sifa kamilifu za Allah zisizokwa na kikomo. Sifa hizi hutusaidia kutambua vyema namna Allah alivyouumba ulimwengu na anavyoudhibiti.

### SIFA THABITI ZA ALLAH

#### Uhai (Al-Hayat)

Allah yu hai na ndiye chanzo cha uhai wote.

#### Ujuzi (Al-Ilm)

Allah ana ujuzi usiokuwa na kikomo.

#### Msikivu (Al-Samî)

Allah ni msikivu wa kila kitu.

#### Mwenye kuona (Al-Baseer)

Allah ni Mwenye kuona kila kitu.

#### Utashi (Iraadah).

Allah ni mwenye utashi na hufanya apendavyo.

#### Uwezo (Al-Qudrah)

Allah ni mwenye nguvu na uwezo usiokuwa na kikomo.

#### Mwenye kuzungumza (Al-Kalam)

Allah ni mwenye kuzungumza

#### Uumbaji (Al-Takwin)

Allah huumba kila kitu kutoka katika hali ya kutokuwa chochote.

**1. Uhai:** Allah yu hai daima. Uhai Wake hauna mwanzo wala mwisho. Tofauti na uhai wa viumbe, uhai Wake hautegemei muda, sehemu wala umbo. Huvipa uhai viumbe vyote, na kila kitu hupata uhai kupitia Kwake.

**2. Ujuzi:** Allah Mtukufu anajua kila kitu Mbinguni na Ardhini. Hakuna asichokijua. Anazijua Mbingu, Ardhi na kila kilichopo baina yake, kanuni zote za ulimwengu, na kila kinachotokea. Anayajua mabilioni ya nyota zilizoko ulimwenguni, anajua kila kitu, na anajua siri ambazo watu huzificha kwa sababu yeye ndiye Muumba wetu sote. Aidha, ujuzi wa Allah hauna mpaka. Nidhamu, mfumo na mizani inayoonekana ulimwenguni ni ushuhudatosha wa ujuzi wa Allah usio na kikomo.


**3. Msikivu:** Allah ni mwenye kusikia kila kitu. Ametakasika na dhana ya ukaribu au umbali katika usikivu Wake. Anasikia na kuelewa yote yanayosemwa na kila kitu katika ulimwengu nyakati zote. Husikia dua na maombi ya dhahiri na batili. Allah ametakasika na zana au kiungo cha kusikia. Uwezo Wake wa kusikia hauna kikomo. Kusikia Kwake kitu fulani hakumzui kusikia kitu kingine.

**4. Mwenye kuona:** Allah ni mwenye kuona kila kitu. Hajjalishi iwapo kitu husika kiko mbali au karibu, kidogo au kikubwa. Anaona tulipo na tunachokifanya. Hahitajii jicho kama sisi.

**5. Utashi:** Kila kitu hutokea kwa utashi wa Allah Mtukufu. Hakuna kinachoweza kufanyika bila utashi na amri Yake. Kuna hekma katika kila anachokitaka na kukifanya. Kila alichokiumba kina sababu na hekma ndani yake. Hakuna nguvu inayoweza kuzuia utashi wake au amri Yake.

**6. Uwezo:** Allah ni mwenye nguvu na uwezo usiokuwa na kikomo. Hakuna asichoweza kufanya. Hakuna kinachomzia kufanya

Allah Mtukufu anasema:



“...Na Yeye anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila analiju...”

(al-An'am, 6: 59)

Allah Mtukufu anasema:

“Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia Mwenye kuona.”

(Al-Muumin, 40:20)

Allah Mtukufu anasema:

“Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.”

( Ya-Sin; 36:82)

ependavyo. Tukiungalia ulimwengu na maajabu yaliyo ndani yake inatosha kuelewa ukoo wa uwezo wa Allah usiokuwa na mipaka wala kikomo. Mzunguko wa nyota na sayari ambazo zina uzito wa mamilioni ya tani na uumbwaji wa mwanadamu kutohana na seli moja ni mifano tu ya uwezo wa Allah.

**7. Kuzungumza:** Allah Mtukufu ana uwezo wa kuzungumza bila kuhitaji viungo na harakati za kimwili tunazozihitajia sisi binadamu ili kuzungumza. Maneno yake hayawezi kulinganishwa na maneno ya binadamu. Mola wetu Mtukufu huzungumza na kila kiumbe kwa lugha ambayo kiumbe hicho kinaweza kuielewa. Kwa kuziamuru mbingu na ardhi, na viumbe vyote vidogo au vikubwa hutangaza maneno Yake. Alizungumza na mitume kupitia vitabu vitukufu alivyoviteremsha na kupitia mitume akazungumza na binadamu wote. Qur'an Tukufu na vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbinguni alivyoviteremsha kwa wanadamu wote ni maneno Yake.

**8. Kuumba:** Allah ndiye Muumba wa ulimwengu na kila kilichomo ndani ya ulimwengu. Allah aliumba kila kitu kuanzia viumbe hai vinavyoweza kuonekana kwa darubini mpaka nyota kubwa ambavyo ni vikubwa kwa maelfu ya mara zaidi ya dunia. Yeye ndiye Muumba, mwenye kutoa uhai, Mwenye kuruzuku, Mwenye kufanya kukipa uhai kila kitu. Yeye ndiye Muumba pekee, hakuna mwininge.

Uumbaji ni sifa ya Allah Mtukufu peke Yake. Huumba kila kitu kutoka katika hali ya kutokuwepo. Zana za kiteknolojia na uvumbuzi unaofanywa na viumbe wa Allah, vyoyote vile utakavyokuwa, ni utengenezaji wa vitu ambavyo tayari vipo.



Allah Mtukufu anasema:

"Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mtengenezaji, Mtia sura."

(Surah Al-Hashr (Exile, Banishment); 59:24)

## ALLAH ANAONA KILA KITU

Baba aliwakusanya wanaye na kumpa kila mmoja pete ya thamani. Aliwataka wazifiche sehemu, ili asiwepo wa kuziona na wazitumie baada ya ye ye kufariki dunia. Baada ya kuzichukua pete hizo, walitafuta sehemu ya kuzificha. Watoto wawili walizificha katika mizigo yao kwa umakini na kurudi kwa baba yao. Walimsubiri ndugu yao wa tatu. Baada ya muda mrefu kupita, mtoto huyo hakurudi. Jioni ililingia na baada ya kuanza kuwa na wasiwasi juu ya ndugu yao, alitokea akiwa na pete mkononi. Waliona kuwa amechukua muda mrefu kuficha kitu kidogo kama pete, wakamtania:

— Ndugu yetu ulitazama kila sehemu lakini hukuweza kupata sehemu ya kuficha pete. Wakati huo huo walikuwa wakijidai kuwa kwa muda mfupi wamefanya kile walichoagizwa na baba yao.

Baada ya kuwatazama kwa makini watoto zake watatu, baba alimwambia yule ambaye hakuweza kupata sehemu ya kuficha pete:

— Mwanangu! Tazama, wenzako wameweza kuficha pete zao. Kwa nini umerudi na pete yako?

— Baba! Si ulitutaka tufiche pete sehemu ambayo hakuna atakayeweza kuziona?

— Ndiyo.

— Baba, nilitazama kila mahali, lakini sikuweza kuipata hiyo sehemu. Kwa sababu kila nilipokwenda nilibaini kuwa Allah Mtukufu ananiona. Ndiyo maana nimeirejesha hii pete.

Baba alifurahishwa na maneno ya mwanaye, akasema:

— Vizuri sana mwanangu! Kwa mtihani huu mdogo nilitaka kuwakumbusha kuwa Allah anatuona kila mahali na kila wakati.



# MOLA WANGU! NIMEKUTAMBUA NA KUKUAMINI KWA MOYO WANGU WOTE

**Mola wangu!** Wewe ni Mwenye kuwepo. Uwepo Wako hauhitajii chochote. Wewe ndiwe uliyetumba na kutuhabarisha kuhusu uwepo Wako. Kila kipo kwa sababu Yako. Wewe ndiwe uliyetumba vitu vyote na kuvipatia uhai. Ukitaka, waweza kuviangamiza vyote.

**Mola wangu!** Huna mwanzo wala mwisho. Wewe ni wa mwanzo na wa mwisho. Wewe ndiwe uliyetumba zama na utaendelea kuwepo baada ya zama. Wewe pekee ndiwe usiyekuwa na ukomo. Vingine vyote ni vyenye kupita. Kila chenye kuzaliwa kitakufa na kila kitu kitaangamia na kutoweka. Wewe pekee ndiwe wa milele.

**Mola wangu!** Wewe ni Mmoja na wa pekee. Huna mshirika na hakuna kinachofanana Nawe. Nguvu na uwezo wote ni Wako. Wewe ndiwe uliyetumba kila kitu na Mwenye kudhibiti kila kitu. Mfumo huu kamili na uwiano unaendelea ulimwenguni ni kazi Yako; na ni ushuhuda kuwa hakuna mungu ila Wewe.

**Mola wangu!** Hatuwezi kuijua dhati Yako. Tunachoja ni kwamba uko tofauti na yote tunayoyajua. Umetakasika na kila chenye kufikirika. Uwepo Wako unatokana na Wewe. Umetakasika dhidi ya kufanana na chochote, huna mfanano na umetakasika. Wewe ndiwe Mola wetu na tunakuamini.

**Mola wangu!** Wewe ndiwe unayetaka kitu na kukiumba kutoka katika hali ya kutokuwepo. Kila kitu huwepo kwa sababu unataka kiwepo. Kuna hekma katika kila unalofanya. Wewe ni Mwenye nguvu na Mkuu. Hakuna anayweza kupinga au kubadili uamuzi wako.



## KWA JINA LA ALLAH

Allah ni neno letu la kwanza,  
Msingi wetu umejazwa imani.  
Kila kazi inayoanza kwa jina la Allah,  
Humalizika kwa furaha,  
Tunapoamka asubuhi,  
Husema "BISMILLAH (kwa jina la Allah)."   
Tunapokula au kunywa,  
Ninapofungua kitabu changu...  
Daima husoma Basmalah (Bismillah)  
Kamwe sisahau, hata mara moja.  
Humuelekea Mola wangu,  
Nguvu hunijia moyoni mwangu.  
Kwa kuwa pamoja na Allah, ehata kidogo  
huwa kingi,  
Tabu na ugumu huondoka,  
Mwenye kusoma Basmalah,  
Huwa sambamba na mafanikio.  
Kamwe siachi kuisoma, na  
Allah hunisaidia.

**M. Asim KÖKSAL**

**Mola wangu!** Wewe ndiwe usemaye maneno ya kweli kabisa kuliko maneno yote. Wewe ndiwe uliyetuletea maneno na vitabu Vyako kwetu kama rehma kwa waja Wako. Lau kama miti yote ikiwa kalamu na bahari zote zikawa wino, haziwezi kutosha kuandika maneno Yako.

**Mola wangu!** Wewe ndiwe Mwenye kuumba kutoka katika hali ya kutokuwa chochote na unayweza kukiangamiza kila chenye kuwepo. Unaviumba vitu vyote kwa uwiano maalumu na kuvidhibiti kwa uwezo Wako Mkuu.



Ewe Mola wangu! Zitakase nyoyo zetu dhidi ya mawazo yasiyolingana na Ukuu

Wako! Tufanye tuishi na kufa hali ya kuwa tukiwa Waislamu!

Usitupatilize kwa sababu ya dhambi na makosa yetu!

Tusamehe dhambi zetu za siri na za wazi

Tujaalie msaada wako katika utoshelevu na ufakir!

Wewe ndiwe ujuwaye mahitaji yetu na kuyasikia maombi yetu. Zikubali dua zetu!

Amin




# KIJANA MWENYE IMANI

Siku moja Mjumbe wa Allah (s.w) alilaambia Maswahaba zake kisa kifuatacho:

Katika umma zilizopita, alikuwepo mfalme na mchawi wake. Mchawi alipozeeka alimwambia mfalme:

— Sasa nimezeeka. Niletee kijana nimfundishe uchawi wangu.

Kutokana na ombi hilo, mfalme alimpelekea kijana mmoja. Kijana huyo alipokuwa njiani kuelekea kwa mchawi huyo, alikutana na mchamungu mmoja jangwani.



Mchamungu huyo aliyejkuwa na imani ya Mungu mmoja, alikuwa amempinga mfalme aliyejai kuwa yeye ni Mungu. Mchamungu huyo alikuwa amejificha eneo hilo dhidi ya mateso ya mfalme na askari wake.

Kijana yule alifanya mazoea ya kumtembelea mchamungu hyu kila alipokuwa njiani kuelekea kwa mchawi. Alipenda maneno aliyojkuwa akiambiwa na mchamungu. Alikuwa akiona tabu kuondoka na wakati mwininge alikuwa akichelewa kwenda kukutana na mchawi. Kila alipokuwa akichelewa, mchawi alikuwa akitasirika na kumpiga.

Siku moja kijana aliona mnyama mkubwa wa hatari aliyejkuwa akiwashambulia wapitaji. Alijisemea moyoni "Sasa nitajua nani mwenye nguvu, mchamungu au mchawi", akachukua jiwe na kumtupia mnyama yule huku akisema: "Ewe Allah! Kama unaona kile kinachofanywa na mchamungu kuwa ni bora kuliko kinachofanywa na mchawi, basi muue mnyama huyu ili watu waweze kuendelea na safari yao." Mnyama yule akafa na watu wakaendelea na safari yao. Yule kijana akawmambia mchamungu yule kilichotokea.

Mchamungu akasema:

- Ewe kijana! Ninaona kuwa umefikia daraja kubwa. Ninahisi baada ya muda mfupi utapata shida. Yakitokea hayo, usimwambie yejote mahali nilipo.

Kijana yule alikuwa akiwaponya vipofu, mabarango na maradhi mengine pia. Wakati huo mfalme alikuwa akimjua mtu mmoja ambaye alikuwa kipofu. Mtu huyo alisikia habari hizo akaenda kwa yule kijana akiwa na zawadi nyinyi za thamani na kumwambia:

— Ukiyaponya macho yangu, zawadi zote hizi zitakuwa zako.

Kijana akasema:

— Sina uwezo wa kuponya mimi mwenyewe. Allah Mtukufu pekee ndiye mponyaji. Ukimuamini Allah nitamuomba akuponye, naye atakuponya.

Kipofu akamuamini Allah Mtukufu. Allah alimponya, akarudi kwa mfalme akiwa mzima, akampatia kiti katika baraza lake la mawaziri.

Mfalme akamuuliza:

— Nani aliyejuponya macho? Mtu yule akasema:

— Mola wangu!

Mfalme akasema kwa sauti kali:

— Una Mola tofauti na mimi?

Mtu yule akasema:

— Allah Mtukufu ndiye Mola wangu na Mola wako.

Mfalme alikasirishwa na maneno hayo na kumtia kifungoni. Walimuadhibu mpaka akawaambia mahali alipo yule kijana. Walipomtafuta kijana yule wakamleta mbele ya mfalme. Mfalme akamuuliza:

— Kijana, yaonekana uchawi wako ni wa kiwango cha juu sana kiasi kwamba unaweza hata kuponya upofu na mabarango. Nimesikia kuwa unafanya mambo mengi, je ni kweli?

Kijana akasema:

— Siwezi kuponya mimi mwenyewe. Allah Mtukufu ndiye anayeponya.

Mfalme alimuweka kifungoni akidhani kuwa elimu hiyo aliipata kutoka kwa yule mchamungu. Walimuadhibu mpaka alipowaambia alipo yule mchamungu.

Walimleta yule mchamungu na kumwambia aikufuru imani yake.

Hakukubaliana na hilo. Mfalme akatoa amri akatwe vipande viwili kwa msumeno. Kisha yule mtu wa mfalme aliletwa akaambiya: "Ikufuru imani yako!" alipokataa naye alipasuliwa vipande viwili. Kisha kijana aliletwa na kupewa vitisho mbalimbali kama vile "Ikufuru imani yako la sivyo utakufa!" akakataa. Mfalme alimkabidhi kwa askari wake na kuamuru:

— Mpelekeni mtu huyu mlimani. Akiikufuru imani yake itakuwa heri kwake, vinginevyo mtupeni kutoka juu ya mlima.

Askari walimpeleka mpaka kwenye kilele cha mlima.

Kijana yule akaomba dua akisema:

— Ewe Allah! Niokoe kutoka mikononi mwao kama upendavyo!

Kwa dua hiyo, mlima ukatikisika na askari wote wakaporomoka kutoka mlimani. Kijana yule akaweza kuokoka na kurudi kwa mfalme. Mfalme aauliza:

— Kitu gani kiliwapata askari wangu?

Kijana akajibu:

— Allah ameniokoa kutoka mikononi mwao.

Mfalme alimkabidhi kwa askari wengine na kusema:

— Mpelekeni mtu huyu katikati ya bahari. Akiikufuru imani yake muachenii, lakini akikataa mtupeni baharini.

Walimchukua kijana kama walivoagizwa na mfalme. Aliomba dua akisema:

— Mola wangu! Niokoe kutoka mikononi mwao kama upendavyo!

Mashua ilipinduka huku kila aliyejukwemo akizama isipokuwa kijana yule, akarudi kwa mfalme.

Mfalme alipomuona aauliza:

— Nini kiliwapata askari wangu?

Kijana akajibu:

— Allah aliniokoa kutoka mikononi mwao. Kisha akaendelea:

— Hutaweza kuniua mpaka utakapofanya nitakavyokwambia.

Mfalme aauliza:

— Ni mambo gani hayo?

Kijana yule akasema:

— Wakusanye watu wako katika uwanja wa wazi. Nifunge kwenye gogo la mtende, chukua mshale katika podo lako, nitupie mshale huo ukisema "kwa jina la Mola wa kijana huyu." Hapo tu ndipo utakapoweza kuniua.

Mfalme aliwakusanya watu wake katika uwanja wa wazi, akamfunga kijana yule kwenye gogo la mtende, akachukua mshale na kuuweka kwenye upinde. Akautupa akisema "kwa jina la Mola wa kijana huyu, Allah." Mshale ulimpiga kijana kwenye pajii lake. kijana yule aliweka mikono yake kwenye pajii lake na kufariki dunia hapo hapo. Hapo watu wakasema:

— Tunamuamini Mola wa kijana huyu.

Waziri yule wa mfalme akasema:

— Umeona kilichotokea? Ulichokuwa wakihofia kimetokea; watu wamemuamini Allah.

(Muslim, Zuhd, 73)

## MWENYEZI MUNGU ANA MAJINA MAZURI KABISA (AL-ASMA AL HUSNA)

Mola wetu Mtukufu amejieleza kwetu kwa majina na sifa Zake. Majina haya, ambayo Allah ametueleza ndani ya Qur'an na kufundishwa katika hadith za Mtume Muhammad (s.a.w), yanaitwa Al-Asma Al-Husna (majina mazuri kabisa). Imeamriwa katika ayah ifuatayo ndani ya Qur'an Tukufu **"Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo..."** (Surah Araf, 7:180) kwamba tunatakiwa kusoma majina Yake mazuri wakati wa kumuomba

Mtume wetu (s.a.w) alituhabarisha kuhusu majina ya Allah Mtukufu akisema:

*"Allah Mtukufu ana majina tisini na tisa. Mwenye kuyahifadhi na kuyasoma atingia Peponi"* (Bukhari, Daawat, 76; Muslim, Dhikr, 5-6)


Makusudio ya "kuhifadhi na kusoma" kulikotajwa katika kauli ya Mtume wetu (s.a.w) ni kumjua Allah kwa majina Yake mazuri na kuyadhukuru majina na sifa hizi, hivyo ataendelea kutukumbusha kuhusu Yeye.

Hutusaidia kuyatazama maisha yetu na matukio yanayotokea kwa mtazamao wa majina ya Allah. Kwa mfano, yatupasa kuwa na uwezo wa kuyakumbuka majina ya Allah ya "Rahman na Rahim" tunashuhudia rehma na huruma ya mama; au tunapopata neema nzuri, tunatakiwa kuwa na uwezo wa kukumbuka jina "Razzak"; tunapoomba msamaha wa dhambi zetu, jina "Ghafur" linapaswa kuwa akilini mwetu; kila tunapofikia majira ya Machipuo, tukumbuke jina "Muhyi," na tunapokabiliwa na mauti jina "Mumit" tunatakiwa kuyatafakari.

Tukijifunza majina haya na maana zake, na kuzirekebisha tabia zetu ipasavyo, tunaweza kuwa miongoni mwa waja wanaopendwa na Allah. Hivyo, tunaweza kustahiki kupata bishara ya Mtume wetu (s.a.w) na kuingia Peponi.

Tuikunjue mikono yetu na tumuombe Mola wetu kwa kusoma baadhi ya majina Yake mazuri...



EWE ALLAH! 	Ewe Allah uliyekusanya majina na sifa zote nzuri! 	Tunakuomba kwa Jina Lako Kuu. Zikubali swala na dua zetu!
EWE RAHMAN! EWE RAHIM! 	Ewe Allah unayeamiliana na viumbe wote kwa huruma na rehma! 	Tunakuomba rehma Zako hapa duniani na Akhera!
EWE RAZZAQ! 	Ewe Allah mwenye kuvipa uhai viumbe vyote! 	Tujaalie neema tele na baraka za halali kutoka Kwako
EWE HAFIDHI! 	Ewe Allah mwenye kukilinda na kukijali kila kitu! 	Nilinde mimi, familia yangu, na Waislamu wote dhidi ya tabu na shari zote!

EWE MUSAWWIR!		Ewe Allah uliyewumba kila kitu katika namna bora kabisa!	Zifanye uzuri tabia zangu kama ulivyoufanya muonekano wangu!
EWE MUJIB!		Ewe Allah mwenye kusikia na kupokea aina zote za dua zinazotoka kwenye nyoyo au ndimi!	Tujaalie kuwa miongoni mwa waja Wako wanaokuomba kwa ikhlasi na ambaa dua zao ni zenye kukubaliwa!
EWE HADI!		Ewe Allah mwenye kuongoa kwenye njia ya haki na mwenye kutufikisha kwenye njia ya kweli!	Usitutengenishe na njia ya kweli ya Uislamu, uaminifu na waaminifu!
EWE HAYY! EWE QAYYUM!		Ewe Allah uliyehai na chanzo cha uhai, mwenye kuudhibiti ulimwengu wote!	Tujaalie kuwa miongoni mwa wale wanatumia uhai utokao Kwako katika njia Yako. Usizifanye nyoyo zetu kushikamana na vitu vya mpito!
EWE WADUD!		Wewe ni chanzo cha upendo. Ewe ndiwe mwenye kustahiki upendo, ewe Allah!	Daima tujaalie tuwapende wale unaowapenda, tuwachukie wale unaowachukia, na tujaalie tuwapende wale waliowaongoa!

# FAIDA ZA KUMUAMINI ALLAH

## KUMUAMINI ALLAH

- Hutupatia hisia isiyokuwa na kikomo ya kujiamini.
- Hutufanya tuwe na huruma kwa viumbe wengine.
- Hutufanya tuyadhibiti matendo yetu.
- Hutufanya kuwa watu wema na waaminifu.

Kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuacha matokeo ya kila kitu Kwake ni chanzo kikubwa cha kujiamini kwa wanadamu ambao kwa asili ni viumbe dhaifu. Kila kitu kipo katika udhibiti wa Allah Mtukufu na hutokea kwa sabbu Yake. Kamwe havunji matumaini ya wale wanaomuamini. Hakuna awezaye kudhuru wala kunufaisha isipokuwa kwa idhini ya Mola wetu.

Kama waumini, hivi ndivyo tunavyomuamini Allah. **Aina hii ya imani hutupatia hisia ya imani isiyokuwa na kikomo.** Hutufanya tuyafungue macho yetu tukiwa na msisimko kila siku kwa kanuni "Allah anatutosha na Yeye ni mbora wa wenye kutegemewa." Huyafanya maisha yetu kuwa yenye amani kwa kutuepusha dhidi ya uvivu, msongo na shinikizo linalotokana na wasiwasi na shaka.

### Allah Mtukufu anasema:

"Akikunusuruni Mwenyezi Mungu hapana wa kukushindenî, na akikutupeni ni nani, basi, baada yake Yeye ataye kunusuruni? Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu."

(Al-Imran; 3:160)

Tunaamini kwamba viumbe vyote ni matokeo ya huruma na rehma ya milele ya Allah. **Imani hii hutufanya tuwe na huruma kwa viumbe wengine.** Kwa sababu, kwetu, kila aina ya kiumbe ni alama ya rehma ya Allah na ushuhuda wa Uwepo na Umoja Wake.

Kuanziahapo, kilakiumbe ambacho Allah amekipa uhai tunakitazama kwa mtazamo wa rehma ya Allah Mtukufu. Nyoyo zetu hujaa huruma. Hatuyadhuru mazingira, familia, marafiki wala hata sisimizi. Tunatambua kuwa viumbe visiviyokuwa na uhai vilumbwa na Mola wetu Mtukufu ili vitutumikie. Tunaepuka kuvitumia vibaya au kuviharibu.

Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Siku moja mtu mmoja alikuwa na kiu sana wakati akitembea. Alipita kwenye eneo liliokuja na kisima, akateremka kisimani, akanywa maji na kisha kupanda. Alipofika juu akamuona mbwa ambaye alikuwa akitweta sana na kulamba udongo kwa sababu ya kiu kali. Mtu yule akajisemea "mbwa huyu ana kiu kama niliyokuwa nayo." Aliteremka kisimani tena na kujaza maji kwenye kiatu chake kwa ajili ya mbwa yule. Alipanda kutoka kisimani akiwa amekishikilia kiatu kwa mdomo wake, akampatia mbwa anywe. Allah alifurahishwa naye kwa sababu ya kitendo chake kisichokuwa na ubinafsí akamsamehe dhambi zake."

(Bukhari, Musakat, 9.)



Mola wetu ambaye yu karibu nasi kuliko hata hulkumu zetu ndiye anayeona, kusikia na kujuu kila kitu. Hakuna kitu asichokijua na kukidhibiti ulimwenguni.

**Kujuu kwamba Mola wetu anajua kila kitu hutufanya tuyadhibiti na tuwe makini na matendo yetu.** Kama binadamu, huwa tunatazama mavazi yetu au matendo yetu hata tunapopiga picha au kurekodi kwa kamera, kwa namna hii tunapata mfumo wa moja kwa moja wa udhibiti. Hatusahau kuwa Mola wetu anatutazama na hilo hutufanya tuwe makini na matendo, tabia na mawazo yetu. Tunakuwa makini na tabia zetu sio kwa kuogopa sheria na utaratibu au mambo mengine, bali hufanya hivyo tukijua kwamba Allah anatuona muda wote. Tunamuabudu Allah tukijua anatuona na anayaona matendo yetu hata kama hatumuoni. Tunafanya juhudhi ya kufanya kila jambo katika namna bora na inayoweza kutufanya tuwe na sifa ya kuwa watu wenyewe tija.

#### Allah Mtukufu anasema:

“... Naye yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayo yatenda.”

(Surah Al-Hadiid ; 57:4)

Tunapomuamini Allah huyaratibu mai-sha yetu kuendana na maamrishi na makatazo Yake. Kutohana na upendo wetu kwa Mola wetu Mtukufu, hufanya juhudhi za kupata radhi Zake. Tunakuwa na khofu ya ghadhabu na Moto Wake na kuepuka matendo anayoyachukia. Hivyo, hupata utambuzi unaoitwa Taqwa (kuacha kuasi maamrishi ya Allah) katika nyoyo zetu. **Tunapokuwa na imani hiyo hutufanya tuwe watu wema na waaminifu.** Tunakuwa sehemu ya watu wanaojulikana kwa wema katika maneno na matendo yao. Kwa hali yoyote ile, hatuachi njia ya watu wema kwa kufanya udanganyifu. Hatukumbattii sifa mbaya kama vile uongo au udanganyifu. Tunavitunza vitu tulivyokabidhiwa kama amana. Kama iliyovukuwa kwa Mtume wetu kipenzi (s.a.w), tunaweza kuwa Waislamu wenyewe kuaminiwa am-bao wanapendwa na kuheshimiwa katika jamii, wanaosema kile wanachofikiri, watu wa mfano kutohana na wema na uaminifu wao.

#### Allah Mtukufu anasema:

“Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu; kisha wakatengenea, hawatakuwa na khofu, wala hawatahuzunika. Hao ndio watu wa Peponi, wata-dumu humo, kuwa ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyatenda.”

(al-Ahqaf, 46: 13-14)

## UPENDO WA ALLAH

Allah ndiye aliyetuumba, ndiye aliyeumba roho zetu na kuweka upendo ndani ya nyoyo zetu. Miongoni mwa majina Yake mazuri ni "Wadud." Kwa maneno mengine, Yeye ni mwenye kupenda na ni mwenye kупendwa.

Mola wetu Mtukufu, ambaye ni chanzo cha upendo, anatupenda sana sisi waja Wake. Amelithibitisha hilo kwa kutuzuku neema Zake zisizohesabika na kwa kutueleza kuhusu neema bora zaidi za Akhera. Anachotaka kutoka kwetu ni kumuamini, kumuabudu kwa namna anavyotaka, na tumpende.

Kumpenda Allah ni sharti la imani yetu na ishara ya shukurani yetu Kwake. Kwa sababu Yeye ndiye mwenye kustahiki kabisa kупendwa.

Kumpenda Allah ndio kilele cha imani ya mtu. Kumpenda ndio mwanzo wa mambo yote mazuri na yenye kupendeza. Kama Waislamu, tunamuamini kwa moyo wote, tunampenda kuliko chochote kile, kuliko hata maisha yetu. Tunajua kwamba upendo wetu kwa mama, baba, wenza, marafiki zetu na watu wengine ni neema ambazo Mola wetu ametupatia. Hatuwezi kuulinganisha upendo wa Allah na aina nyingine za upendo.

Mwenye kupenda daima humkumbuka anayempenda. Hupata furaha kwa kulidhukuru jina la mpendedwa wake na daima hamsahau. Kama waumini, nasi pia tunakumbuka Mola wetu kuititia ibada zetu, swala, visomo vya QU'ran na dua mbalimbali. Tunautafakari ukuu na uwezo Wake kwa majina Yake mazuri. Tunaonesha upendo wetu kwa kumdhukuru na kumkumbuka.



Mtume wetu (s.a.w)anasema:

"Mwenye kuwa na sifa tatu atapata ladha ya utamu wa imani: yule ambaye anampenda Allah na Mtume Wake kuliko chochote. Mwenye kumpenda mtu kwa ajili ya Allah. Mwenye kuchukia kurudi kwenye ukafiri baada ya Allah kumuokoa dhidi ya ukafiri kama anavyochukia kuingia motoni."

(Bukhari, Iman, 9)



Allah Mtukufu anasema:

"Lakini walio amini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana."

(Al-Baqara, 2: 165)

Allah Mtukufu anasema:

"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupenedeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu."

(Al-Imran; 3:31)

Wale wanaompenda Allah hufuata njia ya Mtume wake. Uislamu ni njia inayofundisha upendo. Walimu wa njia hii ya upendo ni mitume ambao ndio wanadamu wema na bora kabisa duniani. Mtume wetu Muhammad (s.a.w) alikuwa "Habibullah," yaani, "kipenzi cha Allah." Tunapofuata njia ya Mtume wetu (s.a.w) tunaonesha upendo wetu kwa Allah nasi pia hupata upendo Wake.

Nyoyo zetu zinapojaa upendo wa Allah, uhai wetu huwa na thamani, tabia na maadili yetu hupata ukomavu zaidi, mienendo yetu huwa mizuri zaidi. Tunafanya juhudu kupata radhi za Allah kwa kumpenda. Tunatii maneno yake, tunawafuata mitume Wake, na hatuiachi njia aliyotuonesha. Tunapofanya hayo, Allah hutupenda na kutupokea pamoja na waja wengine anaowapenda. Tunakuwa mionganoni mwa wateule na marafiki zake. Tunapenda na waumini na malaika.



### Allah Mtukufu anasema:

"Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!"

(Surah Ar-Rad ); 13:28)

Mmoja wa marafiki wa Allah alisema:

- Ninajua ni wakati gani Mola wangu hunikumbuka.

Watu wakakusanyika na kumuuliza:

- Unajuaje?

Akajibu:

- Ni rahisi kulijua hili. Ninapomkumbuka Mola wangu, Naye hunikumbuka.

### Allah Mtukufu anasema:

"Hakika walio amini na wakatenda mema Arrahmani Mwingi wa Rehema atawajaa-lia mapenzi.."

(Maryam; 19:96)

## KIINI CHA IBADA YETU: DUA

Dua ni kukubali udhaifu na unyonge wetu, na hivyo kurejea kwa Allah Mtukufu, na kumuomba msaada. Ni mionganini mwa nyakati ambazo tunakuwa karibu zaidi na Mola wetu. Tunaikunjua mikono yetu, tunaomba na kumsihi. Tunapeleka mahitaji yetu mbele ya Allah kupitia dua.

Hakuna masharti, nyakati au sehemu maalumu kwa ajili ya kuomba dua. Hata hivyo, baadhi ya nyakati na maeneo ni mazuri kwa dua. Siku za mikesha mitukufu, siku za Ijumaa, wakati wa kufuturu au wakati wa daku ni fursa muhimu kwa dua. Maeneo matukufu kama vile Ka'bah na viwanja vya Arafah mjini Makka ni maeneo matukufu ambayo dua hukubaliwa.

Allah Mtukufu huzikubali dua zilizoombwa kwa moyo mmoja na kwa ikhlasi. Allah amrudishi mikono mitupu mja anayeomba kwa moyo wote. Hata hivyo, mja hatakiwi kuharakisha kuona matokeo ya dua zake, kwa sababu Allah ndiye ajuaye zaidi yaliyo na kheri kwa mja Wake. Kuhusu suala hili Mtume wetu kipenzi (s.a.w) anasema: "Dua ya mmoja wenu hujibowi iwapo hatoonesha hali ya kutokuwa na subira kwa kusema: 'Nilimuomba Allah mara nyingi, lakini maombi yangu hayajajibowi'" (Bukhari, Daawat, 22)

Dua ni aina ya ibada inayofanya mawasiliano yetu na Mola wetu yawe hai muda wote. Kama tunavyomkumbuka katika nyakati za shida tunamkumbuka katika nyakati za raha na kumuomba kwa kila fursa inayopatikana.

Ni jambo lenye umuhimu kuombewa dua na wengine pia. Matendo kama vile kuwasaidia mama zetu kupanga meza, kuwapa maji wakubwa zetu, kutatua matatizo ya marafiki zetu, zote hizo ni fursa za kupata dua za watu. Hivyo, kwa kuanzia na wazazi wetu, tunatakiwa kufanya juhudhi ya kupata dua za wakubwa

zetu, watu wema na wenyewe elimu, walimu, wageni, majirani, yatima, mafukara na masikini. Kadhalika, nasi yatupasa tuwaombee dua ndugu zetu Waislamu.



### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Dua ni kiini cha ibada."

(Tirmidhi, Daawat, 1)



### Allah Mtukufu anasema:

"Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba..."

(Al-Baqara ; 2: 186)



### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Mkumbe Allah wakati wa raha ili akukumbuke wakati wa shida."

(Ahmad ibn Hanbal, Musnad, I.)



Ewe Allah! Ulinde Ummah wa Muhammad! Wasamehe! Usiwanyime msaada na rehma Zako. Amin

## NIMEKUITIKA EWE MJA WANGU

Muislamu mmoja alikuwa na mazoea ya kuamka kila usiku na kumdhukuru Allah. Iblisi akamwambia:

— Ewe unayempenda sana Allah, japokuwa walisoma jina la Allah usiku wote, je kuna anayeyajibu maombi yako? Hakuna hata jibu moja liliokujia, utaendelea kuomba dua mpaka lini?

Mtu huyo akavunjika moyo, akaweka kichwa chake chini na kulala. Akiwa ndotoni akasikia:

— Amka! Kwa nini umeacha kuomba dua? Kwa nini umechoka?

Mtu yule akasema:

— Hakuna jibu la "nimekuitika mja wangu" linalonijia, hivyo nikahofu kupotea. Hapo akasikia tena:

— Usomaji wako wa jina "Allah" ni sawa na itikio lake la "nimekuitika mja wangu." Asingekuitikia usingekuwa na uwezo wa kusema "Allah" na kumuomba. Dua zako zinatokana na yeye kupandikiza shauku ya kufanya hivyo ndani ya moyo wako. Juhudi zako zote, na utafutaji wako wa riziki hutokea kwa sababu Allah anataka uwe karibu zaidi Naye na huiruhusu miguu yako kufanya hivyo. Katika kila dua moja inayoanza na "ewe Mola" kuna majibu mengi ya Allah akisema "nimekuitika mja wangu." Mtu anayejiwka mbali na ibada na dua ndiye ambaye

moyo wake umejitenga dhidi ya kusema: "Ewe Mola wangu!" Kwa sababu kwenye moyo na ulimi wake kuna kifunko na kifungo.

Labda Allah hajamfanya apatwe na shida, maumivu na huzuni ili asilie na kulalamika anapoumia. Tambua kwamba shida na tabu zinazokufanya umuombe na kumuita Allah, ni bora kuliko ufalme wa dunia hii. Dua bila tabu ni yenye ubaridi. Dua inayoombwaa wakati wa tabu hutoka moja kwa moja moyoni.

**Mawlana Jalaladdin al-Rumi**



## NITAFAGIA, UTAMWAGILIA



K w a  
miezi kadhaa,  
hakuna hata tone moja  
la mvua lillodondoka.  
Hakuna maji yaliyokuwa  
yamebaki kwa matumizi ya  
wanyama isipokuwa maji ya  
tope katika vidimbwi. Kwa  
upande mwengine, watu  
walijaribu kuishi kwa maji ya  
visima, ambayo yallkaribia  
kukauka. Waliamini kuwa  
hawakuwa na njia ya

kufanya mbele ya ukame huu isipokuwa ku-  
muomba Allah. Kwa siku kadhaa, waliswali  
kwa ajili ya kuomba mvua, wakachinja  
wanyama, wakatoa sa-  
daka, wakawafurahi-  
sha yatima, lakini  
hali iliendelea kuwa  
hivyo hivyo.

Hawakuwa la kufan-  
ya. Baadhi ya wakazi  
wa vijiji vingine waliku-  
sanyika pamoja na  
kuomba zaidi mvua.  
Kuanzia watoto,  
wakubwa, wazee  
vijana, kila mtu ku-  
toka vijiji hivyo alikuwa  
katika uwania wa mku-  
sanyiko. Viongozi wa kidini  
katika kijiji hicho na vijiji jirani nao  
walikusanyika pia. Walisoma Surah  
Yasin kutoka ndani ya Qur'an na mawuli  
(simulizi za maisha na ubora wa Mtume  
(s.a.w)). Walitoa sadaka na kuchinja wanya-  
ma. Waliomba kwa saa kadhaa. Macho yote  
yalielekezwa mbinguni. Lakini, mvua haikunye-  
sha.

Siku iliyofuata, walipanga kuomba tena. Jua lili-  
chomoza na kila eneo lilikuwa jeupe. Siku hiyo,  
hali ya hewa ilionekana kuwa na joto zaidi.  
Wanawake walikuwa wakisubiri katika foleni ya  
maji waliyoyahitaji. Wanaume walimaliza kazi  
zao nyumbani na walijiandaa kwenda kwa ajili  
ya kuomba tena mvua. Vilevile, siku hiyo baa-  
di ya walimu na viongozi maarufu kutoka mjini  
wangejumuika.

Jua lilipoinuka kidogo, watu wa vijiji jirani walianza kuja. Maimam wageni walikuwa wameshawasili. Ibada ilikaribia kuanza. Wakati huo, bibi mmoja alifungua mlango wake huku akiwa ameushikilia mgongo wake. Kutohana na umri wake na maradhi, alishindwa kwenda uwanjani. Alikuwa na huzuni sana kwa kutopatikana mvua hata kidogo na aliendelea kuomba maghfira kwa Allah. Daima aliendelea kuyafanya matumaini yake kuwa ya juu na kusema kuwa Allah ni mwinci wa rehma kwa waja Wake na siku moja itanyesha.

Licha ya maumivu ya mgongo wake, alifagia mbele ya mlango wake kwa tabu. Wakati akiunyosha kidogo mgongo wake, alitazama mbinungi kwa macho yenyeye huzuni. Kwa kawaida alizoea kunyunyuzia maji chini kabla ya kufagia ukumbi wa nyumba yake ili vumbi isisambae. Lakini, kwa sababu ya ukosefu wa maji, mara hii hakupata maji na vumbi liliingia kooni mwake. Alitamani sana kunywa funda la

maji! Hapo akasema: "Mola wangu! Nitafagia nawe utamwagilia maji."

Hicho ndicho alichokisema. Mawingu meusi yalianza kuanekana kwa mbali kabla hata hajaingia nyumbani mwake. Dakika chake, mawingu meusi ya mvua yalikuwa ametanda katika anga lote. Ndani na nusu saa, ilianza kunesha kwa wingi. Umati uliokusanyika uwanjani ulishangazwa namna ilivyoanza kunyesha kabla hata hawajaanza kuswali. Wote walilowa. Wakati wakirudi majumbani, walikuwa wakimshukuru Allah na kulia kwa furaha na mshangao, huku wakilionia kama ni tukio la ajabu.



## NINI MAANA YA KUWA MUISLAMU?

- \* Tukiwa kama waja Wake, kila kitu tulichonacho ni milki ya Allah.
- \* Hatumfanyii Allah washirika.
- \* Hatumkubali mungu mwingine isipokuwa Allah.
- \* Tunampenda Allah kuliko kingine chochote.
- \* Yeye tu ndiye tunayemuabudu.
- \* Allah pekee ndiye tunayemuomba dua na kumtaka msaada.
- \* Tunamtegemea Allah na kuamini kuwa hatatuacha peke yetu wala kututelekeza.
- \* Tunatambua kuwa kheri zote hutoka kwa Allah na kumshukuru Yeye tu.
- \* Yeye pekee ndiye tunayemuabudu na kumsujudia.
- \* Tunataraji rehma Yake na kukhofu ghadhabu Yake.
- \* Tunatekeleza maamrisho ya Mola wetu Mtukufu.
- \* Hatufanyi mambo yaliyokatazwa na Mola wetu.
- \* Tunampenda sana Allah na kulitaja jina Lake kila mahali na katika kila mazingira.
- \* Tunafanya jitihada kusoma, kusikiliza na kuyaelewa maneno ya Allah, yaani Qur'an Tukufu.

KWA SABABU SISI NI WAISLAMU.

## NANI ATAKAYEKUOKOA?

Mtume (s.a.w) alikuwa katika safari ya kijeshi katika eneo la Najd huko Arabia. Walipokuwa wakirudi mjini Madina, askari waliokuwa katika safari hiyo walichoka. Hali ya hewa ilikuwa ya joto na walikuwa na safari ndefu. Ilikuwa muda wa adhuhuri. Walipofika katika eneo lenye miti na kivuli, walipumzika. Ili Mtume wetu (s.a.w) apumzike vizuri, Maswahaba walimuwekea eneo maalumu. Wao walipumzika kivulini mbali kidogo na alipokuwa.

Askari walilala kutohata na safari ndefu, uchovu wa safari na hali ya joto. Mtume (s.a.w) alipumzika chini ya kivuli. Aliuning'iniza upanga wake kwenye mti na kuchukuliwa na usingizi.

Maadui walikuwa wakiwafuata Waislamu kwa siri. Kwa adui ambaye alikuwa akisubiri muda muafaka, basi huu ndio uliokuwa muda wenye. Makafiri walitaka kumuua Mtume (s.a.w), wakamtuma mmoja wao aitwaye Gavres. Alimsogelea Mtume (s.a.w) bila yejote kumuona. Alichukua upanga uliokuwa ukining'inia mtini. Alipokaribia kumpiga Mtume (s.a.w) akafungua macho yake matukufu. Gavres akauliza:

— Ewe Muhammad! Sasa nani atakayekuokoa dhidi yangu?

Mtume wetu (s.a.w) alimjibu adui aliyetaka kumuua bila khofu wala wasiwasi wowote:

"Allah!"

Adui aliyetetemeka kwa kuona imani isiyotetereka ya Mtume wetu (s.a.w) na

kumtegemea Allah alidondosha upanga. Mtume wetu (s.a.w) aliuchukua upanga na kumuuliza mtu huyo:

— Sasa nani atakayekuokoa dhidi yangu?

Mtu huyo ambaye hakuelewa kilichotokea alisema:

— Hapana! Nakuomba usiniadhibu!

Mjumbe wa Allah akamuuliza:

— Utakubali kuwa hakuna mungu ila Allah na kwamba mimi ni Mtume wake?

Mtu huyo akasema:

— Hapana, nisingependa kufanya hiyo. Lakini, ninakuahidi kuwa sitapigana nawe na sitashiriki katika jeshi litakalopigana nawe.

Hapo, Mtume wetu (s.a.w) akamuacha huru mtu ambaye alitaka kumuua. Wakati huo, Maswahaba waliosikia sauti ile walienda kule. Mtu yule aliondoka akiwa anatetemeka kwa jinsi Maswahaba walivyomtazama. Mtu huyo pia aliguswa na kitendo kile cha kuhurumiwa na kusamehewa. Aliporudi kwa wenzake, alisema:

— Nirmetokea kwa Mtu Bora kabisa.  
(Al Boukhari, Jihad, 84)

## MTUME (S.A.W) ALIMPENDA SANA ALLAH

Mtukufu Mtume (s.a.w) alimpenda Allah kuliniko chochote kile. **Kamwe hakuulinganisha upendo wa Allah na chochote kile.** Ili kuilinda hali hii ya upendo alikuwa akimuomba Allah, "Mola wangu! Ufanye upendo wako kuwa bora zaidi kwangu kuliko uhai wangu, familia yangu, na maji baridi!" (Tirmidhi, Daawat, 72)

**Fikra ya kupata upendo wa Allah ilikuwa sera ya msingi kwa Mtume (s.a.w) katika uhusiano wake na ulimwengu, binadamu, wanyama na viumbe wote wengine.** Kwa kuwa alimpenda sana Allah, alivihurumia viumbe Vyake.

Alitaka kupata radhi za Allah katika kila kitendo chake na daima alikuwa akiomba akisema, "Mola wangu! Ninakuomba upendo wako, upendo wa wale unaowapenda, na kupenda amali inayonikurubisha kwenye upendo Wako." (Tirmidhi, Daawat, 72)

**Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akilidhukuru jina la Allah na pia akisema "Tofauti baina ya wale wanaolidhukuru jina la Allah na wale wasiolidhukuru ni kama tofauti baina ya aliye hai na mfu."**

(Bukhari, Daawat, 66)

Alikuwa akianza matendo yake yote kwa jina la Allah na akipata furaha kwa kuyadhukuru majina na sifa Zake njema.

Mtume wetu (s.a.w) alikuwa na khofu kubwa dhidi ya kuasi maamrisho ya Allah. Daima aliweka katika moyo wake khofu ya kukosa upendo na rehma za Allah. Moyo wake ulikuwa ukitetemeka kwa khofu na upendo kwa Mola wetu Mtukufu. Kamwe hakukosa khofu na utii na alikuwa akisema "Mimi ndiye ninayetambua."



### Mtume wetu (s.a.w) alisema:

"Ewe Allah! Wewe ni Mola wangu. Hakuna mola apasaye kuabudiwa ila Wewe. Umeniumba. Mimi ni mja Wako. Bado ninatunza ahadi niliyokupa kabla ya kuja duniani. Ninajilinda Kwako dhidi ya makosa yangu. Ninakiri neema Zako mbele Zako, na kukiri makosa yangu. Nisamehel! Bila shaka Wewe ndiwe pekee unayesamehe dhambi."

(Bukhari, Daawat, 2)



Alikuwa hasahau ukubwa wa adhabu ya Allah upopo mkali unapopiga, radi zinapopiga au mawingu meusi yanapodhihiiri. Alikumbuka namna baadhi ya umma zilizotangulia zilivyoangamizwa. Katika hali kama hizo, alikuwa akiswali na kuomba dua kwa kukhofu ghadhabu ya Allah. Wakati mwingine anaposoma au kusikiliza Qur'an Tukufu, au wakati wa kuswali, moyo wake ulikuwa ukitetemeka kwa khofu ya Allah, na alikuwa akilia sana.

**Mtume wetu (s.a.w) aliuamini msaada na rehma za Allah nyakati zote na kujisalimisha kikamilifu kwa Allah.**

Mtume wetu (s.a.w) akiwa pamoja na Abu Bakr (r.a) walikuwa wakiwakimbia waabudu masanamu wa Makka. Abu Bakr alikuwa na wasiwasi kuwa makafiri hao waliokuwa wamesimama mbele ya




Iango la pango walilokuwa wamejificha wangemdhuru Mtume (s.a.w). Mtukufu Mtume (s.a.w) akamwambia Abu Bakr "Usihuzunike! Allah yu pamoja nasi."

Wakati Mtume (s.a.w) akitambua kuwa ghadhabu ya Allah ni kali, kamwe hakupoteza matumani na rehma Zake. **Aliishi maisha yenyé mizania baina ya khofu na matarajia.** Alikuwa akisema kuwa naye atapata wokovu kwa rehma ya Allah japokuwa yeye ni mtume. Alisema kuwa "Swala ni nguzo ya dini" (Tirmidhi, Daawat, 1) na akimuomba na kumuabudu Allah kila anapopata fursa ili kumfanya kuwa mja mwema. Alikuwa akiomba msaada, rehma na msamaha wa Allah. **Mtume wetu (s.a.w) daima alitoa shukrani za juu kabisa kwa Allah**

Alionesha upendo wake kwa Allah kwa kumuabudu usiku na mchana. Ili kumshukuru Allah, hakuwa akifanya matendo ya wajibu pekee, bali pia alikuwa akifanya matendo ya sunnah. Alikuwa akifunga siku fulani za kila mwezi na kuswali usiku. Wakati mwininge mpaka miguu yake ilikuwa ikivimba kwa sababu ya kusimama kwa muda mrefu. Siku moja aliulizwa "kwa nini anajichosha sana hali ya kuwa ameshasamehewa dhambi zake zilizopita na sasa," akajibu "Je nisiwe mja mwenye kumshukuru Allah?" (Al Boukhari, Tafsir, Surah 48; 2)

Mtume Muhammad (s.a.w), kiigizo na kiongozi bora katika kila uwanda, alitufundisha kwamba shukurani ya kweli ni ile inayofanywa kwa kumtii na

kumuabudu Allah. Alitaka kuwa mja ambaye daima hushukuru. Alikuwa akiomba, "Mola wangu! Nipe msaada wa kukukumbuka, kuzishukuru neema Zako, na kukuabudu katika namna iliyo bora kabisa!" na kutuusia kuomba hivyo pia. **Alimshukuru Allah katika nyakati za shida na raha.** Alikuwa akisema "Alhamdulillah" kwa kila neema anayojaaliwa na Allah na kuonesha kilichokuwa moyoni mwake.



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ  
اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْقَيُّومُ لَا تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ لَهُ  
مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَنْ ذَا أَلَّذِي يَشْفَعُ  
عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا  
يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عَلَيْهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ وَسِعَ كُنْسِيَّهُ  
السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَا يَؤْدُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ

## الْعَظِيمُ

Kwa Jina La Mwenyezi Mungu Mwingi Wa Rehema Mwenye Kurehemu  
Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo  
yote milele.

Hashikwi na usingizi wala kulala.

Ni vyake pekee vyote viliomo mbinguni na duniani.

Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake?

Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao;

wala wao hawajui chochote katika vilio katika ujuzi wake,

ila kwa atakalo mwenyewe. Enzi yake imetanda mbinguni na duniani;

na wala haemewi na kuvilinda hivyo.

Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu.

# MASWALI

Jaza sehemu za wazi kwa maneno muafaka

(kuwa / jani/ mnampenda / Dua / atakupendeni / upeo wa mbali / wanampenda/karibu / nyoyo / Allah / nafsi zao wenyewe)

1. "Tutawaonyesha Ishara zetu katika ..... na katika ....."
2. "Yeye anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki ..... ila analijua"
3. "Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: "....."! Na kikawa."
4. "Lakini walioamini ..... Mwenyezi Mungu zaidi sana."
5. "Sema: Ikiwa nyinyi ..... Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu ..... na atakufutieni madhambi yenu.
6. "Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio ..... hutua!"
7. ".....ni kiini cha ibada."
8. "Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo ..... Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba..."



## Tujipime

- 1. Ni lipi kati ya mambo yafuatayo ambalo litampa Muislamu ladha ya utamu wa imani?**
  - a) Kumpenda Allah na Mtume Wake kuliko yeyote yule.
  - b) Kupenda kwa ajili ya Allah.
  - c) Kuliona suala la kuitelekeza dini kuwa ni hatari kama kuungua ndani ya moto.
  - d) Yote.
- 2. Ni maelezo gani ambayo sio sahihi kuhusu dua?**
  - a) Sio lazima kuwa na sehemu na muda maalumu wa kuomba dua.
  - b) Ni lazima kuchukua wudhu kabla ya kuomba dua.
  - c) Tuombe dua tunapokuwa katika nyakati za raha ili Mola wetu atukumbuke nyakati za shida.
  - d) Tunatakiwa kuswali tunapokuwa katika kipindi kigumu ili Mwenyezi Mungu aweze kutupa msaada katika kipindi kigumu.
- 3. Jambo lipi katika mambo yafuatayo ambalo sio sahihi kuhusu upendo wa Mtume (s.a.w) kwa Allah?**
  - a) Alikuwa akilidhukuru jina Allah muda wote.
  - b) Alilenga kupata radhi za Allah katika matendo na maneno yake yote.
  - c) Alikuwa imam wa Maswahaba wakati wa swala tano.
  - d) Daima alimuomba na kumuabudu Allah kama shukrani.
- 4. Lipi kati ya mambo haya ambalo sio miongoni mwa faida za kumuamini Allah?**
  - a) Hutufanya tupendwe na watu wote.
  - b) Hutupatia hisia ya kujiamini isiyokuwa na kikomo.
  - c) Hutufanya tuwe na huruma wa viumbe vingine.
  - d) Hutufanya tuzidhibiti tabia na mienendo yetu.

5. Ni maelezo yepi kati ya haya yafuatayo ambayo hayaelezei uwepo na umoja wa Allah?

- a) Kila kazi ya usanifu ina msanifu aliyeitengeneza. Na ulimwengu nao pia kuna aliyeumba.
- b) Mfumo na nidhamu kamilifu katika mwili wa mwanadamu haiwezi kutokea yenye tu. Hili linathibitisha uwepo wa muumba.
- c) Haiwezekani kwa juu kuchomoza na kuzama, usiku na mchana na misimu vitokee kwa sadfa. Mfumo kamili ulio ndani ya ulimwengu ni uthibitisho wa uwepo wa muumba.
- d) Kila mtu ana haki ya kuchagua kheri au shari.

**Zilindeni Sala, na khasa Sala ya katikati,  
na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu  
nanyi ni wenge kuqunuti (kunyenyeka).**

(Surah Al Baqarah Ayah ya 238)





ALAMA YA WEMA NA UZURI

# KUAMINI MALAIKA

- ✿ *Viumbe vinavyoonekana na visivyoonekana*
- ✿ *Kuamini Malaika*
- ✿ *Sifa na kazi za malaika*
- ✿ *Faida za kuamini Malaika*
- ✿ *Sifa za Shetani*
- ✿ *Mtume na Malaika*



## SAUTI YA MALAIKA

Halil alikuwa kijana maridadi na makini ambaye alifurahia kutafakari. Alitafuta vyanzo vyatukio aliyoyashuhudia au fikra zinazomjia akilini mwake. Na wakati mwingi, alikuwa akija na hitimisho zuri na lenye faida.

Siku moja alimwambia baba yake:

— Baba, ninapomuona mama yangu akifanya kazi kwa ajili yetu na kuchoka, ninahuzuni sana.

Wakati huo nataka kumsaidia mama, ninafanya hivyo. Lakini wakati mwingine, japo kwa najua kwamba mama anahitaji msaada wangu, ninataka kwenda nje kucheza, ninafanya hivyo. Sielewi kwa nini ninafanya hivi kwa sababu ninampenda sana mama yangu.

Baba yake alikuwa ameyazoa maswali yake kama haya. Alipenda namna mwanaye alivyokuwa akizungumza kwa uwazi bila kuficha hisia zake. Akamwambia Halil:

— Hili suala sio lako peke yako mwanangu, kila mtu yuko hivyo.

— Ni hivyo? Nimefurahi sana. Nilikuwa nikijilaumu kwa kudhani kuwa mimi pekee ndio niko hivyo. Lakini, ninashangaa sababu ya hali hii. Kwa nini mawazo haya yakinzane?

— Ni kweli, yanakinzana. Wanadamu wanakuwa na mawazo yanayokinzana kama hivi kwa sababu wanakuwa chini ya ushawishi wa viumbe wawili wanaopingana ambao hawawezi kuwaona. Wa kwanza ni malaika na mwingine ni Shetani.

— Baba, malaika wanafanya nini?

— Malaika hutupatia ushauri mwema. Htuumba: Kuwa mwema! Fanya mema haya na haya! Hawataki tufanye matendo mabaya. Tunapofanya kitu kibaya, malaika husikitika sana.

— Shetani anafanya nini?

— Hutushawishi kufanya mambo mabaya. Anatutaka tuseme maneno mabaya na tuumize hisia za watu wengine. Anataka tuasi maamrisha ya Allah. Hufurahia tunapoacha kuwatii wakubwa zetu na kutowasikiliza wazazi wetu.

— Lakini baba! Ninapotaka kufanya jambo jema au baya, sisikii sauti ikisema “fanya hivi!” au “usifanye hivyo!”

— Sauti za malaika na Shetani sio kama sauti za binadamu. Huzishawishi moja kwa moja akili zetu. Tuangalie mfano ulionipatia.

Unapowaza, “Mama yangu anajichosha sana. Hana mtu wa kumsaidia; ninataka apumzike kidogo. Anafanya kazi sana kwa ajili yetu. Ngoja nimsaidie kidogo!” unatakiwa kujua kwamba hii ni sauti ya malaika. Ukimuona mama yako katika hali hiyo halafu ukawaza:

“Inanihusu nini mama akichoka? Siwezi kumsaidia mtu yeote kwa sasa,” hapo ujue kuwa shetani anafanya kazi ya kukupumbaza. Wakati mwingine, Shetani huenda mbali zaidi akakufanya ufanye mambo ambayo usingetegemea kuyafanya na kukufanya uwe na mawazo kama vile:

“Kama anafanya kazi sana, anafanya kwa ajili ya nyumba yake, kila mtu anatekeleza wajibu wake. Inanihusu nini akichoka?” Hapo tunapaswa kuzinduka na kuwaka makini tusiangukie kwenye mtego wa Shetani.

Ili kutofautisha kati ya sauti ya malaika na sauti ya shetani, nitakupatia mfano mwingine.

Tukitaka kufanya mambo ambayo Allah au Mtume wetu anataka tuyafanye, tujue kwamba hisia hiyo inatujia kwa sababu ya ushawishi wa malaika. Tukihisi kinyume, basi hiyo ni kwa

sababu ya ushawishi wa shetani. Shetani anatutaka tujitenge na dini, kwa maneno mengine, anataka tuwe mbali na mambo mazuri katika maisha.

— Baba, kwa nini hatuwaoni malaika na shetani? Waweza kuniambia zaidi kuhusu malaika na shetani?

— Hatuwezi kuwaona kwa sababu maumbile yao ni tofauti na yetu. Nitakufafanulia

hili wakati mwagine kwa sababu ninapaswa kwenda kazini sasa.

Halil alimshukuru baba yake na kuanza kutafakari kuhusu malaika na shetani...

**M. Yaşar KANDEMİR**



## VIUMBE WANAOONEKANA NA WASIOONEKANA

Allah aliumba viumbe vyote na kuweka utaratibu na nidhamu maalumu katika ulimwengu. Ameumba idadi isiyokuwa na kikomo ya viumbe wanaoonekana na wasioonekana kwa macho yetu.

Tunaweza kuona na kuwabaini baadhi ya viumbe kwa milango yetu ya fahamu. Lakini, hatuwezi kuona viumbe wote. Kuna baadhi ya viumbe ambavyo haiwezekani kuviona na kuvibaini.

Ili kutambua uwepo wa kitu, sio lazima kukiona. Kuna vitu vingi ambavyo tunakiri kuwa viro hata kama hatuvioni. Kwa mfano, hatuwezi kuziona akili zetu, upendo, huruma na furaha.

Lakini, sote tunakubali kuwa viro. Kadhalika hatuwezi kuuona umeme unavyosafiri katika nyaya, au mawimbi ya sauti yakisafiri hewani. Mifano hii inatuonesha kuwa viumbe sio vile tu vinavyoonekana kwa macho yetu.

Binadamu, wanyama, mimea, milima, bahari, miti, maua, mwezi, juu na nyota vyote ni mifano ya viumbe vinavyoonekana. Malaika na shetani ni miiongoni mwa viumbe visivyoonekana. Sababu ni kwa kuwa macho yetu hayakupewa uwezo wa kuviona. Hatuwaoni malaika na shetani, lakini tunaamini wapo. Kwa sababu Mola wetu ametuhabarisha kuhusu uwepo wa malaika na Shetani ndani ya Qur'an Tukufu.



## KUAMINI MALAIKA

Malaika waliumbwa na Allah kwa ajili ya kutekeleza majukumu fulani fulani. Hatuwezi kuwabaini malaika kwa milango yetu ya hisia na hatuwezi kuwaona kwa macho yetu. Kwa sababu hii tunaweza kupata taarifa zao kutoka ndani ya Qur'an na Mtume wetu (s.a.w) pekee.

Kuamini uwepo wa malaika ni mojawapo ya nguzo za imani katika Uislamu. Kukana uwepo wa malaika ni sawa na kukana ufunuo, mitume, na vitabu viliviyoteremshwa kwa mitume, na dini wanayoihubiri. Kwa sababu Allah alituma ujumbe Wake kwenda kwa mitume kuititia kwa malaika. Kwa hivyo, wale wanaoamini ufunuo kutoka kwa Allah, mitume, na vitabu wanapaswa pia kuamini malaika.

### Sifa za Malaika

Malaika wana sifa ambazo ni tofauti na wanadamu na viumbe wengine. Malaika wameumbwa kwa nuru. Wana nguvu na imara sana. Wanaweza kuhama kwa kasi mno. Kwa sababu hii, wanaweza kwenda umbali mrefu kwa muda mfupi.

Malaika ni viumbe wanaotekeleza majukumu ambayo Allah huwaamuru kuyafanya. Daima wanatii na kumuabudu Allah. Hawaasi maamrisho ya Allah. Hawafanyi dhambi yoyote wala hawakiuki makatazo ya Allah. Kamwe hawakidhuru kiumbe chochote.

Hawana jinsia. Hawali, hawanywi, wala hawalali. Hawachoki kufanya kazi na kufanya ibada.

### Majukumu na kazi za malaika

Jukumu la malaika ni wao kuwa waja na watumishi wa Allah na kutekelezea amri Zake. Malaika hutekeleza amri za Allah kwa usahihi. Wanapotekeleza majukumu yao, hawachoki wala hawazembe. Muda wote wanamuabudu Allah na kamwe hawamuasi.

Jukumu kubwa la malaika ni kumuabudu na kumtii Allah. Mbali na majukumu haya makuu, kuna baadhi ya malaika ambao wamepangiwa kazi maalumu. Malaika maarufu zaidi ni malaika wanne wenye hadhi ya juu:

**Jibra'il (Jibril):** Malaika huyu alipewa jukumu la kufikisha ufunuo wa Allah kwa mitume. Wakati huo huo, Jibril (a.s) hufikisha ujumbe na amri za Allah kwenda kwa malaika wengine.

**Malaika wa Mauti (Azrael):** Kwa idhini ya Allah, jukumu la Azrael ni kuchukua roho muda wa mauti unapofika. Kwa sababu hii, malaika huyu ameitwa "malaika wa kifo" ndani ya Qur'an Tukufu.

**Mikail:** Huyu malaika amepewa jukumu la mchakato wa matukio ya kimaumbile kama

### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Malaika wameumbwa kwa nuru, majinni wameumbwa kwa moto, na Adam ameumbwa kwa udongo."

(Muslim, Zuhd, 10)



ukuzaji wa uoto, mimea na riziki ya kila siku kwa viumbe.

**Israfil:** Huyu amepewa jukumu la kupuliza baragumu (al-Sur) Siku ya Mwisho ili kuwajulisha wote kuwa Qiyama kimeanza.

Mbali na malaika hao wanne wakuu, kuna malaika wengine wengi ambao wamepangiwa kazi maalumu. Miiongoni mwao ni hawa wafuataao:

**Kiram'an Katibin:** Ni malaika wanaoandika kumbukumbu za matendo yetu mema na mabaya. Ni malaika walioko upande wa kulia na kushoto kwa mwanadamu. Malaika aliye ko upande wa kulia huandika kumbukumbu za matendo, maneno na mienendo yetu mizuri. Malaika aliye ko upande wa kushoto huandika kumbukumbu za matendo, maneno na mienendo yetu mibaya. Muda wa kuulizwa utakapofika, malaika hawa ndio watakaokuwa mashahidi wetu.

**Malaika Walinzi:** Ni malaika walinzi. Wamepewa kazi ya kuwalinda watu wanajilinda na kumtegemea Allah. Wanawalinda watu dhidi ya ajali na matatizo mbalimbali kwa idhini ya Allah.

**Al-Munkar na Al-Nakir:** Ni malaika wa maswali. Hawa ni malaika waliopewa kazi ya kutuhoji makaburini mwetu. Watauliza maswali kama vile "Nani Mola wako? Nini kitabu chako?"



na wataamiliana na sisi kulingana na majibu yetu.

**Malaika wengine:** Kuna malaika wengine tofauti na hao walioelezwa, ambapo wamepangiwa kutekeleza kazi nyingine nyingi. Kwa mfano, baadhi ya malaika huzishawishi nyoyo za watu kuiende a kheri na haki, wakati wengine wakiandika kumbukumbu za salam za rehma (salawat) tunazomtakia Mtume wetu (s.a.w), na malaika wengine wakitekeleza majukumu mbalimbali yanayohusu Pepo na Moto.

#### Allah Mtukufu anasema:

"Na hakika bila ya shaka wapo walinzi juu yenu, Waandishi wenye hishima, Wanayajua mnayo yatenda".

(al-Infitar, 82: 10-12)

#### Allah Mtukufu anasema:

"....Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrishwa, na wanatenda wanayo amrishwa."

(Al-Tahir, 66:6)

## MALAIKA HUWAOMBEA WAGONJWA

Asubuhi moja, mtoto wa ami wa Mtume (s.a.w), Ali (r.a) alikutana na rafiki yake Sa'id ibn Ifaqa. Ali (r.a) aliushika mkono wake na kusema:

"Ewe Sa'id! Leo twenda kumtembelea mgonjwa. Hassan anaumwa, twende kumtembelea."

Walianza safari. Walipofika nyumbani kwa Hassan, Abu Musa al-Ash'ari (r.a.) alikuwepo pia.

Ali akauliza:

— Ewe Abu Musa! Je umekuja kwa nia ya kumtembelea mgonjwa au ulisimama kwa ajili ya jambo jingine? Abu Musa akasema:

— Nimekuja kumtembelea kwa sababu anaumbwa.

Hapo, Ali (r.a) akasimulia habari njema aliyoisikia kutoka kwa Mjumbe wa Allah:

"Iwapo Muislamu atamtembelea Muislamu mwenzake anayeumwa wakati waasubuhi, malaikaelfusabini humuombea dua na kumuombea maghfira mpaka jioni. Akimtembelea wakati wa jioni, malaika elfu sabini humuombea mpaka asubuhi. Kadhalika, mtu huyu atapewa matunda peponi."

(Tirmidhi, Janaiz, 2)



## MALAIKA HUMUOMBEA ALIYEFUNGA

Mtume (s.a.w) ambaye alikuwa makini kuhusu uhusiano na majirani alikuwa akiwatemelea sana majirani zake. Siku moja alitembelea nyumbani kwa Ummu Umara anayejulikana pia kama Bibi Nasiba na anayejulikana kwa ujasiri wake katika Vita ya Uhud. Ummu Umara ambaye alifurahishwa pia na ziara hiyo ya Mtume (s.a.w) aliandaa chakula. Alimpatia chakula Mtume wetu na wale waliokuwa pamoja naye. Mtume wetu (s.a.w) alitaka mwenyeji wake ashiriki katika chakula alichowaandalia kwa kusema:

— Njoo ushiriki pamoja nasi! Ummu Amara akasema:

— Nimefunga.

Kwa kuwa Ummu Umara alikuwa amefunga, hakuweza kushiriki katika chakula. Hapo Mtume (s.a.w) akatupatia habari njema:

*"Iwapo chakula kinawila jirani na aliyefunga, malaika humuombea mpaka wenzake watakapomaliza kula au kushiba."*

(Tirmidhi, Sawm, 66)



# FAIDA ZA KUAMINI MALAIKA

## KUAMINI MALAIKA

- Htuongeza hisia ya utii na kutupatia upendo wa kufanya ibada.
- Htuweka mbali na matendo mabaya.
- Huzirekebisha tabia zetu.
- Hutuhamasisha kufanya kazi na kutupa nguvu chanya.

Malaika huendelea kumuabudu na kumtii Allah muda wote. Baadhi yao wanakuwa katika sijda na wengine wakiwa katika hali ya rukuu. Humdhukuru Allah muda wote bila kuacha na kuwaombea msamaha waumini. **Kuamini malaika wenye sifa hizi hutufanya kuwa na utambuzi zaidi juu ya utii wetu mbele ya Allah na kutuhamasisha kumuabudu.** Hutuhamasisha kumuomba msamaha kwa makosa na dhambi zetu na kuwa waja wema kama anavyotaka tuwe. Hutuhamasisha kuutumia vizuri muda wa usiku na mchana. Tunawakumbuka malaika na kujaribu kuwa mionganoni mwa wale wanaomuabudu Allah muda wote.

### Allah Mtukufu anasema:

"Na ni vyake Yeye tu Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na katika ardhi. Na walioko kwake hawafanyi kiburi wakaacha kumuabudu, wala hawachoki. Wanamtakasa usiku na mchana, wala hawanyong'onyei."


(Al-Anbiya ; 21:19-20)

Kuamini malaika Kiram'an  
Katibin walioko pande zetu za  
kulia na kushoto na kuandika  
kumbukumbu za matendo  
yetu, na pia al-Munkar na al-  
Nakir watakaotuhoji katika  
makaburi yetu, huifanya hisia  
yetu ya kuwajibishwa huko Akhera  
iendelee kuwa hai. Hutukumbusha  
kuwa siku moja tutaulizwa kwa  
matendo yetu. Kuamini malaika  
kama Muislamu huturahisishia  
kuweka uwiano na kuyadhibiti  
matendo yetu, na  
uhusiano wetu na watu  
wengine. **Hutuweza**  
**kuyatengeneza**  
**vizuri maisha**  
**yetu na kujiweka**  
**mbali na makosa.**  
Kuamini malaika  
hutufanya sisi  
wanadamu kuwa  
"kama malaika."  
Ili kutowasumbua  
malaika  
wanaokaa pamoja  
nasi, tunaepuka  
maneno mabaya  
na yenye kuudhi.  
Hatuwasangenyi au  
kuwateta wenzetu.  
Tunaepuka kuwa  
waonevu na  
hatumfanyii ukaidi  
mtu yeyote.

Allah Mtukufu anasema:

"Wanapo pokea wapokeaji wawili, wanao  
kaa kuliani na kushotoni. Hatamki neno ila  
karibu yake yupo mwangalizi tayari."

(Surah Qaaf; 50:17-18)



Malaika hutupa hamasa ya kufanya matendo mema, mazuri na ya kweli. Hufurahia kila tendo letu jema tunalolifanya katika kutii maamrisho ya Mola wetu na Mtume wetu (s.a.w). Hutuombea msamaha kwa Allah. Tunapofanya mambo mazuri kwa ajili ya Allah kama vile kuwatendea wema wazazi wetu, kuwasaidia na kuwaombea marafiki zetu, kuwatembelea jamaa zetu au wagonjwa, kuswali, kusoma Qur'an Tukufu, au kutafuta elimu, malaika hutuombea dua na kumuomba Allah atusamehe. Kujua na kuamini kuwa matendo yetu mema yanatambuliwa na kuthaminiwa hutufanya tujisikie vizuri. **Hutuhamasisha kufanya vizuri zaidi; huzirekebisha tabia zetu.**

### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Shetani na Malaika huchochea hisia na fikra ndani nyoyo za wanadamu. Kazi ya shetani ni kuwashawishi watu kufanya makosa, kuwavuta kufanya vitu ambavyo mwisho hugeuka kuwa vibaya na vyenye madhara, na kuwatenganisha na njia ya haki. Kazi ya malaika ni kuwashawishi watu kwenye haki, kheri, wema na kuwaweka mbali na makosa. Mwenye kusikia sauti nafsini mwake ikimshawishi kufanya mema, anatakiwa kujua kuwa hiyo ni sauti ya malaika. Atakiwa kuisikiliza na kumshukuru Allah. Mwenye kusikia nafsini mwake sauti ikimshawishi kufanya maovu, atambue kuwa hiyo ni sauti ya shetani. Yampasa asiisikilize sauti hiyo na ajilinde kwa Allah."

Tirmidhí, Tafsir, 3.

Allah Mtukufu ndiye Mwenye kutoa nguvu ya kufanya kazi. Hivyo, kila mafanikio hutoka Kwake. Mola wetu daima yu pamoja na watu wema na wanaofanya kazi kwa bidii. Kwa sababu anapenda kazi ya waja Wake na kuwapa kile wanachomuomba. Tunapokusudia kufanya jambo jema, Allah hutupatia msaada wake. Malaika alioivateua hukaa pamoja nasi na kutuhamasisha kwa mambo na mawazo mazuri. Wanafurahi tunapofanya mambo mazuri na yenye faida. Htuombea mafanikio kwa Allah. Kwa idhini ya Mola wetu, hutusaidia katika nyakati ngumu. Katika Qur'an Tukufu, tumeambiwa kuwa malaika elfu tano walitumwa kwenda kuwasaidia Waislamu, kuwapa habari njema za ushindi na kuwapa morale katika Vita ya Badr. Kuamini kwamba Allah Mtukufu atatumwa malaika kuja kutusaidia katika nyakati ngumu **hutuhamasisha kuendelea kufanya kazi na kutupatia nguvu chanya**. Hatuhisi mchoko wala kunyong'onyea tunapokabiliwa na shida.

### Allah Mtukufu anasema:

"Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremka Malaika wakawaambia: Msilogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyo kuwa mkiahidiwa. Sisi ni vivenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata kinacho tamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyo vitaka."

(Fussilat); 41:30-31)

## MALAIKA HUWAOMBEA WAUMINI

Malaika huwaombea Waislamu kuwa katika ulinzi dhidi ya maovu na dhambi na waweze kuufikia wema. Mola wetu Mtukufu anatueleza kuhusu jambo hili kama ifuatavyo:

"Wale wanao beba A'rshi, na wanao izunguka, wanamsabih na kumhimidi Mola wao Mlezi, na wanamuamini, na wanawaombea msamaha walio amini kwa kusema: Mola wetu Mlezi! Umekienea kila kitu kwa rehema na ujuzi. Basi wasamehe walio tubu na wakaifuata Njia yako, na waepushe na adhabu ya Jahannamu. Mola wetu Mlezi! Na waingize katika Bustani za Milele ulizo waahidi. Na uwape haya pia wale walio fanya mema miongan mwa wazee wao na wake zao na dhuriya zao. Hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima. Na waepushe na maovu; kwani umwepushaye maovu siku hiyo, hakika umemrehemu; na huko ndiko kufuzu kukubwa."

(Surah Mumín , 40: 7-9)

Unataka kuombewa dua na Malaika?

### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Dua ambayo Muislamu humuombea ndugu yake Muislamu akiwa hayupo, ni yenye kukubaliwa. Muislamu huyo anapomuombea nduguye katika dini, malaika aliyeteuliwa kuwa pamoja naye huomba kwa kusema: 'Allah aikubali dua yako! Nawe pia upewa hayo uliyoomba.'"

(Tirmidhi, Tafsir, 3)



Tunapoomba dua malaika huitikia kwa kusema 'Amiin'

### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

Mtume wetu (s.a.w) alituusia kuomba dua kila wakati, na kutupa habari njema kuwa malaika huitikia kwa kusema 'amiin' kila tunapoomba duna. Alituusia kuomba mambo mazuri kutoka kwa Allah:

"Mnapoomba, ombeni mambo mema na ya kheri, kwa maana malaika husema 'amiin' mnapoomba dua zenu."

(Tirmidhi, Tafsir, 3)



## MALAIKA HUWAOMBEA WANAOTAFUTA ELIMU

Mtume wetu (s.a.w) anatueleza kuwa malaika huwaombea dua maalumu waumini wanaotafuta elimu na wanaofanya juhudzi za kuyatekeleza kwa vitendo yale waliyojifunza:

"Mwenye kusafiri kwa ajili ya kutafuta elimu, Allah humrahishisha kuingia Peponi.

Malaika hufurahishwa sana na kitendo hicho. Huwakinga kwa mbawa zao wale wanaotafuta elimu. Kila kitu mbinguni na ardhini, hata samaki baharini humuombea maghfira mtu huyo."

(Abu Dawud, Ilm, 1)



# MALAIKA, SHETANI NA MWANADAMU

Mwanadamu alikuwa bado kuumbwa. Allah akataka kumuumba mwanadamu ili amjue na kumuabudu. Akawaambia malaika:

— Nitamuumba khalifa na kumuweka ardhini.

Malaika wakasema:

— Mola wetu, utamuumba atakayesababisha matatizo na umwagaji damu? Daima tunasabihî na kukutii.

Allah akasema:

— Ninajua msiyoyajua.

Malaika wakakaa kimya. Kisha wakaambizana:

— Hakika Mola wetu ni mjuzi wa kila kitu, na haumbi vitu bila sababu.

Kisha Allah akawaambia:

— Enyi malaika! Nitamuumba mwanadamu kutokana na udongo na kumpa uhai. Mpeni heshima inayomstahiki na msujudu mbele yake kwa kutekeleza amri yangu.

Malaika wote wakasema:

— Mola wetu! Tumetii amri zako na kuzitekeleza.

Shetani hakuipenda amri hii ya Allah. Alikuwa na kiburi na kujiona kuwa yeye ni bora zaidi ya viumbwe vyote vilivyoumbwa na Allah.

Hatimaye Allah alimuumba mwanadamu. Katika kutii amri ya Allah, malaika walionesha heshima kwa Adam na kusujudu mbele yake. Shetani alitakabari na kuasi. Hakuusujudu mbele ya Adam. Kwa kitendo hiki, alimuasi Allah. Allah akamwambia Shetani:

— Kwanini hukunisikiliza? Kipi kilichokufanya usisujudu?

Shetani akasema:

— Umeniumba kwa moto na yeye umemuumba kwa udongo. Mimi ni bora kuliko yeye.

Hapo Allah akamfukuza mbele Yake.

Baadaye, Allah alimuweka Adam katika Pepo na kumuumba Hawa kama mkewe. Akamwambia Adam:

Ewe Adam! Wewe na mkeo mnaweza kuishi katika Pepo. Mnaweza kula chochote mkitakacho. Lakini, msiukurubie mti huu; vinginevyo mtakuwa mionganî mwa wale waliozidhulamu nafsi zao.

Allah Mtukufu aliwaruhusu kula chochote isipokuwa mti mmoja. Kwa namna hii, alikuwa akimfundisha mwanadamu kuyadhibiti matamano yake na kuimarisha hali yake ya kujidhubiti.

Adam na Hawa walikuwa wakiishi katika Peponi kwa amani. Hawakujua kitu kinachoitwa mchoko au khofu. Walikuwa wakila kila wanachotaka. Allah Mtukufu alimtahadharisha Adam kuhusu Shetani.

— Ewe Adam! Hakika Shetani ni adui yako wewe na mkeo. Tahadhari asikutoeni katika Pepo. Vinginevyo mtakuwa wenye majuto. Mkikaa Peponi hamtahisi njaa wala kuwa watupu. Katika Pepo hamtapatwa na joto wala kuhisi kiu.

Adam na Hawa wakiishi katika Pepo kwa muda fulani. Lakini, Shetani alikuwa akipanga

mipango mibaya. Siku moja aliwakaribia na kusema:

— Ewe Adam! Nikuonesheni mti wa uhai na ufalme wa milele?

Adam alimtazama Shetani na kusema:

— Mti gani huo? Tuuone.

Shetani alipowaonesha mti ambao Allah aliwakataza, Adam hakumuamini, akamfukuza.



Hata hivyo, Shetani hakukata tamaa. Alikuja kwa mara nyingine na kuwaambia:

— Mnajua kwa nini Mola wenu aliwakataza kula katika mti huu? Mkila matunda yake mtaishi hapa milele. Ili hilo lisitokee, aliwakataza msile matunda yake. Fikirieni vizuri, kuleni katika mti huu sasa!

Adam na Hawa hawakumsikiliza Shetani. Waliondoka, Shetani akawafuata. Aliapa kwa jina la Allah na kusema:

— Amini, ninawapa ushauri mzuri.

Shetani alipoapa kwa jina la Allah, Adam na Hawa waliambizana:

— Haiwezekani mtu aape kwa jina la Allah awe anasema uongo. Huwenda anachosema ni kweli. Wakaanza kula matunda ya mtu waliokatazwa na Allah.

— Walipoanza kula mti huo, mavazi ya Peponi yakaondolewa katika miili yao wakabaki watupu, wakaona aibu mno. Walijaribu kujifunika kwa majani makubwa ya miti. Hawakuja la kufanya.

Allah akasema:

— Je sikuwakatazeni kula matunda ya miti? Sikuwambieni kuwa Shetani ni adui yenu? Kwa nini hamkusikiliza amri zangu?

Adam na Hawa wakasema:

— Mola wetu! Tusamehe.

Allah akawaambia:

— Niliwaamuru lakini hamkutii amri zangu.

Adam na Hawa wakaomba:

— Mola wetu! Tumezidhulumu nafsi zetu. Usipotusamehe na kutuhurumia, tutakuwa mionganoni mwa waliopotea.

Allah akamwambia Adam:

— Nilikupeni neema yangu kubwa kabisa, Pepo. Nikakupeni kila mlichotaka. Je, nilichokupeni hakikuwatoshha mpaka mkale katika mti ule?

Adam akasema:

— Ninaapa kuwa sikufikiria kuwa mtu angesema uongo na kuapa kwa jina Lako.

Allah Mtukufu akamwambia Adam aliyekuwa akiomba:

— Ninaapa kuwa mtaenda ardhini. Mtakaa na kuishi huko kwa muda.

Adam alihuzunika sana, akaanza kulia na kusikitika kwa aliyoafanya. Aliomba:

— Mola wangu, Nisamehel! Mola wangu, nisamehe!

Hatimaye Allah alimsamehe kwa kukubali dua yake. Ndio maana Allah huwasamehe wale wanaojutia waliyoyafanya na kutubu kwa kuomba msamaha. Hakika Yeye ni Msamehevu.

(Visa vya Kidini kutoka ndani ya Qur'an Tukufu, Sayyid Qutub – Abdullah Judah as-Sahhar)

(Kwa ayah zinazohusu kisa hicho ndani ya Qur'an tazama: Al-Baqara, 2: 3-37 na A'raf, 7: 11-25)

## SHETANI

Miongoni mwa viumbe wasioonekana ni Shetani. Jina jingine la Shetani katika Qur'an Tukufu ni Iblis. Shetani alifukuzwa mbele ya Allah baada ya kuasi amri ya Allah na kutomsujudia mtu wa kwanza, Adam. Aliumbwa kutokana na moto. Ni alama ya uovu.

Sababu ya Shetani kufukuzwa mbele ya Allah ni kiburi chake na uasi dhidi ya amri ya Allah. Hata hivyo, Shetani aligeuka kuwa adui wa wanadamu, akidai kuwa mwanadamu ndiye sababu ya yeye kuadhibiwa na Allah. Kwa sababu hiyo, Shetani hutumia kila aina ya uongo, mbinu na ulaghai kuwazuia wanadamu wasiipate njia sahihi. Shetani anataka watu wafanye dhambi kwa kuasi maamirisho ya Allah. Kwa kufanya hivyo, Shetani anataka kufanya kisasi kwa kuhakikisha kuwa Adam na kizazi chake wanaingia Motoni. Mola wetu anatutahadarisha kuhusu uadui na hila za Shetani:

**"Hakika She'ani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni."**

(Surah Fatir; 35: 6)

Shetani sio kiumbe mwenye nguvu ambaye tunatakiwa kumuogopa. Shetani anachofanya tu ni kuchochea hisia na fikra hasi ndani ya nyoyo zetu. Hutia wasiwasi katika nyoyo zetu. Shetani huyafanya mambo mabaya na maovu yaonekani kuwa ni mazuri. Hufanya juhud za kutufanya tumsahau Allah na Akhera. Wakati huo huo, sisi wanadamu tuna akili na uwezo wa kujidhibiti. Kwa sifa hizi, sisi tuna uwezo zaidi ya Shetani. Ingawa Shetani ana umbile tofauti na haonekani, hana uwezo wa kutusukuma kufanya makosa. Hawezi kutulazimisha kufanya makosa. Allah Mtukufu anatuahabarisha kuhusu jambo hili kama ifuatavyo:

### Allah Mtukufu anasema:

"Walimsjudia isipo kuwa Iblisi. Yeye alikuwa miongoni mwa majini, na akavunja amri ya Mola wake Mlezi..."

(Surah al-Kahf, 18: 50)

**"Hakika yeye hana madaraka juu ya walio amini na wakamtegemea Mola wao Mlezi. Hakika madaraka yake ni juu ya wanao mfanya rafiki yao, na wale wanao fanya ushirika naye."** (Surah Nahl; 16: 99-100)

Tukitumia akili zetu na uwezo wetu wa kujidhibiti, bila kushawishiwa na hisia na fikra tunazoingiziwa na Shetani, hatutafanya matendo mabaya na maovu. Hivyo, tutashinda vita baina ya Shetani na mwanadamu. Hata hivyo, yatupasa tuisahau kuwa vita hii sio ya mara moja. Hii ni vita itakayoendelea mpaka mwisho wa uhai wetu.



## KUKIRI KWA SHETANI

Na Shetani atasema itapo katwa hukumu: "Hakika Mwenyezi Mungu alikuahidini ahadi ya kweli. Nami nilikuahidini; lakini sikukutimizieni. Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipo kuwa nilikuitenii, nanyi mkaniitikia. Basi msinilaumu mimi, bali jilaumuni wenyewe. Mimi siwezi kuwa

mtetezi wenu, wala nyinyi hamwezi kuwa watetezi wangu. Hakika mimi nilikataa tangu zamani kunishirikisha na Mwenyezi Mungu. Hakika madhaalimu watakuwa na adhabu chungu."

(Surah Abraham; 14: 22)

### Allah Mtukufu anasema:

"Na Shetani akikuchochaea kwa uchochezi wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua."

(Surah Fussilat; 41:36)

## NINAJILINDA KWA ALLAH DHIDI YA SHETANI

### Allah Mtukufu anasema:

"Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko, Na shari ya alivyo viumba, Na shari ya giza la usiku liingiapo, Na shari ya wanao pulizia mafundoni, Na shari ya hasidi anapo husudu."

(Surah Faqqaq, 113: 1-5)

### Allah Mtukufu anasema:

"Sema: Ninajikinga kwa Mola Mlezi wa wanaadamu, Mfalme wa wanaadamu, Mungu wa wanaadamu, Na shari ya wasiwasi wa Shetani, Khannas, Anaye tia wasiwasi katika vifua vya watu, Kutokana na majini na wanaadamu."

(Surah An-Nas; 114: 1-6)

## SWAHABA WA MTUME (S.A.W) AMBAYE JENEZA LAKE LILIBEBWA NA MALAIKA

Salama bin Aslam (r.a) anasimulia:

Swahaba mmoja wa Mtume (s.a.w) aitwaye Sa'd bin Muadh (r.a) alifariki dunia. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipopata taarifa hizo mbaya za Sa'd, alienda nyumbani kwake pamoja na maswahaba. Mtume (s.a.w) alikuwa mbele yetu nasi tulikuwa tukimfuata. Tulifika mlangoni na Mtume (s.a.w) akaingia ndani. Chumbani hakuwemo mtu yeyote isipokuwa jeneza la Sa'd bin Muadh. Lakini, Mtume (s.a.w) alikuwa akitembea kwa uangalifu kana kwamba kuna watu ambaa anahofu kuwakanyaga. Alipoona kuwa ninataka kuingia chumbani, aliniashiria kwa mikono yake kuwa nibaki nilipokuwa. Nilisimama na kuwaashiria wenzangu waliokuuwa nyuma yangu nao wasimame.

Mtume (s.a.w) alipotoka ndani, nilisema "Ewe Mjumbe wa Allah! Sikuona mtu yeyote. Lakini ulikuwa ukitembea kana kwamba unajaribu kupita katikati ya mabega ya watu wengine". Mtume (s.a.w) akasema: "Malaika elfu sabini ambaao hawakuwahi kuja ardhini walikuja kulibeba jeneza la Sa'd. sikupata sehemu ya kukaa. Malaika mmoja alinipisha sehemu ya kukaa, hivyo nikaweza kukaa."

Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa na furaha mno kwa daraja ambayo Sa'd bin Muadh (r.a) alikuwa amefikia, na mara kwa mara akisema kumhusu "Ewe Aba Amr! Hongera sana! Ewe Aba Amr! Hongera sana! Ewe Aba Amr! Hongera sana!"

(Ibn Sa'd, III, 428-430)

*Tuishi maiša ambayo majeneza yetu  
yatagata fursa ya kubebwa na malaika.*



# MTUME (S.A.W) NA MALAIKA

Malaika walioonesha heshima kwa Adam humuheshimu kila Muislamu anayetokana na kizazi chake. Vilevile wanawapenda watu wema ambao Allah Mtukufu anawapenda. Hivyo, malaika huwapenda na kuwaheshimu zaidi mitume.

Mtume Muhammad (s.a.w) ndiye mtume wa mwisho aliyetumwa na Allah kwa wanadamu. Aliteuliwa na Allah ili awe mfano bora na mzuri kabisa kwa wanadamu. Alikuwa na tabia njema ambazo zinaweza kutamaniwa na malaika. Allah alimpenda na akawafanya waja Wake wampende pia. Malaika walimpenda Mtume (s.a.w) tokea utotoni na kupeana habari njema za utume wake.

Mawasiliano ya kina katì ya Mjumbe wa Allah (s.w) na malaika yalianza kwa ufunuo wa Qur'an Tukufu. Mtume wetu (s.a.w) alikuwa na umri wa miaka arobaini. Alikuwa na kawaida ya kwenda katika pango la Hira na kukaa huko kwa siku kadhaa. Huko alikuwa akitafakari kuhusu Mwenyezi Mungu na kutaamali kwa kina juu ya ulimwengu na hali ya binadamu. Siku moja akiwa pangoni, Allah alimtuma malaika Jibril (a.s). Malaika huyo alimtaka Mtume wetu (s.a.w) asome. Mtume (s.a.w)

akamwambia Jibril (a.s) kuwa hajui kusoma. Jibril (a.s) akarudia kumwambia kuwa asome. Alimwambia hivyo mara kadhaa. Alipopata jibu hilo hilo, Jibril (a.s) alisoma ayah za kwanza za Qur'an. Baada ya kupokea ufunuo wa kwanza, Mtume wetu (s.a.w) alitoka pangoni na kumuona Jibril (a.s) akiwa amefunika mbingu yote kwa mbawa zake. Kwa miaka ishirini na tatu baada ya ufunuo huu wa kwanza, Jibril (a.s) alikuja kwa Mtume wetu (s.a.w) mara nyingi, na kumfunulia ayah na surah za Qur'an Tukufu, kwa maneno mengine, alimletea ujumbe mbalimbali kutoka kwa Allah Mtukufu.

Kila mwaka, katika mwezi wa ramadhan, Mtume (s.a.w) alikuwa akimsomea Jibril (a.s) ayah zote alizomteremshia mpaka wakati huo. Katika mwaka wake wa mwisho, aliisoma Qur'an yote mara mbili akiwa pamoja na Jibril (a.s).

Wakati mwagine Jibril (a.s) alikuwa akija kwa Mtume wetu (s.a.w) katika sura na umbile la kibinadamu. Siku moja, wakati Mtume wetu



(s.a.w) akiwa pamoja na Maswahaba zake, Jibril (a.s) alikuja akiwa amevaa mavazi meupe, masafi. Aliuliza maswali mbalimbali kuhusu imani, Uislamu, ihsani na siku ya hukumu. Baada ya kujibiwa, akatoweka. Mtume wetu (s.a.w) akawaambia Maswahaba kuwa mtu huyo alikuwa malaika Jibril (a.s) na alikuja kuwafundisha maarifa mbalimbali kuhusu dini.

Ili kumfanya Mtume (s.a.w) ajisikie vizuri na kumuunga mkono, Allah Mtukufu alikuwa akimtumia malaika katika nyakati ngumu. Mfano mzuri wa hili ulionekana wakati wa kuhamia Madina (Al-Hijrah). Washirikina wa Makka walikuja mbele ya pango ambalo Mtume (s.a.w) alikuwa amejificha. Kama wangesogea mbele kidogo, wangemuona. Allah Mtukufu aliujaalia moyo wa Mtume wetu (s.a.w) amani na utulivu. Alimuunga mkono kwa majeshi ya malaika yasiyoonekana.

Allah Mtukufu alimsaidia Mtume (s.a.w) na Maswahaba zake kwa kutuma jeshi la malaika katika Vita vingi kama vile Vita vya badr. Katika Vita ya Hunayn, ambapo Waislamu walikuwa katika hali ngumu sana, Allah alituma jeshi la malaika kuja kuwasaidia Waislamu.

Mtume wetu (s.a.w) alikuwa akisema kuwa malaika huja katika maeneo ambayo watu hufanya mambo yao kwa mujibu wa maamrisho ya Allah. Alitueleza kuwa malaika huja katika maeneo ambayo elimu hufundishwa, Qur'an husomwa, Allah huabudiwa na matendo mema hutendeka. Alitupa habari njema kuwa malaika huwaombea wale wanaohudhuria katika maeneo hayo na kuleta amani na furaha katika nyoyo zao. Alituusia kujitenga na matendo ambayo yanawaudhi malaika na pia alikuwa makini kutoyafanya matendo hayo. Hakutaka wale wanaokula vyakula vyenye harufu kali, kama vile vitungu, kuingia msikitini

mpaka harufu yao isafike. Alieleza kuwa watu na malaika hawatakiwi kubughudhiwa.

Mtume wetu (s.a.w) alitumwa kuwa rehma kwa ulimwengu wote. Mola wetu, ambaye aliiyanyua darja yake kwa rehma na ridhaa Yak, aliwafanya malaika wampende pia na kuwataka wamtakie rehma (salawat). Kwa sababu hii, humtakia rehma na kumuombea darja yake inyanyuliwe. Kuna hata malaika ambaeo wamepewa jukumu maalumu la kuweka kumbukumbu za waumini wanaomtakia rehma Mtume (s.a.w) na kuzifikisha kwake.

#### Allah Mtukufu anasema:

“...hakika Mwenyezi Mungu ndiye kipenzi chake, na Jibrili, na Waumini wema, na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia.”



(Surah At-Tahrim ); 66:4)

## MSAADAA UNAOLETWA NA MALAIKA

Vita vya Badr ni vita vya kwanza baina ya Waislamu na makafiri wa Makka. Idadi ya askari wa kikafiri walikuwa Badr ilikuwa mara tatu zaidi ya ile ya jeshi la Waislamu. Walikuwa wamepanga kuwaangamiza Waislamu wote kwa pamoja.

Vita vilanza na majeshi ya pande mbili yalikuwa yakipambana. Waislamu walikuwa wakipambana kwa bidii na nguvu zote. Mtume wetu (s.a.w) alinyanya mikono yake kuelekea Mbinguni na kuomba akisema: "Mola wangu! Leo Maqrayshi na jeshi lao lote wanataka kuiangamiza dini Yako. Wanapingana na Wewe. Wanamkataa Mtume Wako. Ewe Allah! Ninakuomba utimize ahadi Yako kuwa utawasaidia mitume Wako. Tunakuomba utupe ushindi. Iwapo watu hawa wachache watauawa, hakuna mtu ardhini atakayekuabudu na kukutii."

Allah Mtukufu alijibu dua ya Mtume wetu (s.a.w). Alituma makundi ya malaika katika nyakati ngumu za

vita hivyo. Aliwaunga mkono Waislamu kwa kutuma jumla ya malaika elfu tano. Waislamu walishinda vita. Ndani ya Qur'an Tukufu Mola wetu Mtukufu anauelezea msaada huo wa malaika alioutuma:

"Na Mwenyezi Mungu alikwisha kunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge... Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na illi nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipo kuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliye tukuka, Mwenye nguvu na Mwenye hekima."

(Surah Al-i Imran 3: 23-126)

### Allah Mtukufu anasema:

"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlilo amini! Msaleni na mumsalimu kwa salamu."

(Surah Al-Ahzab ; 33: 56)

Tumuombie Mtume (s.a.w) darja yake inyanyuliwe mbele ya Allah, kama wafanyakyo malaika. Tumtumie salamu na kumtakia rehma kwa kuzikabidhi katika mbawa za malaika wenyewe nuru.

### Dua hii inaitwa Salah Al-Ummiyah:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ النَّبِيِّ  
الْأُمِّيِّ وَعَلَى أَهْلِهِ وَصَحْبِهِ وَسَلِّمْ

Allahumma salli ala sayyidina Muhammadin Nabiyyil-ummiyyi wa ala alihi wa sahabih wa sallim.

Ewe Allah! Peleka rehma na amani kwa Mtume wetu Muhammad (s.a.w) ambaye hakusoma wala kuandika, kwa familia yake na kwa Maswahaba zake pia.

AMIIIN

## MASWALI

Jaza sehemu za wazi kwa maneno muafaka.

(amin/ Shetani/ andika/ malaika/ adui/ madaraka/ Sherani/ ushirika/ neno/ malaika/ adui)

1. "Kuna malaika wawili wanao....., wako upande wa kulia na kushoto kwa kila mtu. Wanawatazama wanadamu na kuandika kila..... wanalozungumza."
2. "Hakika..... ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni ..... Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni."
3. "Hakika yeye hana ..... juu ya walio amini na wakamtegemea Mola wao Mlezi. Hakika madaraka yake ni juu ya wanao mfanya rafiki yao, na wale wanaofanya ..... naye."
4. "Mnapoomba, ombeni mambo mema na ya kheri, kwa maana ..... husema ..... mnapoomba dua zenu."
5. "Mwenye kusikia sauti nafsini mwake ikimshawishi kufanya mema, anatakiwa kujua kuwa hiyo ni sauti ya..... Atakiwa kuisikiliza na kumshukuru Allah. Mwenye kusikia nafsini mwake sauti ikimshawishi kufanya maovu, atambue kuwa hiyo ni sauti ya ..... Yampasa asiisikilize sauti hiyo na ajilinde kwa Allah."



1- Ni sifa ipi kati ya hizi ambayo sio sifa ya malaika?

- a) Hali wala kunywa.
- b) Hawalali.
- c) Sio wanaume wala wanawake.
- d) Wana uwezo wa kumuasi Allah.

3-

- I- Huongeza utambuzi wa kuwa waja wa Allah
- II- Hutuhamasisha kufanya kazi kwa bidii
- III- Hutuweka mbali dhidi ya kutenda makosa
- IV- Huzitakasa tabia zetu

**Ni lipi kati ya haya ambalo sio mionganoni mwa faida za kuamini malaika?**

- a) I-II-IV
- b) I-III-IV
- c) I-II-IV
- d) I-II-III-IV

2- Ni lipi kati ya haya ambalo sio mionganoni mwa majukumu ya malaika?

- a) Kuwa mfano kwa wanadamu.
- b) Kuwalinda wanadamu.
- c) Kuwaombea waumini.
- d) Kupeleka ujumbe wa mitume.

4-

- I- Mikail
- II- Israfil
- III- Al-Munkar na Al-Nakir
- IV- Jibrail
- V- Azrail
- VI- Yunus

**Kati ya hao ni nani ambao sio mionganoni mwa malaika wa nne wakuu?**

- a) I -IV
- b) II-VI
- c) III-VI
- d) IV-V

5- Mara nyingi tunapotaka kufanya matendo mazuri, hujiwa na fikra zinazopingana. Shetani na malaika huchochea fikra ndani mwetu. Kati ya fikra hizi ni ipi inayotokana na Shetani?


- a) Ukitanya hivi, utajisikia amani na faraja moyoni mwako.
- b) Utakuwa mfano kwa wengine.
- c) Haitakunufaisha hapa duniani.
- d) Utapata upendo na thawabu za Allah.

Allah Mtukufu anasema:

**"Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi  
mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu."**

(Surah Al-Ahzab; 33:56)





MIIRAJ YA MUUMINI, NGUZO YA DINI YETU:

# SWALA (AL-SALAH)

- ✿ *Maana ya Swala*
- ✿ *Faida za Swala*
- ✿ *Aina za Swala*
- ✿ *Hukmu zinazobusu Swala*
- ✿ *Adhana na Iqaamah*

- ✿ *Jinsi ya Kuswali*
- ✿ *Swala ya Pamoja (Jama'ah)*
- ✿ *Swala ya Mgonjwa, Msafiri na Mwenye kulipa*
- ✿ *Kipaumbele cha Mtume (s.a.w) kwenye Swala*
- ✿ *Misikiti na Nyumba za Kuswalia*



## SWALA YA KWANZA

Ilikuwa asubuhi yenyе baridi sana. Nilikuwa nikitetemeka nilipoliacha joto la kitanda changu na kuva viatu vyangu vya wazi viliviyokuwa vimeshika baridi ya usiku.

Alfajiri ilikuwa hajiaingia. Nilichungulia dirishani sikuona mtu yeote katika Mnara wa Msikiti Mkongwe wenye kuchomoza na adhana ya kimaanawi kupita nyumba zote. Hapo, kivuli cha muadhini kijana kilionekana katika mnara. Nilivaa sweta langu zito. Nilipokuwa nikisikia sauti tamu na adhimu ya adhana iliyopenya moyoni mwangu, nilikumbuka swala zangu za alfajiri huko zamani nilizoanza kuziswali tangu miaka kumi na tano iliyopita. Ni miaka kumi na tano imepita tangu niliposwali swala yangu ya kwanza....

Mama yangu muadhamu ambaye ninampenda zaidi katika ulimwengu huu aliniamsha kwa ajili ya alfajiri yangu ya kwanza miaka kumi na tano iliyopita. Nadhani kilikuwa kipindi cha baridi kama hiki. Nilipokuwa nimelala katika chumba changu ambacho kilikuwa mkabala na chumba chake, alikuja na kuzishika nywele zangu kwa vidole vyake vizuri na maridhawa na kuniambia:

"Mwanangu kipenzi, amka!  
Amka mwanangu!"

Niliyafumbua macho  
yangu na kusema:



"Lakini mama bado ni usiku...."

Baada ya kunibusu kwenye paji langu la uso kama aliviyokuwa akifanya kila siku, alinisaidia kuamka kwa kunishika mikono yangu ili muda wa swala usinipite. Nilivaa viatu vyangu vidogo, nikayafikicha macho yangu na kumfuata. Tulipita ukumbini na kufika chumbani kwa mama yangu. Jiko la gesi chumbani kwake lilikuwa likiwaka kwa nguvu, nikasema:

"Alaa... Hadija naye yuko macho....!"

Hadija alikuwa akiipua birika kutoka jikoni. Sikuwaza kama atakuwa macho. Lakini mama akaniambia:

"Hadija huamka kila siku asubuhi."

Ingwa sikuwa nimeamka mapema sana, lakini nilishangaa kusikia kuwa huwa anaamka kila siku asubuhi. Walinisaidia kuvua sweta langu, nikaelekea sehemu ya kutawadha. Mama akaniambia:

"Unaonekana kama umechoka", akanipatia stuli ndogo nikakaa. Baada ya kumaliza kutawadha, nilikaa karibu na jiko ili kupata joto. Nilipogeuka nilimuona mama akitandika mswala... kisha alivaa mtandio wake wa kijani na kuniita:

"Njoo hapa mwanangu..."

Nilienda na kusimama pembezoni mwa mama yangu mpendwa kwenye mswala aliokuwa akiswalia.

Nilikuwa nikifuata kila anachokifanya. Hivyo bila kujua, nilikuwa nikiswali kama mwanamke anavyoswali. Baada ya kumaliza kuswali sunnah, alitabasamu na kuniambia:



"Mwanangu! Wewe sio mwanamke! Wanawake ndio wanaswali hivyo... unapaswa kuswali kama mwanaume," akanionesha jinsi wanaume wanavyopaswa kuswali.

Nilifanya kila alichoniambia na kukamilisha swala yangu. Niliinua mikono yangu midogo na kumuuliza mama yangu:

"Mama! Niseme nini katika dua?"

Mama yangu akaniambia niseme:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninakuhimidi kwa kunijaalia kuwa Muislamu. Ninakuomba uilinde nchi yetu dhidi ya maadui. Ninakuomba uwape afya na ustawi waumini wenye shida, wenye maradhi, wanaokabiliwa na majanga na umaskini."

Kisha mama yangu aliniusia nimuombe Mwenyezi Mungu anijaalie kuwa mtu mwema nisiyeweza kuhadaiwa na hila za Shetani....

Baada ya swala mama aliniuliza iwapo nilitaka kulala au la. Sikuwa na usingizi, hivyo akaniambia:

"Kalete kitabu chako tuangalie kazi yako ya nyumbani uliyopewa na mwalimu".

"Sawa", nilijibu.

Nilipita ukumbini haraka, nikachukua kitabu kwenye meza yangu na kurudi haraka kwa mama. Alipoangalia majibu yangu hakuona kosa lolote. Wakati wa usiku mama yangu alikuwa na mazoea na kuniambia:

"Mwanangu, pitia somo lako mara tatu kabla ya kulala, ili malaika wakufundisha ukiwa usingizini."

Malaika walikuwa wamenifundisha masomo yangu usiku huo pia. Mama alizigusa nywele zangu na kuniambia, "vizuri sana mwanangu". Kwa kuwa bado ulikuwepo muda wa kutosha kabla ya kwenda shule, hivyo nilijilaza kitandani kwake.

Nilikuwa sijasinzia kabisa, nikawa namtazama mama yangu. Akiwa amevaa mtandio wake wa kijani aliichukua Qur'an Tukufu na kutembea kidogo, nilimuona kana kwamba

niko ndotoni. Alikaa kwenye sofa iliyokuwa jirani na dirisha akaanza kusoma kwa sauti nzuri. Sauti yake maridhawa, ambayo iliachaa athari moyoni mwangu, wajhi wake wenye nuru akiwa ndani ya mtandio mkubwa wa kijani, vilinifanya nisinzie. Nilikuwa nikimfananisha na malaika wakati anapoinamisha kichwa chake wakati wa swala na dua. Mawazo ya kwanza malaika walikuwa wamemzunguka mama wakati akisoma Qur'an Tukufu yalinifanya nichukuliwe na usingizi mtamu, nikalala...

**ÖMER SEYFETTİN**  
(Kimenukuwa kwa mukhtasari)

## SWALA NI NINI?

Kila kiumbe ulimwenguni humuabudu na kumhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa namna yake. Swala ni ibada inayojumuisha vipeengele mbalimbali kutoka kwenye ibada na himidi za viumbwe wote. Kwa kuwa ni ibada muhimu sana katika Uislamu, Mtume wetu (s.a.w) aliita kuwa ni "nguzo ya Uislamu."

Swala ambayo hujumuisha dua na kuomba mambo mema, ni "Mi'raj ya muumini kuelekea Mbinguni". Kwa maneno mengine, ni wakati ambaao muumini hukutana na Mola wake. Kwa kutumia swala, hufika mbele ya Mwenyezi Mungu mara tano kwa siku na kuonesha utii wetu Kwake na kukumbuka kuwa daima tunamhitajia.

Swala ni njia ya kuonesha shukrani zetu kwa Mwenyezi Mungu. Kupitia swala tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na Baraka zote anazotujaalia na kumuonesha upendo na utiifu

wetu Kwake; kwa sababu swala ndio njia tukufu kabisa ya kuonesha heshima.

Swala ina maana ya kumuomba dua Mwenyezi Mungu, kumtaka msaada na kumuomba atusamehe dhambi na makosa yetu.

Kwa muhtasari, swala ni nguzo ya dini yetu na ni nuru ya nyoyo zetu. Swala ndio uhai wa ulimwengu wetu wa kiroho. Wakati ikitutakasa kimwili, hutuimarisha utambuzi wetu wa kiroho.

Mtume wetu mpendwa anasema:

"Swala ni nuru katika moyo wa mtu. Yeyote mionganini mwenu anayetaka kupata nuru basi aung'arishe na kuongeza nuru ya moyo wake kwa swala."

(Tirmizi, Deavât 85)

## KWA NINI TUNASWALI?


Kutekeleza ibada ya swala ni dhima yetu kwa Muumba wetu anayetupatia uhai. Tunaswali ili kuwa karibu zaidi na Muumba wetu na kumuonesha upendo wetu Kwake.

Mola wetu ametujaalia Baraka na neema zisizokuwa na kikomo. Tunapaswa kumshukuru kwa Baraka hizo. Tunaswali ili kumshukuru kwa Baraka zote hizo anazotujaalia.

Shukrani inatakiwa kufanyika kwa mujibu wa neema husika. Tunapotoa Zaka tunakuwa tumemshukuru Mwenyezi Mungu kwa Baraka na mali anazotuneemeshi. Tunapofunga tunakuwa tumemshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya afya na vyakula mbalimbali. Tunaposwali tunakuwa tumeonesha shukrani zetu kwa njia bora kabisa na kumhimidi Mola wetu aliyetumba kama wanadamu na pia kutekeleza wajibu wetu wa kumshukuru kwa

kutujaalia neema mbalimbali. Mtume wetu (s.aw) anasema: "**Kila kiungo na mfupa katika mwili wa kila mmoja wenu hutoa sadaka. Kila neno la kumtakasa Mwenyezi Mungu ni sadaka. Kila neno la kumhimidi ni sadaka, kila neno la kukiri Umoja Wake ni sadaka, kila neno la kukiri Ukuu Wake ni sadaka, kuamrisha mema ni sadaka, kukataza mabaya ni sadaka, na rakaa mbili anazoziswali kabla ya adhuhuri hutoshaleza yote.**" (Muslim, Musafirin 84)

Tunatakiwa kusikiliza wosia na ushauri wa Mtume wetu (s.a.w), tuswali mara kwa mara. Hivyo, tunapaswa kumuonesha Mwenyezi Mungu ni kwa kiasi gani tunampenda, na tunapaswa kumshukuru kwa neema alizotujaalia, hususani neema ya mwili.



### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Ushike Sala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi."

**Surah Taha, Ayah ya 14**

### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Enyi mlion amini! Rukuuni na msujudu, na muabuduni Mola wenu Mlezi, na tendeni mema, ili mfanikiwe."

**(Hajj, 22:77)**

## FAIDA ZA SWALA

Swala tunazozitekeleza zina faida nyingi sana kwenye miili, roho na maisha yetu ya kijamii. Baadhi ya faida hizo ni hizi zifuatazo:

### Swala hutupatia uhakika wa kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa njia bora

Mola wetu Mtukufu anatuambia kuwa "kwa kumtaja na kumdhukuru nyoyo hupata utilivu!" Kwa sababu kumkumbuka Mola wetu tunayempenda sana na kulidhukuru jina Lake huzituliza nyoyo zetu zenye shida, kuvipa faraja vifua vyetu na kuzipa utuvu nafsi zetu.

Njia bora kabisa ya kumkumbuka na kumdhukuru Mwenyezi Mungu ni kutekeleza ibada ya swala. Kila swala tunayoitekeleza hutukumbusha kuhusu Mola wetu. Hivyo, swala ni tunu kubwa tuliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kuto-kana na kujua thamani ya neema hii, Mtume wetu (s.a.w) alikuwa akiitumia vizuri kila fursa inayopatikana kwa ajili ya swala. Alielezea furaha na amani anayoipata wakati wa kuswali: "Furaha yangu inapatikana ndani ya swala."

### Swala hutukumbusha juu ya Siku ya Hukumu na Akhera

Duniani kuna mambo mengi ambayo huwafanya watu waisahau Akhera. Wale wanaoisahau na kutowaza kuwa wataulizwa kwa matendo yao hufanya kila aina ya maovu. Hivyo, watu wanatakiwa kufanya kitu kitakachowakumbusha juu ya uwepo wa Akhera.

Swala tunazozitekeleza kwa umakini na utambuzi hutukumbusha kuhusu Mwenyezi Mungu, Akhera na Siku ya Hukumu mara tano kwa siku. Tunapokumbuka kuwa kuna Akhera na Siku ya Hukumu, hujiepusha na maovu. Hatutawadhuru watu au mali zao, na hatutamdhulumu yeyote.

### Swala huziondoshya dhambi zetu

#### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Enyi mlilo amini! Takeni msaada kwa subira na Sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri."

(Al-Baqara, Ayah 153)

#### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!"

(Ar-Ra'd, Ayah 28)

#### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na shika Sala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana. Hakika mema huondoa maovu. Huu ni ukumbusho kwa wanao kumbuka."

(Hud, Ayah 114)

#### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu."

(Ankebut, Ayah 45)

Swala ni wakati maalumu wa kukutana na Muumba wetu. Tunapokuwa katika swala huwa tuko mbele ya Mola wetu Mtukufu. Tunapotaka kutenda dhambi hubadilisha mawazo yetu kwa kukumbuka kuwa muda si mrefu tutaenda kuswali na kusimama mbele ya Mola wetu. Hivyo tutazitakasa nyoyo zetu dhidi ya hisia na mawazo mabaya na kuviepusha viungo vingine vya miili yetu kama vile mikono na ndimi zetu dhidi ya makosa na dhambi mbalimbali.

#### **Swala huimarisha maadili yetu mema**

Swala ni fursa adhimu inayotufanya kutambua makosa yetu na kumuomba msamaha Mwenyezi Mungu kwa kufanya toba. Tunaposwali huwa tunamuomba Muumba wetu msamaha na maghfira. Tunasimama mbele ya Mwenyezi Mungu mara tano kwa siku, tuktambua kuwa anajua kila kitu tunachokifanya, hivyo tunakuwa makini sana na matendo yetu. Kwa namna hiyo, huwa watu wema wenye maadili mema na yenye kupendeza.

#### **Swala huzifanya siku zetu kuwa zenye kheri na Baraka zaidi**

Tunaposwali mara kwa mara, huzipangilia shughuli zetu za kila siku kulingana na nyakati za swala. Tunaamka alfajiri kabla jua halijachomoza na hivyo kuanza shughuli zetu mapema. Wakati wale wasioswali wakiwa bado wamelala, sisi tunakuwa tumekamilisha baadhi ya kazi zetu. Kwa kufanya hivyo tunakuwa tumenufaika na dua ya Mtume (s.a.w):

"Ewe Mola wangu! Zibariki nyakati za mapema za umma wangu."

Swala za adhuhuri na alasiri ambazo huswaliwa nyakati zenye mishughuliko mingi zaidi, hupata fursa ya kumkumbuka Allah na kuzipumzisha nafsi zetu. Hupata fursa ya kumpumzika kwa kuswali, akili zetu hupata utulivu na kupata nguvu mpya kwa ajili ya kuendelea na kazi. Hivyo hupata ufanisi kazini.

Swala ya magharibi na Isha hutupatia fursa ya kutafakari juu ya shughuli zetu za siku nzima. Hivyo, huenda kulala tukiwa na amani kwamba tumetekeleza majukumu na dhima yetu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

#### **Swala hutufanya tuwe na mazoea ya kuwa wasafi**

Tunapochukua wudhu kwa ajili ya swala huosha viongo vya miili yetu vinavyochafuka zaidi wakati wa shughuli zetu za kila siku. Swala hutupa fursa ya kuifanya miili, mavazi na maeneo yetu ya kuswalia kuwa katika hali ya usafi. Kwa kufanya wudhu mara kadhaa kwa siku, mikono, nyuso na miguu yetu huwa safi. Jambo hilo hutujengea mazoea ya kuwa wasafi.



Siku moja Mtume (s.a.w) aliwaauliza Maswahaba:

"Iwapo mbele ya mlango wa mmoja wenu kuna mto unaopita na akawa anaoga humo mara tano kwa siku, je atabaki na uchafu wowote?" Maswahaba wakajibu,

"Hatobaki na alama yoyote ya uchafu." Mtume (s.a.w) akasema:

"Huu ni mfano wa swala tano ambazo Allah amezifanya kuondosha matendo maovu." (Bukhari, Mevakit; 6)

## NANI ANAYEWAJIBIKA KUSWALI?

Swala tano za kila siku zilifaradhihwa kwetu Usiku wa Mi'raj (yaani safari ya Mtume kwenda mbinguni). Swala tano ni faradhi kwa Muislamu aliyefikisha umri wa baleghe na akawa mzima wa akili.

Swala ni mionganini mwa maamrisho ya wazi kabisa ya Mwenyezi Mungu. Wale wanaoamini kuwa ni faradhi lakini wakawa hawaswali kwa kuzembea huwa wamefanya dhambi kubwa.

Dini yetu inatutaka tuwatengenezee mazoea watoto wetu ya kuswali wakiwa katika

umri mdogo. Mtume wetu Mtukufu (s.a.w) anatuusia kuwafundisha watoto wetu jinsi ya kuswali wanapofikia umri wa miaka saba. Pia alisisitiza tuwahimize juu ya umuhimu wa kuswali mara kwa mara kuanzia umri wa miaka kumi.



Mtume wetu mpendwa anasema:

"Amali ya kwanza atakayoulizwa Siku ya Qiyama ni swala. Iwapo swala zake zitakubaliwa, basi atafurahi na kupata thawabu. Iwapo swala zake zisipokubaliwa, atakhasirika na kujuta."

(Tirmidhi, Mawaqit 188)



## AINA ZA SWALA

Kiujumla swala zimegawanyika katika mafungu mawili: Za faradhi na za Sunnah.



### A. SWALA ZA FARADHI

Kuna aina tatu ya swala za faradhi.

#### 1. SWALA TANO ZA KILA SIKU

- a) **Swala ya al-Fajr:** Ina rakaa mbili.
- b) **Swala ya Adhuhuri:** Ina rakaa nne.
- c) **Swala ya Al-Asr:** Ina rakaa nne.
- d) **Swala ya Maghrib:** Ina rakaa tatu.
- e) **Swala ya Al-'Isha:** Ina rakaa nne.


## Idadi ya rakaa katika swala za kila siku

	Sunnah Muakkad	Sunnah zisizokuwa Muakkad	Faradhi	Sunnah Muakkad	Sunnah zisizokuwa Muakkad	Jumla
AL-FAJR	2	-	2	-	-	4
ADHUUHURI	2	2	4	2	2	12
ALASIRI	-	4	4	-	-	8
MAGHRIBI	-	2	3	2	-	7
ISHAA	-	2	4	2	2	10
WITRI	Kiwango cha chini 1 Kiwango cha juu 11					1 ya 3

**2. Swala ya Ijumaa:** Ni swala inayoswaliwa siku za Ijumaa mchana badala ya swala ya Adhuhuri.

Katika swala hii hakuna sijda wala rukuu. Ni swala ya faradhi kwa Umma wote kwa pamoja (Fardh al-Kifai).

**3. Swala ya Maiti:** Ni swala inayoswaliwa kwa ajili ya kuwaombea marehemu Waislamu.



### SWALA ZA SUNNAH:

Sunnah Ni swala ambazo Mtume wetu (s.a.w) aliziswali mara kwa mara mbali na swala za faradhi. Zipo na namna mbili, kwa kuswaliwa pamoja na swala za faradhi:

**1. Zile zinazoswaliwa pamoja na swala za faradhi (Rawatib):** Hizi ni swala za Sunnah ambazo huswaliwa kabla au baada ya swala za Faradhi.

**a) Rakaa za Sunnah za swala tano:** Hizi ni swala za sunnah ambazo huswaliwa kabla au baada ya rakaa za swala tano za faradhi. Ni za aina mbili, yaani zilizowekewa mkazo (muakkad) na ambazo hazijawekewa mkazo (ghayr muakkad):

#### Sunnah za muakkad ni:

1. Rakaa mbili kabla ya swala ya Al-Fajr
2. Rakaa mbili kabla ya swala ya Adhuhuri na rakaa mbili baada ya swala hiyo.
3. Rakaa mbili baada ya swala ya Magharibi.
4. Rakaa mbili baada ya swala ya Isha.

#### Sunnah ambazo sio Muakkad:

1. Rakaa mbili kabla ya swala ya Adhuhuri na rakaa mbili baada.
  2. Rakaa nne kabla ya swala ya Alasiri. Kuswali mbili mbili kwa wakati mmoja ni bora zaidi.
  3. Rakaa mbili kabla ya swala ya Maghribi.
  4. Rakaa mbili kabla ya Swala ya Isha.
- Baada ya kswali rakaa mbili kabla na baada ya swala ya Isha, imewekewa mkazo kuswali Sunnah ya Witri.

#### b) Sunnah za Swala ya Ijumaa:

Kabla ya Swala ya Ijumaa, ni Sunnah iliwekewa mkazo (muakkad) kuswali rakaa mbili.

**c) Swala ya Witri:** Huswaliwa kati ya rakaa moja na kumi na moja. Ni bora kuswali mbili

kwa wakati mmoja na kisha kumalizia na rakaa moja. Kwa mfano, unaposwali rakaa tatu za Witri, unaweza kuanza na rakaa mbili na kisha ukamalizia rakaa moja.

**2. Sunnah zinazoswaliwa nje ya swala tano za kila siku:** Hizi ni zile zisizoswaliwa kabla wala baada ya swala tano za faradhi, bali huswaliwa mbali kabisa na swala hizo. Baadhi ya swala hizo zilizoswaliwa na Mtume wetu ni:

**a) Swala ya Tarawih:** Ni swala yenye rakaa nane mpaka ishirini ambayo huswaliwa wakati wa Mwezi wa Ramadhan baina ya swala ya Isha na swala ya Witri. Inaruhusiwa kuswali rakaa mbili mbili au nne nne.


**b) Swala ya Tahajjud:** Inaweza kuswaliwa baada ya swala ya Isha kabla ya kwenda kulala au baada ya kupumzika na kabla ya swala ya Alfajri. Inaposwaliwa baada ya kulala kidogohujulikana kama Tahajjud. Swala hii inahusisha kuanzia rakaa mbili mpaka kumi na mbili. Inashauriwa kuswaliwa rakaa mbili mbili.

**c) Swala ya Dhuhra:** Ni swala ya rakaa mbili mpaka nane inayoswaliwa kuanzia saa moja baada ya jua kuchomoza mpaka saa moja kabla jua halijapita nusu ya upeo.

**d) Salat al-Awwabin:** Ni swala ya raka mbili mpaka ishirini inayoswaliwa katika muda wa baina ya swala ya Maghribi na Swala ya Isha.

**e) Tahiyyat al-Masjid:** Ni swala ya rakaa mbili inayoswaliwa na wale wanaoingia msikitini kabla ya kukaa ili "kuutolea salamu" msiki.

**f) Swala ya Eid:** Ni Sunnah kuswali swala ya rakaa mbili asubuhi ya kwanza baada ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan na katika Sikukuu ya kuchinjia.



## "NISAIDIE KWA KUSWALI SANA"

Swahaba mmoja aitwaye Rabia ibn Qa'b alikuwa akimhudumia Mtume (s.a.w). Mtume wetu alifurahishwa sana na huduma yake. Swahaba huyu aliyepata heshima ya kumhudumia Mtume wetu alisimulia kisa kifuatacho:

Siku moja nilimuandalia maji Mtume wetu kwa ajili ya wudhu. Hapo akaniambia:

- "Ewe Rabia! Ombo unachotaka!" nikajibu:

- "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nitafikiria na kisha nitakujuza baadaye". Kisha nikawaza "mali ni za mpito, na ninazo za kutosha. Ni bora niombe kitu cha maisha yangu ya Akhera; kwa maana Mtume ana daraja kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu". Nilipoenda kwa Mtume aliniuliza:

- "Ewe Rabia! Umeshafikiria unachokitaka?" nikamwambia:

- "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ninataka kuwa pamoja nawe Peponi. Ninakuomba unionbee kwa Mwenyezi Mungu aniokoe na moto wa Jahannam". Akaniuliza:

- "Hutaki kuomba kitu kingine?" Nikamjibu:

- "Hicho ndicho ninachokihitaji".

Mtume wetu (s.a.w) akasema:

- Basi swalii sana, usujudu sana na unisaide kwa faida yako!

(Muslim, Salat 256)

## MATENDO YA FARADHI KATIKA SWALA

Kuna matendo ishirini na mbili ya faradhi katika Swala. Matano kati ya hayo yanatakiwa kufanywa kabla ya swala na kumi na saba yanatakiwa kufanywa wakati wa swala. Tendo moja kati ya hayo linapokosekana, basi swala hubatilika. Matendo hayo ni haya yafuatayo:

### a. Masharti ambayo yanatakiwa kutekelezwa kabla ya swala:

Ni yale ambayo yanapaswa kutekelezwa kabla ya kuanza kuswali. Htuuandaa kimwili na kisaikolojia kuelekea kwenye swala na hivyo hujulikana kama "shurut al-salah au shuruti za swala".

**1. Al-Taharah min Al-Hadath:** (Kujitwaharisha dhidi ya uchafu): Kwa maneno mengine kuchukua wudhu, kukoga joshoo, au kutayamamu yasipowezekana hayo.

**2. Al-Taharah min Al-Najasah:** (Kujitwaharisha dhidi ya uchafu wa kimaada au unaoonekana): Kutwaharisha mwili, mavazi na eneo la kuswalia dhidi ya najisi.

**3. Satr al-Awrah:** (Kusitiri maeneo nyeti ya mwili): Wanaume wa Kiislamu wanatakiwa kuyasitiri maeneo ya baina ya kitovu na magoti katika miili yao, na Waislamu wanawake wanatakiwa kuisitiri miili yao yote isipokuwa uso na vitanga vya mikono.

**4. Al-Waqt:** (Yaani muda maalumu wa swala): Kuna muda maalumu kwa ajili ya swala ya faradhi, ambapo swala hizo zinatakiwa kutekelezwa ndani ya muda na wakati huo. Swala yoyote inayoswaliwa kabla ya wakati wake huwa ni batili. Ni dhambi kubwa kuchelewa kuswali bila udhuru wa kisheria mpaka muda wake ukapita.

**5. Istiqbal al-Qiblah:** Kuelekea upande wa Ka'bah wakati wa kuswali. Wakati wa kuswali, iwapo mtu atakigeuza kifua chake kwa hiari yake kuelekea upande mwengine usiokuwa ule wa qiblah, swala yake huwa ni batili.

Baada ya kutekeleza shuruti zote hizo, unaweza kuanza kuswali.



Ibn Mas'ud (r.a) anasema:

nilimuuliza Mtume (s.a.w):

- "Ni amali gani inayopendwa zaidi na Allah?" Akasema:
- "Kuswali kwa wakati". Nikamuuliza:
- "Amali ipi inayofuatia (kwa ubora)?" Akajibu:
- "Kuwatendea wema wazazi wako". Nikamuuliza tena:
- "Kisha amali gani (kwa ubora)?" akasema:
- "Kushiriki Jihad kwa ajili ya Allah"

(Bukhari, Mawaqit, 5)



"Kama unavyouelekeza mwili wako kwenye Ka'bah kwa ajili ya swala, unahitaji pia kuelekea moyo wako kwa Allah kwa sababu Ka'bah ya nyoyo ni Allah."

(Mawlana Jalaladdin Rumi)



**b) Masharti ambayo ni sehemu ya swala:**

⦿ Ni matendo ya faradhi yanayotakiwa kufanya wakati wa swala. Hujulikana pia kama "arkan al-salah au nguzo za swala".

**1. Nia (al-Niyyah):** Kunuia kuiswali swala husika. Katika swala za jama'ah, muumini anatakiwa pia kuweka nia yake ya kumfuata imam.

**2. Takbirya ya ufunguzi (Takbir al-Iftitah):** Kusema "Allahu Akbar" unapoanza kuswali.

**3. Kisimamo (Al-Qiyam):** Kusimama wima wakati unaposoma Suratul Fatiha na sehemu nydingine za Qur'an.

**4. Kusoma Suratul-Fatiha:** Kusoma Fatiha katika kila rakaa ya swala pamoja na Bismillah.

**5. Kurukuu (al-Ruku':)** Kuinama katika namna ambayo mikono itashika magoti baada ya kumaliza kusoma cha Qur'an Tukufu.

**6. I'tidal baada ya Rukuu:** Tokusimama wima baada ya kutoka kwenye rukuu.

**7. Kusujudu (Sajdah):** Kusujudu mara mbili katika kila rakaa. Kuwake paji la uso, pua, mikono, miguu na magoti chini baada ya kutoka kwenye rukuu.

**8. Kukaa kitako baina ya sijda mbili.**

**9. Kikao cha mwisho (Qa'dah al-Akhirah):** sKukaa kwenye rakaa ya mwisho kwa kiwango cha kuweza kusoma "tahiyyat".

**10. Kusoma "tahiyyat":** Kusoma dua ya tashahhud (tahiyyat) katika kikao cha mwisho.

**11. Kusoma salawat:** Kurmtakia rehma Mtume baada ya kusoma tashahhud.

**12. Salam ya Kwanza:** Kugeuza kichwa upande wa kulia na kusema "al-Salamu Alaikum [wa rahmatullah]" unapomaliza kuswali (kusoma upande wa kushoto ni sunnah).

**13. Kuchunga mfuatano wakati wa kuswali**

**14. Tuma'ninah:** Kubaki katika hali ya utulivu wakati wa rukuu, baada ya rukuu, wakati wa sijda na kikao cha baina ya sijda mbili.

## ADHANA (AL-ADHAN)

### Nini maana ya adhana na muadhini?

Adhana ni aina ya wito wa kuwafahamisha Waislamu kuwa muda wa swala umefika. Yule anayewaita anaitwa muadhini.

### Wakati gani na vipi adhana husomwa?

Adhana husomwa kwa sauti kutoka kwenye mnadara baada ya muda wa swala kufika. Waislamu huitwa kuswali mara tano kwa siku kwa kutumia adhana.

### Muumini hufanya nini wakati adhana inapotolewa?

Tunaposikia adhana tunapaswa kuwa watulivu na kuisikiliza. Hurudia maneno yanayosemwa na muadhini. Baada ya adhana kumalizika, muumini husoma "dua ya adhana" tuliyofundishwa na Mtume (s.a.w).

### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Watu wangejua thawabu zinazopatikana katika usomaji wa adhana na kusimama katika safu ya kwanza (katika swala za jama'ah) na ikawa hakuna njia nydingine ya kuwapa nafasi hiyo zaidi ya kupiga kura, wangepiga kura".

(Bukhari, Adhan, 9)

### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Unaposikia adhana, rudia kile kinachosemwa na muadhini".

(Boukhari, Adhan, 7)

Maneno ya adhana na maana zake

<b>اللَّهُ أَكْبَرُ</b>	Allahu Akbar (mara 4)	Allah ni Mkubwa.
<b>أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ</b>	Ashhadu an-la-ilaha illa Allah (mara 2)	Ninashuhudia kuwa hakuna mungu isipokuwa Allah.
<b>أَشْهُدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ</b>	Ashhadu anna Muhammadan RasuluAllah (mara 2)	Ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Allah.
<b>حَيٌّ عَلَى الصَّلَاةِ</b>	Hayya 'ala as-Salah (mara 2)	Njooni kwenye swala!
<b>حَيٌّ عَلَى الْفَلَاحِ</b>	Hayya 'ala al-Falah (mara 2)	Njooni kwenye wokovu!
<b>اللَّهُ أَكْبَرُ</b>	Allahu Akbar (mara 2)	Allah ni Mkubwa.
<b>لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ</b>	La ilaha illa Allah (mara moja)	Hakuna mungu isipokuwa Allah!



Maneno hayohayo husomwa katika dhana za swala zote. Hata hivyo, katika adhana na swala ya Alfajri, maneno "Assalatu khayrun min al-nawm" (swala ni bora kuliko usingizi) huongezwa baada ya "hayya 'ala al-falah".

### Adhana hutukumbusha nini?

Adhana hutukumbusha kuwa muda wa swala umefika. Kwa kuwa swala ni ibada yenyewe wakati maalumu kwa Waislamu, tunapoisisikia adhana hutujulisha kuwa kuna Waislamu katika jamii hiyo.

Adhana inayotolewa mara tano kwa siku hutukumbusha msingi wa imani ya Umoja wa Mwenyezi Mungu (Tawheed). Huweka athari katika nyoyo na roho zetu juu ya uwepo na Umoja wa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad (s.a.w) ni mjurbe Wake. Vilevile hutukumbusha lengo la kuumba kwetu na kwamba njia pekee ya wokovu hupatikana kwa kumuabudu Allah.

Siku ya Qiyama Mtukufu Mtume (s.a.w) atamuombea mwenye kumtakia rehma na kisha akafuatisha dua hii baada ya adhana:

اللَّهُمَّ رَبِّ هَذِهِ الدُّعْوَةِ التَّامَّةِ  
 وَالصَّلَاةِ الْفَائِمَةِ آتِ سَيِّدَنَا مُحَمَّدَ أَلْوَسِيلَةَ  
 وَالْفَضِيلَةَ وَالرَّجَةَ الرَّفِيعَةَ  
 وَابْعَثْهُ مَقَامًا مَحْمُودًا الَّذِي وَعَدْتَهُ

إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْمِيعَادَ  
 "Ewe Allah! Mola wa wito huu uliokamilika na swala hii inayotaka kuswaliwa, Mpe bwana wetu Muhammad heshima na ubora wa ukaribu Wako. Na muinue kwenye darja ya juu (al-Maqam al-Mahmud) uliyomuahidi. Hakika weye hukhalifu ahadi".

(Boukhari, adhan 8)

## IQAMAH

### Iqamah ni nini?

 Iqama ni wito wa kuanza kuswali ambaeo hutolewa kabla ya swala za faradhi.

### Nani anayetoe al-Iqamah?

Tunaposwali katika jama'ah, muadhini husoma iqamah kwa sauti. Wanaume wanaoswali peke yao husoma iqama kwa sauti wanayoisisikia wao wenyewe. Wanawake hawasomi Iqamah.

Maneno ya iqama ni kama yale yale ya adhana. Isipokuwa, katika iqamah, huongezwa "qad qaamat as-Salah," yaani "Swala imeanza", na hutamkwa mara mbili baada ya "hayya 'ala al-Falah." Vilevile, wakati adhana husomwa taratibu na kuachananisha vifungu, iqama husomwa haraka haraka na bila kuacha mwanya kati ya vifungu.

### Maneno ya Iqamah:

- Allahu Akbar (mara 2)
- Ashhadu an-la-ilaha illa Allah (mara 1)
- Ashhadu anna Muhammadan-Rasulu Allah (mara 1)
- Hayya 'al-as-Salah (mara 1)
- Hayya 'ala-al-Falah (mara 1)
- Qad-qaamati-s-Salah (mara 2)
- Allahu Akbar (mara 2)
- La ilaha illa Allah (mara 1)

## JINSI YA KUSWALI


Tunachukua wudhu kablaya swala. Tunasitiri viungo vyta miili yetu vinavyotakiwa kusitiriwa. Tunaelekea upande wa Ka'bah tukiwa kwenye eneo safi au mswala. Kisha tunaweka nia (al-

niyyah) ya kuswali swala husika (kwa mfano: "Ninanuia kuswali sunnah ya Swala ya Al-Fajri kwa ajili ya Allah.")

### Rakaa ya kwanza

#### 1 (Wanaume)

Wanaume huinua mikono yao ili ncha za vidole vyao zifike kwenye usawa wa masikio na kisha husoma takbir ya ufunguzi ambao ni "Allahu Akbar".



#### 1 (Wanawake)

Wanawake huinua mikono yao kiasi cha nchi za vidole vyao kufika kwenye usawa wa mabega na kusoma takbir ya ufunguzi ambayo ni "Allahu Akbar".



"(Luqman (a.s) alimuusia mwanaye): Ewe mwanangu! Shika Sala, na amriisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayo kupata.

Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa."

(Luqman 31;17)



**2 (Wanaume)**

Wanaume wanapokuwa kwenye kisimamo wanashikilia kifundo cha mkono wa kushoto kwa kidole gumba na kidole kidogo kabisa cha mkono wa kulia, na kuifunga mikono yao juu ya kitovu. Wakiwa katika hali hiyo, huanza kusoma dua ya "waijaahtu." Baada ya hapo husoma "Audhubillah na Bismillah", na kisha husoma Surah al-Fatiha ikifuatiwa na surah nyingine au Ayah chache za Qur'an.



**2 (Wanawake)**

Wanapokuwa katika kisimamo, huweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto na kuiweka chini ya kifua kuelekea kidogo upande wa kushoto. Wakiwa katika hali hiyo, huanza kusoma dua ya "waijaahtu." Baada ya hapo husoma "Audhubillah na Bismillah", na kisha husoma Surah al-Fatiha ikifuatiwa na surah nyingine au Ayah chache za Qur'an.



**3 (Wanaume)**

Baada ya hapo, wanaume huinua mikono yao sawa na masikio na kisha huinama wakisema "Allahu Akbar". Hufikisha mikono yao kwenye magoti, mgongo wao ukiwa umenyooka. Wakiwa hapo huwa katika utulivu katika hali ya kurukuu na kusema: "Subhana Rabb'iy-al-Adhim" (Ametakasika Mola wangu, Mtukufu) mara tatu.



**3 (Wanawake)**

Baada ya hapo wanawake huinua mikono yao mpaka kwenye usawa wa mabega na kuinama wakisema "Allahu Akbra". Huweka mikono juu ya magoti na kuinama, lakini sio kama wanaume. Wakiwa hapo huwa katika utulivu katika hali ya kurukuu na kusema: "Subhana Rabb'iy-al-Adhim" (Ametakasika Mola wangu, Mtukufu) mara tatu.



**4 (Wanaume)**

Hunyanya kichwa na kusema "Sami'a Allahu limanhamidah" (Allah humsikia anayemhimidi). Wanapoinuka wanainua mikono yao mpaka usawa wa masikio. Wanasmama kikamilifu mikono yao inapotulia na kusimama kidogo huku wakisema "Rabbana laka al-hamd" (Mola wetu, himidi zote ni Zako).

**4 (Wanawake)**

Hunyanya kichwa na kusema "Sami'a Allahu liman hamidah" (Allah humsikia anayemhimidi). Wanapoinuka wanainua mikono yao mpaka usawa wa mabega. Wanasmama kikamilifu mikono yao inapotulia na kusimama kidogo huku wakisema "Rabbana laka al-hamd" (Mola wetu, himidi zote ni Zako).

**5 (Wanaume)**

Husema "Allahu Akbar" huku wakienda kusujudu. Huwa makini kuweka paji la uso na pua chini. Vifundo vya mikono yao huwiweka mbali na miili yao na havifiki chini. Huisimamisha miguu juu ya vidole vikubwa vya miguu yao wakiwa wamevielekeza Qibla. Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.



**5 (Wanawake)**

Husema "Allahu Akbar" huku wakienda kusujudu. Huwa makini kuweka paji la uso na pua chini. Tofauti na wanaume, vifundo vya mikono yao huwiweka karibu na miili yao na huvilaza chini. Huisimamisha miguu juu ya vidole vikubwa vya miguu yao wakiwa wamevielekeza Qibla. Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.



**6 (Wanaume)**

Kisha husema "Allahu Akbar" na kuinuka kutoka kwenye sijda ya kwanza. Hutulia kidogo baina ya sijda mbili na kusoma dua ya "Rabbighfir li warhamni..." wakiwa wameukunjua mguu wa kushoto na kuukalia, huku wakiuinua mguu wa kulia kidole chake kikubwa kikiwa kimeelekea Ka'bah. Huweka mikono yao juu ya magoti na vidole vikiwa vimebanwa pamoja.

**6 (Wanawake)**

Kisha husema "Allahu Akbar" na kuinuka kutoka kwenye sijda ya kwanza. Hutulia kidogo baina ya sijda mbili na kusoma dua ya "Rabbighfir li warhamni..." wakiwa wameukunjua mguu wa kushoto na kuukalia, huku wakiuinua mguu wa kulia kidole chake kikubwa kikiwa kimeelekea Ka'bah. Huweka mikono yao juu ya magoti na vidole vikiwa vimebanwa pamoja.

**7 (Wanaume)**

Kwa mara nyingine, huelekea kwenye sijda kwa kusema "Allahu Akbar". Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.

**8 (Wanaume)**

Kisha huinua vichwa vyao kutoka kwenye sijda ya pili kwa kusema "Allahu Akbar" na kukalia magoti yao kwa muda mdogo. Mkao huu huitwa "mkao wa kupumzika". Kisha husimama wima kwa ajili ya rakaa ya pili.

**Rakaa ya Pili**

**9 (Wanaume)**

Baada ya kusimama wima, hushikilia kifundo cha mkono wa kushoto kwa kidole gumba na kidole kidogo kabisa cha mkono wa kulia, na kuifunga mikono yao juu ya kitovu. Wakiwa katika hali hiyo, huanza kusoma dua ya "wajjahtu." Baada ya hapo husoma "Bismillah", na kisha husoma Surah al-Fatiha ikifuatiwa na surah nyingine au Ayah chache za Qur'an.

**10 (Wanaume)**

Baada ya hapo, wanaume huinua mikono yao sawa na masikio na kisha huinama wakisema "Allahu Akbar". Hufikisha mikono yao kwenye magoti, mgongo wao ukiwa umenyooka. Wakiwa hapo huwa katika utulivu katika hali ya kurukuu na kusema: "Subhana Rabb'iy-al-Adhim" (Ametakasika Mola wangu, Mtukufu) mara tatu.

**11 (Wanaume)**

Hunyanya kichwa na kusema "Sami'a Allahu liman hamidah" (Allah humsikia anayemhimidi). Wanapoinuka wanainua mikono yao mpaka usawa wa masikio. Wanasmama kikamilifu mikono yao inapotulia na kusimama kidogo huku wakisema "Rabbana laka al-hamd" (Mola wetu, himidi zote ni Zako) while and say "Rabbana laka

**7 (Wanawake)**

Kwa mara nyingine, huelekea kwenye sijda kwa kusema "Allahu Akbar". Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.

**8 (Wanawake)**

Kisha huinua vichwa vyao kutoka kwenye sijda ya pili kwa kusema "Allahu Akbar" na kukalia magoti yao kwa muda mdogo. Mkao huu huitwa "mkao wa kupumzika". Kisha husimama wima kwa ajili ya rakaa ya pili.

**9 (Wanawake)**

Baada ya kusimama wima, hushikilia kifundo cha mkono wa kushoto kwa kidole gumba na kidole kidogo kabisa cha mkono wa kulia, na kuifunga mikono yao juu ya kitovu. Wakiwa katika hali hiyo, huanza kusoma dua ya "wajjahtu." Baada ya hapo husoma "Bismillah", na kisha husoma Surah al-Fatiha ikifuatiwa na surah nyingine au Ayah chache za Qur'an.

**10 (Wanawake)**

Baada ya hapo wanawake huinua mikono yao mpaka kwenye usawa wa mabega na kuinama wakisema "Allahu Akbra". Huweka mikono juu ya magoti na kuinama, lakini sio kama wanaume. Wakiwa hapo huwa katika utulivu katika hali ya kurukuu na kusema: "Subhana Rabb'iy-al-Adhim" (Ametakasika Mola wangu, Mtukufu) mara tatu.

**11 (Wanawake)**

Hunyanya kichwa na kusema "Sami'a Allahu liman hamidah" (Allah humsikia anayemhimidi). Wanapoinuka wanainua mikono yao mpaka usawa wa mabega. Wanasmama kikamilifu mikono yao inapotulia na kusimama kidogo huku wakisema "Rabbana laka al-hamd" (Mola wetu, himidi zote ni Zako).

**12 (Wanaume)**

Husema "Allahu Akbar" huku wakienda kusujudu. Huwa makini kuweka paji la uso na pua chini. Vifundo nya mikono yao huwiweka mbali na mili yao na havifiki chini. Huisimamisha miguu juu ya vidole vikubwa nya miguu yao wakiwa wamevielekeza Qibla. Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.

**13 (Wanaume)**

Kisha husema "Allahu Akbar" na kuinuka kutoka kwenye sijda ya kwanza. Hutulia kidogo baina ya sijda mbili na kusoma dua ya "Rabbighfir li warhamni..." wakiwa wameukunjua mguu wa kushoto na kuukalia, huku wakiinua mguu wa kulia kidole chake kikubwa kikiwa kimeelekea Ka'bah. Huweka mikono yao juu ya magoti na vidole vikiwa vimebanwa pamoja.

**14 (Wanaume)**

Kwa mara nyiningine, huelekea kwenye sijda kwa kusema "Allahu Akbar". Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.

**15 (Wanaume)**

Husema "Allahu Akbar" na kukaa kitako. Wakiwa wamekaa huseweka mikono yao juu ya magoti yao na kuvikusanya vidole vyao. Husoma "dua ya tashahhud au At-Tahiyyatu", na dua ya kumtakia rehma Mtume (s.a.w), yaani "Allahumma Salli".

**12 (Wanawake)**

Kwa mara nyiningine, huelekea kwenye sijda kwa kusema "Allahu Akbar". Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.

**13 (Wanawake)**


Kisha husema "Allahu Akbar" na kuinuka kutoka kwenye sijda ya kwanza. Hutulia kidogo baina ya sijda mbili na kusoma dua ya "Rabbighfir li warhamni..." wakiwa wameukunjua mguu wa kushoto na kuukalia, huku wakiinua mguu wa kulia kidole chake kikubwa kikiwa kimeelekea Ka'bah. Huweka mikono yao juu ya magoti na vidole vikiwa vimebanwa pamoja.

**14 (Wanawake)**

Kwa mara nyiningine, huelekea kwenye sijda kwa kusema "Allahu Akbar". Husema "Subhana Rabbiy al-a'la" (ametakasika Mola wangu Mkuu) mara tatu wakiwa katika hali ya sijda.

**15 (Wanawake)**

Husema "Allahu Akbar" na kukaa kitako. Wakiwa wamekaa huseweka mikono yao juu ya magoti yao na kuvikusanya vidole vyao. Husoma "dua ya tashahhud au At-Tahiyyatu", na dua ya kumtakia rehma Mtume (s.a.w), yaani "Allahumma Salli".






16 (Wanaume)

Baada ya kukamilisha dua hizo, hugeuza kichwa upande wa kulia na kusema "Assalamu alaikum wa Rahmatullah", na kisha upande wa kushoto na kurudia kusema "Assalamu alaikum wa Rahmatullah". Wanapofanya hivyo wanawake wamekamilisha swala ya rakaa mbili.

16 (Wanawake)

Baada ya kukamilisha dua hizo, hugeuza kichwa upande wa kulia na kusema "Assalamu alaikum wa Rahmatullah", na kisha upande wa kushoto na kurudia kusema "Assalamu alaikum wa Rahmatullah". Wanapofanya hivyo wanawake wamekamilisha swala ya rakaa mbili.



# UTEKELEZAJI WA SWALA TANO ZA KILA SIKU

SWALA YA ALFAJIRI	Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili
<b>SUNNAH YA SWALA YA ALFAJIRI</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajjahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda ya pili (tuma'nina)</li> <li>* Mkao kupumzika</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya pili</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>
<b>RAKAA ZA FARADHI YA SWALA YA ALFAJIRI (2)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajjahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>

SWALA YA ADHUHURI	Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili	Rakaa ya Tatu	Rakaa ya Nne
<b>SUNNNA YA KWANZA</b> <b>YA SWALA YA ADHUHURI (2)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda ya pili (tuma'nina)</li> <li>* Mkao kupumzika</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya pili</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>		
<b>RAKAA ZA FARADHI</b> <b>YA SWALA YA ADHUHURI (4)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat na salawat</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya tatu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	

**SUNNAH YA  
MWISHO YA SWALA  
YA ADHUHURI (2)**

Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili	Rakaa ya Tatu	Rakaa ya Nne
<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajjahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda ya pili (tuma'nina)</li> <li>* Mkao kupumzika</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya pili</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>		

SWALA YA ALASIRI	Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili	Rakaa ya Tatu	Rakaa ya Nne
<p><b>RAKAA ZA FARADHI</b></p> <p><b>YA SWALA YA ALASIRI (4)</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajjahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat na salawat</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya tatu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajjahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>

SWALA YA MAGHRIBI	Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili	Rakaa ya Tatu	Rakaa ya Nne
<b>RAKAA ZA FARADHI</b>  <b>YA SWALA YA MAGHRIBI (3)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat na salawat</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya tatu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>		
<b>SUNNAH YA SWALA YA MAGHRIBI (2)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>			

SWALA YA ISHAA	Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili	Rakaa ya Tatu	Rakaa ya Nne
<b>RAKAA ZA FARADHI YA SWALA YA ISHAA (4)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajiahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Mkao kupumzika</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya pili</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat na salawat</li> <li>* Kuinuka kwa ajili ya rakaa ya tatu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajiahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>
<b>SUNNAH YA SALA YA ISHAA (2)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajiahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda ya pili (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>	<b>SWALA YA WITR (kwa uchache 1)</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Takbir ya ufunguzi</li> <li>* Dua ya Wajiahtu</li> <li>* Kusema Audhubillah na Bismillah</li> <li>* Suratul-Fatiha</li> <li>* Surah ya ziada</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'nina (kutulia kidogo)</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* Kunyooka (l'tidal)</li> <li>* Tuma'nina</li> <li>* Kusujudu</li> <li>* Kutulia kidogo katika sijda (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako baina ya sijda mbili</li> <li>* Kutulia kidogo (Tuma'nina)</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Kutulia katika sijda ya pili (tuma'nina)</li> <li>* Kukaa kitako kwa ajili ya dua ya Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat</li> <li>- Allahumma Salli na Barik</li> <li>- Rabbana atina</li> <li>* Salaam</li> </ul>

# BAADHI YA DUA ZINAZOSOMWA WAKATI WA SWALA

Dua ya Ufunguzi (Wajjahtu):

وَجَهْتُ وَجْهِي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ  
خَنِيفًا مُسْلِمًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ إِنَّ صَلَاتِي وَ  
سُكُونِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ لَا شَرِيكَ  
لَهُ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ

Dua ya Ufunguzi (Wajjahtu):

"Wajjahtu wajhiya lilladhi fatara al-samawati wal-arda hanifan musliman wama ana min al-mushrikina inna salati wa nusuki wa mahyaya wa mamati lillahi rabbil-alamina la sharika lahu wa bidhalika umirtu wa ana minal-muslimin."

Maana yake:

"(Nimeelekeza uso wangu kwa yule aliyeumba mbingu na ardhi, nikiwa mwenye kumpwekesha, mwenye kujisalimisha kwake, nami si mionganoni mwa wale wenye kumfanyia washirika. Swala yangu, ibada yangu, uhai wangu, na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allah, Mola wa Walimwengu, hana mshirika. Hivyo ndivyo niliyoyaamishwa, nami ni mionganoni mwa wale wenye kujisalimisha Kwake)."

Dua ya Qunut:

اللَّهُمَّ اهْدِنَا فِي مَنْ هَدَيْتَ وَعَافِنَا فِي مَنْ عَافَيْتَ  
وَتَوَلَّنَا فِي مَنْ تَوَلَّتَ وَبَارِكْ لَنَا فِي مَا أَعْطَيْتَ وَقَنَا  
شَرًّ مَا قَضَيْتَ فَإِنَّكَ تَقْضِي وَلَا يُفْضِي عَلَيْكَ وَإِنَّهُ  
لَا يَذُلُّ مَنْ وَالْيَتَ وَلَا يَعْزُزُ مَنْ عَادَيْتَ تَبَارَكْ رَبَّنَا  
وَتَعَالَى إِنَّكَ الْحَمْدُ عَلَيْ مَا قَضَيْتَ نَسْتَغْفِرُكَ وَ  
نَتُوبُ إِلَيْكَ وَصَلَى اللَّهُ عَلَيْ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَيْ  
الله وَصَحْبِهِ وَسَلَّمَ

"Allahummahdina fiman hadayta wa afina fiman afayta wa tawallana fiman tawallayta wa barik lana firma a'tayta wa qina sharra ma qadayt Fainnaka taqdi wala yuqda alayk wa innahu la yadillu man walayta wala yaizzu man adayta Tabarakta Rabbana wa taalayt Falaka'l-hamdu ala ma qadayt Nastaghfiruka wa natubu ilayka wa sallallahu ala sayyiddina Muhamadin wa ala alihii wa sahibihi wa sallam".

Maana yake:

"Ewe Allah, niongoze katika wale waliowaongoa, unipe afya mionganoni mwa wale uliowapa afya, niunge mkono katika wale uliowaunga mkono, nibariki katika vile uliyonijaadila. Nilinde dhidi ya shari ya uliyoviumba, kwani wewe ndiwe mwenye kuamuru na huamuriwi. Unayemuunga mkono hawezi kudhoofika wala kudhalilika, na unayempinga hawezi kuheshimika. Mola wetu, Baraka zako ziongezeke. Hakika Wewe umetukuka na umetakasika dhidi ya upungufu wowote. Himidi zote ni zako kwa yote uliyoyaamua. Ninakuomba msamaha na ninatubia Kwako. Rehma na amani ziwe juu ya bwana wetu Muhammad, ahli zake na Maswahaba wake."

Tahiyyat:

الْتَّحَيَّاتُ الْمُبَارَكَاتُ الصَّلَواتُ الْطَّيِّبَاتُ لِلَّهِ السَّلَامُ  
عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلَامُ عَلَيْنَا  
وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّلِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ  
وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ

109

"At-tahiyyatu al-mubarakatu as-salawatu at-tayyibatu li'l-lahi as-salamu alayka ayyuha'n-nabiyyu wa rahmatu'l-lahi wa barakatuhu as-salamu alayna wa ala ibadi'l-lahi's salihin ashhadu alla ilaha illallah wa ashhadu anna muhammadar-Rasulullah"

Usomaji wa tahiyyat ya kwanza ni sunnah na ya pili ni wajibu.

Dua baada ya tahiyyat:

Ni Sunnah baada ya tahiyyat kujiombea na kuwaombea waumini wote kusema:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَالْمُسْلِمِينَ  
وَالْمُسْلِمَاتِ الْأَحْيَاءِ مِنْهُمْ وَالْأَمْوَاتِ

"Allahummaghfirli wa li'l-mu'minina wa'l-mu'minat wa'l-muslimina wa'l-muslimat al-ahyai minhum wa'l-amwat."

Maana yake:

"Ewe Allah! Nighufurie mimi na waumini wanaume na wanawake, Waislamu wanaume na wanawake, walio hai na wale waliokufa".

## DUA NA DHIKIR ZINAZOSOMWA BAADA YA SWALA

Kila swala baada ya salamu muumini anapaswa kusoma dua ifuatayo mara tatu:

أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ الْعَظِيمِ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ وَاتُّوْبُ إِلَيْهِ

“Astaghfirullah al-adhim alladhi la ilaha illa hu-val-Hayyal-Qayyum wa-atubu ilayhi”. Kisha aseme:

اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ فَحَيَنَا رَبَّنَا بِالسَّلَامِ  
تَبَارَكْتَ وَتَعَالَيْتَ يَا ذَالْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

“Allahumma anta's salamu wa minka's salam, fa hayyina rabbana bissalam tabarakta wa taalayta ya dha'l jalali wa'l ikram” na baada ya hapo aseme:

اللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ وَلَا  
رَأَدَ لِمَا قَضَيْتَ وَلَا مُبْدِلَ لِمَا حَكَمْتَ وَلَا يَنْقُنُ ذَالْجَدْ  
مِنْكَ الْجَدُّ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ

“Allahumma la mania lima a'tayt wa la mu'tia lima mana't wa la radda lima qadayt wa la mubaddila lima hakamt wa la anfaa dhajadi minkal jaddu wala hawla wa la quwwata illa billahil aliyyil adhim”

سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ  
وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ

“Subhanallahi wa'l-hamdu lillahi wa la ilaha illallahu wallahu akbar wa la hawla wa la quwwata illa billahi'l-aliyyi'l-adhim”.

Baada ya dua na dhikri hizo tunasoma audhubillah na bismillah, kisha tunasoma Ayah ijulikanayo kama Ayat al-Kursi (Baqarah, 2: 255). Kisha surah za Ikhlas (112), falaq (113) na Nas (114).


Baada ya kusoma سُبْحَانَ اللَّهِ Subhanallah mara 33, Alhamdulillah mara 33, na اللَّهُ أَكْبَرُ Allahu Akbar mara 33, tunasema:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ  
وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ سُبْحَانَ رَبِّي الْعَلِيِّ الْأَعْلَى  
الْوَهَابِ

“La ilaha illallahu wahdahu la sharika lah. Lahu'l-mulku wa lahu'l-hamdu wa huwa ala kulli shay'in qadir. Subhana rabbiya'l-aliyyi'l-a'l'a'l-wahhab”, na tunamuomba Allah kwa kuinua mikono yetu. Baada ya dua hizi tunafuta nyuso zetu kwa mikono yetu na hivyo kukamilisha dua na dhikri mbalimbali ambazo ni sehemu ya swala.

Mtume wetu (s.a.w) alikuwa akiomba dua ifuatayo na kutuusia kuisoma:

“Ewe Allah! Ninakuhimidi. Wewe ndiwe mwenye kuzitazama mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo.



Himidi zote zinakustahiki Wewe. Wewe ni Kweli na Haki. Ahadi Zako ni Kweli na Haki. Maneno Yako ni kweli na Haki. Marejeo ya waja Kwako ni kweli na Haki. Pepo ni kweli na haki. Moto ni kweli na haki. Ni kweli kwamba Siku ya Kiyama inakuja. Mitume ni kweli na haki. Muhammad (s.a.w) ni kweli na haki.

Ewe Allah! Kwako pekee ninajinyenyekeza kwa kuyatii maamrisho na makatazo Yako. Wewe pekee ndiye ninayekutegemea. Wewe pekee ndiye ninayekuarmini. Ninairekea uso na moyo wangu Kwako pekee.

Ewe Allah! Ipokee swala yangu. Hakika Wewe ni Mwenye kuona, Msikivu.

Ewe Allah! Nisamehe makosa yangu niliyoyafanya kwa kujua au kutojua.

Ewe Allah! Nipe msaada wa kukukumbuka na kulidhukuru jina lako, kuzishukuru neema zako na kukuabudu kama unavyostahiki.

Ewe Allah! Nilinde dhidi ya kufanya makosa katika dini yangu, ambayo ni mwanzo wa amali zangu zote! Zibariki shughuli zangu zote katika dunia hii! Nijaalie katika kuichuma Akhera yangu ambayo ndiyo marejeo yangu! Niwezeshe kufanya mema mengi katika kipindi chote cha uhai wangu!

Ewe Allah! Nilinde dhidi ya kila jambo linalokhalifu umoja, dhidi ya unafiki na dhidi ya tabia zote mbaya!

Ewe Allah! Nioneshe njia ya haki, yatakase maadili na roho yangu, zipendezeshe adabu zangu. Niweke mbali na kila kitu cha haramu.

Ewe Allah! Ninajilinda kwako dhidi ya utovu wa maadili, amali mbaya, imani batili.

Ewe Allah! Ninajilinda kwako dhidi ya ufukara, israfu, majaribu, dhidi ya kuwadhulamu watu na dhidi ya kudhulumiwa na watu.

Mola wetu uliyetuumba na kutufundisha adabu! Tupatiie mema katika dunia na akhera na utuokoe na adhabu ya moto.

Mola wetu uliyetuumba na kutufundisha maadili! Nisamehe mimi, wazazi wangu na waumini wote Siku ya Hukumu”.

Ameen!



Siku moja Mtume wetu (s.a.w) aliushika mkono wa Muadh bin Jabal na kumwambia: "Ewe Muadh! Allah ni shahidi yangu kuwa ninakupenda". Hapo Muadh akamwambia Mtume wetu: "Ewe Mijumbe wa Allah! Hakika ninakupenda pia". Mtume wetu akaendelea kusema: Ewe Muadh! Ninakuusia sana kusoma dua hii kila baada ya swala:

اللَّهُمَّ أَعْنِي عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحْسِنْ عِبَادَتِكَ

"Ewe Allah! Ninakuomba msaada juu ya kukudhukuru, kuzishukuru na kukuabudu kama unavyostahiki!"

( Abu Dawud, Witr, 26)

## RUDIA SWALA YAKO

Akiwa amezungukwa na Maswahaba, siku moja Mtume wetu aliingia msikitini na kukaa kwenye kona moja wapo. Muda mfupi mtu mmoja akaingia na kuanza kuswali. Alikuwa na woga kuwa Mtume anamuona. Baada ya kumaliza swala, alimsogelea Mtume (s.a.w) na kumtolea salamu. Baada ya kumjibu, Mtume (s.a.w) alimwambia: "Rudi ukaswali tena; kwa maana hukuitekeleza swala yako kikamilifu".

Mtu yule alirudi na kuswali kama alivyofanya mwanzo. Aliporudi kwa Mtume, Mtume (s.a.w) alimwambia: "Nenda kaswali tena; kwa maana hujatekeleza swala yako kikamilifu". Jambo hilo lilijirudia kwa mara ya tatu. Mwishowe mtu huyo akasema: "Ninaapa kwa yule ambaye amekutuma

kubainisha ukwelli, sijui namna nyingine ya kuswali. Nifundishe njia sahihi". Mtume (s.a.w) akamfundisha yafuatayo:

"Unaposimama kwa ajili ya swala, soma Takbir (Allahu Akbar). Kisha soma Ayah za Qur'an kwa kiasi unachowenza. Yafuatisho hayo kwa Rukuu. Endelea katika hali hiyo mpaka viungo vyako vinapokaa imara. (Baada ya kusema "Subhana Rabb'iy-al-adhim" mara tatu) inua kichwa chako mpaka unyooke barabara. Kisha elekea kwenye sijdah. (Baada ya kusema "Subhana Rabbiyal-a'la" mara tatu) inua kichwa chako. Kaa kitako huku viungo vyako vikiwa vimetulia. Rudia hayo katika rakaa zote za swala." (Bukhari, Adhan, 95)

## SUNNAH ZA SWALA

### Sunnah za swala ni za aina mbili:

#### A. Sunnah za kabla ya swala:

1. Adhana
2. Iqama

#### B. Sunnah zinazotekelze wa wakati wa swala:

 1. **Sunnah Ba'diyya au Sunnah Kuu:** Hizi ni sunnah sita ambazo huchukuliwa kama sehmu kuu ya swala. Sunnah moja kati ya hizo inapoachwa wakati wa swala, ni sunnah kusujudu sijda ya kusahau mwichoni mwa swala. Sunnah hizo ni:

- a. Katika rakaa ya pili ya swala ya alfajiri, baada ya kutoka kwenye rukuu, kusoma

dua ya Qunut, tahmidi na kumtakia rehma Mtume, ahli zake na maswahaba zake.

- b. Kisimamo wakati wa kusoma dua ya Qunut katika swala ya alfajiri.
- c. Kukaa kitako kwa ajili ya tashahhud ya kwanza mwichoni mwa rakaa ya pili ya swala yenye rakaa tatu na nne.
- d. Kusoma tashahhud ya kwanza.
- e. Kumtakia rehma Mtume baada ya tashahhud katika kikao cha kwanza.
- f. Kuwatachia rehma ahli wa Mtume katika tashahhud ya mwisho (kumtakia rehma Mtume katika kikao cha mwisho ni wajibu).

### C: Sunnah za Hay'ah au Sunnah za kawaida:

Hizi ni sunnah ambazo ni sehemu ya swala lakini hazihitaji sijda ya kusahau. Sunnah hizi huifanya swala kuwa kamili. Maeneo mengine ya swala, tofauti na yaliyotajwa hapo juu, ni sunnah za kawaida. Baadhi yake ni hizi zifuatizo:

- 😊 Kuinua mikono mpaka usawa wa masikio wakati wa kutoa takbir ya ufunguzi.
- 😊 Kusoma dua ya wajahtu kwa kuficha sauti baada ya takbir ya ufunguzi.
- 😊 Kusema "amin" kwa sauti baada ya surah Al-Fatiha katika swala za Jamah.
- 😊 Kumhimidi Mwenyezi Mungu mara tatu wakati wa rukuu na sijda. Kiwango cha mwisho cha himidi hizo ni moja.
- 😊 Kusema "Subhana Rabbi al Adhim" katika rukuu, na kusema "Subhana rabbiy'al- A'lā" wakati wa sijda.
- 😊 Kutoa takbir baina ya nguzo za swala kama vile kisimamo, rukuu na sijda.
- 😊 Kusema "Samiallahu liman hamidah" wakati wa kuinuka kutoka kwenye rukuu na kusema "Rabbana laka al-hamد" baada ya kusimama wima.
- 😊 Kusoma kwa sauti katika swala zinazotakiwa kufanya kisomo kwa sauti [alfajiri, maghribi na ishaa] na kusoma kwa kuficha sauti katika swala zinazotakiwa kuficha sauti [adhuhuri na alasiri].
- 😊 Kuchagua Ayah au Surah zinazosomwa baada ya Al-Fatiha kwa kufuata mfuatano kama ulivyo ndani ya Qur'an. Kwa mfano, tukitaka kusoma Surah Kawthar na Ikhlas, tunatakiwa kusoma Kawthar katika rakaa ya kwanza na Ikhlas katika rakaa ya pili kwa maana surah hiyo ya kwanza ni ya 108 huku hiyo ya pili ikiwa ni ya 112 katika mpangilio wa Surah za Qur'an. Kutochunga utaratibu huu ni jambo ambalo ni makruh.
- 😊 Kuinua mikono mpaka kwenye usawa wa mabega wakati wa kwenda au kutoka kwenye rukuu.
- 😊 Kuinua mikono mpaka kwenye usawa wa mabega unapotoka kwenye sijda au kutoka kwenye kikao.
- 😊 Wakati wa kusoma tahiyyat, mkono wa kushoto huendelea kukaa wazi juu ya goti na vidole vyta ya mkono wa kulia hukunjiwa isipokuwa kidole shahada. Hukunjiliwa wakati wa kusema "illallah" na huendelea kunooshwa mpaka mwisho wa dua.
- 😊 Kukaa kitako katika hali inayoitwa iftirash ambayo ni kuuweka mguu wa kushoto kwenye upande wake na kuukalia katika kikao cha kwanza, na katika kikao cha mwisho kuuweka katika hali ya tawarruk, yaani kulikalia tako la kushoto na kuuweka wima mguu wa kulia huku vidole vyta miguu vikiwa vimeelekezwa qibla na mguu wa kushoto ukiwa chini ya mguu wa kulia.



Mwanazuoni mmoja wa Kiislamu aliulizwa: "Muumini anawezaje kupata khofu na raha kutohana na swala?" akajibu:

- Kwa kuhakikisha kuwa anachokula kimetokana na kazi yake halali.
- Kuwa na tihadhari wakati wa kuchukua wudhu na kutambua kuwa anakwenda mbele ya Mwenyezi Mungu.

- Kwa kutambua kuwa sasa yuko mbele ya Mwenyezi Mungu baada ya takbira ya ufunguzi na kuliweka akilini hilo wakati wote wa swala.
- Kwa kutosahau kamwe kuwa Allah yuko pamoja nasi hata pale tunapokuwa nje ya swala na kutambua kuwa anatuona sote.



114

## MATENDO YASIOFAA WAKATI WA SWALA (MAKRUHAT AL-SALAT) ☹☹

Tunapokuwa ndani ya swala hatupaswi kusahau kuwa tuko mbele ya Mwenyezi Mungu na tutekeleze swala zetu kama tulivyofundishwa na Mtume (s.a.w). Tunatakiwa kutilia maanani Sunnah za swala ambazo hukamilisha matendo ya lazima katika swala. Kuacha Sunnah za swala ni jambo lisilopendeza katika Uislamu au ni jambo lenye kuchukiza (makruh).

### Mambo makuu yenye kuchukiza ni:

- ☹ Kuchezea nguo au viungo vya mwili wakati wa swala.
- ☹ Kuswali huku mikono ikiwa na michoro.
- ☹ Kuswali wakati ukiwa umebanwa na choo.
- ☹ Kusimama peke yako katika swala ya jamah wakati kuna nafasi katika safu ya mbele.
- ☹ Kuswali kwa kumuelekea mwanadamu au picha ya mwanadamu.
- ☹ Kuweka uzito wa mwili kwenye mguu mmoja bila udhuru.
- ☹ Kwa wanawake, kuswali bila kifunko cha kichwa.
- ☹ Kutazama juu au pembeni.
- ☹ Kuzidisha kiasi katika kuinamisha kichwa wakati wa kurukuu au kukipandisha zaidi ya mwili.
- ☹ Kusoma kimya kimya bila kutikisa mdomo.

## NANI AMEKUJA KUSWALI?

Siku moja wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, Khalifa Harun Rashid alimwambia Bahlul Dana:

— Nenda msikitini wakati wa swala ya Maghribi na umualike kila aliyejuka kuswali aje kufuturu.

Muda ulipofika, adhana ilitolewa. Msikitini kulikuwa na swala ya jamah ya zaidi ya safu moja. Baada ya swala, Bahlul Dana alirudi na watu wachache tu. Harun Rashid alishangazwa na hilo.

— Ni hawa hawa tu? Nilitaka umualike kila aliyeswali Maghribi aje kwenye futari hii, lakini umeleta watu wachache tu wanaotosha kukaa kwenye meza moja tu!

Bahlul Dana akajibu:

— Mfalme wangu! Uliniagiza niwaalike wale waliojekeleza swala zao, sio wale waliojuka msikitini. Baada ya swala nilisimama mlangoni na kumuuliza kila mmoja surah gani za Qur'an zilizosomwa na Imam. Watu wengi waliojuka kuswali hawakuweza kukumbuka surah iliyosomwa. Hawa ndio pekee waliojumbuka. Watu walikuwa wengi msikitini, lakini yaonekana watu hawa ndio pekee waliojekeleza swala zao vizuri. Nami nimewaleta kwako kama ulivyoagiza.



## TUSWALI KWA UNYENYEKEVU

Tunapofanya kitu tunachokipenda, huweka akili zetu zote kwenye kitu hicho. Wakati mwagine tunaweka akili zetu hapo kikamilifu kiasi kwamba hatuwezi kusikia mtu anapotuita na hatuwezi kutambua mambo yanayoendelea katika eneo husika. Kuhisi unyenyeketu katika swala ni kutambua kuwa tuko mbele ya Allah, kutoshughulika na kitu kingine, na kuweka akili kwenye swala tu.

Mara nyingi huwa hatupendi kumuacha mtu tunayempenda, au yeye kutuacha. Hata muda ukiyoyoma hatuwezi kuhisi. Tunapokuwa na marafiki zetu au kuzungumza nao, huwa ni kosa kufanya kitu kingine, au sio?

Vivyo hivyo, kushughulika na kitu kingine tunapokuwa mbele ya Allah wakati wa swala litakuwa kosa. Swala zetu hazipaswi kuwa muda wa kukumbuka mambo yetu ya kazini, shulenii, family au marafiki, na

haipaswi kuwa muda wa kupanga mambo yetu ya siku hiyo. Tunapoelekeza mili yetu upande wa Ka'abah, tunapaswa kuzifanya nyoyo zetu pia zimuelekee Allah. Tunapaswa kuwa na adabu tunapotafakari maana ya Ayah tunazoisoma na kuutafakari ukweli kuwa tumesimama mbele ya Allah Mtukufu. Hatupaswi kujishughulisha na mambo mengine tunapokuwa mbele ya Mola wetu, anapotuona, pindi ndimi zetu zinapomtukuza na tunaposoma Ayah alizoziteremsha. Tutasema nini kama Allah akituuliza, "Mja wangu, nilikuwa pamoja nawe, lakini ulikuwa pamoja na nani?"

Kila swala tunatakiwa kuiona kana kwamba ni muda wa marafiki wawili kuwa pamoja, au muda ambao mja anakutana na Mola wake. Tunaweza kuwa katika hali ya khofu na unyenyekevu tunapofanya jitihada za kuiona swala kuwa ni wakati wa kuonesha upendo wetu kwa Mola wetu na kuwa kuwa pamoja naye, badala ya kuiona kama ni mzigo na hivyo kupelekea kuswali haraka haraka.

Tunapoanza kuswali yatupasa kuufikiria ukuu wa Allah na kusimama mbele yake kwa kusema "Allahu Akbar". Tunasimama katika hali ya adabu kwa kuinua mikono yetu mbele ya Muumba wetu. Tunaposoma Ayah za Qur'an yatupasa kuona kuwa Allah Mtukufu anazungumza nasi. Tunaenda kwenye rukuu kwa kuukumbuka ukuu wa Mola wetu. Baada ya kuinuka kwa heshima, tunaweka paji letu la uso sakafuni na kusujudu kwa mwili na roho. Tunakumbuka kuwa wakati wa sijda ni wakati wa kuwa karibu zaidi na Allah, na tunasema "Utukufu ni Wako Mola wangu."

### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

Hakika wamefanikiwa waumini. Ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao.

(Mu'minun, 23; 1-2)

### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

Na taruteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu. Ambao wana yakini kuwa hakika watafutana na mola wao mlezi na ya kuwa hakika watarejea kwake.

(Baqara, 2; 45-46)

Tunataamali kuwa lengo la kuumbwa kwetu ni kumuabudu na kumhimidi Allah, na tunaweza kutoa kila kitu kwa ajili Yake. Tunakamilisha rakaa zote tukiwa na fikra hii akilini mwetu. Mwishoni tunakaa kitako mithili ya mtu mnyenyekevu, fakiri, na kusoma "Al-Tahiyyat, Allahumma Salli, na Allahumma Barik." Tukiwa na furaha ya kutekeleza ibada inayotuweka karibu zaidi na Mola wetu, tunaikamilisha swala yetu kwa kuwatolea salamu (As-Salam) malaika na watu walio upande wa kulia na kushoto.

# MATENDO YANAYOBATILISHA SWALA



- ➊ Kubatilika wudhu wakati wa swala,
- ➋ Kuacha moja ya matendo ya faradhi za swala,
- ➌ Kula au kunywa wakati wa swala,
- ➍ Kuzungumza na mtu, kumsalimia mtu au kujibu salamu,
- ➎ Kucheka wakati wa swala,
- ➏ Kugeuza kifua dhidi ya uelekeo wa Ka'bah Tukufu,
- ➐ Fiil-i Kathir: (amal-i kathir) au kupiga hatua tatu mfululizo katika amali moja ya faradhi ya swala au kutikisika kusikokuwa kwa kawaida kwa viungo vyta mwili kama vile mkono au kichwa. Kujishughulisha na kitu kingine kiasi kwamba watu wanadhani kuwa hayupo katika swala.
- ➑ Kusoma Qur'an kimakosa kwa kiasi kinachobadilisha maana.
- ➒ Kuwa na najisi kwenye mwili au sehemu ya kuswalia.
- ➓ Kiungo cha mwili kinachotakiwa kufunikwa kinapofunuka, hubatilisha swala labda kama kitafunikwa haraka.
- ➔ Kupoteza fahamu wakati wa swala.

## SIKUTAKA KUKATISHA MCHEZO WAKE

Ilikuwa wakati wa swala ya Adhuhuri au Alasiri. Mtume wetu (s.a.w) alilingia msikitini akiwa amewabeba wajukuu zake Hassan na Hussein. Aliingia katika Mihrab, akawaweka wajukuu zake chini na kuanza kuswali. Maswahaba walanza kummfuata katika swala. Wakati wa swala, Mtume alirefusha sijda yake kuliko kawaida, kwa sababu mjukuu wake mmoja alikuwa akicheza mgongoni mwake. Baada ya kukamilisha swala, maswahaba walimuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Uliporefusha sijda yako kuliko kawaida tulidhani kuwa kuna jambo limetokea au umepokea ufunuo". Mtume (s.a.w) akajibu:

"Hapana; bali mjukuu wangui alikuwa akicheza mgongoni kwangu. Nilitulia mpaka alipoteremka. Sikutaka kukatisha mchezo wake kwa kufanya haraka." (Nasai, Tatbiq, 82)



# UMUHIMU WA SWALA YA JAMA'AH

## Maana ya "imam" (kiongozi) na "jama'ah"

✍ Yule anayeongoza angalau mtu mmoja katika swala huitwa imam, na wanaomfuata wanaitwa jama'ah.

## Kwa nini misikiti huitwa "Nyumba za Allah"?

Misikiti ni majengo ambayo Waislamu hukutana na kuswali. Kwa kuwa katika majengo hayo sijda hufanyika kwa ajili ya Allah, ibada hufanyika, huitwa kuwa ni "Nyumba za Allah".

## Ni upi ubora wa swala ya jama'ah?

Daima Mtume wetu (s.a.w) alikuwa akiswali jama'ah na kutuusia nasi kufanya hivyo hivyo. Tumeelezwa kuwa kuswali katika jama'ah kuna ubora mara ishirini na saba kwa upande wa thawabu. Ni jambo lisilopendeza katika Uislamu kutokuswali katika jama'ah bila udhuru. Kujenga mazoea ya kuswali jama'ah ni miongoni mwa sifa njema za Muislamu. Mtume wetu (s.a.w) alitupatia khabari njema kwa wale wanaochukua wudhu na kwenda msikitini kuswali, kwa kila hatua wanayopiga, dhambi zao hufutika na kupewa thawabu.

## Ni zipi faida za kuswali katika jama'ah?

Kuswali na Waislamu wenzetu hutufanya tuwe na utulivu zaidi wakati wa kuswali. Hivyo, akili zetu huwa kwenye swala tu. Vilevile, kuswali katika jama'ah husababisha upendo na mshikamano miongoni mwa Waislamu. Waislamu wanaoswali pamoja hupata taarifa za matatizo ya wenzao. Husaidiana kutatua mambo yao. Tunaweza kujifunza misingi na makatazo ya dini yetu kuititia hotuba, mihadhara na mazungumzo mbalimbali. Pia, msikitini hupata kuongeza maarifa yetu juu ya maisha na tabia za Mtume (s.a.w).

## Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Swala ya jama'ah inazidi ubora wa swala ya peke kwa daraja ishirini na saba!"

(Bukhari, Adhan 30)

## Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Watakao pata malipo makubwa niwale wanao uendea msikiti kutoka mbali, kunamalipo wakubwa kumsubiri Imamu ilikupata swala ya jama'ah kuliko anayeswali peke kisha akaenda kulala."

(Bukhari, Adhan 31)

## Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Yeyote atakae tia Uduh nyumbani kwa lengo la kwenda kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu kutekeleza Faradh, kwa kila hatua atakayo tembea atafutiwa zambi moja na kupandishwa daraja."

(Muslim, Mosque 282)

Tunapokuwa msikitini huhisi furaha na amani ya kuwa pamoja kwa kumuabudu Allah. Malaika hutuzunguka na rehma na baraka za Allah hutushukia. Mwenyezi Mungu huipenda swala inayoswaliwa kwa jama'ah. Pia hutusamehe makosa ambayo tunaweza kuyafanya wakati wa swala.

### Safu zinatakiwa kuwa vipi wakati wa swala ya jama'ah?

- ✿ Wanaume watu wazima wanatakiwa kusimama katika safu za mbele, vijana wa kiume wanaweza kusimama kati yao au kuunda safu mpya nyuma yao, na wanawake wanatakiwa kusimama nyuma.
- ✿ Iwapo maamuma ni mtu mmoja, anatakiwa kusimama nyuma kidogo ya imam, upande wa kulia.
- ✿ Safu zinatakiwa kuwa katika mpangilio na isiwepo nafasi ya wazi katikati ya watu. Haifai kuanzisha safu mpya wakati kuna nafasi katika safu za mbele.

Mjumbe wa Allah (s.w) anasema:

**“Pangeni safu zenu barabara, simameni bega kwa bega, fungeni mianya, kuweni wenye kunyumbuka mbele ya ndugu zenu, na msiache uwazi kwa ajili ya shetani. Allah huzipa amani nyoyo za wale wasioacha nafasi katika safu zao. Allah hawapi baraka wale wanaoacha nafasi katika safu zao”** (Abu Dawud, Salat, 93) na alizungumzia kuhusu nafasi ya safu zilizonyooka katika ukamilifu wa swala. Yeye mwenyewe alikuwa akizungukia safu hizo na kugusa vifua na mabega ya Maswahaba na kusema: “Usisogee mbele wala nyuma, ili nyoyo zenu zisitofautiane.” (Abu Dawud, Salat, 93)

### Nini hukmu ya kuswali jama'ah?

Ni wajibu kuswali swala ya ljumlaha kwa jama'ah, na ni sunnah iliyowekewa mkazo (sunnah muakkadah) kuswali swala nyingine katika jama'ah. Kutoswali jama'ah ni kwenda kinyume na sunnah na Mtume wetu (s.a.w).

## ADABU ZA MSIKITI

Unapokuwa msikitini unatakiwa kuwa makini na mambo yafuatayo:

- ✿ Unapoingia msikitini unatakiwa kuwa twahara na kuingia kwa kutumia mguu wa kulia.
- ✿ Unapotoka msikitini anza kwa mguu wa kushoto.
- ✿ Tusikanyage kwenye miswala tukiwa na uchafu miguuni au soksi chafu.
- ✿ Usiwakarabishe waumini kwa kula vyakula vyenye harufu kali kama vile vitunguu, au kwa harufu ya moshi wa sigara na harufu mbaya ya mavazi.
- ✿ Jiepushe na tabia zisizokuwa na heshima kama vile kunyoosha miguu, kuzungumza kwa sauti ya juu, kelele na kujishughulisha na mazungumzo yasiyokuwa na maana, isipokuwa kama kuna dharura.
- ✿ Qur'an inaposomwa au khutba inapotolewa msikitini tunapaswa kusikiliza kwa umakini na kwa heshima.
- ✿ Tunapochelewa, tunatakiwa kukaa eneo lolote badala ya kuwakarabisha watu kwa kujaribu kwenda kwenye safu za mbele.



### Swala ya jama'ah inaswaliwa vipi?

Wakati wa swala ya jama'ah, imam huweka nia ya kuswali na kuongoza swala. Wanaomfuata hunuia kuswali na kumfuata imam.

Tuangalie mfano wa swala ya Adhuhuri inavyoswaliwa katika jama'ah:

1) Kwanza unanuia kwa kusema "ninanuia kuswali swala ya Adhuhuri na kumfuata imam."

2) Imam anaposema "Allahu Akbar" kwa sauti, huanza kuswali kwa kusoma takbir ya ufunguzi kwa kiasi tunachoweza kujisikia sisi wenyewe. (Kadhalika tunarudia rudia takbir zinazosomwa na imam kwa ukimya).

3) Baada ya takbir ya ufunguzi, huifunga mikono yetu na kusoma dua ya wajjahtu. Kisha tunakaa kimya na kumsikiliza imam. Baada ya imam kumaliza kusoma Al-Fatiha, tunasema "amiin" kisha nasi tunasoma Al-Fatiha. Tunafanya hivyo katika rakaa nyiningine za swala.

4) Tunaporukuu tunasema "Subhana Rabbi al-adhim" mara tatu. Kisha imam huinuka na kusema "Samiallahu liman hamidah", nasi huinuka kutoka kwenye rukuu na kusema "Rabbana laka al-hamd." Tunainua mikono yetu mpaka kwenye usawa wa masikio.

5) Katika sijda tunasema "Subhana Rabbiy al-a'la" mara tatu.

6) Tunapokuwa katika hali ya kukaa pamoja na imam, tunasoma dua za "Al-Tahiyyat," "Allahuma Salli," "Allahuma Barik," "Rabbana Atina na Rabbana-ghfirli," kisha tunamsubiri imam kutoa salamu upande wa kulia na anapotoa salamu upande wa kushoto, nasi tunatoa salamu kulia na kushoto.

Tunaposwali nyuma ya imam tunatakiwa kumfuata na kutomtangulia katika matendo.

### Tunaikamilisha vipi swala tunapoikuta katikati?

Tunapochelewa kujumuika katika swala ya jama'a, tunakamilisha rakaa zilizotupita baada ya imam kukamilisha swala. Tukikuta imam hajainuka kutoka kwenye rukuu, tunakuwa tumeidiriki rakaa husika, hatutahitaji kuirudia rakaa hiyo.

Kwa mfano, tukiidiriki jama'ah katika rakaa ya pili, tutamsubiri imam katika kikao cha mwisho asome Al-Tahiyyat na kutoa salamu. Kisha tutasimama na kukamilisha rakaa zilizotupita kama ifuatavyo:



#### Rakaa ya Kwanza

- \* Audhu, Bismillah
- \* Surah al-Fatiha
- \* Surah nyingine
- \* Rukuu
- \* Tuma'ninah
- \* Kutoka kwenye rukuu
- \* I'tidal
- \* Tuma'ninah
- \* Sijda
- \* Tuma'ninah katika sijdah
- \* Kukaa baina ya sijda mbili
- \* Tuma'ninah
- \* Sijda ya pili
- \* Tuma'ninah katika sijda
- \* Kikao cha Tahiyat
- \* Kusoma Tahiyat, Salli – Barik – Rabbana
- \* Salam

Kama tukiidiriki jama'ah katika rakaa ya tatu, baada ya salam ya imam, tutakamilisha rakaa mbili za mwanzo zilizotupita kama ifuatavyo:



Kama tumeidiriki jama'ah katika rakaa ya nne, baada ya salamu ya imam tutakamilisha rakaa tatu za mwanzo zilizotupita kama ifuatavyo:



Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili
<ul style="list-style-type: none"> <li>* Audhu, Bismillah</li> <li>* Surah al-Fatiha</li> <li>* Surah nyingine</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* I'tidal</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda</li> <li>* Tuma'ninah katika sijdah</li> <li>* Kukaa baina ya sijda mbili</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kikao cha pumziko (Itirahah)</li> <li>* Kusimama kwa ajili rakaa ya nne</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Audhu, Bismillah</li> <li>* Surah al-Fatiha</li> <li>* Surah nyingine</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* I'tidal</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kukaa baina ya sijda mbili</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kikao cha Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat, Salli – Barik – Rabbana</li> <li>* Salam</li> </ul>

Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili	Rakaa ya Tatu
<ul style="list-style-type: none"> <li>* Audhu, Bismillah</li> <li>* Surah al-Fatiha</li> <li>* Surah nyingine</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* I'tidal</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda</li> <li>* Tuma'ninah katika sijdah</li> <li>* Kukaa baina ya sijda mbili</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kikao cha Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat, Salli – Barik – Rabbana</li> <li>* Kusimama kwa ajili ya rakaa ya tatu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Audhu, Bismillah</li> <li>* Surah al-Fatiha</li> <li>* Surah nyingine</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* I'tidal</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kukaa baina ya sijda mbili</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kikao cha Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat, Salli – Barik – Rabbana</li> <li>* Salam</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Audhu, Bismillah</li> <li>* Surah al-Fatiha</li> <li>* Surah nyingine</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* I'tidal</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kukaa baina ya sijda mbili</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kikao cha Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat, Salli – Barik – Rabbana</li> <li>* Salam</li> </ul>

Kama tumeidirika jama'ah katika rakaa ya tatu, baada ya salamu ya imam tutakamilisha rakaa mbili za mwanzo zilizotupita kama ifuatavyo:



Kama tukimdiriki imam baada ya rukuu ya rakaa ya mwisho, baada ya salam ya imam tutasimama na kukamilisha rakaa zote kama kamawaida na kukamilisha swala yetu.



Rakaa ya Kwanza	Rakaa ya Pili
<ul style="list-style-type: none"> <li>* Audhu, Bismillah</li> <li>* Surah al-Fatiha</li> <li>* Surah nyingine</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* I'tidal</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda</li> <li>* Tuma'ninah katika sijdah</li> <li>* Kukaa baina ya sijda mbili</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kikao cha Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat, Salli – Barik – Rabbana</li> <li>* Kusimama kwa ajili ya rakaa ya tatu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>* Audhu, Bismillah</li> <li>* Surah al-Fatiha</li> <li>* Surah nyingine</li> <li>* Rukuu</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Kuinuka kutoka kwenye rukuu</li> <li>* I'tidal</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda</li> <li>* Tuma'ninah katika sijdah</li> <li>* Kukaa baina ya sijda mbili</li> <li>* Tuma'ninah</li> <li>* Sijda ya pili</li> <li>* Tuma'ninah katika sijda</li> <li>* Kikao cha Tahiyat</li> <li>* Kusoma Tahiyat, Salli – Barik – Rabbana</li> <li>* Salam</li> </ul>



# BAADHI YA SWALA ZINAZOSWALIWA KWA JAMA'AH

## A. SWALA YA IJUMAA:

Siku za Ijumaa ni sikukuu za kila wiki kwa Waislamu. Katika siku hizo hukutana msikitini, huulizana hali na kusikilizana khabari zao. Husaidiana.

### Kuna rakaa ngapi katika Swala ya Ijumaa na hufanyika wakati gani?

Uislamu umewaaamrisha Waislamu kuacha shughuli zao zote wakati wa swala ya Ijumaa na kuja kuitekeleza.

Ili kuitekeleza swala hiyo lazima iwepo jama'ah ya Waislamu arobaini wenyе sifa akiwemo Imam.

Swala ya Ijumaa ina rakaa mbili. Huswaliwa mahala pa wakati wa swala ya Adhuhuri na kuwa mbadala wa swala ya Adhuhuri ya siku hiyo. Wale wasioweza kutekeleza swala ya Ijumaa kwa sababu ya udhuru wa kisheria wanatakiwa kuswali swala ya Adhuhuri.

### Nani anayewajibikiwa kuswali swala ya Ijumaa?

Swala ya Ijumaa ni wajibu kwa wanaume, watu wazima, wasiokuwa na matatizo ya akili, wenyе afya inayowawezesha kufika msikitini, na wakazi wa eneo husika; yaani wale wanaoishi hapo na hawatoki isipokuwa kwa haja maalumu.

### Nani asiyewajibikiwa na Swala ya Ijumaa?

Wanawake, watoto, wagonjwa wasioweza kufika msikitini, wale wanaowahudumia wagonjwa, wasafiri, watumwa, vipofu ambaو hawana mtu wa kuwafikisha msikitini, viwete, na vikongwe wasioweza kufika msikitini. Japokuwa sio wajibu kwao, lakini wakiitekeleza swala ya Ijumaa swala hiyo ni sahihi na hawatahitajika kuswali swala ya Adhuhuri ya siku hiyo.

### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

Enyi mlilo amini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wachenii biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua.

(Jumu'a, 62; 9)

### Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

Na itakapo kwisha Sala, tawanyikeni katika nchi mtafute fadhilli za Mwenyezi Mungu, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufanikiwa.

(Jumu'a, 62; 10)

### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Iwapo hayakufanyika madhambi makubwa, swala tano za kila siku huwa ni kafara ya dhambi ndogo zinazofanywa baina ya swala mbili na swala ya Ijumaa huwa ni kafara ya dhambi ndogo zinazofanywa kuanzia Ijumaa moja mpaka Ijumaa ijayo".

(Muslim, Taharat 14)

### Ni zippi shuruti za swala sahihi ya Ijumaa?

1. Eneo la Swala ya Ijumaa linatakiwa kuwa eneo linalokaliwa na jamii inayotosha kuitekeleza, kama vile kijiji au mji.
2. Katika eneo hilo, wanatakiwa wawepo angalau waumini arobaini wenyewe sifa akiwemo imam.
3. Swala ya Ijumaa inatakiwa kuswaliwa katika wakati wa Swala ya Adhuhuri.
4. Swala ya Ijumaa inatakiwa kuswaliwa kwa jama'ah.
5. Kutolewa kwa khutba mbili.

### Ni yapi mambo ambayo ni sehemu ya khutbah?

Shuruti tatu za mwanzo hapa chini zinatakiwa katika khutba zote mbili:

1. Hamdala: Kumhimidi Allah Mtukufu au kusema "al-Hamdu lillah" (Himidi ni za Allah)
2. Salwala: Kumtakia rehma Mtume (s.a.w).

3. Kuusia kuhusu taqwa au uchamungu: Kuwapa wosia waumini katika mambo ya dini na dunia.
4. Kusoma ayah ya Qur'an (hili linatakiwa katika mojawapo ya khutba mbili).
5. Kuwaombea dua waumini. (Hili linatakiwa katika khutba ya pili).

### Ni kwa namna gani tunaswali swala ya Ijumaa?

- ❶ Ni Sunnah kuswali rakaa mbili kabla ya Swala ya Ijumaa.
- ❷ Imam anapanda juu ya minbari na kuketi.
- ❸ Muadhini hutoa adhana ya ndani.
- ❹ Baada ya adhana, imam hunyanyuka na kutoa khutba mbili. Ni lazima khutba hizi kutolewa na kusikilizwa.
- ❺ Baada ya khutba, imam hutoka juu ya minbari na muadhini hukimu swala. Hapo tunaswali rakaa mbili za faradhi ya Ijumaa katika jama'ah.



© Adem Ozdemir

## B. SWALA ZA EID:

Kwa mwaka tuna Sikuu mbili za kidini. Moja inaitwa Eid al-Fitr (sikuu inayoashiria kumalizika kwa mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan) na nyingine ni Eid al-Adh-ha (yaani sikuu inayoashiria kumalizika kwa ibada ya Hijja). Katika sikuu hizi, huwa tunaswali swala yenye rakaa mbili ili kumshukuru Allah.

### **Swala ya Eid inatekelezwa wakati gani?**

Swala ya eid huswaliwa siku ya eid baada ya jua kuchomoza. Inapendekezwa kusubiri dakika 40-45 baada ya jua kuchomoza.

### **Swala ya Eid inaswaliwa vipi?**

Swala za Eid zinaweza kuswaliwa katika jama'ah lakini jama'ah sio lazima. Swala hizi hazina adhana wala iqamah. Tunanuia na kumfuata imam. Kisha tunaanza kuswali kama ifuatavyo:

**Rakaa ya kwanza:** Tunanuia na kuinua mikono yetu, tunatoa takbira ya ufunguzi na kuinua mikono yetu mpaka usawa wa masikio

baada ya imam. Tunasoma dua ya wajjahtu. Kisha tunatoa takbira na kuinua mikono yetu mpaka kwenye usawa wa masikio mara saba kabla ya kusoma audhubillah, bismillah na Surah al-Fatiha. Katikati ya kila takbira tunaifunga mikono yetu juu ya kitovu na kusema "Subhanallah wa al-hamdulillahi wa la ilaha illalahu wallahu akbar (Utukufu ni wa Allah, himidi ni za Allah, hakuna mungu ila Allah, Allah ni mkubwa)".

Baada ya takbira saba, tunasoma audhubillah, bismillah, surah Al-Fatiha na ayah nyingine kutoka ndani ya Qur'an kabla ya rukuu.

**Rakaa ya pili:** Baada ya kuinuka kutoka kwenye sijda za rakaa ya kwanza, tukiwa tunamfuata imam, tunainua mikono yetu mpaka kwenye usawa wa masikio yetu na kusoma takbira kama tuliyofanya katika rakaa ya kwanza. Hata hivyo, mara hii tunatoa takbira mara tano. Baada ya kumaliza takbira hizo, tunasoma audhubillah, bismillah, Fatiha na ayah nyingine kutoka ndani ya Qur'an kabla ya kurukuu. Swala ya eid hukamilika baada ya kumaliza mambo mengine yote yaliyobaki katika rakaa hii.

### **Khutba ya eid hutolewa wakati gani?**

Khutba ya eid hutolewa baada ya swala na ni sunnah ya bwana wetu Mtukufu Mtume (s.a.w).

Kwa kawaida mtu anayetoa khutba huzungumzia maana na umuhimu wa siku hiyo. Baada ya kumaliza khutba na dua, Waislamu husalimiana na kupongezana katika sikuu yao. Hata watu wenye maelewano mabaya hukumbatiana na kusameheana.

### **Takbir al-Tashriq ni nini na inasomwa wakati gani?**

Takbira zinazosomwa baada ya kila swala ya faradhi katika siku za Eid al-Adha huitwa Takbir al-Tashriq. Takbira hizi ni sunnah na husomwa baada ya swala za faradhi kuanzia swala ya al-fajiri ya siku ya kabla ya eid na kumalizika wakati wa swala ya adhuhuri ya siku ya nne ya eid. Tunasoma takbira hizi katika swala za jama'ah au swala binafsi.





Vilevile, Takbir al-Tashriq husomwa baada ya swala za maghribi na Isha siku moja kabla ya Eid al-Fitr na baada ya swala ya alfajiri ya siku ya eid al-Fitr.

#### Ni upi muundo wa Takbir al-Tashriq na inamaanisha nini?

Hapa chini ni muundo wa Takbir al-Tashriq:

اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ  
 اللَّهُ أَكْبَرُ وَلِلَّهِ الْحَمْدُ

"Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar,  
La ilaha illallahu wallahu akbar, Allahu Akbar wa  
lillahi'l-Hamda"

**Maana yake:**

**"Allah ni Mkubwa, Allah ni Mkubwa, Allah  
ni Mkubwa. Hakuna mola apasaye kuabudiwa  
kwa haki ila Allah. Allah ni Mkubwa, Allah ni  
Mkubwa na himidi zote ni za Allah".**

#### C. SWALA YA MAITI

Swala ya maiti ni dua maalumu kwa ajili ya ndugu zetu Waislamu wanapofariki dunia. Japokuwa huswaliwa kwa jama'ah, swala hii inaweza pia kuswaliwa na mtu mmoja mmoja.

#### Nini hukmu ya swala ya maiti?

Kumswalia maiti ni faradhi toshelezi (fardh al-kifayah) kwa umma wa Kiislamu. Kwa maneno mengine baadhi ya Waislamu wanapoitekeleza faradhi hii, hupata thawabu na jukumu la Waislamu wengine huwa limeondoka. Lakini, iwapo hakutokea mtu yeyote wa kutekeleza faradhi hiyo, jamii yote ya Kiislamu katika eneo husika hubebeshwa dhamana na huwa imetenda dhambi.

#### Swala ya maiti inaswaliwa vipi?

Swala ya maiti ni swala isiyokuwa na rukuu wala sijda. Huswaliwa kwa kunuia na kisha kutoa takbira nne:

Tunasimama katika safu na kuacha nafasi ambayo jeneza litawekwa mbele yetu na kunuia kwa kusema "ninanuia kumswalia maiti na kumfuata imam". Kisha tunainua mikono yetu na kutoa takbira ya ufunguzi. Baada ya takbira ya ufunguzi tunawenza mkono wa kulia



#### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Yeyote atakae hudhuria msiba mpaka akaswaliwa maiti, basi atapata malipo ya milima miwili na yeyote atakae lisindikiza jeneza mpaka akazikwa atapata malipo ya miliva miwili."

(Bukhari, Jenazah 59)



kwenye mkono wa kushoto juu ya kitovu na kusoma Surah al-Fatiha.

Tunainua mikono yetu na kutoa takbir ya tatu na kumtakia rehma Mtume (Allahumma salli na Barik). Baada ya takbir ya tatu tunamuombea marehemu. Baada ya takbir ya nne na ya mwisho, ni sunna kusema, "Ewe Allah! Usitunyime malipo yake, usitupe mtihani baada yake, tusamehe sisi na yeye." (Dua hii inatakiwa kusomwa kwa lugha ya Kiarabu kama ilivyoandikwa hapo chini). Kisha tunakamilisha swala ya maiti kwa kutoa salamu upande wa kulia na wa kushoto.

#### Dua ya kumuombea marehemu:

Kama marehemu ni mwanaume unasema:

**اللَّهُمَّ تَحْرِمُنَا أَجْرَهَا وَلَا تَفْتَأِنَا بَعْدَهَا  
وَاعْفُ عَنَّا وَعَنْهَا وَاغْفِرْ لَنَا وَلَهُ**

Kama ni mwanamke unasema:

**اللَّهُمَّ تَحْرِمُنَا أَجْرَهَا وَلَا تَفْتَأِنَا بَعْدَهَا  
وَاعْفُ عَنَّا وَعَنْهَا وَاغْفِرْ لَنَا وَلَهُ**

Baada ya swala hiyo, tunaifariji familia, jamaa na marafiki wa marehemu. Tunakaa nao na kuwaunga mkono kwa kuondokewa na mpendwa wao na kuhuzuniaka pamoja nao.

#### D. SALA YA TARAWIH (Salat-al-Tarawih)

Swala ya Tarawih ina rakaa ishirini na huswaliwa wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan baada ya swala ya Ishaa. Ni Sunnah al-Muakkadah kuswali swala hii kwa wanaume

#### Mtume wetu (s.a.w) anasema:

“Mwenye kuswali swala za usiku wakati wa mwezi wa Ramadhan kwa imani ya dhati na kutarajia kupata malipo ya Allah (sio kwa kujiongesha), atasamehewa madhambi yake yote yaliyopita”

(Bukhari, Iman, 37)

na wanawake. Ni sunnah kuswali tarawih hata kwa wale wenye udhuru wa kutofunga.

#### Je, ninaweza kuswali tarawih nikiwa peke yangu?

Ndiyo. Baadhi ya nyakati, Mtume wetu (s.a.w) alikuwa akiswali tarawih kwa jama'ah na wakati mwininge akiswali peke yake lakini hakuwahi kuacha kuiswali. Wakati wa zama za Sayyidna Umar (r.a) ilianza kuswaliwa kwa jama'ah na kuendelea mpaka hivyo mpaka leo.

Hivyo, kama tunavyoweza kuswali tarawih misikitini kwa jama'ah, vivyo hivyo tunaweza kuiswali majumbani mwetu tukiwa peke yetu. Hata hivyo, tunapata thawabu nyingi zaidi tukiiswali kwa jama'ah.

#### Namna gani tunaswali tarawih?

Tarawih huswaliwa baina ya swala ya Ishaa na witri. Ina rakaa ishirini ambazo zinaweza kuswaliwa kwa rakaa mbili mbili.

## SWALA YA MGONJWA

#### Tunaswali namna gani tunapokuwa wagonjwa?

Dini yetu nzuri imeweka baadhi ya sheria zinazohusu mazingira maalumu ili kulturahisishia kutekeleza majukumu yetu. Tunapokuwa wagonjwa sana kiasi cha kutoweza kusimama, tunaruhusiwa kuswali tukiwa tumekaa. Iwapo hatuwezi kukaa, tunaweza kuswali tukiwa tumelala na kuashiria kwa kichwa kadiri iwezekanavyo badala ya kurukuu na kusujudu.

#### Nitaswali vipi iwapo ninaumwa sana na siwezi kuashiria kwa kichwa?

Iwapo hatuwezi hata kuashiria kwa kichwa, tutaaahirisha swala zetu mpaka tutakapojsikia nafuu. Tukipata nafuu tunalipa swala ambazo hatuwezi kuzitekeleza.



## SWALA YA MSAFIRI

**Ni wakati gani tunahesabika kuwa ni wenyewe kusafiri kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu?**

Tunahesabika kuwa tuko safarini iwapo tunasafiri nje ya mji au kijiji chetu kwa umbali usiopungua kilometra 83 na iwapo tutakaa huko kwa zaidi ya siku nne bila kujumuisha siku za kukaa njiani.

**Safari inaaza na kuishia wakati gani?**

Safari huanza pale tunapoondoka mjini kwetu na kuisha pale tunaporudi.

**Tunatekeleza vipi swala zetu tunapokuwa safarini?**

Tukiwa safarini na tukawa tunaswali nyuma ya imam ambaye sio msafiri (muqim), hatuwezi kupunguza swala zetu. Tunalazimika kumfuata imam na kutekeleza swala zetu kama afanyavyo.

**Iwapo imam ni msafiri, wakaazi (muqim) watakelezaje swala zao?**

Iwapo msafiri ndiye imam wa swala, atapunguza swala yake na kuikamilisha mwishoni mwa rakaa ya pili ya swala zenyeye

rakaa nne. Iwapo katika wanaomfuata kuna ambaio sio wasafiri, hawatapunguza swala zao bali watakamilisha rakaa mbili zilizobaki.

**Nini maana ya kukusanya swala mbili (jam' al-salah) wakati wa safari?**

Wakati wa safari au kuna hali ya dharura kubwa kama vile hali mbaya ya hewa, inaruhusiwa kuzikusanya swala za Adhuhuri na Alasiri kwa wakati wa swala moja wapo; na kadhalika inaruhusiwa kukusanya swala za Maghribi na Isha waliki wa swala moja wapo. Iwapo ukusanyaji huo utafanyika wakati wa swala ya kwanza (yaani Adhuhuri au Maghribi), huitwa jam' al-taqdim; na iwapo utafanyika wakati wa swala ya pili (yaani Alasiri au Isha), huitwa jam' al-Ta'khir..



## KULIPA SWALA (SALAT AL-QADHAA)

**Salat al-Qadhaa ina maana gani?**

⦿ Kutekeleza swala kwa wakati huitwa "adaa", na kutekeleza swala nje ya wakati hujulikana kama "Kulipa Swala Salat al-Qadhaa au kulipa swala".

Wale wanaopitwa na swala hawatakiwi kuswali swala za Sunnah mpaka walipe swala zilizowapita.

**Nini hukmu ya kupitwa na swala?**

Kama ambavyo ni faradhi kwetu kutekelezwa swala ndani ya muda wake sahihi, vivyo hivyo tuna wajibu wa kulipa swala zilizotupita. Kadhalika, ni dhambi

kubwa kuakhirisha swala mpaka baadaye au kutoitekeleza ndani ya wakati wake bila udhuru wa kisheria.

**Tunalipa vipi swala zetu?**

Iwapo tumepitwa na swala ya Alfajiri, tunaweza kuilipa pamoja na sunnah zake mpaka jua linapokuwa kwenye nusu ya upeo. Baada ya jua kupitia nusu ya upeo, ni rakaa za faradhi pekee ndizo zinazotakuwa kulipwa. Ama kwa swala nyingine, rakaa za faradhi pekee ndizo zinazolipwa. Hatutakiwi kuswali sunnah mpaka tunapokamilisha kulipa swala zetu.

### Nia ya kulipa swala inafanywaje?

Kwa mfano unataka kunuia kulipa swala ya alfajiri, unasema "ninanuia kulipa swala ya alfajiri ambayo sikuweza kuiswali leo." Iwapo hatukumbuki siku ambayo swala husika ilitupita, tunanuia kwa kusema "ninanuia kulipa faradhi ya mwisho ya alfajiri ambayo sikuweza kuitekeleza kwa wakati."

### Ni wakati gani tunaoweza kulipa swala (Salat al-Qadhaa)?

Tunaoweza kulipa swala muda wowote wa siku husika.

## SHETANI ANATAKA KUTUZUIA NA SWALA

Swala ni ibada kubwa. Ili kutuzuia tusifanye ibada hii, Shetani haachi kutuvekea mawazo na fikra zenyе kutupa shaka. Muda wa swala unapowadia na tukataka kujijandaa, Shetani hufanya juhudzi za kutuzuia tusiwali kwa kututia wasiwasi na kutunong'oneza kuwa: "Muda bado upo" au "Sasa hivi unafanya kazi, maliza kwanza kazi yako" au "unaweza kuswali hata baadaye. Umechoka sana, hukupata muda wa kulala... lala kidogo..." Hivyo, Shetani hutuvekea vingi na kutusababishia kupitwa na swala.

Wakati mwingine Shetani hujaribu kutuzuia tusiwali kwa kuwatumia watu wengine. Tunapokuwa pamoja na watu wengine, Shetani hutupatia mawazo kama vile: "Bado kuna muda. Maliza kwanza jambo hili. Piga soga kidogo unaweza kuswali baada ya marafiki kuondoka." Katika hali kama hizo, tukifanikiwa kuswalia na kusema "ni muda wa swala", tunakuwa tumemshinda Shetani.

Kitu kingine ambacho shetani hukifanya sana ni kutufanya tuswali haraka haraka. "Una mambo mengi ya kufanya. Swali haraka haraka." Kwa

kutukumbusha mambo tunayotakiwa kufanya huku tukiwa katika swala,

Shetani hutuharakisha kana kwamba tunachelewa. Hivyo, shetani hutufanya tusitekeleze kikamilifu nguzo za swala (arkan al-salat) na kushindwa kufanya rukuu na sajda vizuri. Kwa hakika, tunapoyafikiria, kwakulinganishana muda unaotumika katika swala, tunatambua kiasi gani cha muda tunachokipoteza katika kufanya mambo mengine.

Ili kutuzuia tusiwali, shetani hutumia njia na mitego mbalimbali ambayo hatuwezi kuidhania. Miiongoni mwa mitego hiyo ni hii ifuatayo: shetani huenda kwa masikini na fukara na kuwaambia waache kuswali kwa kuwashawishi:

"Swala haiwafai. Swala inawafaa wale wenye mali na neema mbalimbali walizopewa na Allah." Huenda kwa wagonjwa na kuwashawishi "Acha kuswali, kwa sababu Allah anasema 'hakuna mzigo kwa wagonjwa'. Unaweza kuswali sana utakapopona". Kwa kutumia njia hiyo, shetani huwfanya wanaacha kuswali. Shetani hujaribu kutuzuia kuswali kwa kutengeneza nyudhuru kulingana na hali au kazi ya mtu.

Njia bora ya kuepukana na wasiwasi wa shetani ni kuijiweka katika hali ya wudhu muda wote na kutekeleza swala zetu punde muda unapoingia.

# SAJDA YA KUSAHAU (SAJDAT AL-SAHW)

## Sajdat al-sahw ina maana gani?

✍ Sajdat al-sahw ina maana ya sijda ya kusahau au sijda ya jambo lillilokosewa.

Wakati wa swala tukifanya kosa kwa bahati mbaya, kosa ambalo halibatilishi swala, tunatakiwa kufanya sijda ya kusahau mwishoni mwa swala yetu. Sijda hii hufanywa ili kurekebisha upungufu uliojitokeza katika swala, na ni sunnah.

## Sajdat al-sahw hutakiwa kufanyika wakati gani?

1. Mtu akisahau moja ya sunnah kuu za swala, kwa mfano akisahau kukaa tashahhud ya kwanza au kusoma dua ya qunut, atatakiwa kuleta sijda ya kusahau.

2. Akiwa hana uhakika wa idadi ya rakaa alizoswali, ni sunnah kwake kuleta sijda ya kusahau.

Tunapokuwa na shaka kama tumeswali rakaa fulani au la, tunatakiwa kuendelea na dhana kuwa hatukuiswali rakaa husika na kuleta sijda ya kusahau mwishoni mwa swala yetu. Hufanyika hivyo kwa sababu ya uwezekano kwamba tumeswali rakaa ya ziada. Kwa mfano, unapojiwa na shaka katika rakaa ya tatu katika swala ya rakaa nne kwamba uko katika rakaa ya tatu au ya nne, na kama bado unaswali, unatakiwa kuchukulia kwamba upo katika rakaa ya tatu na kumalizia rakaa moja zaidi kisha utaleta sijda ya kusahau.





3. Iwapo kwa bahati mbaya yamefanyika makosa ambayo yangetabilisha swala kama yangefanywa kwa makusudi. Kwa mfano, kuzungumza maneno machache au kuongeza kwa bahati mbaya rakaa moja na kugundua kosa husika kabla ya kukamilisha swala, basi mtu huyo ataleta sijda ya kusahau.

4. Iwapo mfuatano wa matendo ambayo ni sehemu au ni ya wajibu katika swala ukibadilishwa; kusoma sura au dua


nje ya eneo lake, ni sunnah kuleta sijda ya kusahau. Kwa mfano, iwapo atasoma Surah Al-Fatiha badala ya tashahhud au akasoma qunut wakati wa sijda au akasoma surah ya ziada baada ya kutoka kwenye rukuu badala ya kuisoma baada ya Surah Al-Fatiha, itakuwa sunnah kwake kuleta sijda ya kusahau.

**Tukifanya zaidi ya kosa moja katika swala, tutaleta sijda ngapi za kusahau?**

Sijda moja itatosheleza makosa yote yanayohitaji sijda ya kusahau.

**Sijda ya kusahau (sajdat al-sahw) hufanywaje?**

Katika kikao cha mwisho cha swala, husomwa du azote na kabla ya kutoa salam anatakiwa kusujudu mara mbili. Baada ya sijda hizo, atatoa salam bila kusoma dua nydingine yoyote.



# SAJDA YA KISOMO (SAJDAT AL-TILAWAH)

## Sajdat al-Tilawah ina maana gani?

Kuna ayah fulani ndani ya Qur'an Tukufu zinamlazimu mtu kusujudu anapozisoma, kuzikiliza au kuziskia tu. Sijda tunayoifanya wakati wa kusoma, kusikiliza au kusikia ayah hizi huitwa Sajdat al-Tilawah.

## Kuna ayah ngapi ndani ya Qur'an zinazolazimu sijda (Ayat al-Sajdah)?

Kuna Ayah kumi na nne za sajdah ndani ya Qur'an Tukufu. Ayah hizo hazijumuishi sijda inayopatikana katika Surah Swad (38: 24), ambayo ni sijda ya shukrani, sio sijda ya kisomo. Tofauti na sijda nydingine, sijda hii sio sunnah iliyowekewa msisitizo na hufanywa tu nje ya swala.

## Nini hukmu ya Sajdat al-Tilawah?


Kwa wale wanaosoma, kusikiliza au kusikia moja ya ayah hizi, ni sunnah muakkadah kuleta sijda ya kisomo.

## Sajdat al-Tilawah hufanywaje ndani ya swala?

Tunaposoma moja ya ayah hizi wakati wa swala, tunasema "Allahu Akbar" na kwenda kwenye sijda. Tunasema "Subhana Rabbi al-A'la" mara tatu na kisha husimama kwa kusema "Allahu Akbar" na kuendelea na swala kwa kisomo au kwenda kwenye rukuu.

## Sajdat al-Tilawah inafanywaje nje ya swala?

Tunaposoma moja ya ayah hizi nje ya swala, tunasujudu kama ifuatavyo: Sijda ya kisomo huchukuliwa kama swala hivyo tunatakiwa kuwa na tohara, lakini kisimamo (qiyam) sio lazima, tunaweza kuifanya tukiwa tumekaa. Kisha tunaelekea upande wa qibla na kusema "Allahu Akbar" kwa kuinua mikono yetu. Kisha tunasujudu na kusema mara tatu "Subhana rabbi al-A'la". Tunakaa kitako kwa kusema "Allahu Akbar". Hatimaye tunatoa salamu na kukamilisha sijda yetu.



## NYAKATI ZISIZOFAA KUSWALI (AWQAT AL-KARAHAH)

**Swala zipi ambazo kuna nyakati za karaha kuziswali?**

Hakuna wakati wa karaha kwa swala ambazo sababu zake za kuswaliwa zimeshapitishwa.

Swala hizo ni hizi zifuatazo:

Swala zilizompita muumini, swala ya kukamatwa mwezi au jua, swala ya kuomba mvua, swala baada ya kuizunguka Ka'bah Tukufu, swala baada ya wudhu, swala ya kuuamkia msikiti, na swala ya maiti.

Hakuna wakati wa karaha au uharamu kuswali ndani ya Eneo Tukufu (Haram) la Makka wakati wowote.

**Je, katika siku kuna nyakati ambazo ni karaha kuswali?**

Kuna baadhi ya nyakati ambazo ni karaha kuswali swala za faradhi na swala zinazoswaliwa kwa sababu inayojitokeza baada ya swala husika, kama vile swala inayoswaliwa kabla ya kuingia katika hali ya ihram na swala ya istikhara. Nyakati hizo ni:

1. Baada ya kuswali alfajiri mpaka jua linapochomoza.
2. Kuanzia jua linapochomoza mpaka jua linapokuwa kwenye urefu wa mkuki juu anga. (Takriban dakika 40 – 45 baada ya jua kuchomoza).
3. Kuanzia muda ambao jua linakuwa kwenye nusu ya upeo mpaka linapoendelea.
4. Baada ya kuswali Alasiri mpaka jua linapozama.
5. Dakika 45 kabla ya jua kuzama kwa wale ambao hawakuswali Alasiri.

## SWALA ZANGU

Maneno ya bibi yake yalikuwa yakirindima masikioni mwake:

— Mwanangu, inakuwaje unachelewa kuswali mpaka muda huu?

Bibi yake alikuwa kwenye umri wa miaka sabini. Lakini, kila adhana ilipotoka, alikuwa akifanya haraka kuchukua wudhu kwa kasi isiyotarajiwa kutohama na umri wake, na kuswali. Yeye mwenyewe alikuwa hana uwezo wa kujidhibiti. Kilichokuwa kikitokea ni kwamba, daima alichelewesha swala mpaka dakika ya mwisho, na hivyo kuiswali haraka haraka. Aliamka na kutazama saa yake. Zilikuwa zimebaki dakika kumi na tano tu kuingia swala ya Ishaa.

Aliwaza tena: "Kwa mara nyingine nimechelewa kuswali", akatikisa kichwa chake kulia na kushoto kwa masikitiko. Alichukua wudhu haraka haraka. Bila hata kujikausha, alikimbilia chumbani kwake na kuswali swala ya maghribi haraka haraka. Hakuacha kumfikiria bibi yake wakati akisoma dua na tasbihi.

— Angeniona katika hali hii angekasirika sana

Alimpenda sana bibi yake. Alikuwa akimtazama kwa kumstaajabia mwanamke huyo aliyebarikiwa wakati akiswali, kana kwamba anatazama upinde wa mvua. Mwanamke huyo alikuwa mnyenyeketu sana katika swala kiasi kwamba adhana yake ilionekana. Alijihisi mpweke kila alipomkumbuka. Siku hiyo alichoka sana mpaka wakati wa jioni. Alisujudu na kuomba dua. Baada ya dua alitafakari sana kuhusu hali hiyo. Aliyafumba macho yake.

— "Nimechoka sana", aliwaza. Katika mawazo hayo alipitiwa na usingizi na kuona ndoto.

Katika ndoto hiyo aliona Siku ya Hukumu. Kulikuwa na mkusanyiko wa watu wengi. Kulikuwa na watu kila mahali. Baadhi yao



walikuwa wakitazama pembedi wakiwa wameganda bila kutikisika; baadhi walikuwa wakikimbia, na baadhi walikuwa wamepiga magoti wakisubiri huku wakiwa wamevishikilia vichwa vyao kwa mikono yao. Moyo wake ulikuwa ukipiga kwa kasi, kana kwamba ulikaribia kuchomoka, na alikuwa na jasho baridi. Duniani alisikia kuhusu Kuulizwa na Kuhojiwa, Mizani na Daraja la Sirat. Misamiati hii ya Siku ya Hukumu ilikuwa maarufu kwake. Lakini, hakutegemea kuwa yangekuwa ya kuogopesha kiasi hiki. Maswali kuhusu amali yalikuwa yakiendelea. Hapo jina lake likaitwa. Alitazama kulia na kushoto, akashtuka:

— "Umeliita jina langu?" Alisema kwa sauti yenye kutetemeka.

Ghafla umati wa watu ultengeneza njia na kumpisha. Watu wawili wallishika mikono yake. Ni dhahiri kuwa walikuwa kazini. Alitembea katikati ya umati ule, alikuwa ametatizika. Wote watatu walifika mbele. Malaika wakaiacha mikono yake. Alikiinamisha kichwa chake. Maisha yake yote yalikuwa yakinipa mbele ya macho yake kama mkanda wa filamu. Ilikuwa Siku ya Hukumu.

— “Ninamshukuru Mungu”, alijisemea na kuendelea:

“Nimekuwa mionganini mwa watu wema tangu nilipozaliwa. Baba yangu alikuwa akitoka kwa sheikh mmoja kwenda kwa mwingine kwa ajili ya kujifunza Uislamu na akatumia mali zake kwa ajili ya Uislamu.

Mama yangu alikuwa akiwaalika wageni na muda wote chakula kiliandaliwa nyumbani kwetu kwa ajili yao.

Ama kuhusu mimi, daima nimekuwa nikifuata nyayo zao. Nilijitahidi kuwashudumia na kuwasaidia watu. Nilizungumza nao kuhusu Allah na kutekeleza swala zangu. Nilitekeleza ibada ya funga. Nilitekeleza kila nililofaradhishiwa, na kuijweka mbali na kila kilichokatazwa”.

Wakati machozi yakinirika kutoka machoni mwake, alikuwa akiwaza: “Ninampenda Mola wangu, nadhani angalau hilo nimelifanya.” Lakini wakati huo huo alikuwa akiwaza: “Chochote nilichokifanya kinaweza kisitoshe mbele ya Mola wangu. Amali zangu haziwezi kutosha kunipatia Pepo.”

Rehma ya Allah ndiyo lililokuwa kimbilio lake la pekee.

Hatua ya kuhojiwa ilikuwa ikiendelea. Alikuwa akitokwa na jasho na kutetemeka.

Alikuwa akisubiri matokeo ya Hukumu. Hatimaye matokeo yalikaribia kutangazwa. Malaika wakiwa wameshika karatasi mikono mwao, waliugeukia umati.

Jina lake ndilo lililoanza kuitwa. Miguu yake ilikuwa ikitetemeka mno. Alikaribia kudondoka.

Aliyafumba macho yake akiwa mwenye shauku na kuyatega masikio yake ili kusikia matokeo. Sauti ilisikika kutoka kwenye umati. Alikuwa akisikia sawa sawa? Jina lake lilikuwa katika orodha ya wale waliopelekwa motoni! Alianguka na kushtuka mno. “Haiwezekani”, alipiga kelele na kukimbia.

“Inawezekanaje niwe mionganini mwa wale wanaoenda motoni? Maisha yangu yote nilikuwa pamoja na wale waliomtumikia Allah. Nilifanya juhudhi kubwa pamoja nao. Daima niliwaambia wenzangu kuhusu Mola wangu...”



Alilia sana. Malaika wawili waliishika mikono yake, walipasua njia katikati ya umati. Walitengeneza moto mkubwa wenye miale iliyofika mawinguni. Alihangaika lakini hakuweza kujikoo. Hapakuwa na tumaini la msaada? Hakuna ambaye angekuja kumtetea?

Maneno yaliyochanganyika na hali ya kusihii na kuomba yalimtoka bila hiari:

"Ibada zangu... funga... visomo vyangu vya Qur'an... swala zangu... je, haya yote hayataniokoa?"

Alikuwa akililia msaada. Malaika wa Motoni waliendelea kumkokota. Alikuwa karibu sana na moto. Alitazama pembedi kama hangaiko lake la mwisho. Alikumbuka maneno ya Mjumbe wa Allah (s.a.w):

"Kama ambavyo mto unaopita mbele ya nyumba ya mtu humtakasa mtu huyo anayeokoga katika mto huo mara tano kwa siku, kuswali mara tano kila siku hututakasa dhidi ya dhambi." Aliwaza:

"Je, swala zangu hazitaniokoa?"  
Alilalama:

"Swala zangu... swala zangu... swala zangu...."

Malaika hawakumuacha hata kidogo, waliendelea kutembelea mpaka walipofika kwenye shimo kubwa la Moto. Joto la ndimi za moto lilikuwa likiuchoma uso wake. Aligeuka kwa mara ya mwisho na kutazama nyuma. Sasa, macho yake yalikuwa makavu pia. Matumaini yake yalikuwa yameondoka. Aliinamisha kichwa chake na kuning'inia. Vidole vilivyouwa vimeushikilia mikono yake viliachia. Malaika mmoja alimsukuma. Ghafla akajikuta akielea angani. Alikuwa akianguka kuelekea motoni. Ghafla, mtu akaushika mkono wake. Aliinua kichwa chake na kutazama juu. Mzee mmoja mwenye ndevu ndefunyeupe alimuokoa asiangukie chini.

Mzee yule alimkokota na baada ya kutoka katikati ya ndimi za moto, alimtazama mzee yule usoni.

"Wewe ni nani?" aliuliza.

Mzee alitabasamu na kusema: "Mimi ni swala zako".

"Kwa nini ulichelewa? Umeniokoa mwisho mwisho. Nilikaribia kuanguka".

Mzee akatabasamu, akatikisa kichwa chake na kusema:

"Hukumbuki? Daima ulikuwa ukinitekeleza mwishoni."

Hapo aliamka, akainua kichwa chake kutoka kwenye sijda. Alikuwa amelowa kwa jasho. Alisikiliza sauti iliyokuwa ikitoka nije, ilikuwa sauti ya adhana ya swala ya Isha.

Alisimama kwa haraka, akaenda kuchukua wudhu kwa ajili ya swala ya Isha.

**(ABDULLAH DEMIR – Jarida la Sizinti)**



# MTUME WETU (S.A.W) ALIPENDA SANA KUSWALI

Mtume wetu (s.a.w) aliiita swala kuwa ni "nuru ya macho yangu", kwa sababu aliichukulia kama njia nzuri kabisa ya mtu kuonesha upendo na utii wake kwa Allah. Aliswali kwa wakati. Alipenda kuswali mara muda unapowadia, hakupenda kuchelewesha swala na alisema: "**Radhi ya Allah ipo mwanzoni mwa muda wa swala, na mwishoni kuna msamaha Wake.**" (Tirmidhi, Salat, 13).

Kwa kauli hii, alikuwa akisisitiza kuwa Allah hufurahishwa na wale wanatekeleza swala zao katika muda wake wa mapema, na huwahurumia na kuwasamehe wale wasioichelewesha.

Muda wa swala unapoingia, Mtume wetu (s.a.w) alikuwa akiacha kila kitu pembedi. Mama yetu Aisha (r.a) alisema yafuatayo kuhusu swala ya Mtume (s.a.w):

**"Mijumbe wa Allah alikuwa akizungumza nasi, na tukizungumza naye. Lakini, muda wa swala unapofika, alikuwa kana kwamba hatujui na kumuelekea Allah kwa mwili na moyo wake."** (Fadail-i A'mal, 303)

Mbali na swala za faradhi, alikuwa akiswali swala za sunnah kila alipopata fursa ya kufanya hivyo. Anapofurahi alikuwa akiswali kama ishara ya furaha yake. Kadhalika, anapokuwa na huzuni alikuwa akiswali ili kuimarisha subira yake.

Wakati fulani aliswali mpaka miguu yake ikavimba. Bibi Aisha (r.a) alipomuuliza: "Ewe Mjumbe wa Allah! Kwa nini unaswali sana na kujichosha hali ya kuwa umeshasamehewa dhami zako zote?" akasema "**Ewe Aisha! Je,**

**sipaswi kuwa mja mwenye kumshukuru Mola wake?**"

Kamwe mjumbe wa Allah hakuacha kuswali hata katika nyakati ngumu sana za maradhi yake. Japokuwa ugonjwa wake ulikuwa ukiongezeka na mwili wake kuchoka, alienda msikitini kwa msaada wa maswahaba wawili na kushiriki swala ya Alasiri katika jama'ah. Muda mfupi kabla ya kifo chake, aliwakumbusha wafuasi wake mambo muhimu na kusema: "**Msiache swala! Msiache swala!**

**Muongopeni Allah kwa kuheshimu haki za watumishi, wake na watoto wenu!**" (Abu Dawud, Adab, 123-124)

## Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na waamrishe watu wako kusali, na uendelee mwenyewe kwa hayo. Sisi hatukuombi wewe riziki, bali Sisi ndio tunakuruzuku. Na mwisho mwema ni kwa mchamngu."

(Taha, 20: 132)



## Mtume wetu (s.a.w) anasema:

"Unaposwali, swali kana kwamba ni swala yako ya mwisho! Usiseme mambo ambayo utayajutia kesho!"

(Ibn Majah, Zuhd, 15)



Mtume wetu (s.a.w) ambaye alitumia umri wake wote akieneza na kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa namna bora na kuwafundisha wafuasi wake kupitia mafunzo wa kimaanawi, alitaka swala ambayo ni kitovu cha amani, itekelezwe na kila mtu. Abdullah ibn Rawaha, ambaye alikuwa akifanya maandalizi ya kwenda katika vita vya Mu'tah, alikuja kumuaga Mtume (s.a.w) ambaye angemkumbuka sana, akasema:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Niusie jambo ambalo nitalihifadhi na sitalisahau!" Mtume (s.a.w) akamwambia:

"Kesho utaenda katika nchi ambayo sijda chache sana hufanywa kwa ajili ya Allah. Huko, fanya sijda na swala kwa wingi." (Waqidi, II, 758)



## MISIKITI NA VYUMBA VYA KUSWALIA

### Msikiti au chumba cha kuswalia ni nini?

Masjid ambayo kwa Kiarabu ina maana ya "sehemu ya kusujudia" ni eneo tukufu linalojengwa kwa ajili ya kumuabudu Allah. Katika baadhi ya nchi za Kiislamu kama vile Uturuki, neno "masjid" kwa kawaida hutumika kukusudia maeneo madogo ya kufanya ibada ambapo ni watu wachache tu wanaoweza kuenea; huku neno "jami'" au msikiti likitumika kwa maeneo makubwa zaidi. Katika baadhi ya nchi za Kiislamu maneno yote mawili hutumika bila kutofautisha. Masjid na Jamii pia huitwa ma'bad, yaani sehemu ya kuabudia.

Katika Uislamu, hakuna sehemu maalumu inayolazimu kuswalia au kufanya ibada. Tunaweza kutekeleza ibadazetu mahali popote. Kwa upande mwagine, misikiti na minara inafika mawinguni katika maeneo ya makazi huonesha kuwa maeneo hayo yanakaliwa na

Waislamu. Kadhalika, kuswali jama'ah msikitini ina thawabu nyingi na ubora mkubwa kuliko kuswali peke yako. Misikiti ni mahali pekee ambapo watu huja pamoja na kukutana mara tano kwa siku na kila siku ya Ijumaa.

### Nyumba ipi ya kwanza iliyojengwa kwa ajili ya kumuabudu Allah?

Imeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kuwa eneo la kwanza kujengwa kwa ajili ya kumuabudu Allah ni Ka'bah. Historia ya Uislamu inatuambia kuwa mtu wa kwanza kuijenga Ka'bah ni Nabii Adam (a.s). Nabii Ibrahim na Nabii Ismail (a.s) walijengwa upya Ka'bah kwenye misingi ile ile iliyowekwa na Nabii Adam (a.s). Msikiti wa pili ardhini ulijengwa na Nabii Sulayman (a.s) huko Al-Quds (Palestina) na hujulikana kama Masjid Al-Aqsa.



### Je Mtume wetu (s.a.w) aliwahi kujenga msikiti?

Mtume wetu (s.a.w) alipokuwa Makkah alikuwa akiswali katika Ka'bah kama msikiti. Waabudu masanamu walipozidisha maudhi yao, alikuwa akiswalisha na kufundisha Uislamu katika eneo liitwalo "Dar al-Arqam" yaani Nyumba ya Arqam. Wakati huo kuna maswahaba kama Abu Bakr (r.a), ambao walijitolea nyumba zao zitumike kama masjid.

Wakati Mtukufu Mtume (s.a.w) akihama kutoka Makka kwenda Madina, aliagiza msikiti ujengwe katika kitongoji kiitwacho "Quba". Muda mfupi baada ya agizo lake, msikiti mdogo ulijengwa katika eneo hilo. Alipowasili Madina, kitu cha kwanza alichokifanya ni kununua ardhi na kujenga msikiti uitwao "Masjid al-Nabawi", yaani Msikiti wa Mtume (s.a.w). Mtume wetu (s.a.w) ye ye mwenyewe alishiriki katika ujenzi huo na kubeba matofali mabegani mwake. Masjid al-Nabawi iliyoko leo katika mji wa Madina al-Munawwara ni jengo liliopanuliwa kutokana na masjid hii.

### Kwa nini Msikiti ni muhimu?

Uwepo wa msikiti sehemu fulani huashiria kuwa eneo hilo kuna Waislamu wanaishi. Msikiti ni sehemu maalumu inayotolewa kwa ajili ya Allah. Watu wanaoingia humo huhisi amani na wanaweza kumuabudu Allah katika eneo salama. Hupata maarifa na kujumuika na wenza. Hakuna anayeweza kununua au

kuuza msikiti kama mali yake binafsi. Hiyo ni dhambi kubwa. Watu wanaofanya hivyo na kuwazuia wengine kumuabudu Allah msikitini ni mionganoni mwa watu wakatili sana. Misikiti ni alama ya imani ya Mungu mmoja na yote ni matawi ya Ka'bah Tukufu. Kwa sababu hiyo, katika eneo lolote ambalo Waislamu huenda au nchi wanayoifungua, hujenga misikiti midogo na mikubwa kulingana na mahitaji na mazingira husika.

### Je, misikiti ni kwa ajili ya swala tu?

Hapana. Msikiti, sio sehemu tu ya kutekeleza swala. Kihistoria, msikiti ulikuwa kituo kikubwa cha ustaarabu. Katika zama za Mtukufu Mtume (s.a.w), pembezoni mwa msikiti wa kwanza, kulikuwa na chuo kilichojulikana kama "suffa" ambacho kiliuja kuwa kitovu cha maarifa. Mwalimu wa kwanza wa "suffa" alikuwa Mtukufu Mtume (s.a.w). Msikiti wa Mtume (s.a.w), Masjid al-Nabawi, uligeuka kuwa kituo ambacho Waislamu walikuja pamoja, wakaswali na kusoma Qur'an Tukufu, wakasikiliza mawaidha Mtukufu Mtume (s.a.w), wakajadili mambo yao, wakatafuta ufumbuzi wa matatizo yao, wakawapokea wageni kutoka ng'ambo na kuratibu shughuli za Dola. Baadaye, pembezoni mwa misikiti mikubwa iliyojengwa na Waislamu, palijengwa taasisi zilizohudumia mahitaji ya jamii kama vile madrasa (vyuo), migahawa ya umma kwa ajili ya watu maskini, maktaba, hospitali na maliwato ya umma. Misikiti ikawa vitovu vyaa maarifa, utamaduni na ustaarabu ambapo watu walikutana na kupata elimu na maarifa.

### Watu gani wanaofanya kazi msikitini?

**Imam:** Neno 'Imam' lenye maana ya 'mkuu, kiongozi na mkuu wa dola', linatumika kwa mtu anayeongoza swala na kuwaongoza watu katika masuala ya kidini. Maimamu wa misikiti sio tu wanaongoza swala, bali pia ni watu wanaoongoza jamii kwa maarifa na busara zao, na ni watu wanaohusika na kuifunda jamii kimaadili na kiroho.

**Muadhini:** Muadhini ni mtu anayetoa Adhana pindi muda wa kuswali unapowadia na kufanya aina nyingine ya kazi yenye uhusiano na jambo hilo. Imamu anapokuwa hayupo, hukaa badala yake na kuongoza swala. Hushirikiana na imam katika kuifunda jamii kimaadili na kiroho.

**Mtoe mawaida:** Hawa ni watu wanaotoa nasaha kwa watu kabla au baada ya kuswali katika Siku za Ijumaa, Eid, mwezi Mtukufu wa Ramadhan na siku nyingine za wiki. Kwa khutba zao wanazozitoa juu ya minbar, hutoa mawaidha, kuwaelimisha watu na kuwapa mwangaza Waislamu wanaokuja msikitini kuhusu mada mbalimbali za kidini. Wahubiri wana nafasi kubwa na muhimu katika kuielmisha jamii.

**Qayyum:** Kwa ujumla hawa hufanya kazi katika misikiti mikubwa. Ni wafanyakazi wanaohusika na usafi na uratibu wa misikiti.

### Ni maeneo yapi makubwa katika msikitini?

**Mihrab:** Ni mahali ambapo imam husimama mbele ya waumini wakati wa kuongoza swala.

**Minbar :** Ni jukwaa lilioinuliwa ambapo khutba hutolewa siku za Ijumaa na sikukuu za Eid. Tunapoileka Ka'bah, Minbar huwa upande wa kulia wa Mihrab na ina ngazi kadhaa. Ili kutoa khutba, imam hukwea ngazi za Minbar.

**Kursii:** Kiujumla neno hili lina maana ya kiti. Kama ilivyo kwa minbar, ni eneo lilioinuka ambapo imam au mtoe mawaidha hutoa mawaidha kuhusu Uislamu.

**Sehemu ya Muadhini:** Ni mahali ambapo muadhini huswali na kutoa iqama. Sio kila msikitini unasehemu maalumu ya muadhini. Kwa kawaida, misikiti mikubwa ndiyo pekee yenye eneo hilo.



Mihrab



Minbar



Kursii



Sehemu ya Muadhini

# MASWALI

## TUYAPIME MAARIFA YETU (1)

Angalia vizuri na uchague jibu sahihi kati ya NDIYO AU HAPANA

- |  |                                |                                 |
|--|--------------------------------|---------------------------------|
| 1. Swala tano za kila siku zilifaradhwishwa Usiku wa Mi'raj (Laylat al-Mi'raj).  | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 2. Swala ya Alfajiri ina rakaa 8. Rakaa 4 za sunnah na rakaa 4 za faradhi.   | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 3. Swala ya Adhuhuri ina rakaa 10. Rakaa 2 za sunnah, rakaa 4 za faradhi, na rakaa 4 za sunnah ya mwisho.                | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 4. Swala ya 'Isra ina rakaa 10. Rakaa 2 za sunnah muakkad, rakaa 4 za faradhi, na rakaa 4 za sunnah ghayr muakkad.       | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 5. Ni sunnah kuswali witr.   | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 6. Ni faradhi kuswali swala za Eid.  | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 7. Kutoharisha mwili, mavazi na sehemu ya kuswali dhidi ya najisi zinazoonekana hujulikana kama "Taharah min al-hadath". | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 8. Witr huswaliwa baada ya swala ya Maghribi.  | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 9. Katika swala za jama'ah muumini anatakiwa pia kuweka nia ya kumuufuata imam.  | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 10. Kusema "Allahu Akbar" wakati wa kuanza swala hujulikana kama "Takbir al-Iftitah."                                    | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |

## TUYAPIME MAARIFA YETU (2)

Angalia vizuri na uchague jibu sahihi kati ya NDIYO AU HAPANA

- |   |                                |                                 |
|---|--------------------------------|---------------------------------|
| 1. Wito wa Waislamu kwenye swala huitwa "al-lqamah".                | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 2. Tunasoma dua ya Qunut katika rakaa ya tatu ya swala ya Adhuhuri. | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 3. Ni sunnah kuweka nia ya kuswali.                                 | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 4. Ni wajibu kusoma takbira ya ufunguzi (Takbir al-Iftitah).        | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |
| 5. Ni wajibu kusoma dua ya "wajjahtu" baada ya takbira ya ufunguzi. | <input type="checkbox"/> NDIYO | <input type="checkbox"/> HAPANA |

6. Ni sunnah kusujudu katika swala.  NDIYO  HAPANA
7. Ni sunnah kusujudu sijda ya kusahau pindi unapofanya kosa katika swala.  NDIYO  HAPANA
8. Tunapobanwa na haja (choo) ni haramu kuswali.  NDIYO  HAPANA
9. Ni karaka (makruh) kula au kunywa unapokuwa unaswali.  NDIYO  HAPANA
10. Kugeuza kifua nje ya uelekeo wa qibla hubatilisha swala.  NDIYO  HAPANA

### TUYAPIME MAARIFA YETU (3)

Angalia vizuri na uchague jibu sahihi kati ya NDIYO AU HAPANA

1. Ni lazima iwepo khutba kabla ya Swala ya Ijumaa.  NDIYO  HAPANA
2. Tuna Sikukuu mbili za kidini kwa mwaka. Moja ni Eid al-Fitr na nyingine ni Eid al-Adh-ha.  NDIYO  HAPANA
3. Takbir zinazosomwa baada ya kila swala ya faradhi wakati wa siku za Eid al-Adh-ha hujulikana kama Takbir al-Tashriq.  NDIYO  HAPANA
4. Tunapokuwa safarini, tunapunguza swala za rakaa tatu na kuswali rakaa mbili.  NDIYO  HAPANA
5. Jua linapochomoza, linapokuwa kwenye nusu ya upeo, na wakati linapozama, hakuna swali inayotakiw akuswaliwa.  NDIYO  HAPANA

## TUJIPIME (1)

1.

- I. Kuswali hutufanya tumkumbuke Allah kwa njia bora kabisa.
- II. Kuswali hutukumbusha Akhera na Siku ya Hukumu.
- III. Tutakuwa tumeefanya mazoezi kwa kuswali.
- IV. Swala hututakasa dhidi ya dhambi.

**Kati ya hayo yaliyotajwa hapa juu, ni yepi ambayo ni mionganini mwa faida za swala kwetu?**

- a) I-II-III
- b) I-II-IV
- c) II-III-IV
- d) I-III-IV

**2. Ni Usiku upi ambapo swala tano zilifaradhihwa?**

- a) Usiku wa Mi'raj (Laylat al-Mi'raj)
- b) Usiku wenye Cheo (Laylat al-Qadr)
- c) Usiku aliozaliwa Mtume (s.a.w)
- d) Usiku wa Maombi (Laylat al-Ragha'ib)

**3. Ni sharti lipi kati ya masharti yaliyotajwa hapa chini ambalo sio lazima kwa mwenye kuswali?**

- a) Kuwa na akili timamu
- b) Kuwa mchapakazi
- c) Kufikia umri wa baleghe
- d) Kuwa Muislamu

**4. Katika swala zilizotajwa hapa chini ni ipi ambayo ni sunnah?**

- a) Swala ya Adhuhuri
- b) Swala ya Witr
- c) Swala ya Maghribi
- d) Swala ya Ijumaa

**5. Katika swala zilizotajwa hapa chini ni ipi ambayo ni sunnah?**

- a) Swala ya Jeneza (kumswalia maiti)
- b) Swala ya Adhuhuri
- c) Swala ya Tarawih
- d) Swala ya Ijumaa

**6. Katika swala zilizotajwa hapa chini ni ipi ambayo ni ya faradhi?**

- a) Swala za Eid
- b) Swala ya Jeneza
- c) Swala ya Witr
- d) Swala ya Tahajjud

**7. Ni swala ipi kati ya swala hizi za faradhi huanza kuswaliwa?**

- a) Swala ya Adhuhuri
- b) Swala ya Alfajiri
- c) Swala ya Maghribi
- d) Swala ya 'Isha

**8. Ni sharti zipi kati ya hizi ambazo sio lazima kutekelezwa kabla ya swala?**

- a) Kusitiri maeneo ya utupu (Satr al-awrah)
- b) Muda (al-waqt)
- c) Nia (al-Niyyah)
- d) Kisimamo (al-Qiyam)

**9. Ni lipi kati ya haya ambalo sio sehemu ya ndani ya swala?**

- a) Kisimamo (al-Qiyam)
- b) Muda (al-Waqt)
- c) Kusujudu (al-Sajdah)
- d) Kisomo (al-Qira'ah)

- 10. Ni lipi kati ya haya ambalo ni sehemu ya ndani ya swala?**
- Taharah min Al-Hadath
  - Taharah min Al-Najasah
  - Satr al-Awrah
  - Kusujudu (Sajdah)
- 11. Ni neno gani ambalo hutumika kukusudia kuanza kwa swala?**
- Adhan
  - Iqamah
  - al-Salah
  - Takbira
- 12. Ni swala ipi kati ya hizi ambayo sio sunnah ya rakaa nne?**
- Sunnah ya kwanza ya Adhuhuri
  - Sunnah ya Alasiri
  - Sunnah ya Maghribi
  - Sunnah ya 'Isha
- 13. Ni ipi kati ya hizi ambayo sio sunnah ya rakaa mbili?**
- Sunnah ya Adhuhuri
  - Sunnah ya Alfajiri
  - Sunnah ya Maghribi
  - Sunnah ya 'Isha
- 14. Ni ipi kati ya hizi ambayo sio faradhi ya rakaa nne?**
- Swala ya Adhuhuri
  - Swala ya Alasiri
  - Swala ya Maghribi
  - Swala ya 'Isha
- 15. Ni lipi kati ya haya ambalo ni mionganini mwa matendo ya faradhi katika swala?**
- Kusoma Wajjahtu
  - Kusema Subhana rabbi al-A'la wakati wa sijda.
  - Kusoma surah al-Fatiha
  - Kusema samiallahu liman hamidah unapotoka kwenye rukuu.

## TUJIPIME (2)

- 1. Ni dua ipi kati ya hizi ambayo haisomwi wakati wa tahiyyat ya mwisho?**
- Tahiyyat
  - Rabbena atina
  - Allahumma Salli and Allahumma Bârik
  - Dua ya Qunut
- 2. Ni lipi kati ya haya ambalo sio mionganini mwa matendo ya karaha (makruh) katika swala?**
- Kuchezea nguo au mwili
  - Kusoma tasbih ya Rukuu na Sijda zaidi ya mara tatu
  - Kuswali hali ya kuwa umebanza na haja (choo)
  - Kuswali ukiwa umemuelekea mwanadamu

3. Ni ipi kati ya swala hizi ambayo lazima iswaliwe kwa jama'ah?
- Swala ya Ijumaa
  - Swala ya Adhuhuri
  - Swala ya Alasiri
  - Swala ya Maghribi
4. Neno gani linalotumika kwa swala zenye kulipwa?
- Salat al-Dhuha
  - Salat al-Qadhaa
  - Swala ya mtu mgonjwa
  - Swala ya kuutolea salam msikiti
5. Ni katika mwezi gani tunaswali Tarawih?
- Rajab
  - Shaban
  - Ramadhan
  - Muharram
6. Ni swala gani kati ya hizi ambayo haihitaji rukuu na sijda?
- Swala ya jeneza (kuswalia maiti)
  - Tarawih
  - Swala ya Ijumaa
  - Swala za Eid
7. Ni ipi Qibla ya Waislamu na iko wapi?
- Ka'bah – Makkah
  - Ka'bah – Madina
  - Masjid al-Aqsa – Palestina
  - Rawdha – Madina
8. Wakati gani tunafanya iqama?
- Kabla ya rakaa za swala ya faradhi
  - Kabla ya swala za Eid
  - Kabla ya Swala ya Jeneza
  - Kabla ya swala za Witr
9. Ni lipi kati ya mambo hayo ambalo halibatilishi swala?
- Kuongea
  - Kupiga mwayo
  - Kula au kunywa
  - Kusoma ayah kimakosa kiasi cha kubadilisha maana yake
10. Lipi kati ya haya ambalo ni sahihi kuhusu rakaa za swala ya Adhuhuri?
- Rakaa 10. Rakaa 6 za sunnah, rakaa 4 za faradhi.
  - Rakaa 12. Rakaa 8 za sunnah, 4 za faradhi.
  - Rakaa 8. Rakaa 4 za sunnah, 4 za faradhi.
  - Rakaa 4. Rakaa 8 za sunnah, 4 za faradhi



## TUJIPIME (3)



1. Ina rakaa 2 za faradhi. Kabla ya rakaa za faradhi, khutba inatakiwa kutolewa. Inaweza kuswaliwa katika jama'ah pekee. Ni faradhi kwa wanaume tu.

**Sifa hizo zilizotajwa hapo juu ni za swala ipi?**

  - a) Swala za Eid
  - b) Swala ya Alfajiri
  - c) Swala ya Maiti
  - d) Swala ya Ijumaa

2. **Ni lipi kati ya mambo haya ambalo hubatilisha swala na wudhu?**

  - a) Kugeuza kifua kutoka uelekeo wa qibla
  - b) Kula kitu wakati wa swala
  - c) Kuzungumza wakati wa swala
  - d) Kupoteza fahamu wakati wa swala

3. **Ni viungo gani vya mwili ambavyo wanaume wanatakiwa kuvifunika wakati wa swala?**

  - a) Bainya miguu na mabega
  - b) Bainya kitovu na magoti
  - c) Bainya kitovu na miguu
  - d) Bainya mabega na magoti

4. **Ni viungo gani ambavyo wanawake wanatakiwa kuvifunika wakati wa swala?**

  - a) Mwili wote isipokuwa uso na mikono
  - b) Mwili wote isipokuwa kichwa
  - c) Bainya mabega na miguu
  - d) Bainya mabega na magoti

5. **Ni katika swala ipi ambapo dua ya Qunut husomwa?**

  - a) Swala ya Ijumaa
  - b) Swala ya Tarawih
  - c) Swala ya Alfajiri
  - d) Swala ya Maiti

6. **Nini hukmu ya swala ya Maiti?**

  - a) Ni ya ziada
  - b) Ni faradhi kwa umma wote wa Kiislamu
  - c) Ni faradhi kwa kila Muislamu
  - d) Sunnah

7. **Kuna rakaa ngapi katika swala ya tarawih?**

  - a) 18
  - b) 10
  - c) 20
  - d) 13

8. **Katika maelezo yaliyotolewa hapa chini, ni maelezo gani ambayo sio sahihi kuhusu swala za Eid mbili?**

  - a) Unaweza kuziswali ukiwa peke yako.
  - b) Zinaswaliwa mara mbili kwa mwaka.
  - c) Ni swala isiyokuwa na rukuu na sijda
  - d) Zina khutba.

9. **Ni neno gani linalotumika kumaanisha eneo ambalo khutba hutolewa wakati wa swala ya Ijumaa na Eid?**

  - a) Minbar
  - b) Mihrab
  - c) Sharafa
  - d) Kursii

10. **Ni umbali gani wa safari unaotakiwa ili upunguze swala zenyé rakaa nne na kuswali rakaa mbili?**

  - a) Kilometra 9 km
  - b) Kilometra 83
  - c) Kilometra 100 km
  - d) Kilometra 900

## JAZA SEHEMU ZA WAZI (1)

### Jaza sehemu zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yafuatayo:

(al-Qira'ah/Tahajjud /Sijda/Istiqlal al-Qibla/ Satr al-Awrah)

1. Swala ya sunnah inayoswaliwa baada ya katikati ya usiku huitwa salat al-.....
2. Kufunika viungo vya mwili vinavyotakiwa kufunika katika swala huitwa .....
3. Kuelekea Ka'bah wakati wa swala huitwa .....
4. Kusoma angalau ayah tatu fupi kutoka ndani ya Qur'an katika swala wakati ukiwa umesimama huitwa .....
5. Baada ya kurukuu, kitendo cha kuweka chini paji la uso, pua, miguu na mikono huitwa .....



## JAZA SEHEMU ZA WAZI (2)

### Jaza sehemu zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yafuatayo:

(Takbir al-Tashriq / kulia / Sajdat al-Tilawah / dhambi / khutba/ Sajdat al-Sahw / kuashiria /al-Kifayah)

1. Yatupasa kuingia msikitini tukiwa na wudhu na kutanguliza mguu wa .....
2. .... Inatakiwa kusomwa kabla ya Swala ya Ijumaa.
3. Takbira zinazosomwa baada ya swala za faradhi wakati wa sikukuu ya kuchinja (Eid al-Adha) huitwa .....
4. Ni faradhi..... kuswali swala ya jeneza.
5. Mtu mgonjwa asiyeweza hata kukaa anaweza kuswali kwa kulala na kwa .....
6. Ni..... kubwa kupitwa na swala bila udhuru.
7. Sijda tunayoifanya baada ya kusoma ayat al-sajdah kutoka ndani ya Qur'an Tukufu hujulikana kama .....
8. Sijda tunayoifanya baada ya kusoma ayat al-sajdah kutoka ndani ya Qur'an Tukufu hujulikana kama .....






## NINAJIFUNZA KUHUSU MTUME WANGU



# SIRAH



- ✿ *Miaka ya huzuni*
- ✿ *Mjumbe wa Allah awalingania watu kwenye Uislamu*
- ✿ *Kimbilio la Mwisho: Hijra, Huzuni ya Kuiacha Makka*
- ✿ *Maisha katika Makao Mapya ya Mji wa Madina (Mwaka 622 Miladiya)*
- ✿ *Vita vya Badr (Mwaka 624)*



## MACHOZI YALI-YOGEUKA KUWA CHEMCHEM

Wakiwa njiani kutoka Taif, Mtume (s.a.w) na Zaid walipumzika katika shamba moja la mizabibu. Wamiliki wa shamba hilo waliwaonea huruma kutohana na hali yao na kumtuma mtumishi wao Addas awapeleke zabibu. Addas alimpa mkungu wa zabibu Mtukufu Mtume (s.a.w) na kumwambia "unaweza kula zabibu hizi". Addas alimtazama vizuri mgeni huyo. Alionekana kuwa mtu mgeni mahala hapo. Hakuonekana kama watu wa eneo hilo. Mjumbe wa Allah (s.a.w) alianza kula kwa kusema: "Kwa jina la Allah". Jambo hilo lilimvutia Addas ambaye alishangazwa na kusema:

"Watu wa hapa hawayajui maneno haya wala hawayasemi. Wewe ni nani? Wewe ni mtu tofauti kabisa". Mtukufu Mtume (s.a.w) katika kumjibu akamuuliza:


"Unatokea wapi? Ni ipi dini yako?"

"Mimi ninatokea Nainawa nami ni Mkristo", alisema.

"Hivyo unatokea katika ardhi ya mja mwema Yunus bin Matta", alisema. Mshangao wa Addas uliongezeka zaidi. Mgeni huyu hakuonekana kuwa mtu wa kawaida. Alimstaajabia sana. Mjumbe wa Allah akaendelea kusema:

"Yunus ni kaka yangu. Alikuwa Nabii kama Mimi".

Addas alihisi msisimko wa ajabu mno ndani ya moyo wake. Ni hisia ambayo hakuwa kuipata hapo kabla. Mwishowe, nuru kutoka moyoni mwa Mjumbe wa Allah kwenda usoni mwake ilishuhudiwa tu na mtumwa aitwaye Addas mionganini mwa watu wote wa Taif. Addas alipokuwa akitamka shahadah, chemichemi ya imani ndani ya moyo wake iligeuka kuwa machozi na kuanza kumiminika. Aliinama kwenye magoti ya Mtukufu Mtume (s.a.w) na kuibusu mikono yake. Alikuwa ameamini.





## 1- MIAKA YA HUZUNI

### a) Kifo cha Abu Talib na Khadija

Waislamu walikuwa na furaha kwa sababu kipindi cha vikwazo kilikuwa kimekoma. Hata hivyo, furaha yao haikudumu muda mrefu. Miezi nane baada ya vikwazo kukomeshwa, walipata misiba miwili mzito kwa pamoja. Ami wa Mtume wetu (s.a.w), mzee Abu Talib ambaye alimlinda Mtume (s.a.w) tangu utotoni, umri wake ulikuwa umesonga sana na hivyo akafariki dunia. Siku mbili baada ya kifo cha mzee Abu Talib, mke kipenzi wa Mtukufu Mtume (s.a.w), bibi Khadija naye alifariki dunia.

Abu Talib hakuwa ameingia katika Uislamu. Hata hivyo, alimpenda mno Mtume (s.a.w) na alishikamana nae sana. Alistahmili kila aina ya tabu na kumlinda dhidi ya mateso ya makafiri. Kabla ya kifo chake, aliwausia ndugu zake kumtii Mjumbe wa Allah, kusikiliza maagizo ya Mjumbe wa Allah na kumsaidia katika kazi yake. Ama kuhusu Khadija, alikuwa msiri wa Mtume wetu (s.a.w), alimsaidia na kumnusuru. Alimfariji katika nyakati ngumu

kabisa na kusimama naye kwa mwili na nafsi yake. Alitumia mali zake zote kwa ajili ya Waislamu.

Mjumbe wa Allah alihuzunishwa mno na vifo mfululizo vyta watu wake muhimu na wasaidizi wake wakubwa. Maswahaba nao walishirikiana nae katika huzuni. Ndiyo maana mwaka huu ulijulikana kama "Mwaka wa Huzuni". Wakati wa uhai wa mzee Abu Talib, waabudu masanamu waliogopa kumfanya maudhi Mtukufu Mtume (s.a.w). Lakini, baada ya kifo chake, walianza kutumia kila aina ya maudhi. Kwa mfano, siku moja Mjumbe wa Allah alikuwa akiswali kwenye eneo la Kaabah. Kutokana na uchochezi wa Abu Jahl, Uqba ambaye alikuwa mtu katili na fedhuli, alichukua utumbo na kinyesi cha ngamia aliyejewa amechinjwa muda huo na kukimwaga mgogoni mwa Mtume (s.a.w) wakati akiwa kwenye sijda. Mjumbe wa Allah (s.a.w) hakuweza kuinua kichwa chake kutoka kwenye sijda.

**Kama ungekuwepo wakati huo, ungefanya nini?**



Binti wa Mtume (s.a.w), bibi Fatma (r.a) alienda kumsaidia na kuyasafisha mavazi yake. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipomaliza kuswali, waabudu masanamu walikuwa wakicheka kwa sauti kubwa na kuruka kwa furaha huku wakimzunguka. Mjumbe wa Allah (s.a.w) alinyanya mikono yake kuelekea mbinguni na kusema mara tatu: "Mola wangu! Ninakuachia kundi hili la Maqrayshi. Ninakuachia

Abu Jahl, Uqba ibn Abu Muait, Shuba ibn Hajjaj, Utba na Shaiba watoto wa Rabia, Ubayy na Umayyah watoto wa Khalaf." Aliyataja majina yote ya waabudu masanamu waliokuwepo hapo. Miaka kadhaa baadaye wote hao waliuawa na wanajeshi wa Kisalamu katika Vita vya Badr.

**b) Ziara ya Taif na watu wenyewe hasira wa Saqif (Mwaka 620)**

Ukatili wa waabudu masanamu wa Makka ulifika kiwango kikubwa mno. Mtukufu Mtume (s.a.w) alianza kutafuta msaada na ardhi nyingine ya kuishi. Aliandamana na mwanaye wa kuasili Haritha bin Zaid na kwenda Taifa. Alikuwa akienda kuwalingania watu wa Taif kwenye Uislamu.

Huko Taif wallishi watu wa ukoo wa Bani Sakif. Katika kipindi cha siku kumi alizokaa huko, Mjumbe wa Allah aliwaeleza kuhusu Uislamu. Alikutana na wakuu wa ukoo huo. Hata hivyo, sio tu kwamba walikataa kuukubali Uislamu, bali pia walimjibu vibaya Mtume (s.a.w) kwa kumwambia: "Hakuna mtu

mwingine ambaye angeweza kuwa Mtume tofauti na wewe?" Badala ya kuiona ziara ya Kipenzi cha Allah kuwa ni heshima kwao, walimfukuza wakisema: "Ondoka katika ardhi yetu". Walimkejeli na kumtusi. Wakati Mtume (s.a.w) akiondoka Taif, waliwachochea watoto na wajinga wa mji huo kupanga misitari miwili kandoni mwa barabara na kumtupia mawe. Miguu ya Mjumbe wa Allah alivuja damu kwa sababu ya mawe aliyorushiwa. Alitembea kwa shida kutokana na maumivu ya majeraha yake. Madhalimu hao chakaramu walikuwa wakimfanya Mtume (s.a.w) kusimama kwa nguvu kila alipojaribu kukaa na kuendelea kurushia mawe kwenye miguu yake. Walikuwa wakimcheka, wakimdhihaki na kumkejeli.

**Nini mtazamo wako kuhusu hisia za Zaid (r.a) na yote aliyokuwa akiyaona?**

Zaid (r.a), kwa upande mmoja, alikuwa akitumia mwili wake kama ngao dhidi yam awe ambayo yalikuwa yakirushwa dhidi ya Mjumbe wa Allah, kwa upande mwingine alikuwa akiwaonya akisema: "Mnafanya kitu gani? Je, mnamuogopa Allah? Je, mnajua kwamba mtu mnayemrushia mawe ni Mtume wa Allah?" Lakini maonyo yote hayo hayakuwazuia masafihii wale kuacha ukatili wao.

Hatimaye wakiwa njiani kurudi Makka walipumzika kwenye bustani ya mizabibu ya Utba na Shaiba, watoto wa Rabia na kuweza kuijokoa. Hapo Mtume (s.a.w) alinyanyua mikono yake mbinguni na kuomba dua:

**"Ewe Allah! Ninaukabidhi Kwako udhaifu wa nguvu zangu, uchache wa ujanja wangu na unyonge wangu mbele ya macho ya watu. Ewe Mrehemevu zaidi ya warehemevu wote! Iwapo hautonikasirikia, sitajali mateso na shida nilizopipata. Ewe Mola wangu!"**

**Wape uongofu jamaa zangu, hakika wao hawajui. Mola wangu nitaendelea kukuomba msamaha mpaka utakapokuwa radhi nami!"**

Licha ya mateso na maudhi yaliyomkumba, Mjumbe wa Allah hakuwalaani watu wa Saqif. Hata Malaika Jibril (s.a) alikuwa na kumwambia:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Hakika Allah amesikia waliyokwambia watu hawa, ameona waliyokufanya, na amekutumia Malika huyu wa Milima. Unaweza kumuamuru afanye chochote unachotaka kwa watu hawa". Hata hivyo, Mtume wetu (s.a.w) akasema:

"Hapana, sitaki waangamizwe. Bali ninamuomba Mola wangu alete kizazi kipyaa kutoka migongoni mwao ambacho hakitamshirikisha Allah na chochote na kitamuabudu Yeye tu".

## 2- MJUMBE WA ALLAH AWALINGANIA WATU KWENYE UISLAMU

Baada ya kutoka Taif na kurudi Makka, Mjumbe wa Allah alienda kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu aliolokutana nao. Wakati wa msimu wa hijja, alikuwa akienda kwenye masoko yaliyowekwa pembezoni mwa mji wa Makka, akikutana na watu wa makabila mengine ya Kiarabu waliokusanyika katika masoko hayo, akiwasomea ayah za Qur'an Tukufu na kuwalingania kuhusu Uislamu.

Viongozi wa Maqurayshi walikuwa na khofu ya Uislamu kusambaa kwa makabila mengine nje ya Makka. Walitafuta njia ya kuzikabili juhudzi za Mjumbe wa Allah na kuyazuia makabila mengine wasiyakubali maneno yake.

Walid ibn Mughira alikuwa mtu mwerevu na mwenye kuheshimika. Pia alikuwa mtu mwenye kipawa cha fasihi. Baada ya kuisikiliza Qur'an iliyosomwa na Mjumbe wa Allah, alisema:

"Ninajua aina zote za ushairi. Nilichokisikia kutoka kwa Muhammad sio mashairi. Hivyo huwezi kusema ni mshairi. Wala sio nathari pia. Uzuri na usanifu unaopatikana katika maneno yale haupatikani katika maneno mengine. Hawezi kusemwa kuwa ni mchawi au mpiga ramli. Kwa maana maneno yake hayatusiani na uchawi au uaguzi hata kidogo. Huwezi kusema ni kichaa au mwendawazimu hata kidogo. Ukimuita hivyo, hakuna atakayekuamini. Kwa maana maneno yale mazuri hayawezi

kutoka hata kwa mwenye akili timamu, achilia mbali mwendawazimu. Huwezi kusema ni mnajibu, kwa sababu hafanyi chochote kinachohusiana na unajimu."

"Sasa tumuiteje?" waliuliza.


"Sijui mtamuitaje. Lakini, hakuna sifa yoyote inayomfaa kati ya hizo mnazomnasibisha nazo kama vile ushairi, upigaji ramli, umajuni, unajimu. Hakuna yeote atakayeweza kuyaamini maneno yenu", alisema. Hata hivyo, siku illiyofuata, Walid alisema:


"Itafaa zaidi kumuita mchawi, kwa maana maneno yake yanawatenganisha ndugu na kusababisha mabishano kati ya jamaa. Hivyo, maneno yake ni uchawi. Muitenii mchawi".

Hivyo walihamua kumuita 'mchawi'. Pindi Mjumbe wa Allah (s.a.w) akizungumza na watu wa kundi fulani, walikuwa wakija baada yake na kusema: "Msimsikilize. Msidanganywe na maneno yake. Hakika yeeye ni mchawi. Anawatenganisha ndugu".

Hata hivyo, juhudi zao hazikuweza kuzuia ueneaji wa nuru ya Uislamu. Qur'an Tukufu iliwapo jibu lao:

**"Wanataka kuizima Nuru ya Mwenyezi  
Mungu kwa vinywa vyao, na Mwenyezi  
Mungu anakataa ila aitimize Nuru  
yake ijapo kuwa makafiri  
watachukia." (Tawba  
9: 32)**





**a) Mikutano ya Aqaba na kiapo cha utii (Mwaka 621 na 622)**

Licha ya vikwazo vyote, Mtume (s.a.w) aliendelea kuutangaza ujumbe wa Uislamu kwa wale waliokuja kuyazuru masanamu kwenye Kaabah wakati wa msimu wa hijja. Siku moja, alikutana na watu sita katika eneo liitwalo "Aqaba" kaskazini mwa Makka na baina ya mji wa Makka na Mina. Mjumbe wa Allah (s.a.w) alizungumza nao, akawosomea Ayah za Qur'an Tukufu, akawahabarisha kuhusu imani ya Kiislamu na kuwaita kwenye Uislamu. Watu wa Madina mara kwa mara walikuwa wakisikia kutoka kwa wazee wao kwamba Mtume atakuja muda si mrefu. Pindi Mtume (s.a.w) alipowalingania kwenye dini mpya, walitazamana na kusema "Huyu ndiye Mtume ambaye wazee wetu walikuwa wakimzungumzia na ambaye Wayahudi wanamsubiri. Tumuamini kabla Wayahudi hawajafanya hivyo na tuwatangulie"

na hivyo wakaingia katika Uislamu kwa kutamka shahada.

**b) Kiapo cha utii cha kwanza na cha pili cha Aqaba (mwaka 621 na 622)**

Watu wale sita walirejea mjini Madina baada ya kukamilika kwa msimu wa hijja. Waliwaeleza ndugu na jamaa zao juu ya walichokiona na kukisikia. Walianza kusambaza ujumbe wa Uislamu mjini Madina. Mwaka mmoja baadaye, wakati wa msimu wa hijja, watu kumi kutoka kabilia la Khazraj, wawili kutoka kabilia la Aws, ikiwa ni jumla ya Waislamu kumi walitoka Madina kwenda Makka. Watano kati yao walikuwa wale waliokuwa katika mkutano wa Aqaba mwaka mmoja uliopita. Katika mkutano huu wa pili, Waislamu kumi na mbili kutoka Madina walitoa kiapo cha utii kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w). Waliushika mkono wa Mtume (s.a.w) na kuahidi:

- ✓ Kutomshirikisha Allah na chochote,
- ✓ Kutoiba wala kuzini,
- ✓ Kutowaua mabinti zao,
- ✓ Kutomsingizia yeyote,
- ✓ Kutomuasi Allah na Mtume Wake.

Baada ya mkutano na kiapo hiki cha utii, Waislamu wa Madina walirejea mjini kwao ili kufanya juhud za kueneza ujumbe wa Uislamu huko. Mjumbe wa Allah alimtuma Mus'ab ibn Umair kuandamana nao kama mwalimu ili awafundishe Uislamu na Qur'an Tukufu.

Mus'ab alikuwa akienda kwenye nyumba za wale walioingia kwenye Uislamu kutoka makabila ya Aws na Khazraj. Alikuwa akiwafundisha Qur'an Tukufu na itikadi ya Uislamu. Mus'ab alikuwa mwalimu mwenye tabia njema, mwenye subira, mwema na mwenye hekma sana. Ndani ya kipindi kifupi, kila mtu alimpenda. Kila amtu aliye mjua

alikuwa akimshawishi kuukubali ujumbe wa Uislamu. Kutokana na juhud za Mus'ab na watu wengine waliokula kiapo cha utii kwa Mtume (s.a.w) katika eneo la Aqaba, idadi ya Waislamu mjini Madina ilikuwa ikiongezeka kwa kasi.

Hata hivyo, Sa'd bin Muadh na Usaid bin Hudair, ambao walikuwa watu mashuhuri wa kabilia la Aws, walikuwa bado hawajaukubali Uislamu. Siku moja wakati Mus'ab akilingania Uislamu kwa watu waliokuwa wamemzunguka, Usaid alikuja. Alitaka kumzuia Mus'ab asiwalinganie. Alinung'unika akisema:

"Unataka kufanya nini? Unataka kuwafanya watu hawa waiache njia ya wahenga wao?"

#### Unadhani Mus'ab alifanya nini katika hali hiyo na alijibu nini?



Mus'ab aliamiliana naye vizuri sana kisha akamsomea Ayah kutoka ndani ya Qur'an Tukufu. Usaid aliathiriwa mno na Qur'an Tukufu. Baada ya muda, alihisi hisia isiyomithiliika ndani ya kina cha moyo wake. Alisema: "Haya ni maneno mazuri mno", akasilimu. Baada ya hapo alisema:

"Nitakwenda na kumtuma Sa'd ibin Muadh ibn Jabal. Akiona kuwa ni vyema na kuingia katika Uislamu, hakuna atakayebaki katika mji wetu bila kuingia katika Uislamu.

Sa'd hakufurahishwa hata kidogo kuona Uislamu ukisambaa mjini Madina. Aliposikia kuwa Usaid ameingia katika Uislamu, alielekeea kwa Mus'ab akiwa na hasira. Aliwafokea watu alioawakuta huko akisema: "Enyi watu wa Aws! Kama pasingekuwa na uhusiano wa damu kati yenu na mimi, nisingevumilia kitendo chenu cha kupandikiza mfarakano ndani ya kabilia letu". Mus'ab aliamiliana naye kwa wema na kwa ulaini pia. Alimpatia ujumbe wa Uislamu unaogusa akili na moyo. Akamsomea Qur'an Tukufu. Hatimaye, Sa'd ibn Muadh naye akapata heshima ya kuwa Muislamu.

Muda mfupi baadaye, kutokana na ushawishi wa viongozi hawa wawili, takribani hakuna mtu katika makabila ya Aws na Khazraj ambaye hakuungia katika Uislamu. Mus'ab ibn Umair alimtumia Mtume (s.a.w) ujumbe kuhusu habari hizi zenyet kufurahisha kutoka mjini Madina. Mtukufu Mtume (s.a.w) na Waislamu ambaa walikuwa chini ya ukandamizaji walifurahishwa mno na taarifa hizi. Mwaka ambaa matukio haya yenye kufurahisha yalitokea ukaitwa kuwa ni "**Mwaka wa Furaha**".

Mwaka uliofuata, Waislamu 75, wawili

miongoni mwao wakiwa ni wanawake, walifunga safari kwenda mjini Makka. Walikutana kwa siri na Mtukufu Mtume (s.a.w) kwenye Mlima wa Aqaba. Walimpa mwaliko wa kwenda Madina. Ami wa Mjumbe wa Allah, Abbas, ambaye wakati huo alikuwa hajasilimu, alianza kuongea, kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa amechukua jukumu la kumlinda mpwa wake baada ya kifo cha mzee Abu Talib.

"Enyi watu wa Aws na Khazraj! Hakika mnatambua kuwa mpwa wangu Muhammad ana daraja kubwa miongoni mwetu. Tumekuwa tukimlinda dhidi ya maadui zake mpaka sasa, na tutaendelea kufanya hivyo. Sasa mnamuwa kwenda Madina mkimtaka aishi huko. Naye pia anataka kufanya hivyo. Lakini, muite ni mkiwa na uwezo wa kumlinda dhidi ya maadui zake. Kama hamitakuwa na uwezo wa kumlinda kwa hali yoyote, acheni mpango huo kwa sasa", alisema. Baada ya kumsikiliza Abbas, wajumbe kutoka Madina wakasema:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Tafadhalii zungumza nasi. Kwa ajili ya Allah, tuko tayari kutekeleza ahadi yoyote utakayoihitaji kutoka kwetu na kula kiapo cha utii kwako".

Baada ya kusoma baadhi ya Ayah za Qur'an, Mtume (s.a.w) akasema: "Ninataka mfanye ahadi juu ya:

- ✓ Kutozembea katika wajibu wa kidini katika nyakati za raha na tabu,
- ✓ Kutosita kutekeleza haki,
- ✓ Kunihami kama mnavyozihami familia na watoto wenu nitakapohamia kwenye ardhi yenu.

**Je, watu wa Madina wanaweza kuwa walipata ugumu katika kutekeleza  
ahadi zao? Kwa nini?**



Wajumbe kutoka Madina wakajibu: "Ewe Mjumbe wa Allah! Tumekuja hapa kula kiapo cha utii kwako. Tutafanya utakavyoamuru. Tutakuhami zaidi ya tunavyozihami familia zetu na watoto zetu. Tutekeleza ahadi yetu". Kisha wakaauliza:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Tutakuwa na lipi iwapo tutakufa kwa ajili yako katika njia uliyotunesha?"

Mtume (s.a.w) akajibu:

"Mtalipwa Pepo huko Akhera".

"Basi nyoosha mkono wako", walisema.

Wote waliushika mkono wake, wakala kiapo cha utii na kuahidi kuyatoa maisha yao kwa ajili ya Uislamu kama italazimika kufanya hivyo.

**c) Miujiza ya Isra (Safari ya Usiku) na Mi'raj (kwenda mbunguni) (Mwaka 621)**

Baada ya Mkutano wa Pili wa Aqaba, katika usiku wa 27 wa mwezi wa Rajab, miujiza ya Mtume (s.a.w) ya Isra na Mi'raj ilitokea. Isra ina maana ya safari ya usiku, na Mi'raj

ina maana ya kupaa mbinguni au kifaa cha kupaa. Muujiza huu umeitwa Isra na Mi'raj kwa kuwa ulitokea usiku na Mjumbe wa Allah (s.a.w) alipaa kwenda mbinguni. Hili limeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo: "**SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.**" (Isra 17: 1)

Matukio haya ya kimiujiza yalitokea kama ifuatavyo. Usiku mmoja, wakati Mjumbe wa Alllah (s.a.w) akiwa katika eneo la Ka'bah liitwalo "Hatim" alipanda kipandwa kiitwacho "Burak" kilicholetwa na Jabril (a.s), akaenda mpaka Masjid Al-Aqsa Palestina na kuswali huko. Na kutoka hapo, akapanda kipandwa kiitwacho "Mi'raj" na kupaa mpaka mbinguni. Baada ya kuona matukio mbalimbali huko mbinguni, alifika 'Sidratul- Muntaha' eneo ambalo hakuna kiumbe anayeweka kuvuka. Eneo la baada ya Sidratul - Muntaha halielezeki. Hivyo, Jibril (a.s) aliyesuhubiana na Mtume (s.a.w) hakuvuka hapo, akasema: "Hapa ndio mwisho wangu. Nikisogea mbele nitaungua kabisa".

Katika safari ya Mi'raj, Allah Mtukufu alimuonesha Mjumbe Wake ishara nyingi. Allah Mtukufu alikuwa akimfunulia wahyi Mjumbe Wake akiwa duniani kupertia kwa Malaika Jibril. Lakini, huko alimfunulia moja kwa moja bila kutumia malaika.

Katika usiku wa Isra na Mi'raj, Mtukufu Mtume (s.a.w) alipewa vitu vitatu:

- ✓ Swala tano zilifaradhishwa.
- ✓ Alifunuliwa Ayah mbili za mwisho za surah al-Baqara (Amana al-Rasulu).

✓ Habari njema kuwa watu katika Ummah wake ambao hamshirikishi Alllah na chochote wataingia Peponi baada ya kupata hisabu stahiki kwa makosa yao.

#### d) **Ukaidi wa Wapagani mbele ya Miujiza**

Asubuhi Mtume (s.a.w) aliwaambia watu wa Makka kuhusu safari ya Mi'raj na aliyoyaona huko. Waumini waliamini kila kitu walichoelezwa na Mjumbe wa Allah (s.a.w). Walimwambia: "Iwe yenyе baraka". Kwa upande mwingine, wapagani walikanusha kama walivyofanya siku zote. Walieleza kuwa isingewezeekana kwa mtu kwenda Jerusalem (Palestina) na kurudi ndani ya usiku mmoja.

Miongoni mwa wapagani, kuna wale waliowahi kusafiri kwenda Jerusalem na kuiona Masjid al-Aqsa. Baadhi yao walitaka kuyajaribu maneno ya Mjumbe wa Allah (s.a.w) hivyo walimuuliza maswali mbalimbali kama vile:

"Masjid al-Aqsa ina milango mingapo?"

"Eneo hili au lile likoje?"

"Kuna nini katika eneo hili au lile?"

Baadaye, Mtume (s.a.w) alizungumza kuhusu suala hilo:

"Watu wa Makka waliniuliza maswali kuhusu maeneo niliyopita na hususan kuhusu Masjid al-Aqsa ambayo sikuichunguza katika safari ya Isra. Hata hivyo, waliponiuliza ili kunijaribu, Allah Mtukufu alinionesha Mayt al-Maqdis. Niliyajibu maswali yao kwa kuitazama".

Wapagani ambao walijibiwa kwa usahihi maswali yao yote bado waliendelea kukaidi na kukana. Walielekea moja kwa moja kwa Abu Bakr (r.a):

"Muhammad anatwambia kuwa usiku wa jana alikwenda Jerusalem, akapaa kwenda mbinguni na kurudi. Hili nalo utaliamini?" walisema. Abu Bakr (r.a) akajibu bila kusita:

"Yote anayosema ni kweli. Kwa maana, hakuna sababu au uwezekano wa yeze kusema uongo. Ninaamini kile anachokieleza", alisema. Wapagani wakamuuliza tena:

"Kwa hivyo sasa unasadiki na kuamini kuwa ndani ya usiku mmoja alikwenda Masjid al-Aqsa na kurudi?"

Abu Bakr (r.a) akajibu:

### **Unadhani wapagani walifanya nini baada ya kusikia jibu hilo la Abu Bakr (r.a)?**


Baadaye Abu Bakr (r.a) alikwenda kwa Mtume (s.a.w) ambaye wakati huo alikuwa kwenye Ka'bah. Alisikiliza moja kwa moja yaliyotokea usiku wa Isra na Mi'raj kutoka kwenye kinywa chake kitukufu, akasema:

"Swadakta, ewe Mjumbe wa Allah!"

"Naam, kuna ubaya gani juu ya hilo? Ninaapa kwa Allah, ananiambia kuwa anapokea ufunuo kutoka kwa Allah wakati wowote asubuhi au usiku, na bado ninamsadiki."

Kwa kufurahishwa na usadikishaji wake, Mjumbe wa Allah (s.a.w) alimwambia Abu Bakr (r.a) kwa tabasamu lilioiangaza dunia:

"Ewe Abu Bakr, wewe ni Siddiq (Msadikishaji)!" (Ibn Hisham, II)



## 3-KIMBILIO LA MWISHO: HIJRA, HUZUNI YA KUIACHA MAKKA


Hali ilikuwa ngumu kwa Waislamu kuendelea kuishi Makka kutohana na wapagani kuongeza mateso na maudhi dhidi yao. Kwa sababu hiyo, wakati wa Kiapo cha Pili cha Aqaba, iliamuliwa kuwa Mtume (s.a.w) na Waislamu wahamie Madina. Mjumbe wa Allah (s.a.w) aliwaruhusu Waislamu kuhamia Madina akisema: "Nimeoneshwa sehemu tutakayohamia. Nimeona ardhi yenyeye chumvi, iliyopandwa mitende na iko katika ya milima miwili..." (Bukhari, Kafalah, 4).

Katika mwezi wa Muhamarram (Julai 622), Waislamu walianza kuhamia kwa siri kuelekea Madina katika makundi tofauti tofauti. Baadhi yao walihama mmoja mmoja na wengine walikuwa pamoja na familia zao. Mtu wa kwanza kuhamia Madina ni Abu Salama ibn Abdussamad na wa mwisho alikuwa ami wa

Mtukufu Mtume (s.a.w), bwana Abbas.

Ndani ya kipindi cha kuanzia mwanzo wa Hijra mpaka ufunguzi wa Makka, Waislamu waliohamia Madina kwa ruhusa ya Mjumbe wa Allah wakiyaacha makazi yao, mali zao, familia zao, ndugu zao na kila kitu walichokuwa nacho kwa ajili ya dini yao walijulikana kama Muhibbin. Ama Waislamu wa Madina waliowakaribisha Muhibbin mjini Madina, wakashirikiana nao mali zao na kuonesha uungwana usiomithilika, walijulikana kama Ansar.

Umar (r.a) hakuhamia kwa siri. Hakumuogopa mtu yeoyote. Alipokuwa akijiandaa kwa safari, aliufunga upanga kiunoni mwake na akaueweka upinde wake begani mwake. Aliishika mishale na mkuki wake, akaelekea kwenye Ka'bah. Wakati





huo, viongozi wa wapagani walikuwa jirani na Ka'bah. Baada ya kuizunguka Ka'bah, Umar (r.a) aliwaendea na kusema kwa sauti nzito kana kwamba anaonesha hatua ya kwanza ya ushindi wa baadaye:

"Sasa ninakwenda Madina! Anayetaka kumliza mama yake, kumuacha mkewe akiwa mjane na watoto zake wakiwa mayatima, basi akutane nami nyuma ya bonde hili!" Lakini hakuna ye yote aliyethubutu kumfuata. (Ibn Asir, Usd al-Ghaba, IV, 152-153)

Ndani ya muda mfupi, takribani Waislamu wote wa Makka walihamia Madina. Abu Bakr na Ali pekee ndio walioagizwa na Mjumbe wa Allah kubaki Makka. Hakuna Muislamu aliyekuwa amebaki Makka isipokuwa baadhi ya watumwa na wale waliokuwa wamezuiliwa na familia zao kwa sababu ya kuingia katika Uislamu.

#### a) Mpango Hatari wa Wapagani

Baada ya Kiapo cha Utii cha Aqaba, Uislamu ulianza kusambaa mjini Madina. Wapagani walijawa na wasiwasi mkubwa. Sasa wakaanza kufikiria na kuwaza kipi cha kufanya iwapo Muhammad ataenda Madina na kuwa na udhibiti kwa Waislamu. Hilo liliwatia wasiwasi kwa sababu ya njia yao ya kibashara kwenda Damascus inayopitia karibu na mji wa Madina. Waislamu wangeweza

kuwashambulia kiurahisi kutokea huko. Kwa kuwa waliamiliana nao vibaya, Wapagani walianza kuhofu kwamba Waislamu wanaweza kutaka kufanya kisasi baada ya kujikusanya na kuwa na nguvu.

Wapagani walitaka kuwa na kauli moja ya nini cha kufanya ili kupata suluhisho sahihi la hali yao. Walikusanyika katika Dar al-Nadwa kwa ajili ya kujadiliana. Katika kikao hicho, takribani wakuu wote wa Makka walikuwe po, kama vile Abu Jahl, Abu Sufian, Abu al-Bahtari, Utba ibn Rabia. Kila mmoja alitoa wazo lake la kuufuta Uislamu. Abu al-Bahtari alishauri:

"Tumfunge kamba Muhammad na tumuweke kizuzini katika eneo ambalo limefungwa kila sehemu mpaka afariki dunia."

Hisham ibn Amr akasema:

"Tumpandishe juu ya ngamia, tumfukuze Makka na kumfanya aende mbali."

Ama Abu Jahl, ye ye alisema:

"Tuchague mtu mmoja kutoka kila ukoo wa Maqrayshi na wote wamshambulie Muhammad kwa pamoja na kumuua kwa pigo moja. Haitawezekana kujua ameuawa kwa pigo la nani. Kwa namna hii, ukoo wa Hashim, familia ya Muhammad, hawawezi kupambana na kabilo lote la Maqrayshi kwa lengo la kulipiza kisasi. Hawatakuwa na njia

nyingine zaidi ya kukubali fidia. Na hivyo suala hili litakuwa limemalizwa". Wazo la Abu Jahl lilkubaliwa na wote.

Maongezi na mipango hiyo ya Wapagani waliyoifanya katika Dar al-Nadwa imeelezwa kwa ufupi katika Ayah ya 30 ya surah al-Anfal:

**"Na walipo kupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango."**

### b) Wauaji waingia Kazini

Malaika Jibril (a.s) alimhabarisha Mtume (s.a.w) kuhusu mpango wa kuogofya wa wapagani. Alimwambia: "Usiku huu usilale kwenye kitanda chako kama ufanyavyo siku zote, ondoka nyumbani kwako". Hivyo, Mtume (s.a.w) naye alipewa idhini ya kuhamza. Alimuuta Ali (r.a) na kumwambia: "Ninakwenda Madina. Utalala kwenye kitanda changu usiku wa leo na ujifunike shuka yangu ili wapagani wadhani kuwa mimi ndiye niliyelala. Usiwafanye wakagundua chochote. Asubuhi, chukua vitu hivi niliyokabidhiwa kama amana na usikabidhi kwa watu wake. Baada ya hapo, njoo haraka Madina".

Giza lilipoingia, wauaji waliizingira nyumba. Walipanga kumfanyia shambulizi la ghafla pindi atakapoondoka nyumbani wakati wa asubuhi. Ali (r.a) alilala kwenye kitanda cha Mjumbe wa Allah (s.a.w). Mtukufu Mtume (s.a.w) alichukua udongo kwa mkono wake na kuwamwagia wapagani waliokuwa wamezunguka nyumba yake. Vumbi hiyo iliwafanya wote walale haraka. Mjumbe wa Allah (s.a.w) alisoma Ayah tisa za mwanzo wa surah Yasin.

Baada ya kusoma ayah ya tisa: "**Tumeweka kizuizi mbele yao, na kizuizi nyuma yao, na tumewafunika macho yao; kwa hivyo hawaoni**", alipita katikati yao na kuondoka. Wapagani walidhani kuwa Mtume (s.a.w) bado amelala kitandani kwake. Ilipofika

asubuhi, walipobaini kuwa Ali (r.a) ndiye aliye kuwa amelala kitandani, walitahayari wasijue la kufanya. Walisikitika sana kiasi kwamba bila kupoteza muda wowote, walianza kumsaka. Walitafuta kila mahala katika mji wa Makka lakini hawakumuona.

Baada ya kuondoka nyumbani, Mjumbe wa Allah (s.a.w) alifanya tawaf kwenye Ka'bah. Aliitazama Makka kwa mara ya mwisho huku machozi yakimengalenga na kusema: "**Ewe Makka, hakika wewe ni sehemu bora ninayoipenda zaidi duniani. Laua nisingelazimishwa kuondoka, nisingekuacha**".

Siku iliyofuata, chini ya juu kali, alienda nyumbani kwa Abu Bakr (r.a). Alimtaarifu kuwa watafanya hijra pamoja kwa amri ya Allah. Abu Bakr (r.a), huku machozi yakimengalenga kwa furaha, alimuonesha ngamia wawili aliokuwa amewaandaa kwa ajili ya hijra na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Allah, ngamia mmoja ni wako! Chagua yelete umtakaye". Mtume (s.a.w) alichagua mmoja wao kwa kulipa pesa na kisha wakaondoka.

### c) Siku tatu Pangoni

Wakati wa usiku, walipita kwenye dirisha la upande wa nyuma ya nyumba. Kwa kutumia njia za nyikani zinazoelekeea upande wa kusini mwa Makka, walielekeea kwenye mlima Thawr ambaa ulikuwa kwenye umbali wa saa moja na nusu kwa kutembea kwa miguu. Walifika kwenye pango lililopo kwenye mlima huo. Kwa siku tatu ambazo wapagani walikuwa wakiwatafuta, walikuwa wamejificha ndani ya pango hilo.

Wakati wa usiku, mtoto wa Abu bakr aitwaye Abdullah alikuwa akija kwenye pango na kuwaeleza yaliyokuwa yakiendelea mjini Makka na kurejea Makka kabla ya mapambazuko. Mtumishi wake, Amr ibn Fuhaira, naye pia alikuwa akileta kondoo wakati wa jioni na kuwapa maziwa.

Hatimaye, watu waliokuwa wakimtafuta Mtume (s.a.w) na Abu Bakr walifika kwenye lango la pango la mlima Thawr. Hatua na sauti zao zilikuwa zikisikika.

Kama wapagani hao wangeinama kidogo na kutazama ndani, wangeweza kuwaona kwa urahisi. Walikuwa wakitembea pembezoni mwa pango hilo na kusema:

"Kama wangekuwa wameingia katika pango hili, mayai ya njiwa huyu yangekuwa yamepasuka na utando wa buibui kwenye lango la pango ungekuwa umeharibiwa".

Wengine wakasema:

"Tutazame ndani ya pango."


Hapo Ummayy ibn Khalaf akasema:

"Je, hamatumii akili? Mtafanya nini huko? Mtapita katika mlango wa pango hili ambao buibui ameweka utando wake? Ninaapa kwa Allah, ninadhani buibui huyu alikuwepo hapa kabla hata Muhammad hajazaliwa".

Ama Abu Jahl, yeye alisema:

"Ninaapa kwa Allah, nahisi kuwa yuko karibu nasi! Lakini ametuzubaisha kwa uchawi na kuyafanya macho yetu yasione".

**Kwa mfano, wewe kama Muislamu ungekuwepo huko, ungefanya nini?**



## NYOKA MWENYE KUNG'ATA

Wakati wakiwa pangoni, Mjumbe wa Allah (s.a.w) aliweka kichwa chake kitukufu juu ya magoti ya Abu Bakr na kuchukuliwa na usingizi. Abu Bakr (r.a) aliona shimo dogo pembezoni mwake. Aliliziba shimo hilo kwa kiigizo chake taratibu bila kumuamsha Mtume (s.a.w) ili kama kuna mdudu asitoke kuja kumdhuru.

Baada ya muda, nyoka aliyekuwa ndani ya shimo hilo aliugonga mguu wa Abu Bakr (r.a) na kutema sumu yake. Alipata maumivu makubwa lakini hakutikisika ili kutomuamsha Mjumbe wa Allah. Hata hivyo, alishindwa kuyazuia machozi yake yasidondoke kufokana na maumivu hayo. Tone moja la machozi lilitondoka usoni kwa Mtume

(s.a.w). Hapo Mjumbe wa Allah akaamka na kumuuliza:

"Kuna tatizo gani ewe Abu Bakr? Nini kimetokea?"

Abu Bakr (r.a) akajibu: "Hakuna kitu". Lakini Mtume (s.a.w) alipospositiza kutaka kujua kilichotokea, akamwambia kuwa nyoka amemgonga mguuni mwake.



Wakati huohuo, Abu Bakr (r.a) alikuwa mwenye wasiwasi. Alimwambia Mjumbe wa Allah (s.a.w):

"Nikiuawa, mimi ni mtu mmoja tu. Nitaondoka kwenvye uso wa ardhi.

Lakini chochote kikutokea, umma wote utaangamia".

Mtume (s.a.w) akamjibu swahibu wake:

"Usiogope ewe Abu Bakr! Hakika Allah yuko pamoja nasi".

Baada ya tukio

hilo, Mjumbe wa Allah na Abu Bakr walipanda juu ya ngamia mmoja huku muongozaji Abdulla na mtumishi wa Abu Bakr, Amr ibn Furaira wakitumia ngamia wa pili. Walifuata njia ya pwani, wakasafiri kuelekea Madina bila kupumzika.

Walitumia siku nane kwa safari ya umbali wa siku 13 na kufika katika kijiji cha Quba siku ya Jumatatu tarehe 12 Rabiulawwal au 23 Septemba mwaka 622 Miladiya.

Watu wa Madina walikuwa warmeshapata taarifa kuhusu safari ya Mjumbe wa Allah. Hivyo, kila asubuhi walikuwa wakienda nje ya mji na kusubiri kwa shauku ujio wa Mtume (s.a.w) ili wamkaribishe.





**d) Kuwasili Madina na Swala ya kwanza ya Ijumaa**

Wakazi wa Madina walienda kumlaki Mjumbe wa Allah (s.a.w) katika kijiji cha Quba, ambacho kipo umbali wa saa moja kutoka mjini Madina. Mjumbe wa Allah (s.a.w) alikaa huko kwa Bani Amr ibn Awf kwa muda wa siku 14. Alijenga Masjid Quba na kuswali huko.

Ali (r.a) ambaye aliondoka Makka siku 3 baada ya Mjumbe wa Allah aliwakuta Quba.

Siku 14 baadaye ikiwa ni siku ya Ijumaa, Mtume (s.a.w) alichukua kipando chake na kuelekea Madina akiandamana na watu waliokuja kumlaki. Wakati wa adhuhuri, walikuwa katika bonde la Ranuna. Huko, Mjumbe wa Allah (s.a.w) alitoa hotuba mbili za Ijumaa na kuongoza Swala ya Ijumaa.

Katika hotuba ya kwanza, alisimama na kumhimidi Allah Mtukufu, kisha akasema:

"Enyi watu! Tubuni kwa Allah kabla mauti hayajawadiriki, tangulizeni amali njema wakati bado mna fursa. Imarisheni mafungamano yenu na Allah kwa kumdhukuru, kutoa sadaka kwa siri na dhahiri. Tambueni kuwa katika siku hii ya mwezi huu, Allah Mtukufu amekufaradhishieni Swala ya Ijumaa mpaka Siku ya Hukumu. Wakati wa uhai wangu au baada yangu, yeyote atakayeiacha swala hii kwa sababu ya kuipuza au kuikana, Allah asiyatimize matakwa yake ya dunia na Akhera na asimpe manufaa ya chochote.

Mwenye kuweza kujilinda na Moto wa Jahannam, hata kwa kutoa sadaka ya kipande cha tende, basi afanye hivyo; na asiyeweza kufanya hivyo, basi ajilinde kwa kutamka maneno mazuri kwa masikini, kwa maana amali moja njema hulipwa thawabu mara kumi mpaka mara mia saba".

Baada ya kumaliza hotuba ya kwanza, Mjumbe wa Allah alitoa hotuba ya pili kwa kusema:

"Himidi zote zinamstahiki Allah, ninamhimidi na kumtaka msaada. Tunajilinda Kwake dhidi ya shari za nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu. Yule ambaye ameongozwa na Allah hakuna awezaye kumpoteza na yule ambaye Allah amemuacha apotee hakuna awezaye kumuongoa.

Na ninashuhudia kuwa hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, Wa pekee, hana mshirika. Hakika maneno bora ni Kitabu cha Allah. Amefaulu yule ambaye Allah ameuangaza moyo wake kwa nuru yake akamtoa kwenye giza la ukafiri kumpeleka kwenye nuru ya Uislamu, kwa maana ameyachagua maneno ya Allah juu ya maneno ya wanadamu. Hakika, maneno Yake ndio maneno bora na fasaha kuliko maneno yote. Kipendeni kile kinachopendwa na Allah; mpendeni Allah kwa moyo wenu wote.

**"Msiwe wenye kuyachoka maneno ya Allah, kulidhukuru Jina Lake na msizifanyе nyoyo zenu kuwa na ugumu. Hakika, Allah huchagua katika kila alichokiumba."**

### e) Mwezi umetuchomozea

Baada ya Swala ya Ijumaa, Mjumbe wa Allah (s.a.w) alielekea Madina. Mji wa Madina uliipokea siku muhimu kabisa katika historia yake. Wakazi wake waliojawa furaha walikuwa wamejipanga kwenye pande zote za barabara

ra itokayo Quba. Wanawake waliku wakiimba, watoto walikuwa wakisema kwa sauti: "Mjumbe wa Allah amewasili; Mjumbe wa Allah amefika..." mabinti wadogo walifurahika huku wakipringa matara. Wakazi wa Madina hawakuwahi kuwa na furaha kama waliyokuwa nayo siku ya ujio wa Mtukufu Mtume (s.a.w).

### Kama ungekuwepo, ungeonesha vipi furaha yako kwa kukutana na Mtume (s.a.w)?

Kila mtu alitaka kuwa mwenyeji wa Mtukufu Mtume (s.a.w) na kumkaribisha nyumbani kwake. Walikuwa wakijaribu kumsimamisha ngamia wake kwa kusema: "Ewe Mjumbe wa Allah! Tafadhali njoo ukae nasi..." Ili kutomkosea yeyote, Mjumbe wa Allah alimuacha huru ngamia wake. Alikuwa akisema:

— Iwacheni wazi njia ya ngamia. Ataenda sehemu alipoamrishwa kwenda.

Hatimaye ngamia alipiga magoti mahala ulipo Msikiti wa Mtume kwa sasa, lakini Mtukufu Mtume (s.a.w) hakushuka. Ngamia aliihuka, akaenda mbele hatua kadhaa kisha akarudi

kwanza na hapo hakuinuka tena. Mjumbe wa Allah (s.a.w) aliteremka na kuauliza watu:

— "Nyumba ya nani iliyo karibu zaidi mionganoni mwa ndugu zetu?" Khalid ibn Zaid alimkaribisha akisema:

— Ewe Mjumbe wa Allah, hapa nyumbani kwangu, mlango uko wazi. Karibu sana!

Hivyo, Mtukufu Mtume (s.a.w) akafikia kwa Khalid (r.a). Aliendelea kuwa mgeni wake kwa muda wa miezi saba mpaka ulipokamilika ujenzi wa Msikiti wa Mtume, vyumba vyake na vyumba vyta wake zake.




## 4- MAISHA KATIKA MAKAO MAPYA YA MJI WA MADINA (MWAKA 622 MILADIYA)

Madina ni mji unaopatikana kaskazini mwa Makka na umezungukwa na milima katika pande zake tatu. Upande wa kusini unapakana na mabonde. Hali ya hewa ya Madina ni nzuri; ardhi yake inafaa kwa kilimo na kuna mashamba mengi ya mitende. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipohamia katika mji huo, palikuwa na makabila mawili ya Kiarabu, yaani Aws na Khazraj. Pia palikuwa na makabila mawili ya Kiyahudi, yaani Qaynuqa, Banu Nadhir na Banu Quraydha.

Kulikuwa na uadui kati ya makabila ya Aws na Khazraj ambao ulikuwa ukiendelea kwa miaka mingi. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipofika Madina, alitangaza udugu kati ya wahajirina wa Makka na ndugu zao Ansar wa Madina. Watu wa Aws na Khazraj wakapata fursa ya udugu na upendo wa Kiislamu. Uhasama na uadui uliokuwa kati yao ukabadilika kuwa upendo na udugu.

Mjumbe wa Allah (s.a.w) aliagiza majina ya Waislamu mjini Madina yahesabiwe na kuandikwa. Hivyo, sensa ikafanyika. Idadi jumla ya wahajiri kutoka Makka na Ansar wa Madina ilikuwa 1500.



### a) Ujenzi wa Msikiti wa Mtume (s.a.w)

Wakati wa hijra hapakuwa na msikiti wowote mjini Madina. Mjumbe wa Allah (s.a.w) alikuwa akiongoza swala mahala popote anapokuwa pindi muda wa swala unapowadia. Msikiti wa kwanza ulijengwa katika kijiji cha Quba katika siku za mwanzo za hijra.

Msikti ungejengwa katika eneo la wazi ambalo ngamia wa Mtume (s.a.w) alipiga magoti wakati wa hijra mbele ya nyumba ya Zayd. Eneo hilo ilikuwa likimilikiwa na yatima wawili wa Bani Najjar. Japokuwa walitaka kulitoa bure kama sadaka, Mtume (s.a.w) hakukubali. Abu Bakr (r.a) alilinunua kwa sarafu 40 za dhahabu na ujenzi ukaanza.

Wakati wa ujenzi wa msikiti huo, Mjumbe wa Allah (s.a.w) alishirikiana moja kwa moja na wajenzi wengine. Wanawake na watoto nao pia walishiriki katika ujenzi kwa kufanya kazi wakati wa usiku. Msingi ultengenezwa kwa mawe; kuta zilikuwa za matofali ya udongo; na nguzo zilikuwa za miti ya mitende. Sakafu ilikuwa ya mchanga na juu kulikuwa na matawi ya mitende. Msikiti huu ulikuwa na jumla ya milango mitatu: mlango mkuu ulikuwa ng'ambo ya mihrab, wa pili ulikuwa ukielekeana na nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w), na wa mwisho ulikuwa ukiitwa "Mlango wa Rehma".

## MACHOZI

Mtu aliyeifurahia zaidi swala na kuijua maana hasa ya swala ni Mtume wetu (s.a.w). Alipenda mno kuwa karibu na Allah kwa kuswali. Anapomaliza kuswali, alikuwa akiisubiri kwa hamu swala nyingine. Pia alipenda kuswali pamoja na maswahaba zake. Kwa sababu ya kusimama muda mrefu kwenye swala wakati wa usiku, miguu yake ilikuwa ikivimba. Hata hivyo, wakati wa swala, alikuwa akishindwa kufuata muda kwa sababu ya furaha ya kiroho anayoipata wakati akitafakari kwa kina maana ya Ayah anazosoma. Wakati fulani, machozi yake, yakiambatana na hisia nyingi za moyo wake, yalikuwa yakilowesha mahala anaposujudu.

Siku moja, Bilal al-Habashi (r.a) alikuja msikitini na kumkuta Mtukufu Mtume (s.a.w) akiwa katika hali hiyo, akamuuliza:

— “Ewe Mjumbe wa Allah! Hakika umeshafutiwa dhambi zako zilizopita na zijazo, na hutendi dhambi yoyote, kwa nini unaswali na kulia sana?” Mtukufu Mtume (s.a.w) akajibu:

— “Ewe Bilal, je sipaswi kumshukuru Mola wangu?” (Tazama: Bukhari, Tafsir,48)



### b) Maswahaba walioishi msikitini ili kutafuta elimu: As-hab al-Suffah

Kwenye sehemu moja ya msikiti, walijenga aina ya kivuli (suffa) ambayo kuta zake zilikuwa wazi na upande wa juu ulifunikwa kwa matawi ya mitende. Waislamu ambao hawakuwa na makazi na familia walikuwa wakiishi huko. Ndiyo maana wakaitwa “as-hab al-Suffah”, yaani watu wanaoishi kivilini. Watu hao walikuwa masikini sana. Wanapopata kazi huifanya na muda mwingine hukaa msikitini wakijifunza Qur'an Tukufu na dini, na kutumia muda wao katika kumuabudu Allah Mtukufu.

Eneo hili ni kitovu cha kwanza cha mafunzo, kwa maneno mengine ni shule ya kwanza katika historia ya Uislamu. Msikiti ulikuwa darasa la shule hii, bweni lake ilikuwa suffah na wanafunzi wake walikuwa maswahaba hao

masikini. Mwalimu wao alikuwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.).

Pindi linapotoka hitajio la kutuma walimu wa kufundisha Uislamu kwenye jamii zilizosilimu nje ya mji wa Madina, walikuwa wakitumwa kutoka kundi hili la maswahaba wa Suffah. Mahitaji ya As-hab al-Suffah ambao idadi yao ilikuwa kati ya 70 na 400 yalitolewa na maswahaba wenye mali. Kila jioni, Mjumbe wa Allah (s.a.w) alikuwa akiwaalika baadhi ya maswahaba hawa kwenye chakula cha usiku nyumbani kwake, na wengine walikuwa wakialikwa na maswahaba wengine. Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akiwagawia sadaka zote na pia kutunza sehemu ya zawadi anazoletewa kwa ajili ya watu wa Suffah.

### c) Adhana ya kwanza

Baada ya kukamilisha ujenzi wa Msikiti wa Mtume (s.a.w), ilihitajika kuwa na utaratibu wa kuwatangazia Waislamu muda wa swala. Wale wanaokuja mapema kwenye swala walikuwa wakichelewa katika kazi zao wakati wakisubiri muda wa swala ufike, kwa upande mwingine wale aliochelewa walikuwa wakihuzunika kwa kutoidiriki jamaah. Mjumbe wa Allah (s.a.w) alikuwa na utaratibu wa kuchukua maoni ya maswahaba kuhusu masuala ambayo hakuna ayah iliyoteremka kuyazungumzia. Wakati wa mashauriano kuhusu jambo hili, maswahaba walitoa mapendekezo mbalimbali kama vile: kutumia kengele, ngoma, kuwashaa moto na kusimika bendera kwenye eneo lenye muinuko. Mtukufu Mtume (s.a.w) hakukubaliana na mapendekezo hayo yote, akasema: "Kengele ni mila ya Wakristo, ngoma ni mila ya Wayahudi na moto ni mila ya Wamajusi".

Pendekezo la kupandisha bendera nalo halikukubaliwa. Mashauriano hayo hayakuzaa matunda, hivyo hakuna uamuza uliofanyika. Abdullah ibn Zaid aliota ndoto ambapo

alimuona mtu akiwa amebeba kengele mkononi mwake na akataka kuinunua kwa ajili ya kuitumia kutoa taarifa ya muda wa swala. Lakini, mtu yule aliyemuona ndotoni akamwambia:

— "Ngoja nikufundishe kitu kizuri zaidi", akamfundisha maneno ya Adhana. Abdullah alipoamka, alienda kwa Mjumbe wa Allah na kumtaarifu kuhusu ndoto yake. Mtume (s.a.w) akamwambia:

— "Hakika ni ndoto njema. Sauti ya Bilal ni yenye kuvuma sana kuliko yako. Hivyo, mfundishe uliyoyaona ndotoni. Mwambie ayasome muda wa swala unapowadia."

Adhana iliyotolewa Bilal Mhabeshi kwa sauti yake tamu yenye kuvuma ilisikika katika mji wote wa Madina. Nyoyo za waliosikia adhana zilijawa na furaha ya kiroho isiyoelezeka. Vilevile Umar (r.a) aliona ndoto kama hiyo lakini Abdullah ndiye aliyeanza kuielezea. Baadaye, Bilal aliongeza maneno yafuatayo kwenye adhana ya Alfajiri: "as-salatu khairun min alnawm" yaani: "Swala ni bora kuliko usingizi".

**Kama ungeisikia adhana ya Bilal Mhabeshi kwa mara ya kwanza,  
ungejisikiaje?**



#### d) Udugu wa Kipekee

Waislamu wa Makka walikuwa wameacha mali na milki zao mjini Makka kwa ajili ya imani yao na kuhamia Madina. Ama Waislamu wa Madina, ambao waliwapendelea Muhajirina kuliko nafsi zao, waliwasaidia kwa kila kitu na kukidhi mahitaji yao yote. Hata hivyo, Muhajirina walikuwa wakijisikia vibaya kwa kudhani kuwa watakuwa mzigo kwa Ansar, kwa maana hawakuwa na mali na mapato yao wenye.

Mjumbe wa Allah (s.a.w) aliwakusanya Muhajirina na Ansar ili kuondosha huzuni ya Muhajirina na kuimarisha upendo na usafi wa moyo kati yao. Alianzisha mafungamano ya udugu kati yao. Ansar waliwachukua ndugu zao Muhajirina kuwapeleka majumbani kwao, wakawafanya kuwa washirika wao katika mali zao. Walikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w):

"Ewe Mjumbe wa Allah, gawa mitende yetu kati yetu na ndugu zetu Muhajirina", waalisema. Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema:

"Hapana, umiliki utabaki kwenu, fanyeni kazi pamoja na ndugu zetu Muhajirina, kisha gawaneni mazao na faida".

Sa'd ibn Rabi' kutoka jamii ya Ansar alimwambia Abdurrahman ibn Awf kutoka jamii ya Muhajirina:

"Mimi ni mtu tajiri zaidi katika Ansar. Mjumbe wa Allah (s.a.w) ametufanya kuwa ndugu. Nusu ya mali yangu ni yako, chukua ukipendacho". Abdurrahman akajibu:

"Allah aibariki mali yako. Siihitaji. Nitatosheka ukinionesha soko lilipo, ninaweza kufanya biashara".

#### Ungefanyaje ungepewa ofa kama hiyo? Kwa nini?

Abdurrahman alianza kufanya biashara, ndani ya muda mfupi akawa tajiri. Muhajirina wengi walianza kupata kipato chao kupitia biashara.





## CHUKUA UIPENDAYO NDUGU YANGU

Muhajirina waliyaacha makazi yao, mashamba yao, mali zao, kwa ufupi walichacha kila kitu walichokuwa nacho mjini Makka na kuhamia Madina. Hata hivyo, Ansar walionesha udugu wa ajabu kiasi kwamba walishirikiana na Muhajirina makazi yao, mali zao, mashamba yao na mazao yao.

Wakazi wa Madina walitoa nusu ya mitende yao na kuwapa ndugu zao kutoka Makka. Walifanya kazi na ndugu zao Muhajirina kwenye mashamba hayo na muda wa mavuno unapowadia na tende zilizopatikana ziligawanywa katika mafungu mawili. Ili kuwapa zaidi ndugu zao kutoka Makka, walikuwa wakiweka tende nydingi kwenye fungu moja na tende chache kwenye fungu lingine huku

wakiweka mitawi ya mitende kwenye fungu la pili ili lionekekane kuwa ni kubwa. Kisha huwaambia ndugu zao Muhajirina: "Ndugu yangu, chukua fungu ultakalo". Muhajirina walikuwa wakipendelea kuchukua lenye tende chache ili ndugu zao Ansar wapate tende nydingi. Lakini kiuhalisia hujikuta wamechukua fungu lenye tende nydingi bila kujua. Udugu wa Kiislamu katika nyoyo zao ulikuwa ukiwapeleka kwenye kilele cha ukarimu.



Muhajirina walikabiliana na nyakati hizo ngumu kwa kufanya kazi na kufanya biashara. Baada ya Vita vya Badr, walipopata fungu katika ngawira zao, hawakuhitajia tena msaada kutoka kwa Ansar.

Baada ya Mjumbe wa Allah (s.a.w) kuwaunganisha Muhajirina kutoka Makka na Ansar wa Madina kwa kuanzisha udugu katika yao ili kuulinda mji wa Madina kwa pamoja dhidi ya maadui kutoka nje, aliandika "Mkataba wa Uraia" katika ya Ansar na Wayahudi wa Madina.

### e) Chuki Isiyokwisha Ya Wapagani

Kwa upande mwagine, uadui na chuki ya wapagani haikwisha. Waliendelea kuwachokoza na kuwachochea Waarabu wa Madina dhidi ya Waislamu. Walikuwa wakiwatisha wakazi wa Madina kwa kuwaambia:

"Mnamruhusu Muhammad aishi katika ardhi yenu. Msipomuua au kumkabidhi kwetu, tutawaadhibu. Msipomfukuza kutoka Madina, tutaivamia Madina ili kuwaua nyote na kuwachukua mateka wanawake na watoto wenu".

Waislamu hawakupata utulivu hata baada ya kuhamia Madina. Hivyo, Mtukufu Mtume (s.a.w) alichukua tahadhari zote kuhusu ulinzi wa mji wa Madina. Alifanya makubaliano ya amani na Wayahudi wa Madina na makabila ya wapagani wa Kiarabu waliokuwa wakiishi pembezoni mwa mji huo. Kwa kutuma vikosi vya askari wachache kufanya doria, alihakikisha harakati za maadui zinakuwa chini ya udhibiti. Alizua njia ya biashara iliyokuwa ikitumiwa na wapagani wa Makka kwenda Damascus. Waislamu walikuwa wakilinda na kufanya doria katika mitaa ya mji wa Madina

kama tahadhari ya shambulizi lolote la wapagani ambalo lingefanywa usiku.

Hata Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akilala kwa amani pale tu baadhi ya Waislamu wanapoweka ulinzi kwenye mlango wake dhidi ya shambulizi lolote la adui.

**f) Ruhusa Ya Kupigana (Mwaka 623 – 624)**

Uislamu ni dini ya amani. Katika Uislamu, vita hufanywa tu kwa lengo la kuzuia manyanyaso na kuondosha dhulma. Licha ya manyanyaso, mateso na dhulma walizofanyiwa na wapagani wa Makka kwa miaka kumi na tatu mjini Makka, waumini waliendelea kuwa na subira. Walikuwa wakijaribu kueneza Uislamu kwa amani. Kwa sababu vita havikuwa vimeruhusiwa. Waislamu hawakuwa na nguvu wala rasilimali

za kukabiliana na kupambana na wapagani.

Baada ya kuhamia Madina, taratibu Waislamu walianza kuwa imara kwa upande wa idadi na uwezo wa kiuchumi kiasi cha kuweza kukabiliana na wapagani. Subira ya Waislamu ilikuwa ikizidisha mabavu na manyanyaso ya wapagani. Hatimaye, Ayah ifuatayo iliteremshwa: **"Wameruhusiwa kupigana wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia. Wale ambaao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Allah..."** (Surah al-Hajj 22: 39-40) Hivyo Waislamu wakaruhusiwa kupigana kwa lengo la kujitetea.




## 5- VITA VYA BADR (Mwaka 624)

### a) Uadui usiokwisha

Wapagani wa Makka walikuwa wakijiandaa kufanya shambulizi dhidi ya mji wa Madina, kumuua Mijumbe wa Allah (s.a.w) na kuufuta kabisa Uislamu. Ili kugharamia vita hivyo, walituma msafara mkubwa wa biashara ukiongozwa na Abu Sufian kupitia njia ya Madina kwenda Damascus. Katika msafara huu kulikuwa na bidhaa na mali za Waislamu walizoziacha walipohamia Madina. Wapagani walikuwa wamezinyakua kwa mabavu mali za Waislamu na sasa waliku wameziweka kwenye

msafara huo na kutaka kuziwa. Kupitia pesa ambayo wangeipata, wangegharamia maandalizi ya vita vya kuufuta Uislamu.

Mtukufu Mtume (s.a.w) alipata taarifa za maandalizi hayo yaliyofanywa mjini Makka. Alitaarifiwa kuwa baada ya bidhaa zote kuuzwa, msafara wa wapagani ulikuwa ukirejea Makka. Akiwa na lengo la kuuzuia msafara huo, alimuacha Abdullah ibn Maktum kama imam mjini Madina na kuondoka akiwa na watu 313 tarehe 12 ya mwezi wa Ramadhan.



Akiwa njiani, watu 8 waliomba idhini ya kurudi kwa sababu ya nyudhuru mbalimbali. Walibaki watu 305, miongan mwao watu 64 walikuwa Muhajirina na wengine wote walikuwa Ansar. Hawakuwa na ngao wala vipandwa. Hivyo, walikuwa wakipanda ngamia kwa zamu.

Kwa upande mwagine, Abu Sufyan alikuwa ameshamtuma mtu kwenda Makka kuomba msaada wa kupata ulinzi iwapo Waislamu wataushambulia msafara wake. Wapagani wa Makka ambao walikuwa wamejiandaa kwa miezi kadhaa kwa ajili ya vita walifunga safari wakiwa na jeshi la watu 1000 chini ya uongozi wa Abu Jahl kwa lengo la kuuokoa msafara huo na kulipiza kisasi

dhidi ya Waislamu. Jeshi hili ambalo viongozi maarufu wa Makka walishiriki, isipokuwa Abu Lahab, lilikuwa na askari 200 wa farasi, askari 700 waliopanda ngamia na waliobaki walikuwa wakitembea kwa miguu.

Mjumbe wa Allah alipopata taarifa kwamba wapagani, wakiwa na jeshi kubwa, wanaelekea Madina kwa lengo la kuuokoa msafara wao wa biashara, alifanya mashauriano na maswahaba zake:

"Wapagani wameondoka Makka kuja huku. Je, tuufuatilie msafara au tukabiliane na jeshi la wapagani?"

### Je, nawe unadhani mashauriano ni muhimu? kwa nini?


Kwasababuya ukwelikwamba waliondoka mjini Madina wakiwa hawakujandaa kwa vita, wengi wao walikuwa wakipendelea pendekezo la kufuatilia msafara wa biashara. Baadhi ya maswahaba walisita kupigana na wapagani, jambo ambalo liliimhuzunisha Mjumbe wa Allah. Abu Bakr (r.a) na Umar (r.a) walishuhudia huzuni

yake hiyo, wakasimama na kutoa hoja kuwa itakuwa jambo jema zaidi kulikabili jeshi la maadui. Mtukufu Mtume (s.a.w) alitaka kupata maoni ya Ansar kuhusu jambo hilo. Aswad ibn Miqdad, ambaye alikuwa miongan mwaa watu wa mwanzo kuukubali Uislamu, alianza kuzungumza kwa niaba ya Muhajirina:

"Hatutkwmobia kama walivyofanya Wayahudi kumwambia Mussa kuwa 'henda wewe na Mola wako mkapigane na maadui'. Bali sisi tutapambana bega kwa bega pamoja na wewe dhidi ya maadui. Tutapigana kuliani na kushotoni kwako, mbele yako na nyuma yako. Tumetii amri ya Allah na Mjumbe Wake. Tutaenda popote utakapoenda".

Naye Muadh ibn Saad akazungumza kwa niaba ya Ansar:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Fanya upendavyo. Ninaapa kwa Allah aliyekutuma kwa haki kuwa Nabii, ukituonesha bahari na kuzama ndani yake, nasi pia tutazamia, hakuna yeyote miongan mwetu atakayerudi nyuma. Tunajua namna ya kupambana na adui na kuwa





thabiti katika medani ya vita. Basi twendeni tukalikabili jeshi la adui". Kutokana na hotuba hizo, Mjumbe wa Allah (s.a.w) alifurahi na kusema:

"Sasa, twendeni kwa baraka za Allah. Ninawaeleza kuwa Allah ametuahidi moja kati ya mambo mawili: kuukamata msafara au kulishinda jeshi la wapagani. Hakika tutapata ushindi. Ni kana kwamba tayari ninayaona maeneo ambayo viongozi wa Maqurayshi watauawa katika medani ya vita."

Kisha waliondoka kuelekea Badr.

Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwasimamisha wapiganaji wa Kiislamu katika eneo liitwalo Buyut al-Suqia, umbali wa maili moja kutoka Madina, ili kuwakagua askari wake. Wale waliokuwa na umri mdogo aliagiza warejee


mjini Madina. Saad ibn Abi Waqqas anasimulia tukio hili kama ifuatavyo:

"Mjumbe wa Allah alianza kuwarejesha wale waliokuwa na umri mdogo mmoja baada ya mwagine. Kaka yangu Umair alikuwa mionganoni mwa vijana wapya. Akijua kwamba anaweza kurejeshwa, nilimuona akijaribu kujificha katikati ya wale waliokuwa na umri mkubwa. Nilimuuliza:

'Kaka, kwa nini unafanya hivi?' Akasema:

'Ninahofu kuwa Mjumbe wa Allah anaweza kuniona na kunihamuru nirudi nyumbani! Lakini, hakika ninataka kushiriki katika vita hivi na ninatamani Allah anipe heshima ya kufa kishahidi'

### **Ungemwambia nini ndugu yako kama ungekuwa katika nafasi ya Umair?**



Hivyo, Mjumbe wa Allah alipoulima na kujua umri wake, alisema:

'Unatakiwa kurejea nyumbani.'

Hapo Umair akaanza kulia. Kwa sababu ya bidii ya ndugu yangu, Mtume (s.a.w) hakumkatalia na hivyo akampa ruhusa ya kuungana na jeshi. Kwa sababu ya ukweli kwamba ndugu yangu alikuwa mdogo sana na asiyejewa na uzoefu, mimi ndiye niliyemfunga upanga. Umair alikuwa na umri wa miaka 16 alipokufa kishahidi katika vita vya Badr". (Waqidi, I, 21)

Badr ni kijiji kilichokuwa umbali wa mwendo wa saiku 3 kutoka mjini Madina na umbali wa mwendo wa siku kumi kutoka mjini Makka kwa mwendo wa ngamia. Kila mwaka, maonesho

yalifanyika huko. Misafara ya kibiashara kuelekea Syria ilikuwa ikipitia Badr. Jeshi la wapagani liliwasili Badr mapema zaidi kuliko jeshi la Waislamu na kukishikilia kisima cha maji. Abu Jahl ambaye alijiamini mno nguvu ya jeshi lake alitaka vita.

#### **b) Hatua Kwa Hatua Kuelekea Vitani**

Mwaka 634, siku ya 17 ya mwezi wa Ramadhan, Ijumaa asubuhi, majeshi ya pande mbili yalikutana katika eneo la Badr. Vita hivi vilikuwa tofauti na vita vingine kwa pande zote mbili. Katika vita zote za huko nyuma, Waarabu walipigana dhidi ya makabila mengine kwa maslahi ya kabilalao. Lakini, katika vita hivi, watu wa jamii moja ya Kiarabu, yaani kabilia la Maqurayshi, walikuwa

wakipigana wao kwa wao kwa ajili ya imani zao. Baadhi yao walikuwa na ndugu, wajomba au wapwa kutoka upande wa adui. Hata watoto na wazazi walismama katika safu za pande hasimu na walikuwa tayari kukabiliana. (170/1)

Mus'ab ibn Umair alikuwa mshika bendera wa Waislamu, huku kaka yake Abu Aziz akiwa mshika bendera wa wapagani. Miongoni mwa watoto wa Utvabh ibn Rabia, Walid alikuwa upande wake, lakini mwanaye mwininge Hudhayfa alikuwa upande wa Waislamu. Mtoto wa Abu Bkar, Abdullah alikuwa upande wake, huku mwanaye mwininge aitwaye Abdurrahman akiwa katika safu za wapagani. Miongoni mwa ndugu wa Mtukufu Mtume (s.a.w), ami yake bwana Hamza alikuwa upande wake, lakini ami yake mwininge Abbas alikuwa upande wa maadui. Ali, mtoto wa Abu Talib ami wa Mtukufu Mtume (s.a.w) ambaye alimlea katika kipindi chote cha uhai wake, alikuwa upande wa Waislamu, huko mtoto mwininge wa Abu Talib aitwaye Aqil akiwa katika safu za wapagani.


Jeshi la adui lilionekana kuwa imara mara dufu kuliko jeshi la Waislamu kwa idadi, silaha, uzoefu na suhula za kifedha na kiuchumi. Sehemu waliyokaa pia ilikuwa nzuri zaidi kwa mapambano. Hata hivyo, muda mfupi kabla ya mapambazuko, mvua ilinyesha na kuifanya ardhi ya mchanga kuwa ngumu na kuwarahishtia Waislamu kutembea kwa urahisi. Aidha, mvua hii pia iliwapatia Waislamu fursa ya kukidhi mahitaji yao ya maji. Hivyo, Waislamu ambao wallondosha wasiwasi sasa wakawa na hali ya kuuamini kikamilifu msaada wa Allah. Katika vita hivi ambavyo kwa Waislamu vilikuwa vita vya kufa au kupona, Waislamu walikuwa wakimuomba Allah aupe Uislamu heshima na ukoo.

Ama Mtukufu Mtume (s.a.w), yeeye aliswali usiku wote na kumuomba Allah Mtukufu. Hivyo, Ali (r.a) anaelezea hali yake siku hiyo:

"Kila mmoja wetu alilala isipokuwa Mjumbe wa Allah. Aliswali chini ya mti na kulia mpaka asubuhi."

**Mtukufu Mtume (s.a.w) anaweza kuwa aliomba dua ya nini usiku ule?**





Wakati wa alfariji, Mjumbe wa Allah aliwaita Waislamu kwa ajili ya swala akisema: "Enyi waja wa Allah! Ni wakati wa swala". Aliswalisha swala ya alfajiri na kisha akawahamasisha kuhusu jihad.

### c) Vita Yaanza

Hatua kwa hatua, Maqrayshi walikuwa wakiwakaribia Waislamu. Yalikuwa mazingira yenye kuhamasisha sana. Waislamu wachache wakiwa na lengo la kulitkuza jina la Allah walikuwa wakikabiliana na jeshi kubwa la wapagani lilitokuwa limejipanga kikamilifu kama jeshi. Mjumbe wa Allah alimchukua Abu Bakr(r.a) na kwenda pemberi kwenye hema ambalo litiliwa limeandalila kwa ajili yake, akanyanya mikono kuelekea mbinguni na kuomba:

"Mola wangu! Hakika wapagani wa Makka wamekuja na majivuno na nguvu zao kuja kuifuta dini yako. Wanakupa changamoto na kumkana Mtume Wako. Mola wangu! Nijaalie msaada na ushindi ambao uliwaahidi manabii na mitume Wako. Kama Waislamu hawa wachache wataangamizwa leo, kuanzia leo hakuna yejote ardhini atakayekuabudu".

Mjumbe wa Allah aliomba kwa hamasa kubwa na kuinua mikono yake juu kabisa kiasi kwamba hakuhi kama joho lake lilianguka kutoka mgongoni kwake. Abu Bakr alilirudisha mgongoni mwake, akamshika mkono na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Hakika dua yako umezifanya mbingu kutetemeka. Allah atakupa ahadi Yake."

Waislamu waliposhuhudia hali hiyo ya Mtume (s.a.w) walikuwa wakilia kwa msisimko. Mwishoni Mtume (s.a.w) alisoma Ayah ifuatayo: "**Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma**" (al-Qamar 54: 45) kisha akatoka kwenye hema na kusema: "Allah ametoa habari njema ya msaada Wake na kunipa taarifa kuwa Waislamu watashinda". Wapagani ndio walioanzisha mapambano. Mshale uliorushwa na Amir ibn Hadrami ambaye kaka yake aliuawa katika tukio la Batn al-Nahl ulipiga Mihja ambaye alikuwa mtumwa aliyeachwa huru na Umar na kufa kishahidi.

Ilikuwa ni desturi kwamba mwanzoni mwa mapambano, mtu mmoja au wawili kutoka kila upande huja mbele, wakakabiliana na kuzichochea pande husika kwa kupigana. Utba ibn Rabia ambaye alikuwa mionganoni mwa viongozi wa Kiquraysh, kaka yake Shaiba na mwanaye Walid walijitokeza mbele na kutaka wapiganaji wa upande wa Waislamu wajitokeze kukabiliana nao. Kwa amri ya Mjumbe wa Allah, Ubaida, Hamza na Ali waliwakabili. Hamza alimuua Shaiba na Ali akamuua Walid katika pigo moja, baadaye wallienda kumuokoa Ubaida na kumuua Utba.

### d) Ushindi wa Waliomuamini na Kumtegemea Allah

Vita vilipamba moto na sasa wapagani walikuwa wakiwashambulia Waislamu. Waislamu

walikabiliana nao kwa ushujaa mkubwa. Kwa idhini ya Allah, walilishinda jeshi la wapagani. Wapagani walikimbia huku askari wao 70 wakiwa wameuawa na wengine 70 wakiwa wamechukuliwa mateka katika medani ya mapambano. Miiongoni mwa wapagani waliouawa ni viongozi na watu maarufu 24 wa Kiqrayshi ambaa walivanyanya na kuwatesa Waislamu mjini Makka. Abu Jahl, kamanda mkuu wa jeshi la wapagani, naye alikuwa miiongoni mwa waliouawa.

Kwa upande wa Waislamu, watu 14 walikuwa kishahidi. Kati yao, 6 walikuwa Muhajirina na 8 walikuwa Ansari ambaa walielekea Peponi wakisindikizwa na malaika.

Ushindi wa Badr uliibua shangwe na furaha kubwa mjini Madina. Ama mji wa Makka ulijawa na huzuni. Wiki moja baadaye, Abu Iahab alikuwa kwa huzuni na majonzi. Hata hivyo, Wapagani hawakuomboleza

ili kutowafurahisha zaidi Waislamu. Baada ya ushindi huo, Mjumbe wa Allah alikaa siku tatu zaidi katika eneo la Badr. Maswahaba waliokufa kishahidi walizikwa. Miili ya wapagani waliotelekezwa katika uwanja wa vita (Mapambano) walizikwa katika mashimo yao yalichimbwa. Wakati Mtukufu Mtume (s.a.w) akijiandaa kuondoka Badr, alisimama pembedi ya mashimo hayo. Aliwaita marehemu wote kwa majina yao na kusema:

"Ewe fulani mwana wa fulani! Hakika tumeushuhudia ushindi tulioahidiwa na Mola wetu. Je, nanyi mmeyaona mliyoahidiwa na Mola wenu baada ya kifo?" Umar (r.a) alipomuuliza Mtume (s.a.w):

"Ewe Mjumbe wa Allah! Unazungumza na miili iliyokufa na isiyokuwa na roho?"

Mtume (s.a.w) akajibu:

"Ninaapa kwa Allah kuwa wanasi kia ninachokisema kuliko nyinyi mnavyonisikia".

## MWENYE HURUMA HATA KWA MAADUI

Msingi wa udugu wa nyoyo za Waislamu ulijengwa na Mtume wetu (s.a.w) karne kumi na nne zilizopita. Akiwa kama kielelezo kamili kinachopendwa mno na Waislamu kiasi kwamba walikuwa tayari kuyatoa maisha yao kwa ajili yake, alikuwa na shakhsia ambayo hata adui zake walimstaajabia. Kwa mfano, siku moja kabla ya kuanza kwa vita vya Badr, watu 14 kutoka upande wa wapagani walimomba ruhusa ya kunywa maji kutoka katika kisima ambacho kilikuwa upande wa Waislamu. Baadhi ya maswahaba hawakutaka kuwapa maji wapagani ambaa wangepambana nao muda mfupi ujao. Lakini, Mtume (s.a.w) alionesha huruma hata kwa maadui

zake ambaa walikuja kupambana nao, akawapa maji.





#### e) Wapagani Waliochukuliwa Mateka katika Vita vya Badr

Wakati akirejea kutoka Badr, Mtume (s.a.w) aligawa kwa usawa ngawira za vitu thamani kama vile dhahabu na fedha vilivyoachwa na jeshi la wapagani. Wale maswahaba 8 waliondoka kwa sababu ya nyudhuru mbalimbali, nao aliwahifadhi mgao wao. Mjumbe wa Allah alipofika mjini Madina, alishauriana na maswahaba juu ya mateka. Wale wallolipa fidia waliachiwa huru mara moja. Wale ambao hawakuweza kulipa fidia lakini wakawa wanajua kusoma na kuandika, waliachiwa huru kwa sharti la kila mmoja kuwafundisha watoto 10 wa Madina kusoma na kuandika. Wale ambao hawakujuu kusoma wala kuandika na wakawa hawana uwezo wa kulipa fidia ya kikomboleo nao pia waliachiwa huru. Tukio hili linaonesha ni kwa kiasi gani dini yetu inaweka umuhimu kwenye

elimu na ujuzi. Kwa upande mwagine, hili linaonesha namna mwanadamu alivyo na thamani katika Uislamu, dini ya rehma, hata kama mtu husika ni mateka.

Kuhusu suala hilo, tukio lifuatato linatupatia mwanga mzuri. Ndugu wa Mus'ab ibn Umar aitwaye Abu Aziz anasimulia:

"Katika vita vya Badr, nilichukuliwa mateka na kukabidhiwa kwa kundi moja la Ansar. Mjumbe wa Allah aliwaambia Ansar:

'Watendeeni wema mateka!'

Ili kutekeleza amri hiyo, kundi hilo la Ansar lilinipatia mkate ambao ulikuwa kwenye mgao wao asubuhi na jioni huku wao wakila tende tu. Nilishtushwa na tukio hili nikaurudisha mkate ule kwa mmoja wao. Lakini hakuugusa, alinirudishia".

(Haithami, VI, 86; Ibn Hisham, II, 288)

**Tunatakiwa kuwa na maadili gani ya kijamii katika kukabiliana na maadui wanaokuja kupambana nasi lakini wakachukuliwa mateka?**

## MASWALI

KIASI GANI NILICHOJIFUNZA?

1. Mwaka ambao Khadija na Abu Talib walifariki dunia uliitwaje”?

.....  
.....

2. Watu wa Taif walimpokea vipi Mtume (s.a.w) na ulinganio wake?

.....  
.....

3. Mbinu zippi zilizotumiwa na wapagani wa Makka juhud za Mtume (s.a.w) kuwalingania watu kwenye Uislamu?

.....  
.....

4. Katika mkutano wa Aqaba ya Kwanza, Waislamu wa Madina walikula kiapo cha utii kwa Mtume (s.a.w) kwa kuahidi kuwa watafanya nini?

.....  
.....

5. Surah ipi ndani ya Qur'an Tukufu inayotaja muujiza wa Isra na Miraj?

.....  
.....

6. Umar alioneshwa msimamo gani wakati wa hijra? Kwa nini?

.....  
.....

7. Allah alimuokoa vipi Mtume (s.a.w) na Abu Bakr (r.a) ambao walikuwa wamejificha katika pango la Thawr dhidi ya wapagani wa Makka?

.....  
.....

8. Ilikuwaje hamasa ya watu waliompokea Mtume (s.a.w) mjini Madina?

---

---

9. As'ab al-Suffa ni watu gani?

---

---

10. Wapagani waliochukuliwa mateka katika vita vya Badr walifanywa nini? Ni ipi sababu ya kufanyiwa hivyo?

---

---



NI LIPI JIBU SAHIHI?

- 1) **Mwaka ambao Khadija na Abu Talib walifariki dunia uliitwaje?**
  - a) Mwaka wa huzuni
  - b) Mwaka wa uchungu
  - c) Mwaka wa adha
  - d) Mwaka wa hofu
- 2) **Kabila lipi lililokuwa likiishi Taif?**
  - a) Banu Tamim
  - b) Banu Umayyah
  - c) Saqif
  - d) Khazraj
- 3) **Ni swahaba gani aliyeshirikiana na Mjumbe wa Allah katika safari ya Taif?**
  - a) Abu Bakr
  - b) Zayd
  - c) Umar
  - d) Muadh
- 4) **Wapagani ambao walilenga kuzuia harakati za ulinganiaji wa Mtume (s.a.w) waliamua kumtangaza vipi kwa watu?**
  - a) Mshairi
  - b) Mpiga ramli
  - c) Muongo
  - d) Mchawi
- 5) **Katika Mkutano wa Aqaba ya Kwanza kulikuwa na watu wangapi kutoka Madina?**
  - a) 14
  - b) 15
  - c) 12
  - d) 16
- 6) **Ni jambo lipi kati ya mambo yafuatayo ambalo halikuwa mionganini mwa masharti ambayo Waislamu walikula kiafapo cha utii?**
  - a) Kutomshirikisha Allah
  - b) Kutofanya zinaa na unyang'anyi
  - c) Kutosema uongo
  - d) Kutowazika mabinti wadogo wakiwa hai
- 7) **Baada ya Aqaba ya Kwanza, ni swahaba yupi aliyeagizwa na Mtume (s.a.w) kwenenda kuwa mwalimu wa watu wa Madina?**
  - a) Ali
  - b) Mus'ab
  - c) Ja'far
  - d) Anas
- 8) **Uliitwaje mwaka wa baada ya Aqaba ya Kwanza ambapo idadi kubwa ya watu waliingia katika Uislamu?**
  - a) Mwaka wa amani
  - b) Mwaka wa Furaha
  - c) Mwaka wa Upendo
  - d) Mwaka wa Ushindi

- 9) Baada ya watu wa Madina kumualika Mjumbe wa Allah kwenda mjini Madina, ni mambo gani maalum ambayo Abbas alitaka watu hao wayafanye wakati wa Aqaba ya Pili?**
- Kuutekeleza vizuri Uislamu
  - Kumpenda Mtume (s.a.w) kuliko nafsi zao
  - Kutilia umuhimu kwenye swala
  - Kumlinda Mtume (s.a.w) kwa hali yoyote
- 10) Katika muujiza wa Isra, Mtume (s.a.w) alisafiri kwa muda mfupi sana kutoka wapi mpaka wapi?**
- Kutoka Masjid al-Haram mpaka Masjid al-Nabi
  - Kutoka Masjid al-Aqsa mpaka Masjid al-Haram
  - Kutoka Masjid al-Quba mpaka Masjid al-Aqsa
  - Kutoka Masjid al-Haram mpaka Masjid al-Aqsa
- 11) Ni jambo gani kati ya mambo yafuatayo ambalo halikuwa mionganoni mwa mambo ambayo Allah alimfunulia moja kwa moja Mtume (s.a.w) wakati wa safari ya Miraj?**
- Faradhi ya swala tano za kila siku
  - Ayah mbili za mwisho wa Surah al-Baqara (Aman al-Rasul)
  - Kufunga wakati wa mwezi wa Ramadhan
  - Habari njema kwa wale wasiomshirikisha Allah na chochote kwamba wataingia Peponi.
- 12) Ni swahaba yupi aliyelala kwenye kitanda cha Mtume (s.a.w) wakati wa hijra ya Mtukufu Mtume (s.a.w)?**
- Ali
  - Umar
  - Abdallah ibn Mas'ud
  - Talha
- 13) Swala ya kwanza ya Ijumaa iliswaliwa wapi?**
- Bonde la Ranuna
  - Masjid al-Qubai
  - Masjid al-Nabi
  - Masjid al-Haram
- 14) Katika makabila yafuatayo ni kabilia lipi ambalo halikuwa mionganoni mwa makabila ya Wayahudi waliokuwa wakiishi Madina pindi Mjumbe wa Allah alipowasili huko?**
- Banu Qaynuqa
  - Banu Quraidha
  - Banu Nadir
  - Banu Tamim
- 15) Sababu ipi iliyosababisha mapendelekezo ya mifumo ya kuwaita watu kwenye swala kama vile kupiga kengele, ngoma na kuwashaa moto yakataliwe?**
- Kwa sababu haikutosha.
  - Kwa sababu haikuwa mizuri kwa masikio na macho.
  - Kwa sababu ya kuhofia kufanana na wasiokuwa Waislamu.
  - Kwa sababu haikuwa ikititosheleza.

- 16) Ni uwiano upi sahihi wa idadi ya askari wa Kiislamu na Wapagani waliopigana katika vita vya Badr?
- a) 313 / 2000
  - b) 300 / 1000
  - c) 1000 / 2000
  - d) 313 / 1000
- 17) Waislamu wangapi waliokufa kishahidi katika vita vya Badr?
- a) 16
  - b) 14
  - c) 15
  - d) 21



**Tabia Zinazomfanya Mtu Kuwa Muislamu Mzuri:**



# ADABU



- ✿ *Adabu Za Kusalmiana*
- ✿ *Adabu Za Kulala Na Kupumzika*
- ✿ *Adabu Za Kula Na Kunywa*
- ✿ *Adabu Za Kupiga Mwayo, Kupiga Chafya, Kukohoa Na Kubera*





# ADABU ZA KUSALIMIANA

**Muislamu anapokutana na ndugu yake  
Muislamu hujawa na furaha.**

Waislamu wanapendana sana. Wanapokutana, kwa sababu ya shauku ya kuwaona wale wanaopendana sana, hujawa na furaha na kusalimiana huku nyusu zao zikiwa na tabasamu. Upendo, furaha na amani hii ambayo waumini huihisi katika nyoyo zao pindi wanapokutana ni kielelezo cha sifa ya Allah ya "salaam" (amani).

Kwa sababu hii, Waislamu wanapokutana husalimiana kwa kusema "Assalamu 'alaykum" au "Salamun 'alaykum" (amani iwe juu yako). Wale wanaosalimiwa hujibu kwa kusema "Wa 'alaykum salam" au "'alaykum salam" (nawe pia amani iwe juu yako). Maana mojawapo ya jina la Allah la "salaam" (amani) ni "anayewalinda

waja Wake dhidi ya aina zote za shari, matatizo na masaibu na kuwapa amani." Kwa muktadha huu, kutoa na kupokea salamu kuna maana nzuri sana ya "ewe ndugu yangu, mimi ni Muislamu. Hutapata madhara yoyote kutoka kwangu, uko katika amani na salama" na "sifa ya Mola wetu ya Salaam imetuzunguka sote, hivyo ishi kwa amani na usalama."

Katika Qur'an Tukufu, Allah anatueleza umuhimu wa kupeana salamu:

**"Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo ..."** ((Nisa, 4:86).

Katika Ayah hiyo tunapata kutambua kuwa kujibu salamu ya mtu aliyetusalimia ni faradhi kutoka kwa Allah. Ama kutoa salamu ni sunnah muhimu sana ya Mtume wetu (s.a.w).



# MAMBO GANI TUNAYOTAKIWA KUZ- INGATIA WAKATI WA KUTOA SALAMU?



- ✓ Mtu anaposema “As-Salamu ‘alaykum” tunaweza kusema “Wa ‘alaykum as-salam wa rahmatullah” kwa kuijibu kwa namna nzuri na yenyekutia.
- ✓ Mtu anayesema “As-salamu ‘alaykum wa rahmatullah” (amani na rehma za Allah ziwe juu yako), tunaweza kuitikia vizuri salamu yake kwa kusema: “Wa ‘alaykumu s-salamu wa rahmatul-lahi wa barakatuhu” (amani, rehma na baraka za Allah ziwe juu yako).




Allah Mtukufu anasema:

“Na mnapo amkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo...”

(Nisa, 4: 86)

Tunapata thawabu za ziada kila tunapoitika vizuri zaidi.

- ✓ Mtume wetu (s.a.w) alikuwa na kawaida ya kuanza kutoa salamu. Hivyo, nasi tunatakiwa tujitahidi kuwa wa mwanzo kutoa salamu tunapokutana na mtu.
- ✓ Tunapokutana na mtu tunayefahamiana naye au rafiki, tunapeana mikono baada ya kutoleana salamu.
- ✓ Sio lazima tumsalimie mtu tunayemjua tu, bali tunaweza kuwasilimia hata wale tusiowajua.
- ✓ Tunapoingia kwenye mkusanyiko wa watu tunatakiwa kutoa salamu, na tunapoondoka pia tunatakiwa kutoa salamu.



- ✓ Mtu anapotusalimia tunamjibu hapo hapo kwa sauti inayosikika, isiwe laini sana au ya juu sana
- ✓ Katika kutoa au kujibu salamu, tunatakiwa tuisumie sauti ambayo sio ya upole na ya ukali au nyororo sana.
- ✓ Tunapoingia katika eneo ambalo kuna watu wachache au wengi, salamu ya mmoja wetu itatosha. Kama yeote kati ya watu wale akiitikia, inatosha pia.
- ✓ Katika kupeana salamu, mdogo anatakiwa kuwasalimia wakubwa; vilevile mtu mmoja anatakiwa kuwasalimia wengi, anayetembea awasalimie waliokaa, na aliye kwenye chombo cha usafiri amsalimie anayetembea kwa miguu.

## RAHA YA KUTOLEANA SALAMU

Abdullah ibn Umar (r.a), alikuwa akienda sokono pamoja na Tufayl ibn Ubay.

Siku moja, Abdullah alipokuwa anaelekea sokoni pamoja na rafiki yake Tufayl, alimuona mtu mmoja akiiza vitu vikuukuu na kumtolea salamu. Baadaye alimuona mfanyabiashara akiiza vitu vya thamani akamtolea salamu. Kisha walimuona mtu masikini na fukara, naye akamtolea salamu. Kadhalika walikutana na mtu tajiri, Abdullah akamtolea salamu. Aliwatolea salamu watu wengi, marafiki na hata asiowajua.

Siku iliyofuata Tufayl alikuja tena kwa rafiki yake Abdullah ibn Umar. Abdullah akasema:

"Ewe Tufayl, twende zetu sokoni".

"Unaenda kufanya nini sokoni? Hununui cho-

chote. Unapita kwenye maduka mengi lakini huulizi hata bei ya bidhaa zao."

"Twende tena ndugu yangu".

"Lakini kama huendi kununua chochote kwa nini unataka kwenda sokoni? Hukai na kuzungumza na watu. Tukae zetu hapa tuzungumze".

"Ewe Abu Batin (baba kitumbo)"

Tufayl alikuwa mnene kidogo. Abdullah alipokuwa akimkasirikia rafiki yake au anapotaka kumchokoza, alimuuta Abu Batin.

"Ewe Tufayl, sababu kubwa ya kwenda sokoni ni kuwasalimia watu. Tunawasalimia watu



tunaokutana nao (Malik, Muwatta, salaam 6), kwa sababu Mtume wetu (s.a.w) anasema:

**"Hakika hamtaingia Peponi mpaka muamini; na hakika hamtakuwa waumini wa kweli mpaka mpendane. Je, niwaelezeni kitu ambacho mkikifanya mtapendana? Enezeni salamu kati yenu."** (Muslim, Iman, 93)

## **JE, NAWE UNGEPENDA KUPATA FURAHA NA RAHA KAMA HIYO?**

**Ni katika hali na mazingira gani ambayo hatutoi au kujibu salamu?**

- ✓ Chooni au bafuni hatutoi wala kujibu salamu.
- ✓ Hatutoi salamu kwa mtu anayem-sababishia mtu kufanya dhambi au anayefanya dhambi. Wakitoa salamu, hatujibu.
- ✓ Hatumtolei salamu mtu anayeswali au anayesoma Qur'an.
- ✓ Hatumtolei salamu mtu anayesoma Hadith za Mtume (s.a.w), anayetoa mawaidha au anayetoa adhana.

Mtume wetu (s.a.w) anasema:

**"Hakika hamtaingia Peponi mpaka muamini; na hakika hamtakuwa waumini wa kweli mpaka mpendane. Je, niwaelezeni kitu ambacho mkikifanya mtapendana? Enezeni salamu kati yenu."**

(Muslim, Iman, 93)



# ADABU ZA KULALA NA KUPUMZIKA

## Pindi ninapolala...

Allah Mtukufu aliufanya mchana kuwa muda wa kufanya kazi na kutafuta riziki; na akaufanya usiku kwa ajili ya kupumzika na kulala. Viumbe vyote vilipewa hitajio la kupumzika na kulala. Tunaposwali au kufanya kazi, tunatakiwa kuwa na utulivu, amani na imara. Aidha, tunahitaji pumziko sahihi, yaani usingizi, ili tuwe wenyewe afya.

## Mambo gani tunayotakiwa kuyazingatia wakati wa kulala na kuamka?

- ✿ Tunatakiwa kulala mapema, tukiwa na wudhu, baada ya swala ya al-ishaa.
- ✿ Tunatakiwa kupigwa mswaki kabla ya kulala.
- ✿ Tunatakiwa kulala katika mavazi safi.
- ✿ Tunatakiwa kusoma Ayat al-Kursi, Surat al-Ikhlas, Surat al-Falaq na Surat an-Nas kitandani kabla ya kulala.
- ✿ Ikiwezekana tunatakiwa kulala nyuso zetu zikiwa zimeelekeea qiblah na mikono yetu ya kulia tuiweke chini ya mashavu yetu.
- ✿ Ili kutoubana moyo, ambao uko upande wa kushoto wa miili yetu, na tumbo, tunatakiwa kulalia upande wa kulia.
- ✿ Kwa kuwa Mtume (s.a.w) alikataza, hatutakiwi kulala nyuso zetu zikiwa zimeelekeea chini, kulalia mgongo au miguu yetu ikiwa imepishana.
- ✿ Hatutakiwi kulala kidogo sana wala kulala kupita kiasi. (saa 6-8)

Hatutakiwi kulala jua linapochomoza au linapozama. (dakika 45)

Mtume wetu (s.a.w) alimwambia mmoja wa maswahaba wake:

— “Ukisoma hii dua ukafariki usiku uliosoma, utakufa katika iman. Maneno haya yawe maneno ya mwisho unayosoma kabla ya kufa.

اللَّهُمَّ أَسْلَمْتُ نَفْسِي إِلَيْكَ وَفَوَّضْتُ إِمْرَىءِ  
إِلَيْكَ وَوَجْهَتُ وَجْهِي إِلَيْكَ. وَالْجَاهَاتُ  
ظَهَرَى إِلَيْكَ رَغْبَةً وَرَهْبَةً إِلَيْكَ لَا مَلْجَأَ وَلَا  
مَنْجَأٌ مِنْكَ إِلَّا إِلَيْكَ. أَمْتُ بِكَتَابِكَ الَّذِي  
أَنْزَلْتَ وَنَبَّيْكَ الَّذِي أَرْسَلْتَ

“Ewe Allah! Ninajisalimisha kwa-ko. Ninaacha mambo yangu mikononi Mwako na ninauelekeza uso wangu Kwako. Ninakutegemea na kukimbilia kwako, nina kutarajia na kukuhofu. Hakuna kimbilio na wokovu dhidi yako isipokuwa kupitia kwako. Ninakiamini kitabu chako ulichokiteremsha na Mtume Wako uliyemtuma”,(Al Boukharai, Da'awat, 7)

**Tumuombe Allah ajaalie dua hizi za Mtume wetu (s.a.w), zinazoonesha upendo na ukaribu wake kwa Mola wake, ziwe ndio maneno yetu ya mwisho kila usiku!**

Hatutakiwa kulala tukiwa na nia ya kuamka kwa ajili ya salat al-fajr au salat al-ishaa ili tusikose swala zetu.

- ✿ Kabla ya kulala tunatakiwa kusoma dua tulizofundishwa na Mtume wetu (s.a.w): **اللَّهُمَّ بِاسْمِكَ أَمُوتُ وَأَحْيَا**  
“Ewe Allah ninakufa (ninalala) na kuishi (kuamka) kwa jina Lako”.
- ✿ Baada ya kuamka, tunatakiwa kumhimidi Mola wetu na kuamka kwa upande wetu wa kulia. Kisha tunasoma dua hii: **الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وَاللَّهُ شَرِيكٌ لَّا يَشْرِيكُ بِهِ شَرِيكٌ** “Himidi zote ni za Allah aliyetuhuisha baada ya kutufisha. Kwake ndio kuna Ufufuo.” (Bukhari, Da'wat, 8)

### Shairi kwa ajili ya watoto kabla ya kulala.

Nimelala kwa upande wangu wa kulia  
 Nikageukia upande wangu wa kushoto  
 Malaika wameshuhudia  
 Dini yangu na imani yangu.  
 Allah hunifanya nilale  
 Allah huniamsha  
 Nisipoamka  
 Ninashuhudia kuwa hakuna apasae  
 kuabudiwa ila Allah  
 Na ninashuhudia kuwa  
 Muhammad ni Mjumbe wa Allah.



# ADABU ZA KULA NA KUNYWA

## Kula ni ibada!

Allah anasema: "Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa mnayo yatenda." . ." (Qur'an, Mu'minun, 23:51.)

Mola wetu alituleta hapa duniani ili tuwe waja Wake bora na tupate kuingia Peponi. Vitu ambavyo tunavihitaji ili kutekeleza ibada zetu kwa namna nzuri, mahitaji yetu kama vile kula, kunywa na makazi, navyo pia vimefanywa kuwa halal kwa ajili yetu. Ametujaalia baraka mbalimbali za mbogamboga, matunda, nyama na maziwa. Tunapokula au kunywa neema hizi, tunatakiwa kufanya hivyo kwa nia ya kuwa waja bora wa Mola wetu, Muumba wa ulimwengu, kwa maana kula na kunywa ni sehemu ya ibada. Kwa mfano, mwanafunzi akila kitu kwa nia ya kujifunza zaidi, atalipwa thawabu na Allah kwa kujifunza huko. Kijana akiamka na kuswali salat al-fajr kwa nia ya dhati ya kufanya ibada zote za siku hiyo kwa ajili ya Mola wake,

anapokula chakula cha usiku, atalipwa thawabu kwa aina hiyo ya ibada.

## Ni mambo gani ya kuzingatia kabla ya kula?

- ✿ Tunatakiwa kula tunapokuwa na njaa.
- ✿ Tunatakiwa kusaidia kuandaa meza ya chakula.
- ✿ Kama kuna watu wakubwa na wageni, tunatakiwa kuwasubiri kabla ya kuanza kula.
- ✿ Tunatakiwa kuosha mikono yetu kabla ya kula.
- ✿ Tunatakiwa kutumia kitambaa maalumu ili chakula au mchuzi usitudondokee.
- ✿ Tukila tukiwa tumekaa sakafuni, tunatakiwa kukaa juu ya mguu wetu wa kushoto, huku goti la kulia likiwa limeinuliwa. Hatutakiwi kuegemea chochote.





- ✿ Tukila mezani, hatutakiwi kuegemea sana nyuma, wala kuisogelea sana meza.
- ✿ Tunapoanza kula, tunasema "**Bismillahi r-Rahmani r-Rahim**" ("kwa jina la Allah Mwingi wa rehma, Mwenye kurehemu"). Tukisahau kusema bismillah mwanzo, tunapokumbuka tu tunatakiwa kusema "**Bismillahi awwalahu wa akhirahu**" (Kwa jina la Allah, mwanzo na mwisho").

#### Mambo gani ya kuzingatia wakati wa kula?

- ✿ Tunatakiwa kuunga chumvi chakula chetu mwanzoni na mwishoni. Hii ni sunnah nzuri ya Mtume wetu (s.a.w).
- ✿ Tunatakiwa kula kile kilicho mbele yetu na kwa kutumia mkono wa kulia.
- ✿ Tunatakiwa kutafuna vizuri chakula tu nachokiingiza mdomoni mwetu kabla ya kukimeza, na tunatakiwa kukithamini kabla ya kukimeza.
- ✿ Tunatakiwa kufunga vinywa yetu wakati wa kula ili tusimkere yeyote.

Siku moja Mtume wetu (s.a.w) alikuwa akila pamoja na Maswahaba, akasema:

"Watu hawajajaza chombo kibaya kama tumbo. Inatosha kwa mtu kula chakula kinachotosha kukaza kiuno, yaani chakula kinachotosha kumpa nguvu kwa siku hiyo. Mnapokula bakisheni theluthi ya tumbo kwa ajili ya chakula, theluthi kwa ajili ya kinywaji, na theluthi kwa ajili ya kupumua." (Tirmidhi, Zuhd 47; Ibni Majah, At'ima 50)

Swahaba mmoja, alisahau kusema bismillah na kuanza kula. Likiwa limebaki tonge la mwisho alikumbuka kuwa alisahau kusema bismillah na hivyo akasema "Bismillah awwalahu wa akhirahu." Kwa sababu hiyo Mjumbe wa Allah akatabasamu na kusema:

"Shetani aliendelea kula pamoja naye tangu mwanzo. Ndugu yenu huu alipolitaja jina la Allah, Shetani alitapika chakula chote alichokula." (Abu Dawud, At'ima 16)

Kisha, ili kuhamasisha baraka za chakula, alisema:

"Chakula cha watu wawili kinawatosha watu wanne, na chakula cha watu wanne kinawatosha watu wanane". (Muslim, Ashriba 179; Tirmidhi, At'ima 21)

**Kila neno ambalo Mtume (s.a.w) aliwaambia Maswahaba linatuhusu nasi pia.**

**Nasi pia ni katika Ummah wake!**

**Hatutakiwi kulalamika kuhusu chakula chochote kwa sababu Mjumbe wa Allah alikuwa halalamiki kuhusu chakula asichokupenda. Akikipenda alikuwa akila, kama hajakipenda anakiacha.**

✿ Tunatakiwa kula kilicho mbele yetu, lakin i wakati wa kula matunda, tunawenza kula kokote tunakopenda.

#### **Usifanye haya wakati wa kula na kunywa!**

✿ Usile au kunywa chochote ambacho ni haramu.

✿ Usile au kunywa ukiwa umesimama.

✿ Usinywe maji kwa mkupuo. Pumua mara tatu na unywe katika hali ya utulivu. Usipumulie kwenye chombo.

✿ Unapopiga chafya, kukohoau kupaiga mbweu, usiweke chakula mdomoni mwako; funga mdomo wako. Vinginevyo utakuwa katika hatari au utawakera wengine.

✿ Usiache maji na chakula katika chombo cha wazi. Vinginevyo wadudi warukao na kutambaa wataingia.

✿ Usile au kunywa kwenye sahani au vikombe vyenye mpasuko kwenye ncha zake kwa sabbu vinaweza kujeruhii kinywa chako au ulimi wako.

✿ Wakati wa kula, usiongee maneno yasiyokuwa na maana, kucheka kwa sauti au kupiga makelele na kufanya fujo.

✿ Usizungumze ukiwa na chakula mdomoni, kimeze kwanza.

✿ Usipanguse mikono na kinywa chako kwa mkate, kisha ukaula mkate huo.

✿ Usitupe kipande cha chakula kili-chodondoka kwa kusema kuwa ni kichafu. Badala yake, kisafishe na ukile.

✿ Usipulize chakula cha moto; na usinywe maji ya baridi sana kabla hayajapoa.

✿ Usiache chakula nusu kwenye sahani, na usimwage mchuzi.

#### **Fanya haya baada ya chakula!**

✿ Unapomaliza kula sema: "Alhamdulillah! Ewe Allah ninakushukuru". Kwa namna hiyo tunamshukuru Allah na kusoma dua yetu ya chakula.

✿ Baada ya kula, osha mikono yako.

✿ Tunakusanyika pamoja na kula pamoja. Baada ya chakula, tunasi-mama kwa pamoja.

✿ Tunatakiwa kusaidia kuondoshaa vyombo mezani.

✿ Tunatakiwa kuwashukuru wale walituandalia chakula na meza.



## KUMBUKUMBU YA LADHA YA TENDE

Jina langu ni Rafu bin Amr. Ngoja nikusimulie tukio lililoniathiri sana tangu nilipokuwa na Mjumbe wa Allah nikiwa mtoto.

Nilikuwa na umri wa miaka sita au saba. Nikiwa ninacheza mtaani sikuwa nikihisi namna muda unavyokimbia. Ilikuwa siku moja ambapo nilishikwa na njaa. Kama kawaida, nilikuwa mvivu wa kwenda nyumbani. Niliingia kwenye shamba la mitende lililokuwa jirani kwa ajili ya kuchukua tende kadhaa. Niliingia atika shamba hilo na kuanza kurusha mawe juu ya mti. Nilichukua kila nilichowenza kukiona chini, mawe, uchafu na vijiti, na kujaribu kuangusha baadhi ya tende kwa kurusha mawe. Baada ya muda nilikuwa nimepata takribani tende kumi za kula, mbivu na mbichi, ambazo ziliikuwa zimedondoka kutoka mtini. Nilipokuwa nimekula zile mbivu na kuijaza tumbo yangu, mmiliki wa shamba aliniona. Alinikamata na kunipeleka moja kwa moja kwa Mjumbe wa Allah. Bwana huyo akasema;

"Ewe mjumbe wa Allah! Kijana huyu amekuwa akirusha mawe kwenye shamba langu na kuangusha tende zangu. Huyu kijana ana haribu miti yangu ya tende. Nimekuwa nikisubiri kwa muda mrefu na leo nimemkamata."

Baada ya kusema hayo, alinikabidhi kwa Mjumbe wa Allah. Alitaka niadhibiwe. Nilikuwa mdogo na sikuwa na uelewa mkubwa wa kujua kilichokuwa kikitokea, lakini niliogopa sana. Mjumbe wa Allah alitabasamu, akazipapasa nywele zangu na kusema:

"Mtoto mzuri! Kwa nini unarusha mawe kwenye mitende?" Nikajibu kwa upole:

"Bwana wangu! Wakati nikicheza nilishikwa na njaa na hivyo nikataka kula chochote". Mjumbe wa Allah akatabasamu kwa jibu langu, ambalo ilikuwa limetolewa na mtoto na kuni shika begani kisha akasema:

"Mwanangu! Wakati mwagine utakapokuwa na njaa, chukua tende zilizodondoka. Ni laini na ni tamu zaidi. Kwa kufanya hivyo huto haribu miti au tende". Kisha akaniambea dua:

"Ewe Allah! Lishibishe tumbo la kijana huyu kwa chakula cha halali".

Mpaka sasa sijasahau tabasamu, mguso na wosia wa Mjumbe wa Allah uliojaa maneno mazuri ambao alinipatia nilipokuwa na hofu ya kile ambacho kingenitokea. Kuanzia siku hiyo, sikuwahi kuharibu mali ya mtu. Sikuthubutu tena kuchukua vitu vya watu bila ruhusa yao. Daima nimekuwa mwangalifu kuhakikisha kuwa ninachokula na kunywa ni cha halali. Dakika zile nzuri nilizokuwa mbele ya Mtume (s.a.w) ziliubadili mtazamo na mwelekeo wa maisha yangu. Baadaye katika maisha yangu, nilikuja kutambua vyema umuhimu wa halali na haramu kwa mja wa Allah. Kamwe sikuthubutu kuunysha mkono wangu kutumia kitu chochote cha haramu." (Kisa kimesimuliwa kutoka hadith ya Ibn-i Maja, Tijarat, 67.)



## ADABU ZA KUPIGA MWAYO, KUPIGA CHAFYA, KUKOHOA NA KUBEUA

### Muislamu ni mtu mzuri kama maua.

Sote hupiga miayo, chafya, kukohoa na kubeua kwa sababu haya ni matendo yato-kanayo na asili ya maumbile ya mwanadamu. Hata hivyo, tunapofanya hivyo, hatutakiwi kuwakera au kuwaudhi wale walio mbele yetu. Fikiria unamweleza kwa hamasa kubwa rafiki yako kuhusu fikra na mawazo yako kisha akaanza kupiga mwayo. Fikiria mtu amekuja karibu yako na kuanza kukohoa au kupiga chafya usoni

mwako. Utajisikiaje? Au mtu aliyekula vitunguu saumu na vitunguu maji akapiga makelele sikioni mwako, utafikiriaje? Bila shaka hivi ni vitu vyatukera ambavyo hatupaswi kuvifanya, au sio? Bila shaka!

Daima Muislamu ni mtu mwema, mtarabitu na mwenye kuwajali wengine. Muislamu hamuudhi yeyote kwa matendo yake au hali inayomkuta, na hamkeri yeyote. Huwapa wale walio mbele yake furaha na uzuri.



## MARA TATU

Siku moja wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w) akiwa anaongea na Maswahaba, mmoja wao alipiga chafya taratibu. Hapo Mtume (s.a.w) akasema: "Yarhamukallah". Muda mfupi baadaye, swahaba mwingine akapiga chafya, lakini Mjumbe wa Allah hakusema chohote.

Yule ambaye Mtume (s.a.w) hakumwambia "yarhamukallah" kwa kiasi fulani akajisikia vibaya na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Mtu mmoja alipiga chafya ukasema "yarhamukallah". Nami pia nilipiga chafya lakini hukuniombea dua hiyo. Mtume (s.a.w) akasema:

"Yule alipopiga chafya alisema 'alhamdulillah' lakini wewe hukusema." (Bukhari, Adab, 127)

Kisha akasema:

"Unapopiga chafya sema 'Alhamdulillah' (Himidi zote ni za Allah). Kisha ndugu yako au rafiki yako atajibu kwa kusema 'yarhamukallah' (Allah akupe rehma Zake). Kisha yule aliyepiga chafya atasema, 'Yahdikumullah wa yuslihu balakum' (Allah akuongoze na kurekebisha hali yako)." (Bukhari, Adab, 126) akaendelea kusema:

"Iwapo mtu anapiga chafya zaidi ya mara tatu, basi inatosha kwa nduguye kusema 'yarhamukallah' mara tatu kwa sababu hiyo inaonesha kuwa ana mafua". (Abu Dawud, Adab, 92)

### Ni mambo gani ya kuzingatia wakati wa kupiga mwayo au kukohoaa?

- ✿ Ikiwezekana, tunatakiwa tujidhibiti pin-di mwayo unapotokana na usingizi, mghala au matendo kama hayo.
- ✿ Inapobidi kupiga mwayo, tunatakiwa kufunika vinywa vyetu kwa mkono na kujaribu kufupisha muda wa mwayo husika.
- ✿ Tunatakiwa kuwa waangalifu tusitoe sauti kubwa wakati wa kupiga mwayo.
- ✿ Mara nyngi ukohoaji unasababisha vijidudu vinavyopatikana katika mfumo wa upumuaji na bakteria wanaopatikana mdomoni kurushwa hewani. Ili kulizuia hili tunapaswa kufunika vinywa vyetu kwa kitambaa, au kama hatuna kitambaa, basi tutumie mikono yetu.
- ✿ Ili kuzuia mate wakati wa ukohoaji, na kuepuka kutoa sauti ya makelele, tunatakiwa kufunga vinywa vyetu.
- ✿ Wakati wa kukohoaa, tunatakiwa kugeukia upande wa kushoto au chini. Iwapo wakati huo tuna mazungumzo au tunamsikiliza mtu yeyote, basi tunatakiwa kuomba radhi kwa kusema "kumradhi".

### Ni mambo gani ya kuzingatia wakati wa kupiga chafya na kubeua?

- ✿ Kupiga chanya ni utoaji wa hewa nzito kutoka ndani kwa haraka. Ni kitu kizuri kwa afya ya mili yetu, hivyo kila tunapopiga chafya tunasema, "**Al-Hamdu lillah**" (Himidi zote ni za Allah)

Baada ya kupiga chafya na kusema 'Alhamdulillah', kama mtu atajibu kwa kusema 'Yarhamukallah', unatakiwa

kumjibu kwa kusema “**Yarhamukal-lah**” (“Allah atuongoze sisi na wewe pia”).

- ✿ Japokuwa unaweza kusema maneno mengine badala ya hayo, lakini maneno mazuri kabisa ni yale tuliofundishwa na Mtume (s.a.w).
- ✿ Mara nyingi tunaposhindwa kujizua tusibeue, hutokana na sababu mbalimbali kama vile kula kupita kiasi, kula kwa haraka haraka, kunywa soda, na kula vitunguu maji na vitunguu saumu ambavyo hutengeneza gesi. Tunatakiwa kuchukua hatua dhidi ya jambo hilo.
- ✿ Tunapokula, tunatakiwa kutafuna kila kipande vizuri na kumeza taratibu ili hewa isipate kuingia tumboni mwetu na kusababisha tubeue.

✿ Tunatakiwa tujizuie kula kwa ulafi, tujizue kula sana kupita kiasi.

- ✿ Tunapoelekea msikitini au kwenye mkutano, tunatakiwa kuепuka vyakula kama vile vitunguu maji na vitunguu saumu ambavyo husababisha gesi, kubeua na kutoa harufu isiyopendeza.
- ✿ Tukishindwa kujizuia kubeua, licha ya kujitahidi, basi tufanye hivyo kimya kimya na kufunika vinywa vyetu kwa mikono yetu.
- ✿ Ikiwezekana, tuende sehemu bila kuwa na mtu anayebeua.
- ✿ Daima tunatakiwa kukumbuka kauli ya Mtume wetu kipenzi (s.a.w) kwamba: “**Muislamu ni yule asiyemdhuru ye yote kwa mkono au ulimi,**” na tuiswasumbue au kuwaudhi wengine.

**“Muislamu ni yule asiyemdhuru  
ye yote kwa mkono au ulimi wake”.**



# UFUNGUO WA MASWALI

## MOLA WA WALIMWENGU: KUMUAMINI ALLAH

### Jaza sehemu za wazi

1. nafsi zao wenyewe - upeo wa mbali
2. jani
3. kuwa
4. wanampenda
5. mnampenda/ atakupendeni
6. nyoyo
7. dua
8. karibu

### Tujipime

1- d    2-b    3-c    4- a    5- d

201

## UFUNGUO WA AMANI DUNIANI NA PEPO HUKO AKHERA: IMANI

### Jaza sehemu za wazi

1. Andika/neno
2. Shetani/adui
3. Madaraka/ushirika
4. Malaika/amin
5. Malaika/ Shetani

### Tujipime

1- d    2-a    3-d    4- c    5- c

## SWALA (AL-SALAH)

### Tuyapime Maarifa Yetu 1

1- Ndiyo 2- Hapana 3- Hapana 4- Ndiyo 5- Ndiyo 6- Ndiyo 7- Hapana 8- Hapana  
9- Ndiyo 10- Ndiyo

### Tuyapime maarifa yetu 2

1- Hapana 2- Hapana 3- Hapana 4- Ndiyo 5- Hapana 6- Hapana 7- Ndiyo 8- Hapana  
9- Hapana 10- Ndiyo

### Tuyapime Maarifa yetu 3

1- Ndiyo 2- Ndiyo 3- Ndiyo 4- Hapana 5- Ndiyo

### Tujipime 1

1- b 2- a 3- b 4- b 5- c 6- b 7- c 8- d 9- b 10- d 11- a  
12- c 13- a 14- c 15- c

### Tujipime 2

1- d 2- b 3- a 4- b 5- c 6- a 7- a 8- a 9- b 10- b

### Tujipime 3

1- d 2- d 3- b 4- a 5- c 6- b 7- c 8- c 9- a 10- b

### Jaza sehemu za wazi 1

1- Tahajjud 2- Satr al-Awrah 3- Istiqbal al-Qiblah 4- al-Qira'ah 5- Sajdah

### Jaza sehemu za wazi 2

1- Kulia 2- Khutba 3- Takbir al-Tashriq 4- al-Kifayah 5- kuashiria 6- Dhambi  
7- al-Sajdah al-Tilawat

## NINAJIFUNZA KUHUSU MTUME WANGU: SIRA

**Ni lipi jibu sahihi?**

- 1- a   2- c   3- b   4- d   5- c   6- c   7- b   8- b   9- d   10- d  
11- c   12- a   13- a   14- d   15- c   16- d   17- b

## NOTES

## NOTES

# e-Erkam

FREE ISLAMIC E-BOOKS

You can download over 200 Islamic books in over 23 languages  
on your computer, iphone, ipad etc. FOR FREE.

English – French – German – Spanish – Italian – Russian – Arabic – Portuguese – Chinese – Hungarian – Ukrainian  
Tajik – Albanian – Tatar – Bulgarian – Uzbek – Azeri – Kazakh – Georgian – Bashkir – Uyghur – Kirgiz – Ahiska

Islamic books in various languages are now waiting for you in ten different formats at the popular reading site smashwords.com. You may read the books by downloading them on your PC, iPhone, iPad, Kindle and devices alike FOR FREE.

Our books are available online for free at Amazon, Borders, Sony, B&N, Apple Store, Diesel and Stanza, in all the iBook, Kindle, Nook, Sony and Diesel formats.

You may printout the copies downloaded in word or pdf formats, reproduce them or send to your loved ones via email.

Our special offer of free downloads is limited to 1 year.

## E-books

To obtain a free copy of any one of our Islamic books that are available in 10 different formats, you only need to visit [www.smashwords.com](http://www.smashwords.com) and type 'Erkam' in the search box.

## iPad Book Applications


To obtain a free copy of any one of our books, you only need to type 'Erkam' in the search box of iTunes on your computer or of App Store on your iPad.

## iPhone Book Applications


To obtain a free copy of any one of our books, you only need to type 'Erkam' in the search box of iTunes on your computer or of App Store on your iPad.



**ERKAM PUBLISHING**




**Endowment, Charity,  
and Service in Islam**




**The Story of the Reed**



**Ikhlas And Taqwâ**




**Tears of the Heart**




**The Final Divine  
Religion ISLAM**



**Such a Mercy He Was**



**The Secret in the  
Love for God**




**My Beautiful Religion 1**




**A Peaceful Home**




**The Exemplar  
Beyond Compare**




**Principles from the  
Lives of the Four  
Rightly-Guided  
Caliphs**



**Sufism**



**The Last Breath**



**Hajj Mabrur  
and Umrah**




**The Prophet Muhammad  
Muftafa The Elect (s.a.v) 1**




**Contemplation  
in Islam**




**The Society of  
the Age of Bliss**



**Civilisation of Virtues  
1**



**Civilisation of Virtues  
2**



**40 Hadiths For  
Children With Stories**



**ERKAM**  
YAYIN VE SANAYİ MAMÜLLERİ A.Ş

► Adress : İkitelli Organize Sanayi Bölgesi Mahallesi Atatürk Bulvarı Haseyad 1. Kısım No: 60 / 3-C  
Başakşehir - İstanbul / TURKEY

Phone : (+90 212) 671 07 00 (Pbx)  
E-mail : info@islamicpublishing.org


Fax : (+90 212) 671 07 48

Web Site : <http://www.islamicpublishing.org>

FOR FREE IN PDF FORMAT

# ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT  
**1550 BOOKS IN 59 LANGUAGES FOR FREE**



Islamic books in different languages are waiting  
for you in PDF format at the web site  
[www.islamicpublishing.org](http://www.islamicpublishing.org)